

Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia Dhidi ya Wakimbizi,
Watu Warudio Makwao, na Waliopoteza Makazi.

Miongozo ya Uzuiaji na Ukabilianaji

Mei 2003



UNITED NATIONS
HIGH COMMISSIONER
FOR REFUGEES



YALIYOMO

DIBAJI.....1

Usuli.....2

SURA YA 1 Maelezo ya jumla kuhusu Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia7

Kuwalinda Wakimbizi Dhidi ya nyanyasaji wa Kingono na Kijinsia.....8

Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia ni nini?11

Fasili za Dhana Muhimu14

Aina za Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia19

Lini na Wapi ambapo Unyanyasaji wa Kingono

na Kijinsia Hutokea?25

Sababu na Madhara Yatokanayo na Unyanyasaji

wa Kingono na Kijinsia27

Mambo Muhimu ya Kukumbuka32

SURA YA 2 Kanuni Elekezi35

Kanuni Elekezi za Programu36

Kanuni Elekezi kwa ajili ya Mtu Binafsi37

Mkabala Unaoshirikisha Sekta Mbalimbali40

Mambo Muhimu ya Kukumbuka42

SURA YA 3 Kuzuia Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia45

Kubadili Desturi za Kijamii na Kiutamaduni47

Kujenga Upya Familia na Mifumo Himili ya Kijamii53

Kujenga Mazingira ya Kuboresha Mifumo ya Uwajibikaji55

Uandaaji wa Huduma na Viwezeshaji Stahiki56

Kushawishi Mfumo Rasmi na usio Rasmi wa Kisheria63

Ufuatiliaji na Uwekaji Kumbukumbu za Matukio ya Vitendo	
vya Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia	66
Mambo Muhimu ya Kukumbuka	67

**SURA YA 4: Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kingono
na Kijinsia69**

Kuanzisha Shughuli Uelimishaji na Uhamasishaji wa Jamii	71
Kuelimisha watendaji kuhusu jinsi ya kushughulikia mahitaji ya waathiriwa/wanusurika.....	72
Watendaji wote wakubaliane kutumia mfumo wa aina moja wa kutoa ripoti.....	73
Kuzipatia kamati za wakimbizi uwezo wa kuchukua hatua	75
Kujenga uwezo wa kukabiliana na mahitaji ya kiafya/kitiba ya waathiriwa/wanusurika.....	76
Kupanga namna ya Kukidhi Mahitaji ya Kisaikolojia na Kijamii ya Waathiriwa/Wanusurika	77
Kujenga uwezo wa Kukabiliana na Masuala ya Ulinzi na Usalama	78
Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Masuala ya Kisheria/Haki	79
Kubainisha dhima za watu wengine wawezao kuwa watendaji.....	83
Uandaaji wa Mpango kwa ajili ya Kuwashirikisha Wahalifu	85
Mambo muhimu ya kukumbuka.....	86

SURA YA 5: Mazingatio Mahususi ya Watoto Wakimbizi89

Kanuni za Mwongozo	90
Makundi ya Watoto Wakimbizi walio katika hatari mahususi za unyanyasaji wa kingono na kijinsia.....	92
Aina mahususi za vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya watoto	98
Mazingatio muhimu katika Uzuiaji wa Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia dhidi ya Watoto.....	101

Mazingatio Muhimu katika Kukabiliana na Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia dhidi ya Watoto.....	105
Masuala Muhimu ya Kukumbuka	111
SURA YA 6: Muundo wa Utekelezaji	113
Uandaaji wa Mpango wa utekelezaji	113
Masuala muhimu ya kukumbuka.....	124
SURA YA 7: Ufuatiliaji na Tathmini	125
Kubainisha ufuatiliaji na tathmini	125
Shabaha za Taratibu za Ufuatiliaji na Tathmini	126
Aina za Taratibu za Ufuatiliaji na Tathmini	127
Kubuni Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya Programu Zinazolenga unyanyasaji wa kingono na Kijinsia.....	127
Mfano wa zana za kutolea ripoti.	132
Mambo Muhimu ya Kukumbuka	136
SURA YA 8: Utesaji Kijinsia.....	139
Kushughulikia Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia Katika Kuamua Hadhi ya Ukimbizi	139
Utesaji wa Kijinsia kwa Mujibu wa Kifungu I A(2) cha Makubaliano ya 1951 na /au Nyongeza yake ya mwaka 1967 kuhusu Hadhi za Wakimbizi.	141
KIAMBATISHO 1: Kanuni za Maadili ya UNHCR.....	155
KIAMBATISHO 1.1: Misingi Muhimu ya Kanuni za Maadili	163
KIAMBATISHO 2: Fomu ya Kutolea Taarifa ya Tukio	164
KIAMBATISHO 3: Fomu ya Ripoti ya Kila Mwezi.....	179
KIAMBATISHO CHA 4: Fomu ya Historia ya Matibabu na Uchunguzi...	181
MAREJEO YALIYOPENDEKEZWA	185

DIBAJI


Katika kila jamii ulimwenguni kuna watu ambao wameathiriwa na vitendo vya kikatili. Vitendo vingi vya kikatili vinavyofanywa na vikundi vya watu wenye silaha katika maeneo ya mapambano huwa vinatangazwa kwa ufasaha wakati ambapo vitendo vifanywavyo kwa siri ndani ya nyumba za watu mara nyingi hufichwa. Wakimbizi na watu waliopoteza makazi ndani ya nchi zao ni makundi mawili ya watu wasiofaidika na ulinzi wa serikali za nchi zao. Vilevile ni makundi yaa watu ambao wako hatarini kuathiriwa na vitendo vya kikatili, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Tumejifunza kwamba unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni vitendo ambavyo vinashamiri sana katika mazingira ambapo haki za binadamu kwa ujumla haziheshimiwi. Unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni vitendo ambavyo kwa hakika ni ukiukaji wa haki za binadamu. Wanawake na watoto ambao ndio hasa huwa hatarini kuathiriwa na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu ni kundi la watu ambao huathiriwa sana na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Miongozo hii inatoa ushauri wa kiutendaji kuhusu namna ya kubuni mikakati na kutekeleza shughuli vinavyolenga kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Miongozo hii pia ina taarifa muhimu kuhusu afya, sheria, usalama na haki za msingi za binadamu kuhusiana na mikakati pamoja na shughuli hizo zilivyoitajwa hapo juu.

Miongozo hii ilitayarishwa kwa kushauriana na wabia wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi katika masuala ya uhifadhi wa wakimbizi. Wenza hao ni: serikali, mashirika ya kiserikali na AZISE. Miongozo hii imekusudiwa itumiwe na wafanyakazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi na wanachama wa washirika watendaji wanaojishughulisha na uhifadhi na usaidizi wa wakimbizi na watu waliopoteza makazi nchini mwao. Miongozo hii imejaribiwa katika nchi 32 ulimwenguni kote kwa kushirikisha wabia zaidi ya 60.

Unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni tatizo kubwa ambalo tunahitaji kulikibili kikamilifu. Tumeunda vyombo mbalimbali ili kusaidia kuzuia tatizo hili na kuwasaidia waathiriwa pindi tunaposhindwa kuziuia. Niwajibu wetusisi sote tunaojishughulisha na wakimbizi pamoja na watu waliopoteza makazi katika nchi zao kuvitumia vyombo hivi kikamilifu.



Ruud Lubbers

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi

UTANGULIZI

Usuli

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi lilichapisha kwa mara ya kwanza kijitabu kilichoitwa Unyanyasaji wa kingono dhidi ya Wakimbizi: Miongozo ya Uzuiaji na Ukabilianaji mnamo mwaka 1995. Mpaka kufikia wakati huo, ilikuwa dhahiri kwamba uzito wa tatizo hili ulihitaji mkabala makini wa utatuzi, hatua madhubuti, na jitihada za pamoja ambazo, hadi wakati huo, hazikuwa zimebuniwa wala kutungwa na kuandikwa katika machapisho yoyote ya awali ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi. Miongozo ya mwaka 1995 ilisaidia kuleta utambuzi na ufahamu wa hali ya juu kuhusiana na ukiukwaji wa haki za binadamu uliokithiri. Aidha, Miongozo hiyo iliweka misingi ya kuandaa mipango ya kuzuia na kukabiliana na ukiukwaji huo. Hata hivyo, vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya wakimbizi, hasa watoto na wanawake, bado vinaendelea kwa nguvu ileile. Vinazidi kuwa vibaya zaidi kutokana na kukosekana kwa usawa wa kijinsia katika jamii husika; vimeduwa vikitumika vilevile kama silaha ya vita na kama nyenzo ya udhibiti; vitendo hivi vimeduwa chanzo cha watu kuondolewa katika makazi yao kwa nguvu na vimesababisha kuvunjika kwa mihimili inayolinda mahusiano katika familia na jamii nzima, hali ambayo inaambatana na watu kupoteza makazi yao. Vitendo hivi vilevile vimeduwa vikifanywa na baadhi ya watu ambao hupewa dhamana ya kuwalinda wakimbizi na watu walipoteza makazi.

Tangu mwaka 1995, tumejifunza mengi kuhusiana na majukumu ya mtu mmojammoja, ya asasi na ya kitaifa ya utekelezaji wa Miongozo ya mwaka 1995 na jinsi ya kuwalinda wakimbizi. Katika miaka yote hii, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia wakimbizi, mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa, mashirika ya kiserikali na yasiyokuwa ya kiserikali, wakimbizi, watu wanaorudi kutoka uhamishoni na watu wasiokuwa na makazi maalum nchini mwao, wametathimini mipango na shughuli zilizopendekezwa katika Miongozo ya mwaka 1995 katika muktadha wa hali tata za dharura. Kilele cha mchakato huu wa kutathimini kilikuwa ni Mkutano wa Mashirika kuhusu Masomo Yaliyotokana na Uzuiaji na Uingiliaji-kati wa Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia katika Mazingira ya Ukimbizi, uliofanyika huko Geneva mnamo mwaka 2001.

Washiriki katika mkuu huo walainisha maeneo ya kuboreshwa zaidi na walionyesha waziwazi umuhimu wa kuipitia tena Miongozo ya mwaka 1995 ili kuufanya marekebisho mkabala wa mashirika na sekta mbalimbali wa kushughulikia unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya wakimbizi, watu wanaorejea makwao na walipoteza makazi ndani ya nchi zao. Mapendekezo yaliyotokana na Mkutano huo ni pamoja

na kuimarisha uwajibikaji wa asasi kwa kuanzisha utaratibu wa Maadili kwa ajili ya wafanyakazi na watoa huduma za kijamii; kuweka viwango vya chini vinavyolingana vya kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia; kusaidia mgawo na usimamizi wa pesa na wafanyakazi; na uingizaji wa mtazamo wa usawa wa kijinsia katika utendaji wa asasi mbalimbali. Washiriki walisisitiza umuhimu wa kuihusisha jumuiya ya wakimbizi katika hatua zote za mipango: uandaaji, utekelezaji, ufuutiliajini na tathmini.

Kufuatia mapendeleko ya Mkutano wa mwaka 2001, Miongozo hii mipy ya Uzuiaji na Ukabilianaji na Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia dhidi ya Wakimbizi, Watu warejeao makwao na waliopoteza makazi katika nchi zao iliandaliwa kuitia wa mashirika mbalimbali. Miongozo hii imefanyiwa utafiti nyanjani katika nchi 32 ulimwenguni kote, ukihuisha ushirikishaji wa watendaji zaidi ya 60.

Lengo la Miongozo

Miongozo hii imekusudiwa itumiwe na wafanyakazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, mashirika ya kiserikali na yasiyokuwa ya kiserikali, na mashirika ya serikali wenyiji, ambayo hujishughulisha na utoaji wa ulinzi na misaada kwa wakimbizi na watu ambao wako chini ya uangalizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi. Aidha, Miongozo hii imekusudiwa kuongoza shughuli mbalimbali zinazolenga kuzuia na kushughulikia tatizo la unyanyasaji wa kingono na kijinsia zinazoanzishwa na jumuiya za wakimbizi wenyewe. Miongozo hii vile vile inachunguza chanzo na sababu zinazochangia kuwepo kwa tatizo la unyanyasaji wa kingono na kijinsia, na inapendekeza hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kusaidia kuzuia na kukabiliana na ya unyanysaji huo. Kwa kutambua kwamba unyanyasaji wa kingono na kijinsia unatokana na kukosekana kwa usawa baina ya wanawake na wanaume, Miongozo hii, kwa hiyo, inatoa mkabala mpya wa kulikabili tatizo hili. Miongozo inatoa wito uwepo ushirikiano wa kimkakati – ikiwa ni pamoja na ule wa baina ya wanaume na wanawake, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya haki za binadamu, ya kitaifa na kimataifa, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, na Mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa na Nchi mbalimbali ili kuhamasisha mabadiliko. Miongozo hii pia inasisitiza umuhimu wa ushirikishwaji wa jumuiya ya wakimbizi, hasa wanawake na wasichana katika kupanga, kutekeleza na kutathimini shughuli zilizobuniwa kuzuia na kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Miongozo hii, ambayo inabadilika kulingana na muktadha na mazingira, inatoa mfumo wa uandaaji wa mikakati inayofaa ya kuzuia na kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Miongozo haitoi seti kamilifu ya shughuli inayofaa kwa kila aina ya mazingira. Kwa kuwa uzuiaji naukabilianaji wa tatizo

hili tata la unyanyasaji wa kingono na kijinsia huhitaji ushirikiano baina ya mashirika mbalimbali, mchangamano wa taaluma mbalimbali na ushirikiano wa sekta mbalimbali, Miongozo hii vilevile inahimiza tafakari na majadiliano baina ya mashirika na washiriki wengine. Miongozo hii imekusudiwa kuwa nyongeza na wala siyo kubatilisha maandiko mengine ya kufundishia.

Yaliyomo katika Miongozo

Sura ya Kwanza	Sura hii inatoa maelezo ya ujumla pamoja na taarifa za msingi kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia, chanzo chake, mambo yanayochangia uwepo wake, na madhara yake.
Sura ya Pili	Sura hii inatoa kanuni zinazoongoza jithhada zote za kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Aidha, sura inatoa muundo wa mkabala shirkishi na wenye kuzingatia sekta nyingi zaidi.
Sura ya Tatu	Sura ya tatu inapendekeza mikakati ya kupunguza au kutokomeza kabisa vyanzo na mambo yanayochangia uwepo wa vitendo vyta unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
Sura ya Nne	Inaeleza jinsi ya kuanzisha mifumo ya ukabilianaji kwa kutumia sekta mbalimbali ili kushughulikia tatizo la unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
Sura ya Tano	Inaelezea kwa kina mambo muhimu na ya kipekee yanayopaswa kuzingatiwa wakati wakuwasaidiawatoto ambaowameathiriwa au wako katika hatari ya kukumbwa na tatizo la unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
Sura ya Sita	Inatoa mwongozo wa hatua kwa hatua wa jinsi ya kuandaa mpango wa utekelezaji ambaa unatumia, kama msingi, uwezo uliopo katika hali yoyote ile.
Sura ya Saba	Inajadili taratibu za ufuatilaji na tathmini. Vilevile, sura hii inatoa mifano ya viashiria vyta upimaji wa athari za hatua zilizobuniwa kuchukuliwa ili kuwalinda watu dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
Sura ya Nane	Inaelezea dhana ya utesaji unaohusiana na masuala ya kijinsia kuitumia dhana hiyo wakati wa kushughulika na watu wanaotafuta hifadhi.

Pale inapofaa, wasomaji wa Miongozo hii wataelekezwa kwenye vyanzo vyta ziada vyta taarifa ili kupata taarifa za kina zaidi

kuhusiana na mada mahsus. Vichwa vya makala za marejeo haya vimetolewa katika matini yote hii kwenye visanduku viliviyotiwa kivuli kwa kutumia maneno "Rejea pia:". Fomu za sampuli ambazo zinaweza kubadilishwa ili zitumike katika hali mahsus zimewekwa kama viambatisho. Orodha yenyenye maelezo ya kina kuhusu nyenzo zilizopendekezwa imeambatanishwa baada ya viambatisho. Matoleo ya kielectroniki ya nyaraka teule yamejumuishwa kwenye "CD-ROM" ambayo imetolewa pamoja na Miongozo hii.

Dhana Muhimu

Miongozo hii inatumika katika mazingira ambapo kuna wakimbizi, watu warejeao makwao, waliopoteza makazi nchini mwao na/au watu wanaotafuta hifadhi. Ingawa uwezo na utendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi huweza kutofautiana kutegemea na kama watu wanaohusika ni wakimbizi au watu waliopoteza makazi nchini mwao, vyombo vingine kama vile mamlaka za nchi wenyeji, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali au mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa, vinaweza kuwalinda na kuwasaidia wakimbizi na watu waliopoteza makazi katika nchi zao.

Kwa ajili ya manufaa ya kiuelezaji, neno wakimbizi litamaanisha vilevile watu wanaotafuta hifadhi, watu warudio makwao na watu waliopoteza makazi nchini mwao, wake kwa waume; watoto na watu wazima. Hali kadhalika neno mandhari ya wakimbizi litamaanisha vituo na huduma wakiwa safarini, vituo vya mapokezi, kambi za wakimbizi na sehemu za kuzuia watu wanaotafuta hifadhi, stesheni za njiani wakati wa kurejesha wakimbizi, na kambi za jumuiya ya watu waliopoteza makazi nchini mwao. Wakati mapendekezo mengi kuhusiana na mandhari ya wakimbizi hutumika katika miktadha ya vijiji na mijini, inapobidi, hatua mahsus za kuchukuliwa katika mazingira mahsus zimeonyeshwa.

Neno waathiriwa/wanusurika litamaanisha watu, mmoja mmoja au vikundi, waliokumbwa na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Wakati inabaidi waathiriwa washughulikiwe kwa huruma na upendo, kuwazungumzia kama wanusurika kunaonyesha utambuzi wa nguvu zao na uthabit wao. Wakati mwengine, hata hivyo, mwathiriwa wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia anabaki kuwa mwathiriwa hata kama atafanya jitihada binafsi za kujisaidia au atapata msaada kutoka kwingineko. Katika miktadha fulani ya kisheria, neno mwathiriwa linaweza kuwa linafaa na/au linahitajika kuendana na sheria zinazohusika wakati wa kutafuta haki za kisheria. Katika mazingira yasiyokuwa ya kisheria, hata hivyo, neno mwathiriwa linaweza kumaanisha udhaifu na unyanyapaa; mambo ambayo wahusika wote inabidi wayaepuke. Kwa kutambua uwezekano wa yote hayo kutokea, dhana zote hizi mbili hutumika

Wakati wanaume na wavulana mara nyingi huwa ni waathiriwa/wanusurika na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, takwimu zinathibitisha kwamba wengi wa waathiriwa/wanusurika ni wanawake na wasichana. Katika kuthibitisha ukweli huu, Miongozo inatumia viwakilishi vya kike kuwaelezea waathiriwa/wanusurika.

Neno watendaji linamaanisha watu binafsi, vikundi, mashirika na asasi zinazojihusisha na uzuaji na ukabili anaji wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Watendaji wanaweza kuwa wakimbizi, wenyeji, wafanyakazi au watu wanaojitolea kutoka Mashirika ya Umoja wa Mataifa, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, asasi za serikali mwenyeji, wahisani na wanachama wengine wa jumuiya ya kimataifa.

SURA YA 1

MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UNYANYASAJI WA KINGONO NA KIJINSIA

Unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni ukiukaji wa haki za binadamu. Unyanyasaji wa aina hii Unadumisha fikra mgando kuhusu majukumu ya kijinsia yanayomnyima mtu utu wake na kukwamisha maendeleo ya binadamu. Wengi wa waathiriwa/wanusurika na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni wanawake na wasichana.

Unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni zaidi ya shambulio langono na ubakaji. Ingawa katika baadhi ya miktadha huweza kutokea hadharani, kwa kiasi kikubwa, chanzo chake ni mitazamo binafsi inayofumbia macho unyanyasaji ndani ya familia, jamii na nchi. Kiini na madhara ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia lazima vieleweke kabla ya kupanga mipango inayofaa kuzuia na kukabiliana na tatizo hili.

Kama wakala wa Umoja wa Mataifa, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi limepewa uwezo wa kutoa uhifadhi wa kimataifa kwa wakimbizi. Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, pamoja na nchi mbalimbali, kwa namna hii, hushirikiana katika jukumu la kuhakikisha kwamba wakimbizi wanalindwa dhidi ya dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Ukweli kwa uchache kuhusu Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia

- Duniani kote, inakadirisha kwamba asilimia arobaini hadi sabini ya mauaji ya wanawake hufanywa na wapenzi wao, mara nyingi katika muktadha wa mahusiano ya kudhalilisha.
- Ulimwenguni kote angalu mmoja kati ya wanawake watatu amewahi kupigwa, kushurutishwa kufanya ngono, au amedhalilishwa kwa namna nyingine katika maisha yake.
- Bishara ya utumwa duniani kote imekua karibu kwa asilimia hamsini kutoka mwaka 1995 hadi 2000 na Shirika la Kimataifa la UHAMAJI linakadiria kwamba kiasi cha wanawake milioni mbili wanauzwa kutoka nchi moja hadi nyingine kila mwaka.
- Zaidi ya wanawake na wasichana wa Kiafrika milioni 90 ni waathiriwa wa ukeketaji.

- Wasichana takribani milioni 60 ambao vinginevyo wangelikuwa hai, wamepoteza maisha katika jamii mbalimbali hususani katika bara la Asia, kutokana na utoaji mimba, kuuawa utotoni au kutopewa huduma zinazostahili.
- Katika miaka ya karibuni, ubakaji kwa kundi kubwa uliripotiwa huko Bosnia, Kambodia, Liberia, Peru, Somalia na Uganda. Timu ya uchunguzi kutoka Jumuiya ya Ulaya imekadiria kwamba zaidi ya wanawake wa Kiislam 20,000 walibakwa wakati wa vita vya Bosnia.
- Asilimia 94 ya familia zilizopoteza makazi zilizochunguzwa nchini Siera Leoni zimeripoti matukio ya udhalilishaji kingono, likiwemo la ubakaji, utesaji na utumwa wa ngono. Angalau si chini ya wanawake 250,000, na pengine labda wengi wa kufikia 500,000, walibakwa wakati wa mauaji ya kimbari yaliyotokea nchini Rwanda mnamo mwaka 1994.

Kutoka: Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake: Tatizo la Kiafya Lililofichika (Benki ya Dunia 1994)

Jarida kuhusu Ukweli Juu ya Unyanyasaji wa Kijinsia: Takwimu za kufanya kazi za Jarida la ukweli
(L.Heise, IWTC 1992)
na
Maendeleo ya Wanawake Duniani (UNIFEM, 2000).

Kuwalinda Wakimbizi Dhidi ya nyanyasaji wa Kingono na Kijinsia

Binadamu wote wamezaliwa huru na sawa katika utu na haki.

Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu

Baraza Kuu la Umoja wa ataifa

10 Desemba 1948

Uzuiaji naukabilianaji wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia huwa na uhusiano wa moja kwa moja na ulindaji wa haki za binadamu.

Hakizabinadamunikwaajiliyawoteulimwenguni,hazikengeushiki, hazigawanyiki, zinakamilishana na kutegemeana. Kila mtu bila kujali mbari yake, rangi yake, jinsi, lugha, dini, mtazamo wa kisiasa au mitazamo mingineyo, kuzaliwa kwake au hadhi yake, asili yake ya kitaifa au kijamii, mali zake, anastahili heshima, hifadhi, kutekeleza na kufurahia haki zote za msingi za binadamu na

uhuru wa kufanya atakavyo. Serikali zinawajibu wa kuhakikisha unufaikaji sawa wa haki zote katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia na kisiasa, kwa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana.

Vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia vinavunja kanuni nydingi za haki za binadamu zilizo katika vyombo vingi vya kimataifa kuhusu haki za binadamu. Miongoni mwa nyiningezo, haki hizo ni pamoja na hizi:

- ◎ Haki ya kuishi, uhuru na usalama wa mtu.
- ◎ Haki ya kufikia kiwango cha juu kabisa cha afya ya mwili na akili.
- ◎ Haki ya kuwa na uhuru kuondokana na mateso, kufanyiwa vitendo vya kikatili, kinyama na kudhalilishwa au kuadhibiwa.
- ◎ Haki ya kuwa huru kwenda popote, kutoa maoni, kujieleza, na kushirikiana na wengine.
- ◎ Haki ya kuingia katika maisha ya ndoa kwa ridhaa huru kabisa pamoja na stahili ya kuwa na haki sawa ya ndoa, wakati wa ndoa na baada ya ndoa kuvunjika.
- ◎ Haki ya kupata elimu, hifadhi ya jamii na maendeleo binafsi.
- ◎ Haki ya kushiriki katika shughuli za kisiasa, kiutamaduni na za umma, haki sawa ya kupata huduma za jamii, kazi na ujira sawa kwa kazi iliyo sawa.

Vyombo vingi vya Kimataifa vinalenga hasa kushughulikia suala la unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya wanawake na wasichana. Mapatano ya Utokomezwaji wa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake yaliyofikiwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1981, Azimio la Umoja wa Mataifa la Utokomezwaji wa Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake lililofikiwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1993, na Azimio la Beijing na Ilani ya Utendaji, lililofikiwa huko Beijing mnamo mwaka 1995, hujumuisha aina zote za ubaguzi kama unyanyasaji dhidi ya wanawake na wasichana na husisitiza jukumu la serikali kufanya juhudzi za kuutokomeza. Chombo cha hivi karibuni, Sheria ya Roma ya mwaka 1998 ya Mahakama ya Kimataifa ya Kesi za Jinai, kinafasili ubakaji, utumwa wa ngono, ukahaba wa kulazimishwa, ujauzito wa kulazimishwa, kuhasiwa kwa nguvu au aina nydinge yoyote ya unyanyasaji wa kingono ambaao madhara yake ni sawa makosa yaliyotajwa hapo juu kuwa ni uhalifu dhidi ya binadamu. Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa namba 1325 (2000) linasisitiza kuhusu jukumu la serikali kukomesha tabia ya kutoadhibu uhalifu dhidi ya binadamu na uhalifu wa kivita, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kingono na aina zingine za unyanyasaji dhidi ya wanawake na wasichana.

(Kamati Kuu ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi)...Inalaani na unyanyasaji wa kijinsia na aina zote za ubaguzi zenyne misingi yake katika jinsi ya mtu wanazofanyiwa wakimbizi, wanawake na wasichana waliopoteza makazi nchini mwao, na inatoa wito kwa Nchi mbalimbali kuhakikisha kwamba haki za binadamu za watu hawa pamoja na ukamilifu wao kimwili na kisaikolojia unalindwa na pia wanafahamishwa kuhusu haki zao hizi.

Kamati kuu: Hitimisho Na. 85 (XLIX), 1998

Umoja wa Mataifa, Mashirika ya haki za binadamu, na watoa huduma za kibinadamu wafadhili hushirikiana na serikali za nchi mbalimbali katika kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinalindwa. Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, kama wakala wa Umoja wa Mataifa limepewa jukumu la kutoa hifadhi ya kimataifa kwa wakimbizi na kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa matatizo yao. Kwa hali hii, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi na serikali hushirikiana katika kutekeleza jukumu la kuhakikisha kwamba wakimbizi wanalindwa dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Fasili ya Uhifadhi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi

Shughuli zote zinazolenga kuhakikisha kupata na kufurahia haki zote, kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wanaoshughulikiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, kwa mujibu wa vyombo vyta kisheria vinavyohusika (Sheria ya kimataifa ya kibinadamu, haki za binadamu, na wakimbizi).

Katika mazingira ambapo hakuna hatua zinazochukuliwa kuzuia na kukabiliana na vitendo vyta unyanyasaji wa kingono na kijinsia, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi lazima liongoze uratibu na uanzishwaji, kama sehemu ya shughuli zake muhimu, wa programu za kulinda na kusaidia wakimbizi na waliopoteza makazi, ambazo zinashughulikia vitendo vyta namna hii. Hii ni pamoja na kutetea haki za wakimbizi, kuzishauri serikali za nchi mbalimbali juu ya jinsi ya kurekebisha utungaji wao wa sheria ili uendane na viwango vyta kimataifa na kuchukua hatua za kupunguza hatari ya kuza watu, hatari ambayo inakua wakati ambapo watu wanakuwa wamepoteza makazi.

Kutorosha watu itamaanisha uajiri, usafirishaji, uhamisho, utunzaji na upokeaji wa watu, kwa njia ya vitisho au utumiaji wa nguvu au aina zingine za shurti, za utoroshaji, utapeli, ulaghaji, utumiaji vibaya wa madaraka, au hali ya kudhuriwa, au hali ya kutoa na kupokea malipo au ruzuku ili kupata ridhaa ya mtu mwenye madaraka juu ya mtu kwa madhumuni ya unyonyaji. Unyonjai utajumuisha, kwa kiwango cha kuanzia, unyonyaji wa ukahaba kwa wengine au aina nyininge za unyonyaji wa kingono, kazi au huduma za shurti; utumwa au shuguli zingine zinazo fanana hivyo, utumishi wa kitumwa au utoaji wa viungo vya mwili.

Itifaki ya Kuzuia, Kukomesha na Kuadhibu Utoroshaji w watu, hasa Wanawake na Watoto, nyongezea kwa Mapatano ya Umoja wa Mataifa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa, Novemba 2000

Rejea pia:

- **Mapatano ya Umoja wa Mataifa Dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa (2000).**
- **Sheria ya Roma ya Mahakama ya Kimataifa ya Kesi za Jinai (1998).**
- **Azimio la Beijingi na Ilani ya Utendaji (1995).**
- **Azimio la Umoja wa Mataifa la Utokomezwaji wa Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake (1994).**
- **Mapatano Dhidi ya Utesaji na Vitendo Vingine vya au Adhabu za Kikatili, , Kinyama na Kudhalilisha (1984).**
- **Mapatano ya Utokomezwaji wa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (1979).**
- **Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa (1966).**
- **Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (1966).**
- **Sheria ya Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudmia wakimbizi – GA Res 428 (v) (1950).**
- **Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948).**

Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia ni nini?

Unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya wanawake ni dhana ambazo zinatumika kwa kubadilishana. Dhana zote hizi zinamaanisha ukiukwaji wa haki za msingi za binadamu ambao hudumisha fikra mgando kuhusu majukumu ya kijinsia ambayo humnyima mtu utu wake na uhuru wake na kukwamisha maendeleo ya watu kwa ujumla. Dhana hizi zinamaanisha madhara ya kimwili, kingono na kisaikolojia

ambayo hutia shime udunishwaji wa wanawake na kufanya aendelee kutawaliwa na kudhibitiwa na wanaume.

Wakati ambapo unyanyasaji wa kingono huwa na athari kubwa sana kwa maisha ya wanawake na wasichana ambao ndio wengi wa waathiriwa/wanusurika, unyanyasaji huu hukwamisha vile vile maendeleo ya wanaume na wavulana. Utokomezwaji wa unyanyasaji wa kijinsia na tofauti za kijinsia husaidia kuimarisha jamii nzima.

Dhana ya unyanyasaji wa kijinsia inatumika kupambanua unyanyasaji wa kawaida na unyanyasaji unaolenga watu au vikundi vyta watu kutokana na jinsia yao. Unyanyasaji wa kijinsia umefasiliwa na Kamati ya CEDAW kuwa ni unyanyasaji unaomlenga mtu kutokana na jinsia au jinsi yake. Unyanyasaji huu hujumuisha vitendo ambavyo vinaumiza kimwili, kiakili au kijinsia, tishio la vitendo kama hivyo, shurti na aina nyingine za matendo yanayokosesha uhuru.

Dhana ya unyanyasaji dhidi ya wanawake inamaanisha kitendo chochote cha unaynyasaji wa kijinsia ambacho matokeo yake ni; au ambacho kinaweza kuleteleza, madhara kimwili, kingono na kisaikolojia kwa wanawake na wasichana, kiwe kinatendeka hadharani au faraghani. Unyanyasaji dhidi ya wanawake ni aina ya unyanyasaji wa kijinsia na hujumuisha unyanyasaji wa kijinsi.

Unyanyasaji wa kingono, ikiwa ni pamoja na unyonyaji na udhalilishaji, humaanisha kitendo chochote, jaribio au tishio la kijinsia ambalo matokeo yake ni; au ambalo linaweza kuleteleza madhara ya kimwili, kisaikolojia na kihisia. Unyanyasaji wa kingono ni aina ya unyanyasaji wa kijinsia.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi linatumia mtazamo jumuishi kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia, ambao unatambua kwamba ingawa wengi wa waathiriwa/ wanusurika na vitendo hivi ni wanawake na wasichana, wavulana na wanume vile vile ni walengwa wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Fasili Pana ya Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia inayotumiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudmia Wakimbizi pamoja na Washirika Watekelezaji

(Inatokana na Ibara 1 na 2 za Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu Utokomezwaji wa Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake (1993) na pendekero la 19, aya ya 6 ya Mkutano wa 11 wa Kamati ya CEDAW)

...unyanyasaji wa kijinsia ni unyanyasaji ambao unamlenga mtu kwa msingi wa jinsia au jinsi yake. Unyanyasaji huu unajumuisha vitendo ambavyo vinaumiza kimwili, kiakili au vinaleta madhara au maumivu kingono, vitisho vya vitendo vya namna hiyo, shurti na vitendo vingine vinavyomnyima mtu Uhuru....Wakati wanawake, wanaume, wavulana na wasichana wanaweza kuwa waathiriwa wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, wanawake na wasichana ndio waathirka wakubwa.

...unyanyasaji huu ueleweke kuwa unajumuisha, lakini hauishii katika vitendo vifuatavyo:

- a) Unyanyasaji wa kimwili, kingono na kisaikolojia ambao hutokea katika familia, ikiwa ni pamoja na kupiga, unyonyajiwakingono, uonevuwakingono dhidiyawatoto katika nyumba waishiyo, unyanyasaji unaohusiana na mahari, ubakaji katika ndoa, ukeketaji wa wanawake, pamoja na mila na desturi nyingine zenyenye kuleta madhara kwa wanawake, unyanyasaji usiosababishwa na mume na unyanyasaji unaohusiana na unyonyaji.
- b) Unyanyasaji wa kimwili, kingono na kisaikolojia ambao hutokea ndani ya jamii kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na ubakaji, udhalilishaji wa kijinsia, na vitisho kazini, shulen na penginepo, kuuza wanawake na ukahaba wa kulazimishwa.
- c) Unyanyasaji wa kimwili, kingono na kisaikolojia ufanywayo au kufumbiwa macho na serikali na asasi mbalimbali popote pale unapotokea.

Unyanyasaji wa kingono na kijinsia una misingi yake zaidi katika kutokuwepo na usawa katika mgawanyo wa madaraka. Mahusiano ya namna hii yanababisha na kueneleza unyanyasaji ndani ya jamii. Aidha, mahusiano hayo husababisha unyanyasaji ufumbiwe macho ndani ya familia, jamii na nchi kwa ujumla. Tofauti baina ya nyanja za umma na binafsi isiwe kisingizio cha kutoshughulikia unyanyasaji wa ndani kama aina ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Kuwatenga wanawake na wasichana katika nyanja za umma kunazidisha hatari ya wao kuathiriwa na vitendo vya unyanyasaji wa ndani ya familia.

“Unyanyasaji wa ndani ya nyumba” huchochea ubaguzi wa kijinsia na kufanya wanawake waendelee kutawaliwa na wanaume.

Rejea pia:

- **Ripoti ya Idadi ya Watu: Kukomesha Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake (Shule ya Afya kwa Umma ya Chuo Kikuu cha John Hopkins 1999).**
- **Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake: Tatizo la Kiafya lililofichika (Benki ya Dunia 1994).**

Fasili za Dhana Muhimu

Unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni zaidi ya ushambulizi wa kingono na ubakaji. Ili kuelewa chimbuko na madhara yake, ni vyema kuzifasili na kuzipambanua dhana za jinsia na jinsi.

Dhana ya **jinsi** inamaanisha sifa bainishi za kibayolojia za wanaume na wanawake. Sifa hizi bainishi ni za kuzaliwa nazo na tofauti zake zinaishia kwenye kazi za kimaumbile za uzazi.

Jinsia ni neno linalotumika kumaanisha sifa bainishi za kijamii zilizogawiwa wanaume na wanawake. Sifa hizi za kijamii zimejengwa kwenye misingi ya mambo tofauti kama umri, dini, utaifa, ukabila na tabaka la kijamii. Zinatofautiana katika sehemu mbili ndani ya utamaduni mmoja na baina ya tamaduni mbalimbali. Sifa hizi ndizo zinazofasili utambulisho, hadhi, majukumu, majukumu na mgawanyo wa kimadaraka baina ya wanajamii au wanatamaduni unaofanana. Jinsia hujifunzwa kuititia kuchangamana na wengine. Haiko tuli au si ya kuzaliwa nayo bali inakua polepole ili kukabiliana na mabadiliko katika mazingira ya kijamii, kisiasa na kitamaduni.

Jinsia hujifunzwa na kwa hiyo inabadilika.

Watu huzaliwa wanaume au wanawake (jinsi); wanajifunza jinsi ya kuwa wasichana na wavulana na baadaye wanakuwa wanawake na wanaume (jinsia). Jinsia inamaanisha maana ya kuwa mvulana au msichana, mwanamke au mwanaume katika jamii au utamaduni fulani. Jamii inafundisha misimamo, mitazamo, tabia, majukumu na shughuli zinazotazamiwa. Jinsia inaelezea majukumu, wajibu, vipingamizi, fursa na haki za wanaume na wanawake katika muktadha wowote. Tabia hii inayojifunzwa na mtu hujulikana kama **utambulisho wa kijinsia**.

Wanawake duniani kote daima wako katika nafasi finyu wakilinganishwa na wanaume kwa kiwango kilekile kijamii na kiuchumi. Majukumu ya kijinsia na utambulisho wa kijinsia daima hulusisha tofauti za fursa na kutolingana kimadaraka kati ya wanaume na wanawake. Unyanyasaji dhidi ya wanawake, na kukubalika kwake ndani ya jamii na tamaduni ni moja kati ya ishara za tofauti za fursa na kutolingana kimadaraka.

Njia sahihi ya kuzuia unyanyasaji na mpango wa ukabilianaji unaofaa lazima uzingatie nafasi na mahitaji ya watu wa jinsi zote zote: wanawake na wanaume, na namna ambavyo wote wanavyoweza kuwa mawakala wa mabadiliko. **Kulenga wanawake tu wakati wa kushughulikia unyanyasaji wa kingono na kijinsia kuna uelekeo wa kuwaachia waathiriwa/wanusurika jukumu la kuzuia na kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.**

Unyanyasaji ni nyenzo ya udhibiti na ukandamizaji ambayo inaweza kujumuisha uwezo wa kihisia, kijamii au kiuchumi, matumizi ya nguvu au shinikizo, na pia madhara ya kimwili. Nyenzo hii inaweza kuwa bayana, katika hali ya shambulio la kimwili au kumtishia mtu na silaha; inaweza ikawa si bayana, katika hali ya kitisho, vitisho, mateso, udanganyifu au aina zingine za mashinikizo ya kisaikolojia na kijamii. Mtu aliyelengwa na aina hii ya unyanyasaji anashurutishwa kutenda kadiri inavyotakiwa na mnyanyasaji au kutenda kinyume na matakwa yake kutokana na woga.

Tukio la unyanyasaji ni kitendo au mlolongo wa vitendo vyenye madhara vinayofanywa na mkosaji au kundi la wakosaji dhidi ya mtu au kundi la watu. Unaweza kujumuisha aina nyingi za unyanyasaji zenye kujirudiarudia kwa vipindi virefu, vyenye muda unaotofautiana. Inaweza kuwa kipindi cha dakika fulani, saa, siku au hata maisha.

Udhalilishaji ni matumizi mabaya ya madaraka ambayo yanamwezesha mkosaji kupata udhibiti au manufaa kutoka kwa mdhalilishwaji kwa kutumia au kusababisha madhara kimwili au kisaikolojia au uchocheaji wa hofu ya madhara hayo. Udhalilishaji unawazuia watu kufanya maamuzi huru na kuwalazimisha kutenda kinyume na matakwa yao.

Matumizi ya Nguvu ni kumshurutisha au kujaribu kumshurutisha mtu mwingine kuijingiza katika tabia fulani kinyume na matakwa yake kwa kutumia vitisho, usisitizaji wa kauli, ulaghai, uongo, matazamio kitamaduni au nguvu ya kiuchumi.

“[Unyanyasaji dhidi ya wanawake]...ni ishara ya kihistoria ya kutokuwepo na usawa wa mahusiano kimaisha kati ya wanawake na wanaume ambayo yamepelekea wanawake waendelee kutawaliwa na kubaguliwa na wanaume na kukwamisha maendeleo ya wanawake, na kwamba unyanyasaji dhidi ya wanawake ni moja kati ya mbinu nyeti ambazo zinatumwiwa kuwashuisha wanawake katika hali duni ikilinganishwa na wanaume”

Azimio la Umoja wa Mataifa la Utokomezwaji
wa Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake
23 Februari 1994

Mamlaka yanaeleweka kuwa uwezo wa kufanya maamuzi. Mahusiano yote yanaathiriwa na matumizi ya madaraka. Wakati madaraka yanapotumiwa kufanya maamuzi kuhusiana na maisha ya mtu binafsi, yanakuwa kama uthibitisho wa kujikubali na kujiheshimu ambako, hatimaye huendeleza heshima na kukubalika kwa wengine kama wenyewe usawa. Yakitumiwa kutawala, madaraka hulazimisha wajibu kwa wengine, hubana, hukataza, hudhibiti na hufanya maamuzi yanayohusu maisha ya watu wengine. Ili kuzuia na kukabiliana na matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa namna inayofaa, mahusiano ya kimadaraka kati ya wanaume na wanawake, wanawake na wanawake, wanaume na wanaume, wakubwa na watoto na baina ya watoto ni vyema yachanganuliwe na yaeleweke.

Katika migogoro ya kibinadamu, watu wanaoathiriwa wanategemea hifadhi na msaada wa asasi mbalimbali. Wafanyakazi, , maafisa wa serikali, wa vyombo vyta ulinzi na vyombo vyta sheria, wako katika fursa ya pekee kwa vile wana madaraka ya kutoa maamuzi ambayo yataathiri hali njema ya watu wanaowasaaidia. **Unyonyaji na udhalilishaji** hutokea iwapo tofauti ya madaraka itatumia vibaya bila kuwajali watu ambaa hawawezi kujadiliana au kufanya maamuzi kwa msingi wa usawa. Unyonyaji na udhalilishaji unaweza kuwa katika hali ya nguvu ya kimwili au kisaikolojia au nyenzo nyingine ya ushawishi wa nguvu (vitisho, motisha, udanganyifu au utozaji wa pesa kwa nguvu) kwa lengo la kupata fadhila ya ngono au fadhila zingine kwa kubadilishana na huduma zitolewazo.

Kwa kuzingatia makubaliano ya asasi, unyonyaji na udhalilishaji wa kingono ufanywao na wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu unawakilisha kushindwa kwa mashirika ya kibinadamu ambayo jukumu lao ni kutoa hifadhi na matunzo.

Kamati ya Kudumu ya Kiuhusiano Bainya ya Mashirika.
Mwongozo wa sera kuhusu uhifadhi dhidi ya unyonyaji
na udhalilishaji katika Migogoro ya Kibinadamu.
Rome Aprili 2002

Ridhaa ni pale ambapo mtu anafanya uchaguzi wa uhakika kukubali kwa hiari na bila kulazimishwa kufanya jambo fulani. Kifungu cha maneno kinyume na matakwa yake hutumiwa kuonyesha kutokuwepo kwa ridhaa. Hakuna ridhaa iwapo makubaliano yanapatikana kutokana na utumiaji wa vitisho, nguvu na njia zingine za kushawishi kwa nguvu, utoroshaji, utapeli, uongo au uwakilishaji mbaya.

Matumizi ya vitisho ili kujipatia manufaa, au ahadi ya kupata manufaa, au kupata ridhaa ya mtu ni matumizi mabaya ya madaraka vile vile. Makubaliano yanayofikiwa kwa njia hii hayahesabiki kama yana ridhaa. Hakuna ridhaa ikiwa mtu anayehusika yuko chini ya umri unakubalika kisheria wa kuridhia

au iwapo anafasilika kama mtoto ambaye sheria zinamhusu (tazama Sura ya 5).

Mhalifu ni mtu au kundi au asasi ambayo, moja kwa moja, huumiza husaidia au kuunga mkono, hufumbia macho unyanyasaji au udhalilishaji mwingine wowote dhidi ya mtu au kundi la watu. Wakosaji wako katika nafasi halisi au hali kudhaniwa ya madaraka, utoaji wa maamuzi na/au mamlaka na, kwa hiyo, wanaweza kuwadhibiti wale watu ambaeo ni waathiriwa wao.

Ni fikra potofu kuamini kwamba unyanyasaji wa kingono na kijinsia daima hufanywa na watu wageni. Ukweli ni kwamba, matukio mengi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia hufanywa na watu ambaeo wanafahamika kwa wanusurika na vitendo vyanamna hiyo, matukio mengi ya unyanyasaji huwa yamepangwa awali.

Unyanyasaji wa kijinsia unaweza vilevile kufanywa na wanafamilia na wanajamii. Serikali na asasi mbalimbali hufumbia macho na kufanya unyanyasaji wa kingono na kijinsia wakati vitendo vyakibaguzi vinapokuwa havipingwi na kukatazwa ikiwa ni pamoja na kupitia vyombo vyya sheria na sera. Wakati wa vita na migogoro, unyanyasaji wa kingono na kijinsia hufanywa mara nyingi na wapiganaji wa vikundi vinavyopigana.

Wahalifu wa unyanyasaji wa kijinsia na kingono mara nyingine ni watu wale wale ambaeo wanategemewa na wanusurikaji katika kuwasaidia na kuwalinda.

Idadi kubwa ya matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia huhusisha waathiriwa/mnusurikaji wa kike na mkosaji wa kiume. Vitendo vingi vyya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wavulana na wanaume vilevile hufanywa na wakosaji wa kiume.

Wandani (waume na wapenzi wa kiume): Katika jamii nyingi, jukumu la kijinsia la mwanaume linalokubalika kwa wandani ni lile la kutoa maamuzi na madaraka juu ya mwandani wa kike. Kwa bahati mbaya madaraka haya na uwezo huu mara kwa mara hutumiwa kiubaguzi, kiunyanyasaji na kiudhalilishaji.

Wanafamilia, ndugu wa karibu na marafiki: Wasichana wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuathiriwa na vitendo vyaa unyanyasaji wa kingono na kijinsia katika mazingira ya kifamilia. Kuathiriwa kwao kunaanzia katika hali ya kutojaliwa hadi kujamiihana na ndugu wa karibu; vitendo ambavyo ni ukiukwaji wa haki za binadamu lakini haviripotiwi mahala panapotakiwa kama vile kwa polisi au mjumbe kwa kuwa vinawahuisha baba wazazi, baba wa kambo, mababu, kaka watu na/au wajomba kama wakosaji. Mila na desturi zenye madhara vilevile hufanywa tena kwa uelewa mzuri tu, na mara nyingine kwa wanafamilia na marafiki na jamaa wa karibu kushiriki.

Wanajamii mashuhuri (walimu, viongozi, wanasiasa): Viongozi na wanajamii wengine walio katika ngazi ya madaraka wanaweza

kutumia madaraka yao vibaya kwa kupitia vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Mwathiriwa/aliyenusurika katika mazingira haya huwa hayuko tayari kuripoti unyanyasaji wa namna hii kwa vile mkosaji yuko kwenye wadhifa wa kuaminiwa, na wenyе madaraka kwenye jumuiya.

Vikosi vya usalama na wanajeshi, wakiwemo walinzi wa Amani: Wanajeshi aghalabu huwa ndiyo wenyе mamlaka ya juu kabisa. Daima huwa wana silaha na wana madaraka ya kuhakikisha kwamba kuna usalama katika jumuiya. Katika mazingira fulanifulani, wanajeshi wanaweza kuweka na kwa hakika huweka watu kizuzini na/au kushika watu bila ya wao kutoadhibiwa. Mara nyingi wanajeshi na vyombo vya usalama viko katika nafasi ya kuidhinisha au kutoidhinisha haki na heshima wanazostahili wakimbizi. Wakati wa kuvuka mipaka, vituo vya ukaguzi, na wakati wa kuomba bidhaa na huduma kutoka kwa wanajeshi kunaongeza uwezekano wa wakimbizi kunyanyaswa kingono na kijinsia, hasa kwa wakimbizi wanawake.

Wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu: Wafanyakazi wa Kimataifa, Kitaifa na wale wanaofanya kazi katika mashirika ya misaada ya kibinadamu, yakiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Wizara za Serikali wenyеji, wana nafasi za madaraka makubwa katika mazingira ya wakimbizi. Jamii huwachukulia kwamba wana pesa, ushawishi na madaraka. Kwa bahati mbaya, kumekuwa na matukio kadha wa kadha ambapo wafanyakazi wamekuwa wakitumia vibaya madaraka haya na wamekuwa wakifanya vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Ni muhimu wafanyakazi wote wa mashirika ya misaada ya kibinadamu wakapata mafunzo na ufahamu juu ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia na kwamba wawajibishwe pale wanapoonyesha mwenendo usiofaa. (Tazama kiambatanisho 1 kuhusu Muongozo wa Maadili ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi. (mwaka 2002).)

Asasi: Mienendo ya kibaguzi wakati wa kutoa huduma za kijamii inasaidia kudumisha na kuongeza tofauti za kijinsia. Uzuiaji wa habari, kuchelewesha au kutotoa misaada ya huduma za afya, kutoa mishahara isiyolingana kwa kazi ileile na uzuiaji wa haki ni aina za unyanyasaji zinavyofanyika kupitia asasi.

Rejea pia

- **Makala ya Sera ya Kamati ya Kudumu ya mahusiano ya kishirika kuhusu Hifadhi dhidi ya Unyonyaji na Udhaliilishaji wa Kingono wakati wa Migogoro ya kibinadamu (2002).**
- **Mwongozo wa Maadili ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi.**

Aina za Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia

Jedwali lifuatalo linaelezea aina zinazojitokeza mara nyingi za unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Orodha hii si kamilifu na wala si ya pekee. Ni kifaa ambacho kinaweza kutumika katika kila sehemu kusaidia kutambua aina mbalimbali zilizopo za unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia vimegawanywa katika makundi matano:

- ◎ Unyanyasaji wa kingono.
- ◎ Unyanyasaji wa kimwili.
- ◎ Unyanyasaji wa kihisia na kisaikolojia.
- ◎ Mila na desturi zenye kuleta madhara.
- ◎ Unyanyasaji wa kijamii na kiuchumi.

Unyanyasaji wa Kingono

Aina ya kitendo	Maelezo/Mifano	Linawezwa kutendwa na
Ubakaji na ubakaji katika ndoa.	Uvamizi wa sehemu yoyote ya mwili wa mwathiriwa au wa mkosaji kwa kutumia kiungo cha kujamiiana, au uvamizi wa tundu la mkundu au mlango wa uzazi wa mwathiriwa kwa kutumia kifaa chochote au kiungo cha mwili kwa nguvu, tishio la kutumia nguvu, mabavu, kujinufaisha na hali ya kimabavu au dhidi ya mtu ambaye hawezi kutoa ridhaa ya kweli (Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai)	Mtu yeyote mwenye madaraka, mamlaka na udhibiti, ikiwa ni pamoja na mume, mwandani au mtoa huduma.
Kosa la kumwingilia kimwili mtoto; unajisi na kujamiiana kwa ndugu wa karibu.	Kitendo chochote ambapo mtoto anatumia kukidhi haja ya ngono. Mahusiano yoyote ya kingono yanayomhusisha mtoto/ maingiliano yoyote ya kimwili yanahusisha mtoto.	Mtu yeyote anayeaminiwa na mtoto, akiwemo mzazi, umbu, ndugu wa ukoo, rafiki au mgeni, mwalimu, mzee, kiongozi au mtoa huduma yeyote mwenye madaraka, mamlaka au udhibiti wa mtoto.
Kulawiti kwa kulazimisha/ ubakaji kinyume na maumbile	Kumwingilia mtu kinyume na maumbile kwa kulazimisha, ambako aghalabu huwa kati ya mwanaume na mwanaume au mwanaume na mwanamke.	Mtu yeyote mwenye madaraka, mamlaka na utawala.
Jaribio la kubaka au jaribio la kulawiti/ ubakaji kinyume na maumbile	Jaribio la kujamiiana kwa nguvu; bila kuingiliana.	Mtu yeyote mwenye madaraka, mamlaka na utawala.
Udhgilishaji wa kingono	Kumvamia mtu au jaribio la kumwingilia kimwili la asili ya kingono, ikiwa ni pamoja na kumgusa mtu kinyume na matakwa yake, kwa kutumia nguvu au katika hali isiyokuwa ya usawa au hali ya kimabavu.	Mtu yeyote mwenye madaraka, mamlaka na utawala, wanafamilia / wanajumuiya, wafanyakazi wenza, wakiwemo wasimamizi, wageni n.k.

Unyonyaji wa kijinsi	Udhalilishaji wowote unaoambatana na hali ya udhaifu wa mtu, utofauti wa madaraka au dhamana kwa, lengo la kujinufaisha kingono ; udhalilishaji huu hujumuisha kuneemeka kwa muda, kijamii au kisiasa kwa kumyonya mwagine kijinsi; Unyonyaji kingono ni moja ya malengo ya biashara ya kuuza watu (kutumikishwa kingono , kushurutishwa kuvua nguo na/au hali ya kuwa uchi, kulazimishwa kuolewa, uzazi wa shurti, ushiriki katika picha za uchi, au ukahaba, kutumikishwa kingono kwa lengo la kupatiwa bidhaa, huduma, misaada, utumwa wa ngono).	Hutendwa na mtu yeyote mwenye madaraka, umaarufu na utawala, wafanyakazi wa mashirika ya misaada ya kibinadamu, wanajeshi/maafisa katika vituo vya ukaguzi, walimu, wafanya magendo, mitandao ya biashara ya watu na bidhaa haramu.	Sura ya 1
Ukahaba wa kulazimishwa (vile vile huitwa unyonyaji wa kijinsi)	Biashara ya kulazimishwa ya ngono kwa kubadilishana na rasimali, huduma na msada aghalabu ikilenga wanawake na wasichana walio hatarini sana kuathiriwa ambao hawawezi kujikimu na/au kuwakimu watoto wao.	Mtu yeyote aliyekuwa katika nafasi nzuri, mwenye pesa au mmiliki wa rasimali na huduma anayedhaniwa kwamba ni mwenye madaraka, mfanyakazi ya shirika la misaada ya kibinadamu.	Sura ya 2
Udhalilishaji kingono	Utongozaji wa kulazimisha unaorudiwarudiwa, ushawishi wa kingono wa, kulazimisha, ombi la kujamiihana au kupata fadhila za ngono, mafumbo ya ngono na maneno mengine au tabia ya kimwili inayoashiria tendo la ngono, kuonyesha picha/vitu vya ngono, hali hii ikiingiliana na kazi, ikifanywa kuwa sharti la kupata kazi au kuunda mazingira ya vitisho, uadui au chuki kikazi.	Waajiri, wasimamizi au wenzi, mtu yeyote mwenye madaraka, mamlaka au utawala.	Sura ya 3
Unyanyasaji wa kingono kama silaha ya vita na utesaji	Uhalifu dhidi ya ubinadamu wenyewe asili ya jinsi, ikiwa ni pamoja na ubakaji, utumwa wa ngono, utocaji mimba wa kulazimishwa, au kuhasiwa au namna yoyote ile inayozuia uzazi, ujauzito wa kulazimishwa, uzazi wa kulazimishwa, na kutunza watoto kwa kulazimishwa, kati ya mengine mengi. Unyanyasaji wa kingono kama aina ya utesaji hufasiliwa kuwa ni tendo lolote au tishio la kingono ambalo linalleta maumivu makali kiakili au kimwili au maumivu yanatumwiwa kwa lengo la kupata habari, kukiri au adhabu kutoka kwa mwathiriwa au mtu mwagine, kuumuogofya yeye au mtu mwagine au kumdhaliisha, kwa ujumla au sehemu, kundi la kitaifa, kikabila, kimbari, kijamii au kidini .	Mara nyingi hufanywa, kuidhinishwa na kuamriwa na jeshi, polisi, vikundi vyenye silaha au vikundi vingine vyenye migogoro.	Sura ya 4

Unyanyasaji kimwili

Aina ya Tendo	Maelezo / mifano	Linaweza kutendwa na
Ushambuliaji kimwili	Kupiga, kupiga ngumi, kupiga mateke, kuuma, kuchoma kwa moto, kulemaza au kuua kwa kutumia silaha au bila kutumia silaha; aghalabu kunakotumiwa pamoja na aina zingine za unyanyasaji wa kingono na kijinsia.	Mume /mke, wanafamilia, rafiki, mwandani, mgeni, mtu yoyote mwenye madaraka au washiriki katika ugomvi
Utoroshaji wa watu	Kuuza na/au kufanya biashara ya watu kwa lengo la shughuli za ngono za shurti, kazi za shurti, au huduma za shurti, utumwa au shughuli zilizo sawa na utumwa, utwana au uondolewaji wa viungo vya mwili.	Mtu ye yeyote mwenye madaraka na utawala.

Unyanyasaji Kihisia na Kisaikolojia

Aina ya Tendo	Maelezo / mifano	Linaweza kutendwa na
Udhaliishaji/Uonevu	Udhaliishaji wowote wa maneno usiokuwa wa kingono, yaani matusi, fedheha, kushushiwa hadhi, kudharauliwa; unaomshurutisha mwathiriwa/aliyenusurika kuijingiza katika vitendo vya kudhalilisha, iwe hadharani au faraghani; kumnyima matumizi ya msingi ya kuiwezesha familia.	Mtu ye yeyote mwenye madaraka na utawala; aghalabu udhaliishaji huu hufanywa na wake au waume wandani au wanafamilia wenye nyadhifa za mamlaka.
Kifungo	Kumtenga mtu na marafiki/familia, kumwekea mipaka ya nyendo zake, kumnyima uhuru au kuzuia/kuwekea mipaka uhuru wake wa kutembea.	Mtu ye yeyote mwenye madaraka na utawala; aghalabu unyanyasaji huu hufanywa na wake au waume, wandani, au wanafamilia walio katika nyadhifa za mamlaka.

Mila na Desturi zenyе Madhara

Aina ya Tendo	Maelezo / mifano	Linaweza kutendwa na
Ukeketaji	Kukata sehemu za siri kwa sababu zisizo za kitabibu, ambako aghalabu hufanywa wakati wa umri mdogo; kuanzia kukata kiasi kidogo cha sehemuzasirihadiukatajiwasehemu zote za siri, kushona iwe kwa sababu za kitamaduni au sababu zingine zisizo za kitiba; aghalabu kitendo hiki hupitiwa kwa mara nyingi wakati wa uhai wa mwathiriwa, yaani baada ya uzazi au ikiwa msichana/mwanamke amekuwa mwathiriwa wa shambulio la kingono .	Wanajadi, wakiungwa mkono, kufumbiwa macho na kusaidiwa na familia, makundi ya kidini, jamii nzima na baadhi ya nchi.
Ndoa katika umri mdogo	Ndoa zinazopangwa chini ya umri unaotambulika kisheria (kujamiina katika mahusiano ya aina hiyo ni kosa la kumwingilia kimwili msichana chini ya umri unaotambulika kisheria, kwa vile wasichana katika umri huo, kisheria, hawajawa na uwezo wa kukubaliana na mahusiano ya namna hii).	Wazazi, jumuiya na serikali.
Ndoa za kulazimishwa	Ndoa inayopangwa kinyume na matakwa ya mwathiriwa/aliyenusrika; mara nyingi mahari hulipwa kwa familia husika; wakati inapokataliwa, hutokea matumizi ya nguvu na/au udhalilishaji.	Mzazi, wanafamilia.
Mauaji au kulemaza kwa nia ya kulinda Heshima.	Kumlemaza au kumuua mwanamke au msichana kwa kudhamiria kama adhabu kwa kulipiza vitendo ambavyo vinachukuliwa kama havifai kutendwa na jinsia ya mwanamke na ambavyo vinasadikiwa kuleta aibu kwa familia au jamii (kwa mfano, kumwagia tindikali kwenye uso wa mwanamke kama adhabu kwa kuiletea aibu familia kwa kujaribu kuolewa na mtu mwingine ambaye hakuchaguliwa na familia), au kulinda heshima ya familia (yaani kama wokovu dhidi ya kosa lililofanywa na wanafamilia wa kiume)	Mzazi, mume, wanafamilia wengine au wanajamii.


Mauaji ya watoto wachanga na/au kuwatelekeza	Kuwaua, kuwanyima chakula, na/ au kuwatelekeza watoto wa kike kwa sababu wanafikiriwa kuwa na thamani ndogo katika jamii kuliko watoto wa kiume.	Mzazi, wanafamilia wengine.
Unyimwaji Elimu kwa wasichana na wanawake	Kuondoa wasichana kutoka shulen, kupiga marufuku au kuzuia njia ya kufikia elimu ya msingi, kiufundi, kitaalam au kisayansi kwa wasichana na wanawake.	Wazazi, wanafamilia wengine, jumuia, serikali fulani.

Unyanyasaji wa kijamii na kiuchumi

Aina ya tendo	Maelezo/Mifano	Linaweza kufanywa na
Ubaguzi/Unyimaji wa fursa, huduma	Kumtenga mtu, kumnyima elimu, huduma za kiafya au ajira yenye kipato kizuri; kumnyima haki zake za kumiliki mali.	Wanafamilia, jamii, asasi na mashirika mbalimbali, watendaji wa serikali.
Kutengwa na jamii/ utengwaji wenyewe misingi ya kijinsi.	Kumhini mtu huduma, misaada na kufurahia haki za kiraia, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa, uwekaji wa adhabu kwa wahalifu, desturi za kiubaguzi au madhara ya kimwili au kisaikolojia pamoja na kufumbia macho ubaguzi, ushoga na usagaji, ubadilishaji wa viungo vya uzazi.	Wanafamilia, jamii, asasi na mashirika mbalimbali, watendaji wa serikali.
Matumizi ya sheria pingamizi	Kumhini mtu, hasa mwanamke, huduma, misaada na kufurahia haki za kiraia, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa	Familia, jumuiya, asasi mbalimbali na serikali

Lini na Wapi ambapo Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia Hutokea?

Unyanyasaji wa kingono na kijinsia unaweza kutokea popote, wakati wowote. Unatumika kama silaha ya vita, unafanyika katika mazingira yanayodhaniwa kuwa ni salama, nyumbani kwa mtu. Kama vile sheria na miundo inayotawala jamii inavyoathiri tabia ya kila mtu, vilevile mitazamo ya kila mtu inaweza kuathiri jinsi familia, jamii, na jumuuya zinavyopokea aina fulani za tabia. Mchoro ufuatao unaonyesha muunganiko bayana uliopo baina ya mtu na jamii.



Katika ngazi ya mtu binafsi, kiwango cha ufahamu, usalama binafsi, kupata na kumiliki rasilmali, huduma na mafao ya kijamii, historia binafsi na mitazamo ya kijinsia huweza kuathiri kama mtu atakuwa mwathiriwa /aliyenurusika au mkosaji wa vitendo vyatya unyanyasaji.

Ngazi ya pili, yaani mahusiano, inaonyesha muktadha wa karibu ambamo udhalilishaji unaweza kutokea; baina ya watu binafsi, au hata ndani ya familia. Katika ngazi hii, madaraka yaliyopo yasiyozingatia usawa mionganoni mwa watu huanza kuimarishe hali za watu kujineemesha na wengine kudunishwa.

Ngazi ya jumuuya inaonyesha mabadiliko mionganoni mwa wanajumuuya, ambayo yanaathiriwa na mahusiano yaliyopo ndani ya miundo kama shule, asasi za afya: hospitali na zahanati, makundi-rika na mahusiano kazini. Kwa wakimbizi, muundo wa jumuuya unapatikana katika kambi au mandhari za wakimbizi ambamo upatikanaji na uingilikaji wa huduma za kijamii na vile kambi zilivyokaa huweza kuwa na athari ya moja kwa moja katika utokeaji wa vitendo vyatya unyanyasaji wa kingono na kijinsia au la.

Jamii hujumuisha mila na desturi za kijamii na kiutamaduni kuhusu majukumu ya kijinsia, mitazamo kuhusiana na watoto, wanawake na wanaume, miundo ya kisheria na kisiasa inayotawala mienendo ya jamii husika, pamoja na mitazamo kuhusu utumiaji wa nguvu kama njia ya utatuzi wa migogoro.

Ni dhihiri kuona kwamba mabadiliko ya tabia na mitazamo katika maeneo yoyote yanaweza kuwa na athari kwa maeneo yote hayo.ukabilianaji ili kuzuia au kukabiliana na vitendo vyatya unyanyasaji wa kingono na kijinsia lazima ulenge ngazi zote.

Unyanyasaji wa kingono na kijinsia unatokea kwa watu wa matabaka yote, tamaduni zote, dini zote, mataifa yote, mbari yoyote, jinsia na umri wowote.

Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia wakati wa Ukimbizi

Wakati wa mapigano, miundo ya kijamii huharibiwa. Wanawake na watoto hukabiliwa na hatari za nyongeza za kuathiriwa na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia wakati wa kukimbia mapigano na kutafuta hifadhi sehemu nyingine. Wanafamilia huwa wanatawanyika wakati wa kukimbia, wakiwaacha watoto wakiwa wametenganishwa na kundi lingine lilosalia la familia zao na wanawake ndio wanabaki kuwa wenyewe jukumu pekee la kulinda na kutunza kaya zao. Chati ifuatayo, ambayo imechukuliwa kutoka jedwali lililoandaliwa na S. Purdin, inaelezea aina za unyanyasaji zinazoweza kutokea wakati wa awamu mbalimbali za mzunguko wa kikimbizi.

Awamu	Aina ya Unyanyasaji
Wakati wa mapigano, kabla ya kukimbia	Kudhalilishwa na watu wenyewe madaraka, ubadilishanaji wa wanawake kingono, kuvamiwa na watu wenyewe nia ya kukidhi haja za kingono, ubakaji, utoroshaji wa watu unaofanywa na vikundi vinayopigana, yakiwemo majeshi ya usalama, ubakaji kimakundi, na ujauzito wa shurti.
Wakati wa kukimbia	Kuvamiwa na majangili, walini wa mipakani kwa lengo la kukidhi haja zao za kingono; kutekwa na walanguzi, wafanyabiashara ya utumwa.
Katika Nchi ya Hifadhi.	Kuvamiwa na wenyewe madaraka, matumizi ya nguvu, kwa lengo la kukidhi haja za kingono; kudhalilishwa kingono kwa watoto walioko kwenye matunzo ya walezi, udhalilishaji ndani ya nyumba, udhalilishaji wa kingono wakati wa kuwa katika kambi za muda, wakati wa kutafuta kuni, maji na kadhalika; ngono kwa ajili ya kulinda uhai/ukahaba wa kulazimishwa, unyonyaji wa kingono wa watu wanaotafuta hadhi ya kisheria katika nchi ya hifadhi au kupata msaada na rasilmali; kuanzishwa upya kwa mila zenyeye madhara.
Wakati wa kurejea nyumbani	Udhalilishaji wa kingono wa wanawake na watoto waliojitenga na familia zao; udhalilishaji wa kingono unaofanywa na watu wenyewe madaraka; kuvamiwa, kubakwa na majangili, walini wa mipakani, kwa nia ya kukidhi haja ya kingono; urejeshwaji wa kulazimishwa au kutumia mabavu.
Wakati wa kuanza maisha upya baada ya kurejea	Udhalilishaji wa kingono dhidi ya watu warudio makwao kama namna ya kulipiza kisasi; fadhila ya ngono ili kuhalalisha hadhi ya kisheria; kutengwa katika mchakato wa ufanyaji maamuzi, kuhiniwa au kukwazwa katika kupata rasilmali, haki ya kuandikishwa na haki ya kurudishiwa au kumiliki mali

Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia wakati wa Uhai

Jedwali lifuatalo, liliandoandaliwa na L. Heise, linaleza namna za unyanyasaji ambao wanawake wanaweza kutendewa wakati wa vipindi mbalimbali vya maisha yao.

Awamu	Aina ya Unyanyasaji uliopo
Kabla ya kuzaliwa	Utoaji mimba kwa kuchagua jinsia, kupigwa kwa mwanamke wakati wa ujauzito, ujauzito wa shurti.
Utotoni	Kuua watoto wa kike, unyanyasaji wa kihisia na kimwili; tofauti za njia za kupata chakula na matunzo ya kiafya.
Usichanani	Ndoa katika umri mdogo; ukeketaji, udhalilishwaji kingono na wanafamilia na wageni; njia za kitabaka za kupata chakula, matunzo ya kiafya na elimu.
Balehe	Unyanyasaji wakatiwa uchumbiaji, ngono ya kulazimishwa na nguvu za kiuchumi (kwa mfano kwa ajili ya karo ya shule); udhalilishwaji wa kingono mahali pa kazi; ubakaji; unyanyasaji kijinsia, ndoa za kupangwa; kuuzwa.
Umri wa kuzaa watoto	Unyanyaswaji kimwili, kisaikoloja na udhalilishwaji unaofanywa na wandani wa kiume na ndugu; kubeba mimba kwa kushurutishwa na mwenzi, udhalilishwaji wa kingono mahali pa kazi, unyanyasaji kijinsia, ubakaji, unyanyasaji wajane, ikiwa ni pamoja na kunyang'anya mali; na mila potofu za kujitakasa kijinsi.
Uzee	Unyanyasaji wajane, ikiwa ni pamoja na kunyang'anya mali, tuhuma za uchawi; unyanyasaji kimwili na kisaikoloja unaofanywa na wanafamilia vijana; utofauti wa njia za kujipatia chakula na huduma za kiafya.

Sababu na Madhara Yatokanayo na Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia.

Kupanga mipango inayofaa ya kuzuia na kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, ni muhimu kuchanganua sababu na madhara ya unyanyasaji wa namna hiyo kila unavyotokea. Kuelewa sababu za unyanyasaji wa kingono na kijinsia kutakusaidia kubuni njia sahihi za kuuzuia; kuelewa madhara ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia kutakuwezesha kuandaa ukabilianaji unaofaa kuhusiana na waathiriwa/wanusurika na vitendo vya unyanyasaji.

ABABU -- Shughuli za Uzuiaji
MATOKEO -- Shughuli za Ukabilianaji

Sababu za Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia

Chimbuko la unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni mtazamo wa jamii kuhusu mila za ubaguzi wa kijinsia zinazomweka mwanamke katika nafasi ya kuwa chini ya mwanaume. Kukosekana kwa thamani ya mwanamke kijamii na kiuchumi pamoja na kwa kazi za mwanamke na kukubali majukumu ya kijinsia kunaochochea na kuendeleza mawazo ya kwamba mwanaume ana nguvu za kufanya maamuzi na kumtawala mwanamke. Kupitia vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, iwe ni kwa mtu mmoja mmoja au kikundi cha watu, wakosaji hutafuta kuendeleza nafasi za kujineemesha, madaraka na kutawala wengine.

Majukumu na utambulisho wa kijinsia hutegemeana na jinsi, umri, hali ya kiuchumi na kijamii, makabila, utaifa na dini. Mahusiano kati ya mwanamke na mwanaume, mwanamke na mwanamke, mwanaume na mwanaume hutambulishwa pia kwa ngazi mbalimbali za mamlaka na madaraka ambazo zinadumisha nafasi za wanaume kujineemesha na kuwadunisha wanajamii wengine. Kutojali ukosefu wa uelewa wa haki za binadamu, usawa wa kijinsia, demokrasia na njia zisizokuwa za kiunyanyasaji za kutatua matatizo kunasaidia kuziendeleza tofauti hizo za kijinsia.

Sababu Zinazochangia Hatari

Wakati ambapo tofauti na ubaguzi wa kijinsia umekuwa chimbuko la sababu za unyanyasaji wa kingono na kijinsia, sababu nydingine pia zinasaidia kuukilia aina na kiwango cha unyanyasaji katika kila tukio. Ni muhimu kuzielewa hizi sababu ili kuweza kubuni mikakati inayofaa ya kuzuia na kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Usawa wa kupata na kumiliki mali, manufaa yatokanayo na misaada pamoja na ushirikishwaji wa wanawake katika mchakato wa kufanya maamuzi ni lazima uzingatiwe katika nyanja zote, ukiwa dhahiri unalenga unyanyasaji wa kingono na kijinsia au ni mwitikio wa mahitaji ya dharura, au ya uokoaji wa maendeleo ya watu

Chati ifuatayo inaelezea sababu au mambo ya hatari yanayoweza kuongeza hatari za mtu kuwa mwathiriwa/aliyenurusika au mkosaji wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Sababu au Mambo Hatari Kuhusiana na Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia

Hatari kwa mtu Mmoja mmoja	<ul style="list-style-type: none"> • Upotevu wa usalama • Utogemezi • Ulemavu wa kimwili na kiakili • Ukosekanaji wa mbadala wa kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii • Ulevi/utumiaji wa dawa za kulevyia • Kihoro na kukata tama kisaikolojia kutokana na migogoro, ukimbizi, kupoteza makazi • Mparaganyiko wa majukumu ndani ya familia na jumuiya kwa ujumla • Ujinga/ukosefu wa uelewa wa haki za mtu binafsi zilizomo katika sheria za nchi na za kimataifa
Mila na desturi za kijamii na kitamaduni	<ul style="list-style-type: none"> • Imani za kibaguzi za kimila na kitamaduni. • Imani za dini.
Mhimili wa kisheria na utekelezaji wake katika Nchi wenyewe au nchi ya asili	<ul style="list-style-type: none"> • Ubaguzi na ufumbiaji macho unyanyasaji wa kingono na kijinsia • Ukosekanaji wa ulinzi wa kisheria wa haki za wanawake na watoto • Ukosekanaji wa sheria dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia • Ukosekanaji wa imani kwenye mamlaka za utekelezaji wa sheria. • Matumizi ya sheria za jadi, mila na desturi zinazochochea ubaguzi wa kijinsia. • Ukosekanaji wa mwamko kwa ujumla pamoja na kampeni za utetezi zenye kulaani na kukataa unyanyasaji wa kingono na kijinsia. • Mienendo ya kibaguzi katika usimamizi wa haki na utekelezaji wa sheria. • Kuripotiwa kwa uchache kwa matukio ya unyanyasaji pamoja na kukosekana imani katika usimamizi wa haki. • Kukosekana msukumo au utayari wa kuendesha mashitaka kwenye mamlaka zinazohusika juu ya matukio yote yanayoripotiwa. • Idadi ndogo ya mashitaka yanaokuwepo ikilinganishwa na matukio yanayoripotiwa • Polisi na mahakama kutofikika kutokana na kuwa mbali na kambi. • Kukosekana kwa watekelezaji wa sheria wanawake • Kukosekana kwa raslimali na vitendea kazi katika mahakama za ndani pamoja na vyombo vya ulinzi. • Sheria au taratibu katika usimamizi wa haki zinazounga mkono jinsia
Vita na migogoro ya kutumia silaha	<ul style="list-style-type: none"> • Kusambaratika kwa mifumo ya jamii. • Matumizi ya madaraka ya kisiasa na udhibiti dhidi ya jumuiya nyingine. • Tofauti za kikabilia • Ubaguzi wa kijamii na kiuchumi.

Haliza wakimbizi, watu warudio makwao na waliopoteza makazi	<ul style="list-style-type: none">• Kuanguka kwa mihimili ya kifamilia na ya kijamii.• Eneo la kijiografia na mazingira ya karibu {eneo ambamo uhalifu huwa wa kiwango cha juu}• Muundo na mfumo wa kijamii wa kambi (Msongamano wa watu/makazi ya kaya nyingi/hifadhi ya jumuia)• Muundo wa miundo mbinu ya huduma.• Uongozi wa kiume kutawala katika makambi hali inayopelekea kutojali jinsia wakati wa kufanya maamuzi• Kutopatikanakwachakula, mafuta, kazizakujingiziakipato, hali inayopelekea kuyahama maeneo yaliyojtenga.• Ukosefu wa ulinzi wa Polisi.• Kukosekana kwa uwepo wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi/ Asasi Zisizo za Kiserikali kambini• Ukosefu wa doria za ulinzi• Ukosekanaji wa usajili wa watu na utoaji wa vitambulisho.• Uhasama wa wenyejji {wakimbizi wanadhaniwa kuwa wananufaika sana kwa kupata mali nyingi)
--	--

Madhara Yatokanayo na Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia

Waathiriwa/wanusurika na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia wako katika hatari kubwa ya matatizo ya kiafya na kisaikolojia na kijamii na pengine vifo hata bila ya kuwepo shambulio la kuumiza kimwili. Uwezekano wa kudhoofishwa kihisia kwa muda mrefu na kuleta hali ya kihoro usipuuzwe kamwe.

Kuelewa madhara ya yanayoweza kutohana na unyanyasaji wa kingono na jinsia kutawasaidia watendaji kubuni mikakati inayofaa ya ukabilianaji na kuzuia madhara zaidi.

Mchanganuo wa madhara unatumiwa katika ufupishoo ufuataao.

Afyä

Kuna matokeo mabaya ya kiafya na yanayotishia maisha katika aina zote za unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Matokeo yanayoweza kusababisha kifo

- Mauaji ya binadamu
- Kujiuu
- Vifo vya uzazi.
- Vifo vya watoto wachanga.
- Vifo vinavyohusiana na UKIMWI

Matokeo Yasiyoweza kusababisha kifo

Madhara makubwa mwilini	Madhara sugu	Uzazi
<ul style="list-style-type: none"> • Kuumia • Mshtuko • Maradhi • Maambukizo 	<ul style="list-style-type: none"> • Ulemavu • Maumivu ya maungo • Maambukizi sugu • Maumivu sugu • Ulevi/utumiaji wa dawa za kulevyu • Kuchafuka tumbo • Matatizo ya kulala • Matatizo ya kula 	<ul style="list-style-type: none"> • Mimba kuharibika • Mimba zisizotakiwa • Utoaji mimba usio salama • Maambukizo yatokanayo na ngono ikiwa ni pamoja na VVU/UKIMWI • Matatizo ya hedhi • Matatizo ya mimba • Matatizo ya akinamama • Hitilafu za kijinsia

Matokeo ya Kisaikolojia/Kijamii

Madhara ya kihisia & kisaikolojia	Madhara ya kijamii
<ul style="list-style-type: none"> • Mfadhaiko wa utokanao na kihoro • Masononeko • Wasiwasi, hofu • Hasira • Aibu/kutojiamini/ kujichukia/ kujilaumu • Maradhi ya akili • Tabia, mawazo ya kuijua 	<ul style="list-style-type: none"> • Kumlaumu mwathiriwa/ aliyenurusika • Kupotea kwa majukumu katika jamii (mf.kuingiza kipato, malezi ya watoto) • Unyanyapaa • Kukataliwa na jamii • Njaa itokanayo na ufukara • Ongezeko la tofauti za kijinsia

- ◎ Jamii nyingi zina mazoea ya kuwalaumu waathiriwa/ wanusurika.Kukataliwanajamiikwanamnahiihuwasababishia mvurugiko wa kihisia, ikiwa ni pamoja na aibu, kujichukia na masononeko.
- ◎ Kutokana na hofu ya kunyanyapaliwa na jamii, waathiriwa/ wanusurika wengi hawaripoti matukio wanayokumbana nayo. Ama kwa hakika, matukio mengi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia huwa hayaripotiwi.

Sheria/Haki

- ◎ Kama sheria za nchi hazitoi ulinzi wa kutosha dhidi ya unyanyasaji wa kingono na jinsia, au kama taratibu katika tawala za kisheria na vyombo vyta kisheria kuna ubaguzi, aina hii ya unyanyasaji unaweza kufanywa na ukafumbiwa macho.
- ◎ Mitazamo ya baadhi ya wanajamii kumlaumu mtu mwathiriwa au aliyenusurika mara nyingi hujibainisha mahakamani. Kesi nyingine za unyanyasaji wa kingono na kijinsia hufutwa au mhalifu hupewa adhabu nyepesi kwa sababu ya mitazamo kama hiyo. Katika nchi nyingine adhabu anayopewa mhalifu huwa ni ukiukwaji mwingine wa haki za mwathiriwa/aliyenusurika pamoja na uhuru wake, kwa mfano pale mtu anapolazimishwa kuolewa na mhalifu. Hii humvuruga mwathiriwa/aliyenusurika kihisia kwa kuona kwamba mhalifu hana makosa.

Usalama

- ◎ Mwathiriwa /aliyenusurika hana ulinzi, ana hofu, mwoga, si salama na yuko kwenye hatari tena ya kufanyiwa fujo.
- ◎ Katika kushughulikia maswala ya usafirishaji wa watu, askari na walini wanakuwa katika hatari ya kulipiziwa kisasi.
- ◎ Ikiwa askari na walini hawatakuwa makini na mahitaji ya uangalizi wa haraka wa utu na heshima ya waathiriwa/wanusurika, madhara zaidi na kihoro vinaweza kutokea kutokana na ucheleshwaji msaada na tabia za kutojali.

Mambo Muhimu ya Kukumbuka

- ◎ Unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni ukiukaji wa haki za binaadamu. Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhuduma Wakimbizi na nchi husika hushirikiana katika jukumu la kuhakikisha kuwa wakimbizi na watu wengine waliooteza makazi wanalindwa. Hivyo, kuzuia na kukabiliana na vitendo vyta unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya wakimbizi ndio sehemu mojawapo ya mkakati mzima wa kuwalinda wakimbizi.
- ◎ Wanawake na watoto ndio wafanyao asilimia kubwa ya waathiriwa/wanusurika kutokana na vitendo vyta unyanyasaji wa kingono na kijinsia, ingawa watoto wa kiume na wanaume wanaweza pia kuwa waathiriwa/wanusurika.
- ◎ Jinsia inamaanisha ni nini hasa huchukuliwa kwa mtu kuwa mvulana au msichana, mwanamke au mwanaume, katika jamii fulani au utamaduni fulani.
- ◎ Matukio mengi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia hufanywa na watu ambao wanafahamika kwa waathiriwa/wanusurika.

- ◎ Njia sahihi ya kuzuia unyanyasaji na mpango wa ukabilianaji unaofaa lazima uzingatie nafasi na mahitaji ya watu wa jinsi zote zote: wanawake na wanaume, na namna ambavyo wote wanavyoweza kuwa mawakala wa mabadiliko.
- ◎ Watendaji wa kosa hilo la unyanyasaji wa kingono na kijinsia pengine huwa ni watu wale ambaao wanategemewa kuwasaidia na kuwalinda waathiriwa.
- ◎ Unyanyasaji wa kingono na kijinsia huwapata watu wa matabaka yote, tamaduni zote, dini zote, mataifa yote, mbari yoyote, jinsia na umri wowote. Uingiliaji kati ili kuzuia au kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia unazofaa ulenge mtu mmoja mmoja, ndugu wa karibu, jumuiya na jamii kwa ujumla.
- ◎ Kuelewa sababu za unyanyasaji wa kingono na kijinsia kutakusaidia kubuni njia sahihi za kuuzuia; kuelewa madhara ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia kutakuwezesha kuandaa ukabilianaji unaofaa kuhusiana na waathiriwa/ wanusurika na vitendo vya unyanyasaji.
- ◎ Ubaguzi wa kijinsia na kutokuwepo kwa usawa ndilo chimbuko la unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Usawa wa kupata na kumilliki mali, manufaa yatokanayo na misaada pamoja na ushirikishwaji wa wanawake katika mchakato wa kufanya maamuzi ni lazima uzingatiwe katika nyanja zote, ukiwa dhahiri unalenga unyanyasaji wa kingono na kijinsia au ni mwitikio wa mahitaji ya dharura, au ya uokoaji wa maendeleo ya watu.
- ◎ Uwezekano wa kudhoofishwa kihisia kwa muda mrefu na kuleta hali ya kihoro usipuuzwe kamwe.

SURA YA 2

KANUNI ELEKEZI

Unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni tatizo linaloathiri mtu mmojammoja, jamii na jumuiya. Kutokana na utata wake, njia bora ya kupambana na tatizo hilo ni kwa kushirikisha sekta, asasi na taaluma mbalimbali katika kubainisha na kubuni mikakati ya pamoja ya kukabiliana na ukiukwaji huu wa haki za binadamu. Wadau wote wanaoshiriki katika upangaji wa mikakati hiyo wanapaswa kukubali uzingatiaji wa seti ya Kanuni Elekezi pamoja na kuafiki kwa dhati kwamba udhalimu wa namna hiyo ni uvunjaji wa haki za binadamu. Kanuni Elekezi ambazo zitaongoza shughuli zote za programu ni zile ambazo zinazingatia mambo yafuatayo: ushirikishaji kikamilifu wa jamii ya wakimbizi; uhakikishaji wa fursa sawa baina ya wanawake na wanaume, wavulana na wasichana katika kushiriki kwenye upangaji, utekelezaji, ufuatilaji na tathmini ya programu; uwepo wa utendaji wa watendaji wote unaoratibiwa na unaohusisha sekta mbalimbali; uhimizaji wa ubainishaji na uoanishaji wa majukumu ya msingi; na uhakikishaji wa uwepo wa uwajibikaji katika ngazi zote. Kanuni Elekezi ambazo zitaongoza majukumu yote ya mtu mmojammoja nazo zinajumuisha mambo yafuatayo: ulinzi na usalama wa kimwili wa waathiriwa/wanusurika; utunzaji wa siri na uadilifu; kuheshimu matakwa, haki na hadhi za waathiriwa/wanusurika; na uzingatiaji kikamilifu wa maslahi ya msingi kabisa kwa mtoto wakati wa kufanya maamuzi yoyote kuhusu njia sahihi zaidi ya namna ya kuchukua hatua katika uzuiaji au ukabilianaji na tukio la unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Mapambano dhidi ya tatizo gumu la unyanyasaji wa kingono na kijinsia yanahitaji ushirikiano pamoja na jitihada za pamoja baina ya sekta, asasi na taaluma mbalimbali. Wadau wote wanaoshiriki katika kubuni na kuandaa mikakati ya kuzuia na kukabiliana na tatizo la unyanyasaji wa kingono na kijinsia watalazimika kuzingatia seti ya Kanuni Elekezi zitakazowaongoza katika majukumu yao. Kanuni hizo zinaweza kuainishwa katika zile zinazoongoza masuala ya kubuni, kutekeleza na kutathmini programu kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine zile zinazohusu masuala ya uhifadhi na usaidizi kwa waathiriwa/wanusurika wa ugomvi bila kujali kama ni wanaume, wanawake au watoto. (Tazama Sura ya 5 kwa Kanuni Elekezi ambazo ni mahususi zaidi kwa watoto).

Kanuni Elekezi

Programu

- **Shirikisha kikamilifu jamii ya wakimbizi**
- **Hakikisha fursa sawa katika ushiriki wa wanaume na wanawake, wavulana na wasichana katika upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya programu**
- **Hakikisha utendaji ulioratibiwa wa watendaji wote na unaoshirikisha sekta mbalimbali**
- **Jitahidi kuoanisha na kubainisha majukumu makuu**
- **Hakikisha uwepo wa uwajibikaji katika ngazi zote**

Mtu mmojammoja

- **Hakikisha usalama wa kimwili wa waathiriwa/ wanusurika**
- **Tunza usiri**
- **Heshimu matakwa, haki na hadhi za waathiriwa/ wanusurika, na zingatia maslahi ya msingi kabisa kwa mtoto wakati wa kutoa maamuzi wowote kuhusu hatua bora zaidi ya kuchukuliwa kuzuia au kukabiliana na tukio la unyanyasaji wa kingono na kijinsia**
- **Hakikisha kutokuwepo na aina yoyote ya ubaguzi**

Aidha wadau wote wanaohusika na programu hii wanapaswa kuzingatia na kubadilishana miongoni mwao Kanuni Elekezi zinazopatikana katika maandiko mengine, kama vile katika maandiko ya maadili ya kazi.

Kanuni Elekezi za Programu

Shirikisha jamii ya wakimbizi kikamilifu. Jamii ya wakimbizi ndiyo inayopaswa kuwa kitovu cha shughuli zote za programu zinazohusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Ni jambo muhimu kuishirikisha jamii katika mchakato wa kufikia maamuzi. Utafiti makini unahitajika ili kupata uelewa sahihi wa mahusiano baina ya madaraka na jinsia kwa upande mmoja, na mienendo mingine ya kimadaraka katika jamii.

Hakikisha fursa sawa katika ushiriki wa wanaume na wanawake, wavulana na wasichana katika upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya programu. Makundi mengi mbalimbali na watu binafsi katika jamii washiriki katika hatua zote za uandaaji wa programu ya kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Jitahidi kubainisha na kuoanisha majukumu makuu. Hatua zozote za kuzuia au kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia sharti zibainishwe na kuoanishwa katika programu na sekta zilizopo. Hatua hizo zisianzishwe kama programu au miradi maalumu kwa sababu kufanya hivyo kunazipunguzia uwezo wa kudumu kwa muda mrefu.

Hakikisha utendaji ulioratibiwa wa watendaji wote na unaoshirikisha sekta mbalimbali. Ufanisi wa programu zinazojihusisha na masuala ya kuzuia au kukabiliana na udhalimu wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia unategemea sana kiwango cha ushirikishwaji wa sekta za msingi (mathalani, huduma za jamii, afya, ulinzi, usalama). Aidha watendaji wakuu (ikiwa ni pamoja na serikali, AZISE, na UNHCR) wanapaswa kuwa tayari kuungana, kushirikiana na kuelekezana.

Hakikisha uwepo wa uwajibikaji katika ngazi zote. Watu wote ambao kwa njia moja au nyingine wanahusika na programu za kuzuia udhalimu wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia wanapaswa kuwajibika kikamilifu kwa yote yanayowapasa kutenda na katika ufanikishaji kazi na majukumu yaliyokubaliwa.

Kanuni Elekezi kwa ajili ya Mtu Binafsi

Hakikisha usalama wa mwathiriwa/mnusurika pamoja na familia yake wakati wote. Ni jambo muhimu kukumbuka kuwa mwathiriwa/mnusurika anaweza akagubikwa na hofu kiasi cha kumfanya ahitaji kuhakikishiwa usalama wake binafsi. Na kwa vyovyothe vile, hakikisha kuwa hakabiliwi na hatari ya kudhuriwa tena na mtu aliyemshambulia mara ya kwanza au mtu mwininge ye yeyote kutoka katika jamii yake. Iribidi omba msaada kutoka kwa vyombo vyenye uwezo wa kumlinda, mathalani, walinzi wa kambi, jeshi la polisi, au vyombo vingine vinavyohusika na kazi za usalama na amani, maafisa wa ugani, na kadhalika. Aidha hakikisha pia usalama na ulinzi wa watu wote ambao wanafanya kazi ya kuwasaidia waathiriwa/wanusurika, kwa mfano, familia, marafiki, watoa huduma kwa jamii au watumishi wanaohusika na uzuaji wa udhalimu wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia pamoja na wahudumu wa masuala ya afya.

Heshimu na tunza siri za waathiriwa wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia pamoja na familia zao wakati wote. Maana ya sharti hili ni kwamba unaruhusiwa kutoa taarifa muhimu peke yake kulingana na maombi au makubaliano ya mwathiriwa/mnusurika kwa watu wengine ambao wanahusika na utoaji wa misaada. Aidha utambulisho wa mhalifu unapaswa kuhifadhiwa kwa siri. Ni marufuku kutoa taarifa ambazo zinajumuisha majina ya waathiriwa/wanusurika. Kabla ya kutoa taarifa za waathiriwa/wanusurika kwa watu wengine ni lazima upate kibali cha maandishi kutoka kwa wahusika (au wazazi wao kama waathiriwani watoto).

Taarifa zote za maandishi sharti zihifadhiwe katika mafaili na kufungiwa mahali ambapo ni salama. Kukitokea haja ya kutoa hadharani ripoti au takwimu kazi hii ifanywe na afisa mmoja tu na ambaye ana madaraka ya kufanya hiyo. Mtu huyo atoe taarifa za jumla tu kuhusu waathiriwa/wanusurika. Jambo lolote ambalo linaweza kufichua utambulisho wa mhusika (kwa mfano, jina, anwani, n.k.) liondolewe katika taarifa.

Watumishi wote wanaohusika moja kwa moja na matukio ya vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia sharti wale kiapo cha utunzaji wa siri.

Wakati mwingine ili kufanikisha masailiano na waathiriwa/wanusurika panahitajika msaada wa wakalimani au wafasiri. Katika hali kama hizo inashauriwa kuwatumia wataalamu kutoka nje ya jamii husika na kuwawekea hadidu za rejea kuhusiana na utekelezaji wa kazi zao. Kwa vile kuna upungufu wa wakalimani na wafasiri ambao ni mabingwa na wanaojitegemea, mashirika yanapaswa kutenga kiasi kinachotosha cha fedha pamoja na kuwa na watumishi wanaofaa ili kuhakikisha kuwa wakati wa masailiano zinapatikana huduma bora za ukalimani/ufasiri.

Hatua zozote zitakazochukuliwa ni lazima ziheshimu matakwa, haki na utu wa mwathiriwa/mnusurika.

- ◎ Fanya masailiano faraghani na kwa kadri iwezekanavyo tumia wafasiri wa jinsia moja.
- ◎ Kadiri iwezekanavyo, kila mara endesha masailiano na uchunguzi kwa kuwatumia watumishi wa jinsia moja na waathiriwa/wanusurika (kwa mfano, mwathiriwa/mnusurika akiwa mwanamke asailiwe na mwanamke).
- ◎ Jitahidi kuwa msikilizaji makini.
- ◎ Usiwe mwamuzi kwa upande wowote.
- ◎ Kuwa mvumilivu; usimshinikize msailiwa ili akupatie taarifa kuhusu jambo ambalo yeye hataki kulizungumzia.
- ◎ Waulize waathiriwa/wanusurika maswali yanayohusu tu hoja na madhumuni ya masailiano.
- ◎ Hali ya ubikira wa mwathiriwa/mnusurika siyo suala muhimu na kwa hiyo liszungumziwe.
- ◎ Epukana na tabia ya kumfanya mwathiriwa/mnusurika kurudiarudia maelezo yaleyale katika masailiano tofautitofauti.
- ◎ Usimcheke msailiwa wala usimwonyeshe kwamba humheshimu, au huheshimu utamaduni, familia yake au hali aliyomo.
- ◎ Kama hakuna watu wenye sifa za kuendesha masailiano, basi mwathiriwa/mnusurika atafutiwe na kupelekwa kwa watendaji wengine wenye sifa.
- ◎ Muulize mwathiriwa/mnusurika kwa faragha kama angependa mwenzake wa ndoa au asiye wa ndoa awepo kwenye masailiano au la.

Kama mwathiriwa/mnusurika ni mtoto, kanuni ya kuzingatia maslahi bora ya mtoto itumike kuongoza maamuzi bora kuhusu aina ya huduma na misaada inayotakiwa kutolewa. Rejea Sura ya 5 kwa maelezo zaidi.

Hakikisha kuwa hakuna ubaguzi wa aina yoyote. Kila mtu, awe mtu mzima au mtoto, na bila kujali jinsia yake, anastahili kupewa huduma na usaidizi unaostahiki. Waathiriwa/ wanusurika wa udhalimu wa kuitia unyanyasaji wa kingono na kijinsia wanastahili kuhudumiwa kwa haki na usawa pasipokujali tofauti zao za kikabila, kidini, kitaifa au kijinsia.

Majukumu Matano ya UNHCR kwa Wanawake Wakimbizi

UNHCR imejipangia kutekeleza majukumu matano ya msingi kwa ajili ya kufanikisha uimarishaji wa haki za wanawake wakimbizi, uhamasishaji wa sasawa wa kijinsia na uzuiaji pamoja na uharakishaji wa uchukuaji wa hatua dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Japokuwa majukumu haya matano hayakamilishi orodha kamili ya mambo yanayostahili kipaumbele kwa ajili ya wanawake wakimbizi, majukumu hayo ni msingi wa utokomezaji wa mianya ya udhalimu wa unyanyasaji kingono na kijinsia kwa wakimbizi. Majukumu hayo matano ni:


1. Kubuni mikakati jumuishi ya kitaifa ya kupambana na unyanyasaji wa kingono ,ukiwemo wa majumbani, dhidi ya wanawake wakimbizi.
2. Kuwasajili wanawake wakimbizi kipekee na kuwapatia taarifa zote zinazohitajika kwa ajili ya usalama na uhuru wao binafsi wa kwenda mahali popote na kupata huduma za lazima. Wakimbizi wa kike na wa kiume wanapaswa kushiriki sawa katika mchakato wa usajili.
3. Kuhakikisha kuwa asilimia 50 ya wawakilishi katika kamati zote za menejimenti na katika vyombo vingine vinavyowawakilisha wakimbizi katika UNHCR kwenye maeneo ya mijini, vijijini na kambinini wanawake.
4. Kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki ama moja kwa moja ama kwa njia nyinginezo katika usimamizi wa ugavi wa vyakula mahitaji mengine ili kuhakikisha kwamba wanawake walio watu wazima katika kaya ndio wanaodhibiti bidhaa kwenye kaya zao.
5. Ugawaji wa vifaa vya kujitunza kiusafi kwa wanawake na wasichana wanaohudumiwa na UNHCR liwe ni jukumu la kipaumbele katika Programu za misaada za UNHCR.

Mkabala Unaoshirikisha Sekta Mbalimbali

Mkabala unaoshirikisha sekta anuwai ndio msingi wa mapambano dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Mchoro ufuatao ni kielelezo kinachoonyesha jinsi watendaji mbalimbali wanavyoshirikiana katika kushughulikia mahitaji ya waathiriwa/wanusurika.

Kiunzi cha Ushirikishaji wa Mashirika na Sekta Mbalimbali katika Kuzuia na Kupambana na Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia

Utaratibu,
Kanuni Elekezi,
Mtandao wa Rufaa



- * Mashirika ya Umoja wa Mataifa
- * AZISE (za ndani na za nje)
- * Mamlaka za Serikali
- * Jumuiya za wenyeji/zilizopokea wakimbizi

		Sura ya 1	Sura ya 2	Sura ya 3	Sura ya 4	Sura ya 5	Sura ya 6	Sura ya 7	Sura ya 8
Ulinzi	Ulinzi wa kimataifa unajumuisha hatua zote muhimu za kuhakikisha kwamba wakimbizi wanapata ulinzi wa kutosha na wanakuwa na fursa ya kutumia na kufaidi uhuru wao. Shirika la UNHCR halina budi kuongoza jitihada za kuzuia na kupambana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya wakimbizi.								
Shughuli za Jumuia ya Wakimbizi	Wakimbizi hawana budi kushirikishwa kikamilifu katika kubuni, kupanga na kutekeleza shughuli zote, zikiwemo zile ambazo zinakusudia kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Hasa ni muhimu kuwashirikisha wanaume na vijana barobaro, pamoja na wanawake katika harakati za kuzuia na kupambana na uonevu wa aina hii. Kwa kawaida wanaume ndio wanaokiritimba nafasi za uongozi ndani ya kambi za wakimbizi. Viongozi wa kiume wana ushawishi mkubwa mionganini mwa wanaume wenzao na kwa sababu hiyo wana uwezo mzuri zaidi wa kuhamasisha mapambano dhidi ya uonevu huu unaozungumziwa. Aidha wana uwezo wa kuhakikisha kuwa vitendo viovu vya udhalilishaji wa kingono na kijinsia vinajadiliwa katika mahakama za wenyeji na zile za kijadi. Faida ya kuwashirikisha vijana barobaro ni kwamba unaweza kuanza kubadilisha misimamo na mitazamo ambayo inachochea unyanyaaji wa kingono na kijinsia. Ushirikishaji wa tabaka zote za jamii katika harakati za kuzuia na kupambana na uovu huu unasaidia kuinua kiwango cha uwajibikaji wa jamii nzima katika kuziba mianya ya matukio ya unyanyasaji wa aina hii pamoja na walengwa wake.								
Shughuli za Uratibu	Kisanduku cha juu kinawakilisha kanuni na mienendo ya Utendaji ambayo imekubaliwa na watendaji wote kama ndiyo Mwongozo wa utekelezaji wa kazi zao zote. Kielelezo hicho kinajumuisha njia za uratibu, Kanuni Elekezi na mifumo rejea inayopaswa kuwaongoza watendaji wote.								
Ushirikishaji Wa Washiriki Wote wakuu	Kisanduku cha chini kinaonyesha kwamba kuna watendaji wengine wengi ambao michango yao ni muhimu, lakini hawakushirikishwa mahususi ama katika makundi ya wakimbizi ama katika makundi ya kisekta. Dhima na majukumu yao vinapaswa kufafanuliwa kinagaubaga.								

Uzuiaji na uchukuaji hatua dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia hujumuisha hatua zinazochukuliwa na watendaji wengi, ambapo idadi kubwa ya watendaji hao huwakilisha moja kati ya maeneo makuu manne ambayo ni afya, nafsjamii, ulinzi na usalama, na sheria/haki.

Afya. Watendaji katika eneo hili ni hawa wafuatao: watumishi katika masuala ya afya, madaktari, manesi, wakunga, wakunga wa jadi, watoa huduma za afya kwa jamii, waganga wa jadi, wasimamizi, watawala na waratibu wa afya, maafisa na watumishi wa wizara ya afya katika nchi mwenyeji walimo wakimbizi.

Watendaji wa **Saikolojia-Jamii** ni: watumishi na watu wa kujitolea katika jamii, wanajamii, Jumuia Zisizo za Serikali (AZISE) zinazotekeleza shughuli za programu ya kupiga vita unyanyasaji wa kingono na kijinsia, watumishi wa sekta ya elimu, makundi ya wakimbizi, wakufunzo ya stadi za kazi, wataalamu wa mbini za uzalishaji mali na usimamizi wa mikopo midogomidogo, pamoja na maafisa na watumishi wa wizara zinazoshughulikia masuala ya huduma na ustawi wa jamii katika nchi walimo wakimbizi.

Watendaji wa **Ulinzi na Usalama** ni: jeshi la polisi, vyombo vya usalama, maafisa wa usalama na wa uwandani wanaotumikia shirika la UNHCR na AZISE, walinzi wa wakimbizi, na viongozi wa wakimbizi na wanajamii kwa jumla.

Watendaji wa **Sheria/Haki** ni: Watendaji wa eneo hili ni: watumishi wanaohusika na majukumu ya hifadhi katika shirika la UNHCR na asasi zinazojishughulisha na haki za binadamu, majaji na maafisa wengine wa nchi mwenyeji, wabunge na watunga sheria, viongozi wa jamii ikiwa ni pamoja na kamati ndogondogo za Kamati za Wakimbizi ambazo husimamia hatua za ulinzi na adhabu zinazoanzishwa na jamii yenyewe, vyombo vya kusimamia wa sheria, AZISE na makundi ya harakati ambayo yanajihuisha na masuala ya kuboresha sheria za kitaifa na sera kuhusu udhalimu wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Mambo Muhimu ya Kukumbuka

Wadau wote sharti wazingatie kanuni elekezi zifuatazo:

Programu

- ◎ Shirikisha kikamilifu jamii ya wakimbizi.
- ◎ Hakikisha fursa sawa katika ushiriki wa wanaume na wanawake, wavulana na wasichana katika upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya programu.
- ◎ Hakikisha utendaji ulioratibiwa wa watendaji wote na

- unaoshirikisha sekta mbalimbali.
- ◎ Jitahidi kuoanisha na kubainisha majukumu makuu.
 - ◎ Hakikisha uwepo wa uwajibikaji katika ngazi zote.

Mtu Binafsi

- ◎ Hakikisha usalama wa kimwili wa waathiriwa/wanusurika.
- ◎ Tunza usiri.
- ◎ Heshimu matakwa, haki na hadhi za waathiriwa/wanusurika, na zingatia maslahi ya msingi kabisa kwa mtoto wakati wa kutoa maamuzi yoyote kuhusu hatua bora zaidi ya kuchukuliwa kuzuia au kukabiliana na tukio la unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Hakikisha kutokuwepo na aina yoyote ya ubaguzi.

Tumia mkabala unaoshirikisha sekta mbalimbali katika harakati za kuzuia au kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Sura ya 1

Sura ya 2

Sura ya 3

Sura ya 4

Sura ya 5

Sura ya 6

Sura ya 7

Sura ya 8

SURA YA 3

KUZUIA UNYANYASAJI WA KINGONO NA KIJINSIA

Mikakati sahihi ya kupambana na udhalimu unaohusiana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia inaweza kuandaliwa iwapo tu pamefanyika ubainishaji makini wa mambo ambayo yanachangia na kuchochaea aina ya tatizo lenyewe pamoja na kiwango chake. Walengwa wa hatua za uzuiaji wa udhalimu huu ni watu wanaoweza kufanya uovu huo, wanusurika wake na watu ambaao wanaweza kuwapatia misaada. Kwa hiyo juhudii hazina budi kuelekezwa kwa watu wafuatao: jamii za wakimbizi, watoaji misaada ya kibinadamu, raia wa nchi mwenyeji pamoja na vyombo vyake vya dola. Kama ilivyo kwa programu zote zinazojihusisha na mapambano dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, mikakati ya uzuiaji yenye ufanisi mkubwa zaidi ni ile ambayo inashirikisha sekta mbalimbali wakati mmoja, wakiwemo wakimbizi wenyewe, katika kubuni na kuandaa, kutekeleza na kutathmini mikakati hiyo.

Mikakati yenye nafasi kubwa ya kufanikiwa lazima ijumuisha hatua zenye malengo makuu matano: kubadili mitazamo ya kijamii na kiutamaduni kwa kuweka msisitizo mahususi katika kuwawezesha wanawake na wasichana; kujenga upya mifumo ya kifamilia na kijamii pamoja na mihimili yake; kubuni huduma na viwezeshaij ambazo ni bora zaidi; kushirikisha mifumo ya sheria za kijadi na za kisasa ili kuhakikisha kwamba matumizi yake yanaendana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu; na kufuatilia na kuhifadhi kumbukumbu za matukio ya vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Uzuiaji wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia unahusu ubainishaji na ukomeshaji wa mambo ambayo yanawaweka baadhi ya wakimbizi katika hatari ya kukabiliwa na unyanyasaji wa aina hii. Aidha harakati hizo za uzuiaji zinajumuisha uandaaji wa mikakati kadhaa kwa ajili ya kuboresha hali ya ulinzi kwa wakimbizi wote. Kiwango cha ufanisi kitakuwa kikubwa iwapo sekta zote zinazohusika na hifadhi na utoaji huduma kwa jamii ya wakimbizi, pamoja na wakimbizi wenyewe, zitashiriki katika kuandaa, kutekeleza na kusimamia mikakati hiyo.

Ili KUZUIA unyanyasaji wa kingono na kijinsia, ni lazima ubainishe, uelewe na ukabiliane na VYANZO vyake pamoja na MAMBO YANAYOCHOCHAEA kutokea kwake.

Awali ya yote, inashauriwa kubainisha mambo na masuala ambayo yanatawala mazingira husika kwa lengo la kutathmini mahitaji au kufanya uchambuzi wa hali halisi (Rejea Sura ya 6 kwa maelezo zaidi). Hatua hii ya kutathmini mahitaji au kuchambua hali halisi itasaidia katika mambo yafuatayo:

- ◎ Kupanua uelewa juu ya utamaduni wa wakimbizi na ule wa nchi mwenyeji au jamii yake, mifumo ya ulinzi wa kijadi, mila pamoja na mahusiano ya kijinsia na kimadaraka.
- ◎ Kubaini maeneo ambamo watu wanahofwa wanaweza kukabiliwa na hatari ya kunyanyaswa kingono au kijinsia, kwa mfano, vituo vya ugavi, mahabusu, sehemu za mipakani, baa za pombe na kadhalika.
- ◎ Kushirikiana na vyombo vinavyojihusisha na masuala ya afya, saikolojia-jamii, usalama, na huduma za kisheria katika nchi mwenyeji, AZISE na mashirika ya Umoja wa Mataifa, kwa ajili ya kubuni na kuandaa kwa pamoja hatua za uzuiaji wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Mikakati yenye uwezo wa kuzaa matunda sahihi inaweza kuandaliwa iwapo tu patakuwa pamefanyika ubainishaji makini wa mambo yanayochangia na kuchochea aina ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia pamoja na viwango vyake. Ifuatayo ni orodha ya mambo yanayoweza kuathiri mtu binafsi, makundi na asasi:

- ◎ Muundo wa kidemografia wa watu (inapendekezwa muundo huo ujumuisho uchambuzi wa kitakwimu kwa vigezo vya umri na jinsia).
- ◎ Maadili ya kijamii na kiutamaduni katika jamii ya wakimbizi.
- ◎ Miundo ya kifamilia na mifumo himili ya jamii kabla na baada ya kusambaratika.
- ◎ Elimu, misimamo, mienendo ya watu walio katika nafasi za uongozi na maamuzi.
- ◎ Huduma na fursa zilizopo, ikiwa ni pamoja na mazingira ya kijiografia, mpangilio wa kambi, na hali ya upatikanaji wa huduma.
- ◎ Mfumo wa sheria, utendaji wa utoaji haki na uzingatiaji wa mila na desturi katika mazingira rasmi na yasiyo rasmi.

Kama ilivyo kwa programu zote za unyanyasaji wa kingono na kijinsia, jamii ya wakimbizi inapaswa kuwa ndiyo kitovu cha watendaji wanaoshiriki katika kubaini na kubuni mikakati ya kukabiliana na udhalimu huu.

Walengwa wa hatua za uzuiaji wa ukatili huu ni wale wote wanaoweza kufanya uovu huo, wanusurika wake na wale wanaoweza kuwapatia misaada. Kwa hiyo hatua zinapaswa kuelekezwa kwa watu wafuatao: jamii za wakimbizi, watoaji misaada ya kibinadamu, raia wa nchi mwenyeji pamoja na vyombo vyake vya dola.

Aidha uzuiaji ni mchakato unaojumuisha ufuatiliaji na upimaji endelevu wa programu na ukusanyaji na uchambuzi wa data

zinazohusu ripoti za matukio ya vitendo vyta unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Mikakati thabiti ya harakati za uzuiaji wa ukatili huu sharti ijumuishetumaini hatua zinazokumbatia malengo makuu matano yafuatayo:

- ◎ Kubadilika desturi za kijamii na kiutamaduni kwa kutilia mkazo uweseshwaji wa wanawake na wasichana.
- ◎ Kujenga upya mifumo ya kifamilia na kijamii pamoja na mifumo ya huduma yake.
- ◎ Kubuni huduma na fursa ambazo ni bora zaidi.
- ◎ Kushirikisha mifumo ya sheria za kijadi na ya kisasa ili kuhakikisha kwamba vinatenda kazi katika kiwango cha kimataifa cha haki za binadamu.
- ◎ Kufuutilia na kuhifadhi kumbukumbu za matukio ya vitendo vyta unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Kubadili Desturi za Kijamii na Kiutamaduni

Kama ilivyojadiliwa katika Sura 1, sababu halisi za vitendo vyta unyanyasaji wa kingono na kijinsia zimejikita katika masuala ya ubaguzi na ukosefu wa usawa katika desturi za kijamii na kiutamaduni. Kwa hiyo uzuiaji wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia unahitaji mabadiliko katika mahusiano ya kijinsia ndani ya jamii yaani; mambo ambayo wanajamii huyapata kwa kigezo cha jinsia zao, mathalani, dhima, majukumu, matarajio vikomo, fursa pamoja na mafao mengine.

Hatua za uzuiaji ambazo shabaha yake ni desturi za kijamii na kiutamaduni zinakusudiwa kuleta mabadiliko katika elimu, mitazamo na tabia. Malengo yanayokusudiwa kufikiwa katika kila mojawapo ya maeneo haya ni:

Elimu	Uelewa wa haki za binadamu; kuheshimu majukumu ya uzazi na kazi za nyumbani; jinsia moja kukubali kubeba majukumu ya jinsia nyingine; kuepuka mbinu ya ugomvi kama njia ya kutatua matatizo wakati wa hasira na maudhi; kufahamu huduma na misaada inayoweza kupatikana kwa ajili ya waathiriwa/ wanusurika na hata kwa watenda uovu huo.
Mitazamo ya Kijamii	Kuamini kwa dhati haki za binadamu kwa kila mtu katika ngazi ya jamii na mtu binafsi; kuenzi thamani ya mchango wa kila mtu kwa jamii; kushirikisha kwa kuzingatia michakato yote inayohitajika katika kufanya maamuzi; kuwaunga mkono na kuwasaidia waathiriwa / wanusurika unyanyasaji wa kijinsi na kijinsia; kutowavumilia hata kidogo watu ambao wanatumia vibaya mamlaka yao.

Tabia	Kutatua matatizo pasipo kutumia nguvu au mabavu; Kuwaheshimu watu wote bila kujali jinsia au majukumu yao ya kijinsia; kuripoti matukio yote ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia na papo hapo kukemea mhalifu na kitendo chenyewe kwa upande mmoja, na kwa upande mwininge kumuunga mkono na kumsaidia mwathiriwa/mnusurika.
--------------	--

Wakimbizi wengi tayari wameanza kukabiliwa na mabadiliko ya dhima za kijadi za kijinsia kwa sababu ya kusambaratika na kuvurugika kwa mienendo ya kawaida ya maisha yao. Programu za uzuiaji wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia zikipewa muda wa kutosha zinaweza kuhimili na kuchochea mabadiliko chanya katika mahusiano ya kijinsia ndani ya jamii. Aidha hatua hizi za uzuiaji wa udhalimu wa aina hii zinaweza kuchangia pia kukomesha mila mbovu za kijadi, kama vile ukeketaji wa wasichana.

MKAKATI.

Andaa Kampeni za Habari, Elimu na Mawasiliano (HEM).

Kuza na imarisha kampeni kwa ajili ya kuhamasisha mabadiliko katika mienendo, elimu na tabia za jamii. Zoezi hili linaweza kujumuisha mada zifuatazo:

- ◎ Jinsia;
- ◎ Haki za binadamu ikiwa ni pamoja na haki za wanawake na haki za watoto;
- ◎ Unyanyasaji wa kingono na kijinsia;
- ◎ Dhima za kijinsia na matarajio katika jamii;
- ◎ Huduma za usaidizi zinazopatikana kwa ajili ya wanusurika na jinsi ya kuzifikia; na
- ◎ Mbinu za kutatua migogoro na kujenga amani.

Taarifa ziwe na ujumbe unaolenga makundi maalumu katika jamii, yakiwemo ya wanawake, wanaume, vijana, watoto, vikundi vyta kidini, wanafunzi, wafanyakishwa wa kike na kiume, viongozi/wazee, waganga wa kijadi na wengineo.

Jamii ya wakimbizi haina budi kushirikishwa kikamilifu katika suala zima la kubuni na kusimamia kampeni za HEM. Mbinu mbalimbali zitumike ili kuhimiza uhamashishwaji wa jamii. Mbinu hizi zinapaswa kuelekeza shabaha yake kwenye ujenzi wa hali ya kujiamini, kuaminiana na kuafikiana mionganini mwa wanajamii ili wawewe kuzingatia masuala yanaopiganiwa. Wakimbizi wanapaswa kupewa mafunzo ya kuwawezesha kuendesha kampeni hizi kwa ufanisi. Kila inapowezekana mbinu za teknolojia mpya katika uwanja wa mawasiliano, ikiwemo Intaneti, zitumike kuendeshea kampeni kuhusu masuala ya HEM. Kadhalika kila inapowezekana

watu wenge utaalamu katika masuala ya mawasiliano ya umma washirikishwe katika mipango ya kuandaa na kusambaza taarifa wakati wa kampeni zinazohusu masuala ya HEM.

Njia thabit za kukuwezesha kusambaza taarifa zako ni pamoja na :

- ◎ mabango yenye maandishi na vijarida;
- ◎ mashindano ya mabango;
- ◎ maigizo, nyimbo na ngoma;
- ◎ majadiliano redioni;
- ◎ matangazo ya huduma za umma;
- ◎ filamu za video;
- ◎ kaulimbiu kwenye fulana/mavazi;
- ◎ warsha za mafunzo; na
- ◎ majadiliano yasiyo rasmi.

Wakati wa kuandaa mikakati kwa ajili ya kampeni za HEM, daima jitahidi kuepuka matatizo yanayoweza kusababishwa na lugha na zingatia kiwango cha elimu ya watu/walengwa.

MKAKATI:

Imarisha Mitando ya Kijamii.

Jamii ya wakimbizi inapaswa kushiriki kikamilifu katika kubuni, kuandaa, kutekeleza na kutathmini mikakati ya kuzuia unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Watendaji wanaoshughulikia masuala ya ubinadamu wanapaswa kushirikiana na makundi mbali mbali ndani ya jamii ya wakimbizi—vikundi vya wanawake; vikundi vya vijana, wahudumu wa afya, waalimu, viongozi wa wakimbizi n.k.—kwa ajili ya kubaini watu ambao wako tayari kujitolea ili kuendesha shughuli hizi ndani ya jamii. Jitihada zifanyike kwa ajili ya kuhakikisha uwiano wa kijinsia katika idadi ya watu walioeteuliwa kufanya kazi za kujitolea. Mtu mmojammoja anaweza kufanya kazi kama mwelimishaji wa jamii au rika, mshauri na watendaji wanaweza pia wakajigawa katika makundi kuunda timu za kushughulikia matukio ya dharura.

AZISE, shirika la UNHCR na vyombo vya serikali ya nchi mwenyeji washirikiane kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wahudumu wa kujitolea pamoja na kuwapatia misaada ya kiufundi.

Rejea pia:

- **Jinsi ya Kuongoza: Programu kuhusu Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia Nchini Guinea (UNHCR 2001)**
- **Jinsi ya Kuongoza: Programu kuhusu Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia Nchini Liberia (UNHCR 2001)**
- **Jinsi ya Kuongoza: Ujenzi wa Mkabala wa Kitimu kwa ajili ya Kuzuia na Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kingono, Kigoma, Tanzania (UNHCR 1998)**
- **Jinsi ya Kuongoza: Mwitiko wa Kijamii kuhusu Unyanyasaji wa Kingono**
- **Dhidi ya Wanawake, Ngara, Tanzania (UNHCR 1997)**

MKAKATI:

Hakikisha Uwepo wa Uwiano wa Kijinsia katika Mfumo wa Uongozi na Mchakato wa Kufanya Maamuzi.

Wakimbizi wanawake washirikishwe katika mchakato wa kufanya maamuzi na katika uongozi. Uwiano wa kijinsia katika uongozi wa jamii ya wakimbizi utahakikisha kwamba mahitaji ya kila kundi yanashughulikiwa kwa uzito sawa -yaani mahitaji ya wanawake, wanaume, wasichana na wavulana. Aidha uwiano huo utawawezesha wanawake na wanaume kuwa na usawa wa kufikia na kudhibiti rasilimali na mafao mengine.

Wakati mwingine inabidi kutumia vigezo vyta kijinsia na umri ili kutoa nafasi tofauti kwa ajili ya majadiliano. Hali hii inatoa uhuru zaidi wa majadiliano na hivyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu vitendo vyta unyanyasaji wa kingono na kijinsia vinavyoweza kujitokeza ndani ya jamii. Kwa hiyo kila inapobidi au kuwezekana mikutano ya jinsia tofauti iruhusiwe; lakini ihakikishwe kuwa wanawake wanahuishwa katika majadaliano na utaratibu wa kufanya maamuzi yanayogusa jamii. Kama utamaduni wa jamii ya wakimbizi hauruhusu kushiriki kwa wanawake na watoto katika mikutano ya wanaume, hakikisha kuwa maoni ya wanawake na watoto yanawasilishwa na kushirikishwa katika maamuzi yanayofikiwa na wanaume. Wakati huohuo jitihada zifanyike kwa ajili ya kujenga na kuimarisha makundi ya wanaume wanaounga mkono ushirikishwaji wa wanawake kwa lengo la kuhamasisha polepole mabadiliko ya misimamo na mitazamo mionganoni mwa wanaume.

MKAKATI:

Wawezeshe wanawake

Japokuwa watu wazima wanaume na wavulana wanaweza pia kufanyiwa uovu kupitia unyanyasaji wa kingono na kijinsia, lakini kwakiwango kikubwa watu wanaokabiliwana hatariyakuvunjija haki hii ya msingi ya binadamu ni wanawake na wasichana. Kwa maana katika tamaduni nyingi wanawake wanahesabika kama jinsia ya wanyonge na tegemezi kwa wanaume. Msigano huu katika mahusiano ya kijinsia unawafanya wanawake kukabiliwa na hatari yenye sura mbili: kutokana na maumbile yao wanawake wanakabiliwa na manyanyaso ya kimabavu na kisaikolojia;; na pindi wanapofanyiwa manyanyaso hayo kwa kawaida huwa na fursa finyu za kufidiwa au kujitegemea kiuchumi.

- ◎ Inawezekana kwamba mfumo wa sheria za wenyeji hautambui vitendo vyta unyanyasaji wa kingono au kijinsia kama makosa.

- ◎ Taarifa ya mwanamke kuhusu alivyodhalilishwa inaweza ikapuuzwa na hata kudhihakiwa.
- ◎ Mwanamke anaweza kuamua asitoe taarifa ya tukio la unyanyasaji lililomkabili kwa kuogopa mhalifu kulipiza kisasi au kufanyiwa uonevu zaidi yeye mwenyewe au wanafamilia yake.
- ◎ Kama mhalifu mwenyewe ni mume wake, mwanamke anaweza kujikuta katika mtego wa kulazimika kuendelea kuishi naye, jambo ambalo linamweka katika hatari ya kudhalilishwa zaidi, kwa sababu ya kukosa uwezo wa kukidhi mahitaji yake mwenyewe na ya watoto wake.

Unaweza kuanza kubadili dhima za wanawake katika jamii na jinsi wanavyojifikiria wao wenyewe kwa kuwapatia shughuli ambazo zinaongeza uhuru wao na hali yao ya kujitegemea kiuchumi, pamoja na uwezo wao wa uongozi na kufanya maamuzi. Shughuli hizo zinaweza kuwa:

- ◎ Uendeshaji wa programu za kufuta ujinga.
- ◎ Utoaji wa mafunzo ya kiufundi.
- ◎ Uandaaji wa miradi midogomidogo ya uzalishaji kipato.
- ◎ Kuhakikisha kuwa wanawake wanapewa uwakilishi linganifu katika uongozi wa wakimbizi na kamati za ugavi wa misaada.
- ◎ Kuzingatia uwiano wa kijinsia wakati wa kutoa nafasi za kazi kwa wakimbizi.
- ◎ Kutoa fursa sawa kwa wasichana wakimbizi katika suala la elimu.
- ◎ Kusaidia na kuunga mkono makundi na jumuiya za wanawake.
- ◎ Kutoa mafunzo ya uongozi.
Mbali ya kukuza dhima za wanawake katika masuala ya uongozi na michakato ya kufanya maamuzi ndani ya jamii, wanawake wakimbizi wahimizwe kuanzisha mitandao itakayowasaidia kupigania haki sawa katika jamii zao.

Rejea pia:

Kanuni za Uhifadhi wa Wanawake Wakimbizi (UNHCR 1999)

MKAKATI:

Washirikishe wanaume

- ◎ Kuelekeza mikakati yote ya kuzuia na kupambana na unyanyasajijiwa kingono na kijinsia kwawanawake, kunapuuzia ukweli kwamba kwa kiasi kikubwa udhalimu huu hutendwa na wanaume. Kwa hiyo, ni lazima wanaume washirikishwe katika ufumbuzi wa tatizo hili. Wanaume wanapaswa kuchukua msimamo imara dhidi ya udhalilishaji huu ili mafanikio na maendeleo halisi yaweze kupatikana.
- ◎ Wanaume walio katika nafasi za uongozi mabadiliko. Wanaweza kuwa mifano ya kuigwa kwa watu wengine.
- ◎ Wanaume wanapaswa kueleweshwa kuwa watendaji wa makosa haya ya unyanyasaji wa Kingono na kijinsia wataadhibiwa. Na adhabu hizo zitazisababishia familia na jamaa zao madhara na aibu.

Saidia katika uundaji na uimarishaji wa makundi ya wanaume wanaouna mkono harakati za kukomesha unyanyasaji wa Kingono na kijinsia katika jamii yao. Makundi haya yanaweza kuimarisha msimamo kwamba unyanyasaji wa Kingono na kijinsia siyo 'suala la wanawake' peke yao. Mafundisho muhimu yanaweza kupatikana kutoka kwa wale ambao wanafanya kazi na wanaume wanaohusika na maandalizi ya programu za uzazi na familia. Wanaume wanapoonekana wakijihusisha na harakati za kukomesha unyanyasaji wa Kingono na kijinsia husaidia kulipatia saula hili urahisi wa kukubalika mionganoni mwa wanaume wengine na hivyo kuwavuta ili washiriki katika harakati hizo.

Kamwe usisahau kwamba wanaume na wavulana wanaweza pia kunyanyaswa kuitia unyanyasaji wa Kingono na kijinsia. Kwa hiyo inashuriwa kwamba wanaume wapatiwe fursa na mazingira mwafaka ya kujadili suala hili kwa lengo la kulitafutia njia za kulikomesha. Kumbuka kwamba kinyume na ilivyo kwa wanawake, wanaume inawawiwa vigumu zaidi kuelezea matukio ya udhalilishwaji wa Kingono na kijinsia walofanyiwa.

Jitihada zianze mapema: wapatiie wazazi mafunzo kuhusu masuala ya kijinsia, usawa na hatari za vitendo vya unyanyasaji ili na wao waweze kutoa mafunzo hayo kwa watoto wao. Shule zitumike kuwapatia vijana mafunzo kuhusu masuala ya mapenzi na afya ya uzazi, haki za binadamu na uelewa wa masuala ya kijinsia. Vinginevyo wapatiwe mafunzo hayo kuitia programu za kijamii.

Rejea pia:

- **Uzuiaji na Ukabilianaji na Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia katika Mazingira ya Wakimbizi: Chapisho la Makala za Warsha kuhusu Mafundisho toka kwa Mashirika Mbalimbali (UNHCR 2001)**
- **Ripoti za Idadi ya Watu: Kukomesha Magomvi Dhidi ya Wanawake (John Hopkins University School of Public Health 1999)**

MKAKATI:

Washirikishe Watoto na Vijana

Kazi ya kujenga maarifa, kubadili misimamo na tabia huwa rahisi iwapo itaanza kufanyika mapema.

- ◎ Wahimize wazazi ambao wamepatiwa mafunzo kuhusu haki za binadamu, uelewa wa masuala ya kijinsia, na mbinu za kutatua matatizo kwa njia za amani wawapatie watoto wao taarifa hizi.
- ◎ Wapatie walimu mafunzo ya kuwawezesha kujumuisha masuala haya katika mitaala.
- ◎ Anzisha na imarisha vikundi vyta watoto wanaojihusisha na mafunzo ya kirika na uhamasishaji wa uelewa wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Himiza uundaji wa vikundi vyta wasichana mashulenii kwa ajili ya kusaidiana na kutoa ushauri nasaha kwa wasichana wadogo zaidi.
- ◎ Ingiza majadiliano kuhusu jinsia, mahusiano, na unyanyasaji wa kingono na kijinsia katika harakati ambazo tayari zinashughulikiwa na jamii, kama vile elimu na programu za mafunzo ya maarifa na stadi mbalimbali pamoja na kampeni dhidi ya VVU/UKIMWI ambazo zinawalenga vijana.
- ◎ Buni njia makini za kubadilisha fikira za watoto kuhusu uelewa wao wa maana halisi ya mvulana au msichana. Njia hizo zinaweza kutumia tamthiliya, mashairi, au kazi za sanaa.
- ◎ Wapatie watoto fursa ya kuelezea mahitaji na mashaka yao pia.

Rejea pia

- Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Masuala Tunduizi: Unyanyasaji na Unyonyaji (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children Revised 2002)
- Watoto Wakimbizi: Kanuni za Uhifadhi na Ulezi (UNHCR 1994)

Kujenga Upya Familia na Mifumo Himili ya Kijamii

Watu wanapokimbia ili kujiepusha na migogoro, aghalabu mifumo himili ya jamii huvurugika. Wakati wa mapigano na kukimbia familia husambaratika na wanafamilia hypotezana. Idadi kubwa ya wakimbizi huwa ni watoto na wanawake ambao hulazimika kuisha bila wanaume wao na familia zao. Kutokana na shida, wanawake wengi ambao ni wakimbizi wamelazimika kubeba majukumu ya wanaume ili waweze kukidhi mahitaji

yao wenyewe na yale ya familia zao. Wanaume wakimbizi hujisikia kana kwamba hawana mamlaka, huchanganyikiwa na hugubikwa na hasira; kwa maana dhima yao ya kijadi ya kubeba jukumu la kutunza na kutetea familia yake huchukuliwa na asasi zitoazo misaada ya kibinadamu kama chakula na makazi hata kama ni kwa muda tu.

Mifumo ya kijamii ambayo ndiyo inayotawala viwango vya maadili na tabia ya jamii hudhoofika au hata kuvurugika kabisa wakati wa kukimbia. Katika mazingira kama haya kuna uwezekano mkubwa wa kushamiri kwa udhalimu wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Kwa hiyojambo muhimu ni kujaribu kujenga upya haraka iwezekanavyo miundo na mifumo ambayo ndiyo mihimili ya kuheshimu na kuzingatia haki sawa kwa wanajamii wote.

MKAKATI:

Andaa Programu za Kijamii na Burudani

Wakati wa kuandaa kambi ya wakimbizi hakikisha kuwa unatoa nafasi ya kutosha kwa ajili ya michezo, burudani na shughuli za kijamii pamoja na majengo ya kuendeshea mambo haya. Washirikishe wakimbizi, hususani wanawake na wasichana, katika kubuni na kuandaa shughuli za burudani na zile za kijamii. Shule hazittoi elimu peke yake, zinaweza kutumika kama vyombo vya kuwalinda watoto dhidi ya manyanyaso ya kingono Ána kijinsia. Kwa hiyo, hakikisha kuwa wasichana na wavulana wana fursa sawa ya kupatiwa elimu.

MKAKATI:

Himiza Ufufuaji wa Shughuli za Kidini na Kiroho

Wakati wa kuandaa plani ya kambi, tenga sehemu kwa ajili ya makanisa, misikiti na majengo mengi ya ibada. Wahimize wanajamii kuhisha uzingatiaji wa dini zao na mafundisho yao ya kiroho. Viongozi wa kidini washirikishwe kama wadau katika jitihada za kuhimiza uzingatiaji wa haki za wanawake na watoto na kuendesha vita dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Rejea pia:

- **Kiongozi cha Dharura - Toleo la Pili (UNHCR 2000)**

Kujenga Mazingira ya Kuboresha Mifumo ya Uwajibikaji

Wakati wa kuchambua hali halisi, jaribu kubaini hali ya mahusiano ya madaraka ndani jamii ya wakimbizi na baina ya watu wanaotoa misaada kwa wakimbizi. Watu wanaoweza kutenda uhalifu ni pamoja na wale watu wenyewe mamlaka/nyadhifa, wale walio katika nafasi zinazowawezesha kuathiri maadili ya kijamii na utamaduni, na/au wale wanaotoa misaada kwa wanusurika wa ukatili wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Maswali muhimu ya kuijiliza ni haya:

- ◎ Ni nani anayefanya maamuzi kwa ajili ya jamii?
- ◎ Je, asasi zitoazo misaada ya kibinadamu zinashirikisha na kushauriana na nani wakati wa kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini shughuli zao?
- ◎ Ni watu gani wanaopewa misaada?
- ◎ Ni nani anayedhibiti rasilimali katika jamii na ndani ya familia?

MKAKATI:

Imarisha Uelewa

Watumishi wa mashirika yote lazima wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara na kuhimizwa kuhusu umuhimu wa masuala ya haki za binadamu, jinsia, sheria na sera za kitaifa na kimataifa, na kanuni husika kwa ajili ya kuzuia unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Aidha pawepo na utaratibu maalumu wa kuendesha warsha kwa ajili ya 'kuwapiga msasa'. Shughuli zote hizi ziwahusishe watumishi wa Umoja wa Mataifa, AZUSE, vyombo vyya serikali ya nchi mwenyeji na wadau wengine.

Jamii ipatiwe mafunzo kuhusu haki za binadamu na uelewa wa masuala ya jinsia, kazi za jeshi la polisi, mahakama na watoaji misaada ya kibinadamu wa kitaifa na kimataifa.

MKAKATI:

Hakikisha Uzingatiaji wa Viwango vya Uwajibikaji na Maadili ya Kazi

Hairuhusiwi kwa mtu ye yeyote anayehusika na utoaji wa misaada ya kibinadamu kutumia vibaya madaraka yake. Inashauriwa kwamba majukumu, matarajio, maadili, na viwango kwa ajili ya watumishi yaandikwe katika mwongozo wa maadili na kanuni

za kazi husika. Aidha panapaswa kuwepo na utaratibu wa kuwaadhibu watumishi wa asasi zitoazo misaada wanaoshindwa kuzingatia maadili na kanuni za kazi.

Maadili ya kazi ni vyombo vya kinga. Ni ishara ya utashi wa kujidhibiti, Kujiwekea na kuzingatia viwango sahihi na kupiga vita tabia mbovu ambazo zinaweza kurejesha tena uonevu kwa wanyonge mionganoni mwa watu wanaohitaji msaada wetu, kukiuka haki za binadamu, kudhoofisha mamlaka za asasi husika na kuzivunja heshima.

Ruud Lubbers, Balozi wa Umoja wa Mataifa kwa Wakimbizi, 2002

Tumia taarifa na shughuli za kielimu kuifahamisha jamii ya wakimbizi kuhusu vigezo vinavyoongoza huduma za misaada ya kibinadamu pamoja na maadili ya kazi yanayohusu vigezo hivyo. Unda utaratibu ambao unaweza kutumika kwa ajili ya kuripoti na kuchunguza kwa siri makosa yatendwao na watumishi wa asasi zitoazo misaada ya kibinadamu. Watu wataao ripoti za matukio kama haya na wanusurika wake sharti wahakikishiwe kwamba hawatafichuliwa. Hakikisha kuwa wakimbizi wanafahamu mahali pa kwenda kutoa ripoti za matukio kama haya. Upelelezi wa makosa yanayodaiwa kutendwa na watumishi wanaotoa misaada ya kibinadamu sharti uanze mara moja na uendeshwe kitaalamu. (Angalia Kiambatisho 1 cha UNHCR kuhusu Mwongozo wa Maadili na Kiambatisho 1 cha IASC kuhusu Kanuni za Mwongozo wa Maadili).

Uandaaji wa Huduma na Viwezeshejji Stahiki

Kambi iliyopangiliwa vizuri pamoja na upatikanaji kirahisi wa mahitaji ya msingi ni mambo yanayoweza kusaidia katika kuzuia unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Kwa hiyo unapoandaa viwezeshejji na utaratibu wa huduma kwa ajili ya kambi ya wakimbizi:

- ◎ Jiepushe na kusongamanisha watu pamoja na nyumba za kaya zaidi ya moja.
- ◎ Wape makazi ya muda watoto waliotenganishwa na familia zao mpaka hapo watakafanyiwa mipango bora ya walezi wa kuwatunza.
- ◎ Zipatie kaya zinazoongozwa na wanawake makazi yasiyojumuisha wanafamilia wa kiume ambao ni watu wazima.
- ◎ Jitahidi kuhakikisha kuwa familia zisizokuwa na udugu hazichangii sebule au vyumba vya kulala.
- ◎ Hakikisha kuwa bidhaa muhimu, mathalani vyakula, maji na mafuta ya kupikia, zinatolewa kwa wanawake moja kwa moja au vinagawiwa kupitia kwa wanawake. Hakikisha pia kuwa bidhaa hizi zinafikika kwa urahisi pasipo kuwalazimu wanawake kuzifuata sehemu zilizojitenga au mafichoni.
- ◎ Jenga vyoo mbali na mahali pa kuishi na uhakikishe kwamba

- sehemu za wanawake zimetengwa na zile za wanaume.
- ◎ Hakikisha kuwa sehemu za vyoo zina mwanga wa kutosha, hususani vinjia vya kwendea vyoo vya wanawake.
 - ◎ Hakikisha kuwa milango ya bafu za wanawake ni imara na inafungika vizuri ili kuwahakikishia faragha wanawake na wasichana wanapotumia bafu hizo.
 - ◎ Wahimize wanawake kupigania usawa katika uongozi wa kambi na mifumo ya kufanya maamuzi.
 - ◎ Fanya mipango ya kulitumia jeshi la polisi kusimamia ulinzi na usalama kambini na hakikisha kuwa polisi wanapatiwa mafunzo ya mara kwa mara yatakayowawezesha kuwa wadau thabiti katika uziaji wa manyanyaso kupitia unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
 - ◎ Hakikisha kwamba uwakilishi wa shirika la UNHCR na/au AZISE unakuwepo kambini mara kwa mara.
 - ◎ Hakikisha kuwa wakimbizi wote wamesajiliwa.
 - ◎ Jitahidi kuzishinikiza serikali husika kutoa nyaraka za utambulisho kwa wakimbizi
 - ◎ Elewa misimamo ya raia wazalendo kuhusu wakimbizi. Baadhi ya raia wa nchi mwenyeji wanaweza kufikiri kuwa wakimbizi wanapendelewa kwa vile wanapatiwa misaada. Fikira kama hii inaweza kuzaa chuki mionganoni mwa wazalendo dhidi ya wakimbizi.

MKAKATI:

Sajili Wakimbizi Wote

Kama wanaume ambaa ni wakuu wa kaya natio waliosajiliwa peke yao na kupewa kadi za kugawiwa bidhaa, wanawake wanaweza kukabiliwa na tatizo la kuishi daima katika mahusiano na mazingira ya kunyanyaswa kwa hofu ya kupoteza fursa ya kupatiwachakulanamisaadamingine. Kwahiyonijambomuhimu kumsajili kila mkimbizi kipekee na kumpatia kila mtu kitambulisho chake. Kama haiwezekani kumpatia kila mwanafamilia nyaraka za usajili wa peke yake, basi inashauriwa kwamba wanawake ambaa ni watu wazima wapewe kipaumbele katika kupatiwa nyaraka za kuthibitisha uhalali wa kupatiwa misaada.

Rejea pia:

- **Hitimisho la UNHCR EXCOM kuhusu Usajili wa Wakimbizi na Watu wanaotafuta hifadhi ya ukimbizi Na 91. (LII) (UNHCR 2001)**
- **Kiongozi cha Dharura—Toleo la Pili (UNHCR 2000)**
- **Kanuni kuhusu Uhifadhi wa Wanawake Wakimbizi (UNHCR 1991)**

MKAKATI:

Waeleweshe Wakimbizi Kuhusu Haki, Stahiki na Mafao yao

Wakimbizi wanastahili kuelewa haki zao, mafao na majukumu yao pia. Kwa kutumia mikutano ya kijamii na/au maandiko, waelimishe wakimbizi kuhusu mambo yafuatayo:

- ◎ Huduma, mafao na haki ambazo kila mkimbizi anastahili kupewa.
- ◎ Jinsi ya kufikia na/au kuwasilisha misaada na huduma, na kanuni zinazotawala upatikanaji na ushiriki wa misaada hiyo.
- ◎ Mifumo ya utoaji taarifa, na vituo vya kutolea ushauri na maoni vilivyopo kwa matumizi ya watu ambaa wamenyanyaswa kupitia unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Sheria za kitaifa zinazolinda haki ambazo zimeidhinishwa chini ya sheria ya kimataifa ya haki za binadamu pamoja na katiba ya nchi ambamo wakimbizi wanaishi.
- ◎ Taratibu za kisheria na mifumo ya kiutawala inayotumika kwa ajili ya kuripoti malalamiko kuhusu matukio ya manyanyaso kupitia unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Watendaji wanaohusika na utoaji wa misaada na huduma, dhima na majukumu yao kwa jamii na mipango ya programu za baadaye.
- ◎ Wawakilishi wa serikali Mashirika ya misaada ya kibinadamu, haki za binadamu na makundi ya wanawake, na vyama vya kiraia vinavyofanya kazi katika eneo husika.
- ◎ Sera za shirika la UNHCR zinazotumika na miongozo ambayo inaimarisha ulinzi wa wanawake na watoto dhidi ya unyanyasaji kupitia unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Hakikisha kwamba taarifa hizi zinasambazwa kwa wakimbizi wote: wanaume, wanawake, vijana na watoto, waliosoma na ambaa hawakusoma kwa kutumia lugha ambayo inaeleweka kwa kila kundi na kwa kupitia njia ambazo zitaufikisha kirahisi kwa makundi mbalimbali ya walengwa kama vile mikutano ya kamati za wanawake, kamati za vijana, n.k.

MKAKATI:

Ishirikishe Jamii katika Kupanga, Kuanda na Kutekeleza Majukumu

Programu za kuzuia unyanyasaji wa kingono na kijinsia zitafanikiwa vizuri zaidi iwapo tu maandalizi yake yataishirikisha kikamilifu jamii ya wakimbizi katika kila hatua ya mchakato huo, kuanzia hatua ya kubaini tatizo na kulijadili, hadi kufikia hatua

ya ufuatiliaji na upimaji wa ufanisi wa mikakati ilioandaliwa kwa ajili ya kuzuia unyanyasaji wa aina hiyo. Jamii ndiyo yenyewe uwezo mkubwa wa : kubaini vyanzo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, kushauri njia bora za kusambaza taarifa kuhusu tatizo, na kujua ni hatua gani zinazofaa kuchukuliwa kwa ajili ya kukomesha tatizo.

- ◎ Hakikisha unawashirikisha viongozi wa wakimbizi—wanaume kwa wanawake, watu maarufu na wenye ushawishi katika jamii ya wakimbizi, kwa mfano, wazee, viongozi wa kidini na wakimbizi wengine wenye hamu ya kushiriki. Watu hawa wote washirikishwe katika mikutano ya awali kabisa baada ya kujitokeza kwa dharura.
- ◎ Wasikilize wakimbizi. Wape nafasi ya kujieleza kuhusu mahitaji na mashaka yao, hata kama hatua hii itakulazimu kuandaa majadiliano tofauti kwa ajili ya makundi tofauti ya wakimbizi. Inawezekana wanawake wakashindwa kujieleza ipasavyo mbele ya wanaume; na vijana wanaweza kuona ugumu wa kujieleza ipasavyo mbele ya watu wazima.
- ◎ Heshimu na jitahidi kutumia mapendekezo ya wakimbizi katika masuala yafuatayo:
- ◎ kuandaa mpangilio wa kambi.
- ◎ kugawa nyumba.
- ◎ kugawa vyakula na vifaa vingine.
- ◎ kuandaa hatua mahususi kwa ajili ya kuzuia unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ kuunda mifumo ya kutoa taarifa na kukata rufaa.

Maisha ya kambini aghalabu huwasababishia wakimbizi uchovu na fadhaa. Kwa hiyo kuna haja ya kuwashirikisha wakimbizi katika kuandaa mambo ya kujishughulisha nayo kwa ajili ya kutumia nguvu zao vizuri, kwa mfano, shughuli za michezo na burudani. Aidha kanuni zinazotawala uendeshaji wa vilabu vya pombe, nyumba za mapumziko na shughuli nyingine za aina hii zizingatie umuhimu wa kupunguza hali za kuchochea matatizo. Shirikiana na mamlaka ya mahali husika ili kuchukua hatua za kuzuia udhalimu unaosababishwa na ulevi wa pombe. Andaa kampeni za mafunzo kuhusu jinsi matumizi mabaya ya pombe yanavyoweza kusababisha udhalimu wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Inawezekana ukahitaji kurekebisha mikakati ili kuboresha ufanisi wake ikitumika kwa wakimbizi ambao wamerejea nchini mwao au wakazi wa maeneo ya mijini. Kinyume na wakimbizi wanaoishi ndani ya kambi zenyne mipaka yake, wale waliorejea nchini mwao aghalabu hutawanyika ndani ya jamii. Ili kuhakikisha kuwa watu hawa wana ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa kupitia vitendo vya kingono na kijinsia mambo yafuatayo sharti yazingatiwe:

- Hamasisha wanawake waliorudi nchini mwao kutoka ukimbizini pamoja na wale wanaoishi mijini kuunda vyama na mitandao mingine ambayo inaweza kuchangia harakati za kuzuia udhalimu.
- Walengwa wa programu za kuzuia unyanyasaji wa kingono na kijinsia wasiishie kwenye wanawake wanaorudi nchini mwao bali pia wajumuishwe viongozi na wawakilishi ya jamii ya wakazi wa maeneo ambako waliorudi kutoka ukimbizini wanaishi.
- Andaa mafunzo kwa ajili ya kuhamasisha na kuinua uelewa kuhusu haki ya kuzuia unyanyasaji wa kingono na kijinsia ili kuimarisha uwezo wa vikundi na vyama vinavyofanya kazi katika maeneo ya waliorudi nchini mwao kutoka ukimbizini.

MKAKATI:

Unda Mifumo ya Ugavi yenyne Uwiano wa Kijinsia

Mifumo ya ugawaji wa vyakula na vifaa vingine iandaliwe kwa uangalifu mkubwa ili kuzuia vitendo vya ufisadi, ufujaji na unyonyaji. Kila mbinu iliyopo itumike kuwaelimisha wakimbizi, hususani wanawake na watoto, kuhusu haki zao. Wanawake na wanaume wanapochangia ukuu wa kaya zao inakuwa rahisi kushirikiana katika kupata na kudhibiti rasilimali, kuhakikisha kuwa wanafamilia wote wanafaidika na rasilimali hizo kwa viwango sawa, na hali hii inapunguza mikwaruzano na misigano ya kijinsia na kuwaimarishia wanawake uwezo. Aidha hali hii inasaidia kupunguza unyanyasaji wa majumbani. Ikiwezekana jaribu kuwapatia wanawake kadi zao za posho. Wanawake wanapaswa kuhimizwa kubeba wajibu mkubwa katika masuala ya usimamizi, ugavi na ufuutiliaji wa misaada. Hii itasaidia katika kuhakikisha kwamba wanafamilia wote wanafaidika na posho za vyakula vinavyotolewa, na inaweza kuchangia kuzuia vitendo vya unyonyaji ambavyo wanawake hufanyiwa kwa kulazimishwa kufanya ngono ili wapatiwe vyakula. Wakati wa mgawo hakikisha kuwa wawakilishi wa kike wanalingana na wale wa kiume. Kamati za wanawake wakimbizi zinapaswa kushiriki katika kufuutilia zoezi la migawo na shughuli zinazofuatia baadaye. Watumishi wanaotoa misaada lakini ambao si wakimbizi wanapaswa kuwepo katika maeneo ya kugawia bidhaa ili kufuutilia taaratibu za migawo.

MKAKATI:

Tekeleza Programu za Afya ya Uzazi

Hatua nyingi zinazotekelze wa na sekta ya afya kwa ajilia kupambana unyanyasaji wa kingono na kijinsia zitaelekeza msisitizo wake kwenye kushughulikia unyanyasaji na kuwasaidia waathiriwa auwanusurika. Lakinisektaya afyainawezakuchangia katika kuzuia udhalimu unaofanywa kuitia unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa kufanya mambo yafuatayo:

Kuwachujawagonjwa kwakubainishawale ambaowanakabiliwa na hatari ya kujikuta katika unyanyasaji wa kingono na kijinsia na kuepusha hofu na madhara zaidi kwa waathiriwa/wanusurika.

Utekelezaji wa shughuli za afya ya uzazi, ikiwa ni pamoja na majadiliano kuhusu jinsia, mahusiano, pamoja na unyanyasaji wa kingono na kijinsia ambayo huwalenga wanaume na vijana pamoja na wanawake (kazi ya kutoa uelewa sahihi kuhusu uzuiaji wa UVV/UKIMWI nayo ijumuishwe katika juhudii hizi).

Ushirikishaji wa wakunga wa jadi kama wadau katika masuala ya afya ya uzazi. Wakunga na wasaidizi wa jadi katika afya ya uzazi wanaweza kuwa vyanzo vya taarifa muhimu na vyombo murua vya kusambazia taarifa kuhusu hatua za kufanikisha uzuiaji na ulinzi katika eneo hili.

Rejea pia:

- **Kiongozi cha Ugani na mbalimbali kuhusu Afya ya Uzazi katika Kambi za Wakimbizi (Inter-Agency 1999)**

MKAKATI:

Tekeleza Programu za Ulinzi na Usalama

Usalama unagusa ngazi mbali mbali za jamii: nyumbani, kambi za wakimbizi, jamii mahalia, na mazingira ya kitaifa. Kimsingi jukumu muhimu la kusimamia usalama wa wakimbizi linapaswa kubebwa na serikali ya nchi mwenyeji. Lakini katika mazingira ambapo serikali imeshindwa kutokana na sababu mbalimbali kama vile kukosa uwezo udhaifu, watu watoao misaada ya kibinadamu aghalabu huingilia katiili kusimamia ulinzi na usalama wa wakimbizi. Ili kufanikisha ulinzi na usalama wa wakimbizi zingatia mambo yafuatayo:

- ◎ Wawezeshe viongozi wa jamii—wa kike na wa kiume—pamoja na mitandao ya ulinzi ambayo inasimamiwa na wakimbizi wenye ndani ya kambi zao.

- ◎ Hamasisha na uongeze uwezo wa jeshi la polisi mahalia ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa uhakika.
- ◎ Unda mpangilio wa kambi ambao unawapunguzia wanawake hatari za kushambuliwa.
- ◎ Ajiri wanawake kadhaa ili wafanye kazi na jeshi la polisi au vyombo vingine vinavyohusika na usimamizi wa sheria na ambavyo viko jirani na kambi.
- ◎ Hakikisha ulinzi na usalama wa wanawake wanapokwenda kutafuta kuni, kuchota maji, kufanya biashara au kufanya shughuli nyingine za uzalishaji mali.
- ◎ Unda vikundi nya ulinzi wa jamii, kwa kuteua wajumbe wake kutoka katika jamii yenyewe, na uhakikishe kuwa wanawake wanashirikishwa kwa idadi inayofaa.
- ◎ Shirikisha watendaji wengine na jamii kwa jumla kuchambua data za matukio na kujadili hali zinazohatarisha usalama na masuala mengine.
- ◎ Tatua matatizo yaliyobainishwa kwa kutumia njia mbalimbali, mathalani, kujenga uzio, kuboresha taa, kutumia radio, n.k.
- ◎ Shirikiana na wakimbizi ili kuzuia hatari zaidi kwa waathiriwa/wanusurika kwa kubuni mipango mara moja ya kuwalinda wanusurika baada ya tukio (k.m. kwa kuwahamisha, kutenga eneo lenye ulinzi maalumu kambini, kutenga nyumba kadhaa ambazo usalama wake ni imara zaidi n.k.).
- ◎ Hakikisha uwepo wa ulinzi wa doria katika maeneo ya hatari zaidi.
- ◎ Amua kama kuna haja ya kuwahamisha wahalifu ili kuimarisha na kuhakikisha usalama wa waathiriwa/wanusurika na kuzuia marudio ya uhalifu.

Rejea pia:

- **Kuzuia na Kukabiliana na Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia katika Mazingira ya Wakimbizi: Chapisho la Makala za Warsha ya mafunzo Toka kwa Mashirika Mbalimbali (UNHCR 2001)**
- **Kanuni kuhusu Uhifadhi na Usalama wa Wanawake Wakimbizi (UNHCR 1991)**

MKAKATI:

Kuwa Makini kwa Hisia za Wenyiji

Wenyiji wengi katika maeneo ya wakimbizi huishi maisha ya umaskini na kwa sababu hiyo wanaweza kujenga chuki dhidi ya wakimbizi ambao ama ni majirani au wanaishi nao kutokana na misaada na huduma wanazopewa. Andaa majadiliano na wakazi hao kuhusu wakimbizi—kwa madhumuni ya kuzuia mivutano baina ya makundi haya mawili. Kila inapowezekana wenyiji wajumuishwe pia katika programu na huduma zinazotolewa. Huduma za afya ndizo zinazofaa zaidi kuwahuishwa wenyiji na ndizo zinazothaminiwa zaidi.

MKAKATI:**Bainisha na Ingiza Maswala yote ya Kijinsia katika Hatua zote za Maandalizi na Utekelezaji wa Programu**

Watendaji wote wanaotoa misaada ya kibinadamu, yakiwemo mashirika ya Umoja wa Mataifa, AZISE, serikali za nchi wenyeji, na wadau wengine wanapaswa kuzingatia uchambuzi wa kijinsia wakati wa kuandaa programu zao. Programu zote lazima zitilie maanani masuala ya kijinsia kwa kuzingatia mahitaji ya wanawake na wanaume. Watumishi wa shirika la UNHCR sharti wahakikishe kuwa Mipango ya Utekelezaji Kitaifa inaanishi mtiririko wa vipaumbele vya ofisi husika kwa vigezo vya kijinsia na umri.

Mashirika ya kimataifa na yale yasiyo ya serikali lazima yaongeze jitihada za kufikia fursa sawa kijinsia (jinsia mbili zichangie watumishi kwa asilimia hamsini kila moja) kwa ngazi za viongozi waandalizi na katika utendaji wa shughuli za uwandani. Hali hii itasaidia kuhakikisha kuwa masuala ya kijinsia yanapewa uzito unaostahili katika maandalizi ya programu.

Rejea pia:

- **Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Azimio la Kurasimisha Jinsia (A/52/31997)**

Kushawishi Mfumo Rasmi na usio Rasmi wa Kisheria

Wakati mwingine ukubwa wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia ndani ya jamii unachochewa na sheria zinazosimamia udhalimu wa aina hii au kiwango cha uzingatiaji wa sheria katika nchi mwenyeji na ile wanakotoka wakimbizi. Makosa ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia hutendwa bila hofu iwapo:

- ◎ Sheria na sera zinaunga mkono ubaguzi wa kijinsia na kufumbia macho unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Haki za wanawake hazina utetezi wa kutosha kisheria.
- ◎ Hakuna sheria dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Matumizi mabaya ya sheria yamesababisha kutoweuka kwa imani mionganini mwa vyombo vya kusimamia sheria.
- ◎ Usimamizi wa sheria na uendeshaji wa mashtaka vinachochea vitendo vya upendeleo kijinsia.

Hatua ya kwanza unayopaswa kuchukua ni kujelimisha kuhusu mifumo ya sheria rasmi, sheria za kimila na za kijadi katika nchi

mwenyeji na nchi wanakotoka wakimbizi. Angalia kama kuna sheria ambazo zinapiga vita vitendo vya ubaguzi wa kijinsia na unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Tafakari jinsi sheria hizo zinavyoweza kuimariswa. Shirikiana na asasi zinazojihusisha na haki za binadamu pamoja na haki za wanawake katika nchi husika.

MKAKATI:

Shirikiana na Mifumo ya Sheria za Kijadi

Mifumo ya sheria za kijadi au kimila, ambazo kwa kawaida husimamiwa na wazee, hutumika katika jamii nyingi za wakimbizi. Kanuni, mienendo na maamuzi ya makundi haya huakisi maadili, imani na mitazamo. Makundi haya yanaweza kutoa hukumu katika kesi zinazohusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia, ikiwa ni pamoja na yale yanayotokea majumbani. Iwapo mahakama au kamati za aina hii zimetoa hukumu ambazo zinakinzana na matakwa ya kimataifa ya haki za binadamu kuhusu haki za waathiriwa, inakubidi uchukue hatua za kuwaelimisha wajumbe wa vyombo hivyo kuhusu viwango vya kimataifa vinavyotumika kuhusiana na haki za binadamu.

Andaa programu za kampeni na mafunzo kuhusu haki za binadamu na masuala ya kijinsia kwa ajili ya kuwaelimisha wahusika wa makundi haya. Waonyeshe kuwa uzingatiaji wa haki za binadamu kwa kila mtu na uzuiaji wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni mambo yenye manufaa kwa jamii nzima. Kwa vile wazee wanaosimamia haki kuititia mifumo hii wana mamlaka makubwa ndani ya jamii, misimamo yao itakuwa na ushawishi mkubwa kwa watu wengine. Himiza ushiriki wa wanawake na vijana katika mifumo hii ya kijadi. Wajumbe wa vyombo vya kijadi vya kusimamia haki wahimizwe kutoa taarifa katika mfumo wa sheria rasmi kuhusu vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia pale ambapo matukio kama hayo yanachukuliwa kuwa ni makosa ya jinai.

MKAKATI:

Shirikiana na Mfumo wa Taifa wa Kutetea Haki

Jenga mahusiano na mahakimu mahalia, majaji na mahakama. Toa mafunzo kuhusu sheria ya kimataifa inayotawala haki za binadamu. Waalike maafisa wa idara ya mahakama na watetezi wa haki za kiraia ili wajadili suala la ulinzi wa haki za binadamu chini ya sheria za kitaifa, pamoja na mwenendo wa kesi za jinai na michakato ya kiraia kuhusiana na makosa ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Katika nchi ambako kuna uhaba wa

rasilimali, jenga mitandao na majaji, waendesha mashtaka na jeshi la polisi ili kuhakikisha kwamba sheria za nchi zinafuatwa.

Kama mahakama hazifiki kwa urahisi, pengine kutokana na kuwa katika sehemu zilizo mbali na zilizojitenga, fikiria kutumia mahakama zitembeazo kwa ufadhilli wa UNHCR au mashirika mengine. Katika sehemu kadhaa matumizi ya mahakama za aina hii yamefanikisha kuongezeka kwa taarifa kuhusu vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Aidha mfumo huu umesaidia kuongeza idadi ya wahalifu wanaopatikana na hatia na papo hapo kuimarisha uelewa wa mfumo wa sheria ndani ya jamii husika.

MKAKATI:

Imarisha Sheria na Sera za Kitaifa Zinazolinda Haki za Binadamu

Shirikiana asasi za kitaifa zinazojishughulisha na masuala ya haki za binadamu, mathalani, vikundi vya wanasheria wanawake na jumuiya za kiraia, kwa ajili ya kupigania uboreshaji wa sheria na sera za nchi mwenyeji dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Mfumo wa sheria unaokataza makosa ambayo yanahusiana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia unasaidia sana katika ujenzi wa mkakati thabiti wa uzuiaji wa uonevu huu.

Shirikiana na asasi zinazojihusisha na masuala ya marekebisho ya sheria zinazoshughulikia tatizo la unyanyasaji wa kingono na kijinsia na uvunjaji wa haki za wakimbizi. Hakikisha kuwa sheria, mienendo na sera za nchi husika haziwabagui wakimbizi.

Kwa ushirikiano wa mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa pamoja na vikundi vya jumuiya za kiraia, lihimize taifa ambalo ni mwenyeji wa wakimbizi kukubali na kuridhia mikataba na makubaliano yote ya kimataifa kuhusu haki za binadamu.

Rejea pia:

- **Uhifadhi wa Wakimbizi : Mwongozo wa Ugani kwa ajili ya AZISE (UNHCR 1999)**

MKAKATI:

Weka Adhabu Kali kwa Wahalifu

Adhabu kali kwa wahalifu wanaofanya makosa ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia zinaweza kusaidia kuzuia au kupunguza uhalifu huu. Wakimbizi wanaotenda makosa haya wanapaswa

kutendewa kama wanavyotendewa raia wa nchi husika: kwa maana ya kutendewa haki mahakamani ikiwa ni pamoja na kutolewa kwa adhabu. Lakini kwa kawaida adhabu itolewayo kwa watendaji wa makosa ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia sharti izingatie kanuni ya msingi ambayo inakataza kurejesha mhalifu nchini mwake kwa nguvu.

Kila inapowezekana adhabu zitolewazo zijumuushe mipango ya kurekebisha tabia za wahalifu. Hili linaweza kutendeka kuititia njia mbali mbali, kwa mfano, elimu/ueleweshaji wa wahusika kuhusu masuala ya haki za binadamu na jinsia pamoja na fidia kwa waathiriwa wa uonevu.

Ufuatiliaji na Uwekaji Kumbukumbu za Matukio ya Vitendo vya Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia

Ili uweze kujenga hatua madhubuti za kufanikisha uzuaji wa udhalimu huu, sharti uwe na picha na uelewa kamili wa mazingira mahususi. Ufuatiliaji wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni jukumu la wahusika/watendaji wote wa maeneo yafuatayo: afya, hifadhi, sehemu zinazoshughulikia hali ya kisaikolojia na kijamii pamoja na jamii nzima ya wakimbizi. (Angalia Sura ya 7 kwa ufanuzi zaidi kuhusu masuala ya ufuatiliaji na tathmini). Katika hatua za mwanzo za kuandaa mipango hakikisha kuwa unatenga kiasi cha kutosha cha pesa na rasilimali-watu kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini.

Kitengo kimoja kikuu ndicho kinachopaswa kubeba jukumu la kukusanya na kuchambua data zinazohusiana na matukio ya vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia kila mwezi. Maafisa wa hifadhi wahakikishe kuwa data kuhusiana na vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu zinahifadhiwa kama zinavyohifadhia data za matukio ya uvunjaji wa haki nyingine.

Ili kuhakikisha usahihi na manufaa ya taarifa zinazokusanywa, unashuriwa kuandaa mkuano wa watendaji wote kwa ajili ya kufafanua masharti (kuhakikisha kuwa watendaji wanatumia alama zinazofanana kwa tukio linalotambulishwa kwa jina moja) na kukubaliana juu ya njia za kuhesabu matukio. Taarifa zinazokusanywa zinapaswa kujumuisha mambo husika yakiwemo haya yafuatayo: aina ya tukio, mahali pa tukio, habari za kidemografie kuhusu mhalifu na mwathiriwa/mnusurika, na mambo yanayoweza kusababisha hatari. Ripoti za kila mwezi zinapaswa kujibu maswali yafuatayo:

- Nini kilichotokea mwezi huu?
- Ni mkakati gani wa uzuiaji ulifanikiwa? Ni upi ambao haukufanikiwa? Kwa nini?
- Je, kulingana na ripoti ya mwezi ni jambo gani linalostahili kufanyika sasa?

Wadau wote wakubaliane kuhusu njia na mifumo ya kutolea taarifa, namna ya kuzisambaza na watu wanaostahili kupewa taarifa hizo (Angalia Kiambatisho 2 kwa ajili ya mfano halisi wa Fomu ya Kutolea Ripoti ya Tukio).

Itisha mikutano inayoshirikisha watendaji kutoka sekta mbalimbali, wakiwemo wakimbizi wenyewe, kwa ajili ya kupitia data. Tumia mikutano hii kubainisha mambo ambayo yanaweza kuchangia utokeaji wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia na ubuni mipango ya kutockomeza mambo hayo (angalia Sura 6 kwa maelezo zaidi).

Ufutiliaji makini wa matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia utakuwezesha kupima ufanisi wa mikakati ya uzuiaji wa uonevu huu, kuimarisha uzoefu, kueneza mbinu za harakati na kukusanya data ambazo ni sahihi na nyooofu kwa ajili ya kufutilia mielekeo na kufanya chambuzi za kulinganisha.

Rejea pia:

- **Jinsi ya Kuongoza : Ufutiliaji na Upimaji wa Programu za Kukabiliana na Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia, Tanzania (UNHCR 2000)**

Mambo Muhimu ya Kukumbuka

Kama unajaribu kushawishi mabadiliko katika maarifa, mitazamo na tabia kijamii na kiutamaduni:

- ◎ Endesha kampeni za habari, elimu na mawasiliano.
- ◎ Teua watu wa kufanya kazi za kujitolea katika jamii.
- ◎ Hakikisha kwamba kuna uwiano wa kijinsia katika mfumo wa uongozi na utaratibu wa kufanya maamuzi
- ◎ Wawezeshe wanawake.
- ◎ Washirikishe wanaume.
- ◎ Washirikishe watoto na vijana pia.

Mifumo mihili ya familia na/au jamii inaposambaratika:

- ◎ Unda programu kwa ajili ya shughuli za kijamii na burudani.
- ◎ Shirikiana na viongozi wa kidini na jamii kwa jumla ili kufufua maadili ya kijamii ambayo yanahimiza haki sawa na heshima kwa wanajamii wote

Kama unajaribu kubadili misimamo na tabia za watu walio madarakani:

- ◎ Kuwa na msimamo usioonyesha hali ya kukinzana au kuegemea na kuhukumu upande wowote.
- ◎ Toa mafunzo ya kupanua uelewa wa masuala ya jinsia na haki za binadamu.
- ◎ Jenga mifumo ya uwajibikaji, inayojumuisha utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya kazi.

Wakati wa maandalizi ya huduma na viwezeshaji kwa ajili ya wakimbizi:

- ◎ Hakikisha kuwa watoaji huduma za msingi wanashirikishwa, yaani, ulinzi, huduma za jamii, afya, usalama, jeshi la polisi na mamlaka nyingine husika pamoja na wakimbizi wenyewe.
- ◎ Kila mkimbizi ambaye ni mtu mzima (mwanamume na mwanamke) apewe kadi ya usajili.
- ◎ Waelimishe wakimbizi kuhusu haki zao, marupurupu na mafao mengine.
- ◎ Ishirikishe jamii katika upangaji, uandaaji na utekelezaji wa shughuli za kambini.
- ◎ Jenga mifumo ya ugavi ambayo ina uwiano wa kijinsia.
- ◎ Tekeleza programu za afya ya uzazi.
- ◎ Kuwa makini na hisia za wenyeji wa wakimbizi.
- ◎ Bainisha na ingiza masuala ya jinsia katika hatua zote za upangaji na utekelezaji wa programu.

Kama unajaribu kushawishi mifumo ya sheria rasmi na zile za kijadi:

- ◎ Jielimishe kuhusu mifumo ya sheria rasmi na zile za kijadi katika nchi mwenyeji na ile wanakotoka wakimbizi.
- ◎ Shirikiana na wasimamizi wa mifumo ya sheria za kijadi ili kuhamasisha mabadiliko.
- ◎ Shirikiana na watumishi wa idara inayosimamia sheria na masuala ya haki nchini ili uimarishe imani ya wakimbizi katika mfumo wa sheria.
- ◎ Imarisha sheria na sera za kitaifa zinazolinda haki za binadamu.

Wakati wa kufuatilia matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia:

- ◎ Kusanya na chambua data za matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia kila mwezi.
- ◎ Fafanua masharti na teua njia ambazo zinapaswa kutumiwa na watendaji wote katika kuhesabu matukio ya vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Kubaliana na wadau wote kuhusu njia na mifumo itakayotumika katika utoaji wa taarifa.
- ◎ Itisha mikutano ya sekta mbalimbali, ikijumuisha wakimbizi, kwa ajili ya kupitia data.

SURA YA 4

KUKABILIANA NA UNYANYASAJI WA KINGONO NA KIJINSIA

Ili kuandaa programu madhubuti kwa ajili ya kuwasaidia waathiriwa/wanusurika wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia, ni lazima kuelewa athari na matokeo ya uovu huo. Athari hizo zinaweza kutofautiana kulingana na aina ya kitendo cha ukatili kilichotendwa.

Kila mtu katika jamii ya wakimbizi anapaswa kufahamu jinsi na mahali pa kuripoti matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Kwa maana kama mwathiriwa/mnusurika hakutoa taarifa kuhusu uovu uliomsibu hawezu kupewa usaidizi unaofaa. Jamii inapaswa kuwa msitari wa mbele katika jithada za kuwasaidia waathiriwa/wanusurika. Hatua za mwitikio zinajumuisha mambo haya: kuanzisha shughuli za elimu na uhamasishaji wa jamii dhidi ya maovu haya; kutoa mafunzo kwa watendaji kuhusu mbinu za kukabiliana na mahitaji ya waathiriwa/wanusurika; kujenga mifumo ifaayo kwa ajili ya kufanikisha masuala ya kukata rufaa, kutoa taarifa, kufuatilia na kutathmini; kuziwezesha jamii za wakimbizi kupambana dhidi ya maovu haya; kujenga njia ya kushughulikia mahitaji ya kiafya/matibabu kwa ajili ya waathiriwa/wanusurika; kujenga mpango wa kukidhi mahitaji ya kisaikolojia na kijamii ya waathiriwa/wanusurika; kujenga njia ya kushughulikia masuala ya ulinzi na usalama; kukabiliana na maovu haya kisheria/haki; kubainisha majukumu ya watendaji wengine; na hatimaye kuandaa utaratibu wa namna ya kuwashirikisha wahalifu. Kanuni elekezi kuhusu usiri, usalama wa kimwili na umuhimu wa kuheshimu matakwa, haki na hadhi za wanusurika, zinapaswa kuzingatiwa katika shughuli zote.

Ni jambo muhimu kubaini na kuelewa athari za aina mbali mbali za unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa vile ni kwa njia hii peke yake utaweza kujenga mbinu sahihi za makabiliano. (Angalia Sura 1 ili kujikumbusha orodha ya athari na matokeo ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia). Athari hizi zinaweza kuwekwa katika mafungu makuu manne: afya; hali ya kisaikolojia-kijamii; usalama/ulinzi; na masuala ya kisheria/haki. Kwa hiyo miitikio na makabiliano dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia sharti vielekeze msisitizo na nguvu zake zote kwenye maeneo haya manne.

Ili kukabiliana na mahitaji ya waathiriwa /wanusurika wa unyanyasaji wa kijinsi na kijinsia, ni lazima uelewa ATHARI za udhalimu wa aina hii.

Muhtasari wa baadhi ya athari kubwa za unyanyasaji wa kingono na kijinsia

KIAFYA	KIHISIA/KISAICO - LOJIA/KIJAMII
<ul style="list-style-type: none"> • Majeraha, ulemavu, kifo • Magonjwa ya zinaa na UKIMWI • Matatizo ya afya ya uzazi • Mimba zenye matatizo, shida wakati wa kujifungua • Kuharibu mimba • Mimba zisizotakikana • Njia hatari za utoaji mimba • Mfadhaiko kama ugonjwa sugu • Mshtuko • Ambukizo, maambukizo sugu • Kuvuja damu kwa wingi 	<ul style="list-style-type: none"> • Hasira, hofu, uchungu, Kujichukia • Aibu, ukosefu wa usalama, Kupoteza hadhi katika familia na jamii • Mfadhaiko • Matatizo ya kukosa hamu ya kula na kulala usingizi • Magonjwa ya akili • Kutengwa na jamii • Kujiua • Kumlaumu mwathiriwa • Kumtenga/kumkataa Mwathiriwa • Ugumu wa upatikanaji wa rasilimali na misaada kwa jamii

KISHERIA/KIULINZI	KIUSALAMA/MAZINGIRA YA JAMII
<ul style="list-style-type: none"> • Mzigo zaidi kwa jeshi la polisi na mahakama ambavyo tayari vimeelemewa • Matumizi ya sheria zisizofaa katika kushughulikia aina mbali mbali za vitendo vya unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia yanaweza udhoofisha ulinzi wa kisheria kwa waathiriwa/wanusurika; ukosefu wa utaratibu wa kuwaadhibu wahalifu • Hatua za kisheria zisizofaa Ambazo zinaweza Kumuumiza zaidi mwathiriwa au mnusurika, mathalani, kumlazimisha kuoana na mhalifu wake • Utoaji taarifa usioridhisha Kutokana na kutokuwa na Imani katika mfumo mbaya wa sheria na utoaji haki • Ongezeko la marudio ya uonevu dhidi ya mwathiriwa mnusurika yuleyule au wanawake au wasichana wengine katika jamii 	<ul style="list-style-type: none"> • Mwathiriwa/mnusurika hujisikia kwamba hana usalama, anatishiwa na anaogopa • Hali ya woga na ukosefu wa Usalama ama kwa jamii nzima au mionganini mwa wanawake peke yao • Jamii inaweza kujihisi vibaya au kutojitosheleza iwapo itashindwa kuunda vikosi vya kuzuia vitendo vya unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia • Jamii inaweza kujichukulia ‘sheria’ dhidi ya wahalifu. • Unyanyapaa kwa watoaji huduma za jamii na waathiriwa/wanusurika.

Hatua halisi zinazotakiwa kuchukuliwa katika kukabiliana na mahitaji ya waathiriwa/wanusurika wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia zimetolewa katika muhtasari unaofuata. Kama ilivyo kwa mikakati ya uzuijji, hatua hizi huzaa matunda bora zaidi iwapo maandalizi yake yameshirikisha sekta mbali mbali, ukiwemo mchango wa wakimbizi wenye. Wakimbizi au watu watu waliorejea toka ukimbizini wanaposambaa na kuishi katika mazingira ya mijini, hapo watendaji wengi zaidi wanahitajika ili kusimamia vizuri mahitaji yao

Muhtasari wa hatua za kuchukua
<ul style="list-style-type: none"> • Anzisha shughuli za kutoa elimu na kuhamasisha jamii • Toa mafunzo kwa watendaji kuhusu jinsi ya kushughulikia mahitaji ya waathiriwa na wanusurika • Jenga mifumo ya kurufaa utoaji taarifa, ufuatiliaji na Tathmini • Iwezeshe jamii ya wakimbizi katika kuchukua hatua • Jenga mbinu za uchukuaji hatua kuhusu masuala ya kiafya/matibabu ya waathiriwa/wanusurika • Buni jinsi ya kukidhi mahitaji ya kisaikolojia/kijamii ya waathiriwa/wanusurika • Hakikisha ubora wa hatua zinazochukuliwa kuhusu masuala ya ulinzi na usalama • Wezesha uchukuaji wa hatua za kisheria/utoaji haki • Bainisha dhima za watendaji wengine wanaoweza kujitokeza • Jenga mpango wa kukuwezesha kuwashirikisha wahalifu

Kuanzisha Shughuli, Uelimishaji na Uhamasishaji wa Jamii

Anzisha kampeni za umma kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia zinazoakisi masuala nyeti ya kiutamaduni, maadili na mambo maalumi katika mazingira yako.

Kampeni hizi zinaweza kujumuisha mada zifuatazo: jinsi na mahali pa kutafuta msaada kwa mtu ambaye ameshambuliwa kingono umuhimu wa kutoa taarifa za tukio na kuomba msaada haraka iwezekanavyo; sheria za kitaifa na kimataifa zinazokataza unyanyasaji wa kingono na kijinsia; na adhabu zitolewazo kwa makosa yanaohusu mashambulizi ya kimapenzi. Unaweza kutumia njia zifuatazo kusambaza taarifa na ujumbe kuhusu mambo haya: makabrasha; vijarida na mabango; burudani, kwa mfano nyimbo na tamthiliya; hotuba/utoaji mada wakati wa mikutano ya jamii, ibada za kidini, au wakati wa mikusanyiko mingine; matangazo ya radio na vyombo vingine vya habari; na filamu za video.

Kuelimisha watendaji kuhusu jinsi ya kushughulikia mahitaji ya waathiriwa/wanusurika.

Licha ya kuishirikisha jamii katika mijadala kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia na kuwashimiza wanajamii kutoa taarifa kuhusu matukio ya uonevu kama huo, watendaji wote ambao wanabeba wajibu wa kukidhi mahitaji ya waathiriwa/wanusurika wanapaswa kujiweka tayari kwa ajili ya kutoa huduma.

Watumishi wote ambao wanashughulikia matunzo wanapaswa kuwa makini katika masuala ya kijinsia na wapatiwe mafunzo kuhusu masuala hayo. Mafunzo kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia yatoe kipaumbele kwa mambo yafuatayo:

- ◎ Watumishi wa sekta ya afya watoe mitihani ya awali katika masuala ya matibabu na watoe huduma za tiba na ufuatiliaji.
- ◎ Wanasihi katika masuala ya kisaikolojia/kijamii wawe na uwezo wa kutoa ushauri wa kisaikolojia na kijamii pamoja na kushughulikia masuala ya rufaa.
- ◎ Watumishi wa sekta ya usalama wawe na uwezo wa kuwatafutia maeneo salama waathiriwa/wanusurika ambao wamegubikwa na vitisho au hofu.
- ◎ Watumishi wa sekta ya sheria/Hifadhi wawe na uwezo wa kumsaidia mwathiriwa au mnusurika kuchukulia hatua za kisheria dhidi ya mtu aliyemtendea uovu, kama ataamua kufanya hivyo.

Kukitokea hali ambapo mwathiriwa/mnusurika ameripoti tukio lakiniakakosahuduma auikatolewalakinikiwaimecheleweshwa, au akakosa kuonewa huruma na kushughulikiwa kwa faragha, basi katika hali ya namna hii mhusika anaweza kupoteza imani na kusababisha wengine kughairi kutoa taarifa za uonevu.

MCHORO 6.1

Uzito wa tafizo la unyanyasaji wa kijinsi

Shambulizi hatari la kijinsi

Matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa polisi

Matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa katika tafiti

Matukio ya ubakaji ambayo hayakuripotiwa kwa sababu ya kuona au sababu nyingine aibu, kuogopa lawama

Ngono ya kujazimisha katikandoa na midii

Kubakwana mgeni

Ngono isiyopangwa lakin ilivyopangwa kwa kuoneango
humu, kujekwa, vitispo oukulogha iwa

Ngono inayochochewa na hali ngumu ya maisha

Chanzo: World report on violence and health: WHO 2002

Sura ya 1

Sura ya 2

Sura ya 3

Sura ya 4

Sura ya 5

Sura ya 6

Sura ya 7

Sura ya 8

Watendaji wote wakubaliane kutumia mfumo wa aina moja wa kutoa ripoti

Sifa moja muhimu ya mfumo madhubuti wa kutolea ripoti kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni kutumia aina moja tu ya Fomu ya Kutolea Ripoti ya Tukio. Ni jambo bora kuitafsiri fomu hii kulingana na mahitaji halisi na watendaji wote wafundishwe jinsi ya kuitumia. Angalia Sura ya 7 kwa ufanuzi wa kina kuhusu uandaaji wa mfumo wa jumla wa kutolea taarifa na aina ya taarifa kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia zinazostahili kuwekwa katika fomu za Kuripoti Tukio. Rejea Kiambatisho 2 kuhusu mfano halisi wa Fomu ya Kutolea Ripoti ya Tukio. Watendaji wote washirikiane kuunda utaratibu wa kufuatiliaji na kutathmini hatua zilizochukuliwa pamoja na ufanisi wa mifumo ya utoaji taarifa na urufani.

Madhumuni ya kuunda mfumo wa ufuatiliaji ni kuhakikisha kuwa zoezi la uchukuaji hatua linatekelezwa kulingana na jinsi ilivyopangwa. Tathmini huwasaidia watendaji kuweza kubaini utendaji bora, mguso na uthabiti wa hatua zilizochukuliwa, na kutambua kama kuna mahitaji ya mwathiriwa/mnusurika ambayo hayatimizwi. Watendaji wote wanapaswa kushiriki katika uundaji wa mifumo ya ufuatiliaji na tathmini. Angalia Sura ya 7 kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuandaa mifumo bora kwa ajilia ya ufuatiliaji, utoaji taarifa na tathmini.

Mfano wa Mfumo wa Kutoa Ripoti /Kurufaa

Mwathiriwa/Mnusurika anamweleza mtu kuhusu tukio

**Mwelekeze na msindikize mwathiriwa/mnusurika kwenye kituo
cha wanawake au kituo cha afya**

AU mwathiriwa/mnusurika anaamua kujipeleka yeye mwenyewe

Kituo cha Wanawake

Kituo cha Afya

(kituo cha ushauri wa harakaharaka, mpatie mwathiriwa taarifa juu ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia kupitia simu maalumu zilizowekwa makusdi kwa ajili hiyo, au wasiliana na jumuiya zisizo za kiserikali zinazotoa taarifa kwa waathiriwa katika mazingira ya mijini au wasiliana na kituo cha kushughulikia matukio ya dharura)

Kama mwathiriwa/mnusurika anataka kuchukua hatua za kipolisi

AU

Kama mwathiriwa/mnusurika ni mtoto

AU

Kama kuna mazingira yanayohatarisha usalama na ulinzi

- Familia, rafiki au mtumishi humshauri na kumsindikiza wathiriwa/mnusurika hadi kituo cha polisi kuandikisha maeleo, kupatiwa fomu rasmi
- Mwathiriwa/mnusurika hupeleka fomu katika kituo cha afya kwa ajili ya kujazwa
- Mwathiriwa/mnusurika hurejesha fomu katika kituo cha polisi
- Polisi hufanya upelelezi, hukamata wa/mhalifu, na kufungua mashtaka

UFUATILIAJI NA MSAADA VINAWEZA KUJUMUISHA MAMBO YAFUATAYO

(kulingana na uchaguzi wa mwathiriwa/mnusurika)

Huduma za Afya

Msaada wa kisaikolojia na kijamii

Usalama/ Ulinzi

Msaada wa kudai haki

Daima kumbuka kuzingatia kanuni ya utunzaji wa usiri

Kuzipatia kamati za wakimbizi uwezo wa kuchukua hatua

Ni lazima kuishirikisha jamii katika kuandaa programu na utekelezaji endelevu

Imethibitika kuwa programu ambazo zimeandaliwa kwa ushirikiano kati ya watoaji huduma za kibinadamu na kamati za wakimbizi ndizo zenye ufanisi mkubwa mno. Ili kushirikisha jamii fanya mambo yafuatayo:

- Jenga ujuzi na uelewa wa mahusiano ya kijinsia kwa upande mmoja na wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa upande mwingine kupitia kampeni za uhamasishaji.

Kampeni hizi zilenge tabaka zote za jamii: wanaume, wanawake na watoto kutoka makabila yote na dini zote. Wanaume wanaoshiriki katika utoaji wa ushauri nasaha na uhamasishaji wanaweza kushawishi misimamo ya mahakama za kijadi juu ya waathiriwa/wanusurika. Aidha wanaweza pia kusaidia katika ujenzi wa mifumo ya ulinzi iliyojikita kwenye jamii kwa ajili ya kukabiliana na kuzuia vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, na wanaweza kuwasaidia wanaume wengine kuelewa kwamba unyanyasaji kama huu una madhara kwa jamii nzima.

- ◎ Dumisha na imarisha mitandoi iliyopo ya kutolea misaada ya kijamii.
- ◎ Unga mkono dhima ya wanawake kama washiriki sawa katika michakato ya kufanya maamuzi na katika safu za uongozi.

Viongozi wanawake katika jamii wametoa mchango mkubwa kwa kuwahimiza waathiriwa na wanusurika kujitokeza kuomba misaada. Wakipatiwa mafunzo ya uhamasishaji na utoaji wa ushauri nasaha, viongozi wanawake katika jamii huhakikisha kwamba masuala ya kijinsia, ukiwemo unyanyasaji wa kingono na kijinsia, yanajadiliwa na kuchunguzwa.

- ◎ Waathiriwa/wanusurika wahamishiwe mahali ambako ni salama na wapewe msaada wa dharura mara moja.
- ◎ Wasindikize waathiriwa/wanusurika kwenda kutafuta misaada ya kijamii, kiafya na kisheria.
- ◎ Hakikisha usalama wa mwathiriwa/mnusurika, mhalifu, familia zao, na jamii kwa jumla.

Hatuaza mwitikioziwalenge pia wahalifu. Waathiriwa/wanusurika wa mashambulizi ya majumbani aghalabu huamua kuendelea kuishi na wabaya wao kwa sababu za kiuchumi. Kwa hiyo kama mhalifu hakupewa msaada kwa ajili ya kujirekebisha ataendelea kutenda uovu.

- ◎ Ratibu jitihada za jamii pamoja na zile za watendaji wengine kwa lengo la kuimarisha na kuboresha hatua za kuzuia na kukabiliana na vitendo viovu.

- ◎ Pigania ushirikishwaji wa wakimbizi katika kuamua aina za huduma zinazopaswa kutolewa, mahali pa kutolea huduma hizo, watu wa kuzitoa na lugha zinazofaa kutumika.

Ndani ya kambi za wakimbizi misaada inaweza kutolewa katika 'vituo vya muda', vituo vya wanawake, vituo vya jamii au vijana, au mahali pengine ambako waathiriwa/wanusurika wanapendelea kutoa taarifa za tukio lililowasibu. Huduma zitolewe mahali ambapo pana uhakika wa kumtunzia mwathiriwa/mnusurika siri na hadhi yake.

- ◎ Pigania utolewaji wa huduma ambazo zina uzito na umuhimu wa kitamaduni
- ◎ Pigania haki za waathiriwa/wanusurika na haki za wanawake kwa jumla.

Serikali nyingi za nchi wenyeji haziruhusu wakimbizi kujishughulisha na mambo ya kisiasa, kwa mfano, kupigania mabadiliko ya sheria. Hali hii inadhibiti uwezo wa wakimbizi wa kuunda vikundi vya wanawake kwa ajili ya kupigania masuala yao. Ujenzi wa mahusiano na jumuiya zisizo za kiserikali katika nchi mwenyeji ambazo zinaendesha harakati mbali mbali ni njia ambayo inawawezesha wakimbizi kufaidika na harakati hizo pasipo kuvunja sheria za nchi mwenyeji.

Kujenga uwezo wa kukabiliana na mahitaji ya kiafya/kitiba ya waathiriwa/wanusurika

Aina ya ugomvi na muda uliopita kati ya wakati wa tukio mpaka mwathiriwa/mnusurika anapofika kwenye kituo cha afya ni mambo ambayo kwa pamoja yataamua aina ya msaada ambao unaweza kutolewa.

Ni jambo muhimu sana kwa mwathiriwa/mnusurika kufika kwenye kituo cha afya haraka iwezekanavyo mara tu baada ya tukio ili aweze kupatiwa huduma bora iwezekanavyo

Toa huduma kamili ya afya ambayo ni rahisi kupatikana.

- ◎ Uchunguzi wa kiafya na matibabu vitolewe na mtaalamu na hasa wa jinsia moja na mtu anayehitaji kuhudumiwa. Utaratibu mwafaka, vifaa, na dawa bora ni baadhi ya mambo yanayohitajika kwa ajili ya:

- kuzuia magonjwa (magonjwa ya zinaa na mengine)
- kuzuia mimba zisizotakikana
- kutibu majeraha
- kukusanya ushahidi kwa ajili ya mahakama
- kutoa ushauri nasaha na matibabu ya hofu ya kisaikolojia
- kuchunguza wagonjwa wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia

- ◎ Kama ikilazimu, mrufae mhusika kwa ngazi sahihi za kumsaidia na mpatie usafiri wa kufika huko.
- ◎ Toa huduma za ufuatiliaji.
- ◎ Toa ushahidi wa kitiba kwa mtu ambaye ameamua kuchukua hatua za kisheria (ikiwezekana ufanye hivyo mahakamani wakati wa kusikilizwa kwa kesi).
- ◎ Shirikiana na waganga wa jadi katika kubaini, kuripoti, kurufaana kutoa misaada ya awali kwa waathiriwa/wanusurika.
- ◎ Kusanya, weka kumbukumbu na chambua data.
- ◎ Fuatilia kwa makini huduma za afya zinazotolewa, ikiwa ni pamoja na fursa sawa ya upatikanaji wake kwa wanawake, wanaume na vijana. Aidha hakikisha ubora wa huduma hizo.
- ◎ Fuatilia mahitaji ya kiafya ya waathiriwa/wanusurika.
- ◎ Bainisha na unda mikakati kwa ajili ya kukabiliana na mambo yanayochangia hali husika, mathalani, ulevi.
- ◎ Endesha harakati kwa niaba ya waathiriwa/wanusurika.
- kwa ajili ya ulinzi na usalama
- kwa ajili ya mabadiliko ya sheria na sera za nchi mwenyeji ambazo zinakinzana na haki au mahitaji ya waathiriwa/wanusurika
- ◎ Shirikiana na watoaji huduma za afya, waganga wa jadi pamoja na jamii kwa jumla katika kuendesha mafunzo na uhamasishaji.

Rejea pia:

- Usimamizi wa Matibabu ya Wanusurika wa vitendo vya Ubakaji (UNHCR/WHO 2002)
- Kuzuia na Kukabiliana na Unyanyasaji wa kingono na kijinsia katika mazingira ya Wakimbizi: Mafundisho ya asasi changamano Yaliyotokana na Majadiliano ya Mkutano (UNHCR 2001)
- Njia Halisi ya Kukabiliana na Unyanyasaji wa kingono na kijinsia : Programu ya Mwongozo kwa ajili ya Watoaji wa Huduma za afya na Mameneja (UNFPA 2001)
- Kiongozi cha Ugani cha asasi changamano kuhusu Afya ya Uzazi Katika Kambi za Wakimbizi (Inter-Agency 1999)

Kupanga namna ya Kukidhi Mahitaji ya Kisaikolojia na Kijamii ya Waathiriwa/Wanusurika

Baada ya tukio la unyanyasaji wa kingono na kijinsia, mwathiriwa/mnusurika anaweza kukabiliwa na hali mbalimbali za kihisia na kisaikolojia, ikiwa ni pamoja na hofu, aibu, kujilaumu, mfadhaiko na hata hasira. Mhusika anaweza kuchukua hatua za makusudi za kujilinda, mathalani, kujisahaulisha, kujidharau na mfadhaiko mkubwa kutohuna na hofu ya tukio alilonusurika nalo. Aidha

wanafamilia wanaweza kugubikwa na hisia mbalimbali na wakahitaji msaada wakati wa kipindi hicho cha kihoro.

Waathiriwa/wanusurika wahudumiwe kwa huruma na upole.

Shughuli zilizobuniwa na jamii ndizo zenyenye uwezo mkubwa wa kusaidia katika kupooza machungu. Shughuli hizo ni pamoja na

- ◎ Kutambua na kuelimisha watendaji wa kijadi katika jamii kama wasaidizi wa shughuli zilizopangwa.
- ◎ Kuunda vikundi vyatyanawake au vikundi vingine kwa ajili ya kuwasaidia waathiriwa/wanusurika wa unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia pamoja na familia zao.
- ◎ Uanzishaji wa 'vituo vyatyanawake' vitakavyotumika katika kuwahudumia waathiriwa/wanusurika kwa faragha na kwa upendo pamoja na kuwapatia taarifa na ushauri.
- ◎ Zaidi ya hapo, watu wanaoshughulikia masuala ya kisaikolojia na kijamii wanapaswa:
 - kutoa ushauri wa dharura (kwa kusikiliza, kutuliza na kutia moyo) kwa waathiriwa/wanusurika na familia zao pamoja na kuwarufaa wahusika mahali pa kupewa misaada ya muda mrefu ya kuwasaidia kihisia.
 - kuuunga mkono uhuishaji wa tiba za kijadi zinazokubalika au mila za utakasajji ambazo katika nchi ya mkimbizi hutumika na kusaidia katika kupunguza machungu.
 - kubuni matendo ya pamoja kwa ajili ya waathiriwa/wanusurika na wanawake wengine yenye lengo la kujenga mitandao ya kutoa misaada, kuchangamana tena na jamii, kujenga stadi na hali ya kujiamini, pamoja na kuhimiza uvezeshaji wa kiuchumi. Anzisha miradi ya kuzalisha kipato kwa ajili ya kuwasaidia kuhuisha moyo wa kujitegemea.

Rejea pia:

- **Jinsi ya Kuongoza: Mwitikio uliojikita katika Jamii kuhusu vitendo vyatyanayaji wa Kingono vinavyofanywa dhidi ya Wanawake, Ngara, Tanzania (UNHCR 1997)**
- **Afyaya Akili ya Wakimbizi (UNHCR/WHO 1996)**

Kujenga uwezo wa Kukabiliana na Masuala ya Ulinzi na Usalama

Wakati mwingine, baada ya tukio la udhalilishaji huwepo haja ya kumhamishia mwathiriwa/mnusurika katika sehemu yenye salama zaidi. Mwanamke anaweza kushindwa kurudi nyumbani kwake kama mshambuliaji wake ni wanafamilia, jirani au ni mtu kutoka katika jamii yake. Familia na jamii wanapaswa kuwa katika msitari wa mbele katika kuwatafutia waathiriwa/wanusurika sehemu ambazo ni salama.

- ◎ Andaa mikakati na njia mbadala kwa ajili ya ulinzi wa haraka kwawaathiriwa/wanusurika, kwa mfano, uhamisho, kuanzisha eneo maalumu na lenye usalama zaidi ndani ya kambi, na kadhalika. Lakini uendeshaji wa nyumba zenyenye usalama ni jambo la kutumika kama hatua ya mwisho kwa sababu nyumba hizo zikiwa mbali na jamii na chini ya usimamizi wa wadau wengine, hujenga mazingira ambapo wahusika huonekana kama wametengwa jambo ambalo ni mbaya zaidi kwao.
- ◎ Washirikishe wakimbizi wazee katika kuwasaidia waathiriwa/wanusurika.
- ◎ Chambua data zote za matukio na uwafahamishe watendaji wengine pamoja na jamii husika kuhusu hatari za kiusalama pamoja na masuala mengine.
- ◎ Hakikisha kuweko kwa uzingatiaji na usimamizi imara wa sheria. Aidha jitahidi kuzingatia kutendeka kwa haki na kuharakisha mashtaka dhidi ya watuhumiwa.
- ◎ Ishirikishe jamii nzima katika masuala yote ya usalama wa jamii. Hakikisha kuwa wanawake wakimbizi wanashirikishwa katika kazi za kipolisi au vikundi vya ulinzi wa kijadi.
- ◎ Tafakuri njia mbadala kwa ajili ya kumlinda mwathiriwa/mnusurika, ikiwa ni pamoja na kumhamishia katika kambi nyingine au makazi mapya kama ni bora kufanya hivyo.
- ◎ Hakikisha kuwa wanawake ambaa wamepewa mafunzo ya kipolisi wanaunda vikundi vinavyosimamia usalama wa wakimbizi.
- ◎ Wapatie maafisa wa usalama na wale wa jeshi la polisi mafunzo kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Rejea pia:

- **Kuzuia na Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kingono na kijinsia katika mazingira ya Wakimbizi : Chapisho la Makala za Warsha ya Mafunzo toka kwa Mashirika Mbalimbali (UNHCR 2001)**

Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Masuala ya Kisheria/Haki

Anzisha mfumo na mamlaka za wenyeji ili waathiriwa/wanusurika wanaotaka kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watu waliovatendea unyanyasaji waweze kufanya hivyo katika wakati mwafaka

Jambo hili linahitaji kujenga na kudumisha uhusiano na ushirikiano wa karibu kikazi na vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria, kwa mfano, jeshi la polisi, idara ya mahakama, pamoja na ofisi ya mwendesha mashtaka. Zaidi ya hapo shirikiana

na mahakama za kijadi za jamii husika ili kuhakikisha kuwa waathiriwa/wanusurika wanatendwa haki.

Ufahamu mfumo wa sheria unaotumika.

◎ Afisa wa hifadhi na usalama anapaswa kufahamu sheria husika ya nchi inayoshughulikia mambo yafuatayo:

- Sheria ya kitaifa na mienendo inayotumika. Maana halisi za kisheria za aina mbalimbali za unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Kama mashambulizi ya majumbani yanatafsiriwa kuwa makosa ya jinai na yanatofautishwa na mashambulizi ya kawaida ya aina nyininge.
- Kama katiba ya nchi husika inatamka Haki za Binadamu, je, sehemu husika zinaweza kutumika kwa ajili ya kushughulikia makosa yanayohusiana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia?
- Je, kuna sheria zipi kuhusu suala la utoaji mimba? Kama kuharibu mimba kunakatazwa, je, kuna mazingira maalumu ambapo kufanya hivyo kunaruhusiwa? Mathalani, mimba zitokanazo na vitendo vya ubakaji, mimba inayohatarisha maisha ya mwanamke, au kama kuna sababu za kuhofia afya ya kisaikolojia ya mwanamke. Na je, unahitajika ushahidi gani ili kuruhusu utoaji wa mimba?

Elewa namna ya kushughulikia mlalamiko yanayohusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia

- Watendaji ambao wanamsaidia mwathiriwa/mnusurika ambaye ameamua kuchukua hatua za kisheria ili kudai haki zake wanapaswa kuwa wasikivu na wenye huruma. Wakati huohuo wanapaswa kumpatia mhusika taarifa kamili kuhusu mchakato wa kisheria unaotumika katika nchi anamoishi mkimbizi.
- Mwathiriwa/mnusurika anastahili kufahamishwa matarajio yake kutoka kwenye mfumo wa sheria. Watendaji wanaoshughulikia masuala ya ulinzi na huduma za jamii wanapaswa kuhakikisha kuwa mlalamikaji anafahamu fika haki zake, taratibu na muda utakaotumika katika mchakato wa kisheria. Wanapaswa kuwa na uwezo wa kujibu maswali yoyote ambayo wataulizwa na mlalamikaji. Aidha mlalamikaji anastahili kupewa ushauri wa kisheria kuhusu uonevu aliotendewa, muda ambao unaweza kutumika katika kupeleleza na kusikiliza kesi, matokeo yanayotarajiwa kutohana na mkondo wa sheria, majukumu ya shirika la UNHCR pamoja na wadau wengine ambao wanashiriki katika mchakato mzima.
- ◎ Wasimamizi wa ulinzi wanapaswa kumshauri mwathiriwa/mnusurika kuhusu huduma za afya ya uzazi zinazopatikana, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ushauri nasaha, na taratibu za kutibu majeraha, kuzuia magonjwa na kutoa mimba zisizotakiwa, kama inavyoruhusiwa na sheria za kitaifa.
- ◎ Zaidi ya hapo wasimamizi wa ulinzi wanapaswa pia kufanya mambo yafuatayo:

- kuhakikisha kuwa mnusurika na mhalifu wana nyaraka za usajili na vitambulisho;
- kushirikiana na wanasheria wenyeji ambao wanaelewa sheria za nchi na mienendo ya kutoa ushauri kuhusu unyanyasaji wa kingono ;
- kuhakikisha kuwa ripoti ya malalamiko imewekwa katika kumbukumbu za polisi wa eneo husika;
- kuhakikisha kuwa ripoti ya hospitali pamoja na maelezo ya mwathiriwa/mnusurika vimehifadhiwa na kufikishwa kwa vyombo husika vya kitaifa (polisi na mwendesha mashtaka);
- kuhakikisha kuwa mashahidi muhimu kutoka katika jamii ya wakimbizi wanatii matakwa ya kisheria kwa kuandikisha maelezo na kufika mahakamani kila wanapohitajika kufanya hivyo;
- kupitia ushirikiano wa wanausalama na polisi, kuhakikisha kuwa watu wanaohusika na unyanyasaji wa kingono na kijinsia wanapewa ulinzi dhidi ya vitisho na madhara mengine ya kimwili;
- kuhakikisha kuwa shirika la UNHCR au wadau/watumishi wa mashirika mengine wanawasindikiza waathiriwa/wanusurika wakati wa kwenda mahakamani.

Fahamu wajibu wa shirika la UNHCR na watumishi wa kitaifa wanaohusika na utoaji wa huduma za kisheria.

- ◎ Wasimamizi wa ulinzi wanapaswa kubaini vyombo vinavyojishughulisha na haki za wanawake katika eneo husika pamoja na vyama vya wanasheria vinavyojihuisha na masuala ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa lengo la kujenga ushirikiano katika kukabiliana na tatizo hili. Katika mazingira ambapo shirika la UNHCR linagharimia msada wa kisheria, linapaswa kuhakikisha kuwa waathiriwa/ wanusurika wanatetewa na mawakili mahiri katika taaluma yao. Wawakilishi wa jumuiya zisizo za kiserikali ambao wanashirikiana na wanausalama wa shirika la UNHCR katika utoaji wa huduma za kisheria wanapaswa kufanya mambo yafuatayo:
- kumpatia mlalamikaji taarifa zote muhimu kuhusu mwenendo wa sheria na uendeshaji wa kesi za jinai kwa lengo la kumwandaa mlalamikaji na familia yake ili waweze kushiriki ipasavyo katika vikao vya mahakama;
 - kumsaidia na kumwelekeza mlalamikaji jinsi ya kuomba ufadhili wa kugharimia misada ya kisheria, kama ufadhili wa aina hii unapatikana chini ya sheria ya nchi husika (na kama ufadhili huu haapatikani, shirika la UNHCR lihakikishe kuwa bajeti zake zinajumuisha fungu la kugharamia mawakili wanaowatetea waathiriwa wa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia);
 - kumsindikiza mlalamikaji hadi kituo cha polisi na mahakamani pamoja na kuhudhuria masailiano na vikao vya mahakama;
 - kuiomba mahakama iwave wadhifa wa kuwa watazamaji

- katika kesi zote ili waweze kuruhusiwa kuchangia mahakamani (hili ni jambo muhimu sana katika kesi zinazowahusu watoto);
- kuchunguza uwezekano wa mahakama kusikiliza kesi kwa faragha ili kuwalinda waathiriwa, wanusurika na familia zao dhidi ya kupatwa na uchungu zaidi;
 - kutunza usiri wa kesi zote na mara kwa mara kuwasiliana na watumishi wa shirika la UNHCR wanaohusika na masuala ya ulinzi

Fahamu haki za mhalifu

- Mhalifu anastahili kupewa haki sawa na zile apewazo mtu ambaye hajapatikana na hatia. Shirika la UNHCR lina wajibu wa kuhakikisha kuwa washtakiwa wanatendewa haki mahakamani na wanapewa heshima wanayostahili wakati wa kusailiwa na kushikiliwa. Watumishi wa shirika la UNHCR wa kitengo cha masuala ya ulinzi wanawajibika kuhakikisha kuwa washtakiwa wanapewa haki na heshima zao wakati wa upelelezi na wakati wa kusikiliza kesi zao. Hasa, shirika la UNHCR linapaswa kuhakikisha kuwa:
- hakuna ucheleweshaji usiokuwa wa lazima;
- mhalifu hateswi wakati wa kushikiliwa kwake;
- mhalifu anatendewa ubinadamu wakati wa kushikiliwa kwake;
- kama mhalifu atatendewa uovu, shirika la UNHCR liwasilishe malalamiko kwa vyombo husika kwa ajili ya kuhakikisha kuwa mhalifu anatunzwa kwa mujibu wa sheria.

Fahamu hukumu na adhabu zinazotumika

Wasimamizi wa masuala ya ulinzi wa shirika la UNHCR watapaswa kuhakikisha kuwa wakimbizi wanaopatikana na hatia ya kutenda makosa ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia wanapewa adhabu zilezile ambazo hutolewa kwa wenyeji, yaani, wanahukumiwa kwa mujibu wa sheria husika za nchi. Shirika la UNHCR kwa ushirikiano na jumuiya zisizo za kiserikali ambazo zinajihusisha na masuala ya kisheria na haki katika nchi husika, wahakikishe kuwa wahalifu wanaadhibiwa kwa namna ambayo haitoi taswira ya kubaguliwa kwa sababu ya hali yao ya ukimbizi. Hukumu dhidi ya watoto wahalifu zilenge katika kurekebisha tabia zao. Kila inapowezeekana, wakati wa kutumikia adhabu zao, watoto wahalifu wasichanganywe na wahalifu ambaeo ni watu wazima.

Fahamu kuhusu fidia

Mwathiriwa/mnusurika ambaye anataka fidia kutoka kwa mshtakiwa anastahili kupewa msaada wa kisheria wa jinsi ya kufanya hivyo. Kama shirika la UNHCR halitoi msaada wa aina hii, juhudhi zifanyike kumtafutia mhusika chombo cha kumpatia ushauri na msaada wa bure. Vyombo vitoavyo msaada wa aina hii vinajumuisha vyama vya wanasheria/mawakili na asasi za kupigania haki za wanawake ndani ya jumuiya za kiraia.

Fahamu njia mbadala za kutatua migogoro

Katika baadhi ya jamii, waathiriwa/wanusurika wanapendelea kutafuta haki kuititia mifumo ya kijadi ya utatuvi wa magomvi. Wakati mwingine waathiriwa na familia zao hushinikizwa kutumia njia hizi za kijadi kwa kuogopa uwezekano wa kutengwa iwapo watakataa kufanya hivyo. Wasimamizi wa ulinzi wa shirika la UNHCR wanapaswa kuchunguza njia hizo ili kuhakikisha kwamba hazikinzani na sheria za kitaifa au matakwa na viwango vya kimataifa. Kama mbinu hizo zinakiuka sheria za kitaifa, wasimamizi wa masuala ya ulinzi wanapaswa kuandaa mafunzo na kuendesha kampeni za ueleweshaji na uhamasishaji kwa ajili ya jamii husika, na kuwahimiza wanajamii kurekebisha mbinu zao za utatuvi wa migogoro ili ziendane na viwango vya kimataifa kuhusiana na haki za binadamu. Kazi ya kubadilisha mila na desturi huchukua muda, kwa hiyo zoezi hili linahitaji uvumilivu na msimamo usioonyesha upendeleo wa aina yoyote ile.

Rejea pia:

- **Kiongozo cha Hatua kwa Hatua kwa Ajili ya Maafisa wa Ulinzi, Kuzuia na Kukabiliana na Unyanyasaji Kingono na Kijinsia (UNHCR 1998)**
- **Watoto Wakimbizi: Kanuni kuhusu Ulinzi na Matunzo yao (UNHCR 1994)**
- **Kanuni za Ulinzi wa Wanawake wakimbizi (UNHCR 1991)**

Kubainisha dhima za watu wengine wawezao kuwa watendaji

Licha ya watendaji wanaohusika na masuala ya afya, huduma za jamii, usalama na ulinzi, kuna watu wengine ambaeo nao wana majukumu muhimu katika kukabiliana na mahitaji ya waathiriwa/wanusurika. Watu wote wanaojishughulisha na masuala ya wakimbizi wanapaswa kufahamu majukumu yao pamoja na majukumu ya watu wengine ambaeo wanashiriki pia katika kutoa misaada kwa waathiriwa/wanusurika wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Majukumu ya watumishi sekta ya ugani

- ◎ Kupokea na kuititia ripoti za matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Kuhakikisha usalama wa waathiriwa/wanusurika na kuwarufaa mahali ambako watahudumiwa kwa huruma na kupewa msaada bora na watendaji wote .
- ◎ Kuendesha kampeni za kuhakikisha kuwa mwathiriwa/

mnusurika anapata msaada kutoka kwa watendaji wote kama inavyotakiwa.

- ◎ Kuwezesha utawala kukabiliana na mahitaji ya usalama wa mwathiriwa/mnusurika, kwa mfano, kwa kugawa kadi ya posho ya kaya na kumpatia mwathiriwa/mnusurika makazi tofauti pamoja na bidhaa nyingine ambazo si vyakula.
- ◎ Kuhifadhi kumbukumbu kwa ajili ya kufuatilia mielekeo ya vitendovyaunyanyasajiwa kingonona kijinsia, kuchambua matatizo, na kujenga mikakati ya kushughulikia masuala ya uzuiaji na ukabilianaji.
- ◎ Kushirikiana na sekta nyingine zote na watendaji wake.

Majukumu ya watumishi sekta ya programu

- ◎ Kusaidiana na sekta nyingine zote katika uandaaji wa mpango wa uzuiaji na ukabilianaji ambao unashirikisha sekta zote.
- ◎ Kugawa rasilimali kwa ajili ya kusaidia shughuli zinazostahili.
- ◎ Kupokea na kupitia mihtasari ya ripoti za data, mielekeo, uchambuzi na hatua za ulinzi na za ukabilianaji pamoja na mahitaji.
- ◎ Kuzihimiza jumuiya za kimataifa ambazo si za kiserikali kutenga rasilimali kwa ajili kusaidia programu za kushughulikia masuala ya ulinzi na ya ukabilianaji.
- ◎ Kushirikiana na sekta nyingine zote na watendaji wake.

Majukumu ya watumishi wa Makao Makuu

- ◎ Kupokea na kupitia ripoti na chambuzi za data za matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, shughuli zilizotekelezwa kwa mujibu wa programu na matokeo yake.
- ◎ Kuwasaidia watumishi wa shirika la UNHCR kuandaa, kutekeleza, kufuatilia na kupima mikakati ya uzuiaji na ukabilianaji.
- ◎ Kushiriki katika kuratibu shughuli baina ya sekta na mashirika mbali mbali.
- ◎ Kushirikisha watumishi wote wa UNHCR, wakimbizi, wadau, na serikali ya nchi mwenyeji katika uandaaji wa programu.
- ◎ Kuhimiza na kukuza kiwango cha harakati na kuunga mkono shughuli za uzuiaji na ukabilianaji; kusaidia kutatua matatizo na kupigania upatikanaji wa rasilimali zinazotosheleza.
- ◎ Kushirikiana na watumishi wa shirika la UNHCR katika ofisi zake nyingine pamoja na wale wa mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa katika jitihada za kutumia vyema rasilimali zilizopo na kupeana taarifa.

Majukumu ya Jeshi la Polisi

- ◎ Kupokea malalamiko na kufanya upelelezi, kwa kuzingatia taratibu na kanuni za kisheria na uendeshaji mashtaka kama sheria zinavyoelekeza.
- ◎ Kwa kuzingatia mienendo ya utendaji kazi za kipolisi, kukamata watuhumiwa, kufanya upelelezi, kutayarisha mashtaka, kusambaza hati za kuitwa mahakamani pamoja na kuhakikisha kuwa mashahidi wote wanafika mahakamani.
- ◎ Kila inapobidi, kuwahimiza wahusika ili kuharakisha upelelezi na usikilizaji wa kesi zinazohusiana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Kumweleza mwathiriwa/mnusurika mchakato wa kisheria na uendeshaji wa mashtaka ya makosa ya jinai.
- ◎ Kuwa msikivu na makini kwa mahitaji ya mwathiriwa/ mnusurika yanayohusu umuhimu wa kumtunzia siri, kumhakikishia uaminifu na heshima.
- ◎ Kushiriki kikamilifu katika kampeni za kukuza uelewa wa masuala ya kisheria na haki, pamoja na utoaji elimu, ambazo zinaendeshwa na wasimamizi wa ulinzi kwa manufaa ya jamii ya wakimbizi.

Majukumu ya Mahakama

- ◎ Kutayarisha kitabu cha kumbukumbu za kesi za kila wiki ambapo masuala muhimu ya pande za wakimbizi husika yamebainishwa (mlalamikaji au mhalifu).
- ◎ Kulingana na taratibu zilizowekwa, kuzishughulikia kesi zinazohusu makosa ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, kwa mfano, kupokea kesi, kusimamia usikilizaji wa kesi, kuwaita mashahidi mahakamani, kutoa hukumu na adhabu.
- ◎ Kushiriki katika warsha na shughuli za uhamasishaji na ueleweshaji zinazoandaliwa na kuendeshwa na watumishi wa kitengo cha ulinzi.

Uandaajiwa Mpango kwa ajiliya Kuwashirikisha Wahalifu

Kuwashirikisha wahalifu wa magomvi ni suala gumu lakini liliilo muhimu sana. Ni lazima wahalifu wapewe haki zao, ikiwa ni pamoja na usalama wao kwa mujibu wa tamko la haki za binadamu. Kama mhalifu ni mkimbizi, anastahili pia ulinzi wa kimataifa. Timu ya watendaji kutoka sekta mbalimbli iandae mipango ya kuwashirikisha wahalifu.

- ◎ Ombo ushauri kutoka kwa vyombo vya nchi kuhusu hatua ambazo huchukuliwa dhidi ya watendaji wa makosa ya

unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

- ◎ Wahuushe wanausalama na polisi, wakiwemo walinzi wanaotoka katika jamii husika, katika jitihada za kushughulikia na kufuatilia matendo ya wahalifu wanaojulikana.
- ◎ Kama inawezekana, wahalifu watengwe na jamii nyingine.

Mambo muhimu ya kukumbuka

Jamii inapaswa kuwa msitari wa mbele katika kuandaa njia za kuwasaidia waathiriwa/wanusurika.

Andaa shughuli za kuelimisha na kuhamasisha jamii

- ◎ Anzisha kampeni za upashanaji habari kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa ajili ya wanajamii wote.

Anzisha utaratibu wakurufaa na kuripoti

- ◎ Panahitajika mfumo mzuri kwa ajili kukata rufani katika kila mazingira ambao utamwezesha mwathiriwa/mnusurika kufahamu mahali pa kuomba na kupatiwa msaada kwa wakati mwafaka.

Iwezeshe jamii ya wakimbizi kukabiliana na hali

- ◎ Ili uweze kuandaa mikakati madhubuti na ya kudumu kwa ajili ya ukabilianaji ni muhimu kuishirikisha jamii husika katika zoezi hili.

Andaa namna ya kukabiliana na mahitaji ya kiafya/kitiba ya waathiriwa/wanusurika

- ◎ Toa huduma za afya, rufaa na ufuatilaji ambazo ni rahisi kwa wengi.

Kabiliana na mahitaji ya kisaikolojia na kijamii ya waathiriwa/wanusurika

- ◎ Waathiriwa/wanusurika wanastahili kushughulikiwa kwa huruma na uangalifu.

Andaa namna ya kukabiliana na masuala ya usalama na ulinzi

- ◎ Mwathiriwa/mnusurika anastahili kuhakikishiwa usalama baada ya tukio la kufanyiwa unyanyasaji wa kingono na kijinsia na jamii inapaswa kuwa msitari wa mbele katika kumpatia mahali ambapo ni salama zaidi.

Andaa namna ya kukabiliana na masuala ya kisheria/utoaji haki

- ◎ Kwa kushirikiana na mamlaka za mahali husika jenga utaratibu kwa ajili ya matumizi ya waathiriwa na wanusurika wanaopenda kuchukua hatua za kisheria ili kudai fidia dhidi ya maovu walijotendewa na fanya hivyo kwa wakati mwafaka.

Bainisha dhima na majukumu ya watu wengine wanaoweza kushiriki

- ◎ Watumishi wa Ugani wa programu na wa menejimenti, wanaweza kutoa michango muhimu sana katika kushughulikia mahitaji ya waathiriwa/wanusurika.

Jenga mpango wa kukuwezesha kufanya kazikwakuwashirikisha wahalifu

- ◎ Haki za binadamu za wahalifu, ukiwemo usalama wao, zinapaswa kuheshimiwa na kuzingatiwa.

Sura ya 1

Sura ya 2

Sura ya 3

Sura ya 4

Sura ya 5

Sura ya 6

Sura ya 7

Sura ya 8

SURA YA 5

MAZINGATIO MAHUSUSI YA WATOTO WAKIMBIZI

Wakati kanuni na miongozo ilijojadiliwa katika sura nyingine huwahuusu watoto wakimbizi, kuna masuala mahususi mengine yanayopaswa kuzingatiwa kwa makini zaidi wakati wa kuwahudumia watoto wakimbizi. Watoto wakimbizi hukabiliwa na aina mahususi za vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia kama vile: vitendo hatari vya kimila na kitamaduni, biashara ya magendo ya watoto, ukahaba wa watoto, unyanyasaji na unyonyaji wa kingono ndani ya familia, pamoja na vitendo vingine vya unyanyasaji vinavyofanywa na wazazi au walezi dhidi ya watoto.

Makundi fulani ya watoto wakimbizi yako katika hatari zaidi ya kukabiliwa na unyanyasaji wa kijinsia na kingono. Makundi hayo ni kama: watoto wasio na wazazi/walezi au walio tenganishwa, watoto walio kizuizini, askari watoto, vijana walio katika umri wa balehe, watoto walemvu wa akili na wa viungo, watoto wanaotumikishwa, wasichana waliozaa wakiwa na umri mdogo, watoto waliozaliwa kutokana na athari za vitendo vya ubakaji, wavulana wanusurika/waathiriwa na watoto wahalifu.

Unaposhughulikia watoto wakimbizi unapaswa kuyafahamu Mapatano kuhusu Haki za Mtoto (1989) yanayoweka hatua bainifu za jinsi ya kulinda haki za watoto wote. Zaidi ya orodha ya Kanuni za Mwongozo zinazoelezwa katika Sura ya 2, kanuni nyingine nne zinapaswa kuzingatiwa ili kuimarisha kazi yako ya kuwahudumia watoto wakimbizi. Kanuni hizo nne ni: haki ya mtoto ya kuishi, haki ya kufaidika na usalama na kujiendeleza, haki ya kuhakikishiwa maslahi yaliyo bara zaidi kwa mtoto, haki ya kutobaguliwa na haki ya kushirikishwa.

Mapatano kuhusu Haki za Mtoto (CRC), yanamfasili mtoto kama mtu yoyote mwenye umri chini ya miaka 18, isipokuwa kama sheria husika za kitaifa zinatamka umri wa utu uzima ulio chini ya huo. Kwa maana hiyo kanuni ya CRC itatumika kwa kila mtu mwenye umri chini ya miaka 18 isipokuwa kama sheria ya nchi mahususi inasema vinginevyo.

Watoto wakimbizi kwa mujibu wa sheria za nchi husika wanaweza kujikuta wakikabiliwa na hatari mahususi za unyanyasi wa kingono na kijinsia kutokana na kiwango chao cha utegemezi, mathalani, uwezo mdogo wa kujitetea, pamoja na kuwa na madaraka na ushirikishwaji finyu katika michakato ya kufanya maamuzi. Aidha kutokana na udogo wa uzoefu wao wa maisha, ni jambo rahisi sana kwa watoto kunyanyaswa na kudhulumiwa kwa mabavu

kuliko ilivyo kwa watu wazima. Inawezekana wakashindwa kuelewa baadhi ya vitendo na tabia za kingono kwa sababu ya uduni wa kiwango chao cha kukua, na kwa sababu hiyo hawawezi kutoa maamuzi yatokanayo na ujuzi na uelewa sahihi. Mambo mengine yanayoweza kuzidisha uwezekano na hatari za kuwafanya watoto wakimbizi kuwa waathiriwa wa vitendo viovu vya kingono na kijinsia ni: masuala ya ukabila, jinsia, utamaduni, pamoja na matatizo ya kiuchumi na kijamii.

Vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia vina madhara makubwa kwa makuzi na afya ya kiakili na kimwili ya watoto.

Kama ilivyoadiliwa katika Sura 1, unyanyasaji wa kingono unaweza kufanywa kwa njia mbalimbali, ambapo nyingi ya njia hizo huwalenga watoto. Vitendo maalumu vilivyojikita katika udhalilishaji wa kijinsia, pakiwemo vitendo viovu/hatari vya kiutamaduni, mara nyingi hutendwa kuanzia tangu utoto wa mtu. Na watu wanaotenda vitendo hivyo viovu vya kingono na kijinsia dhidi ya watoto wakimbizi aghalabu huwa ni watu wanaofahamika na hata kuaminika yaani watoto wenzao au watu wazima wenyе dhamana ya kuwalea na kuwatunza. Kumbuka kwamba uelewa wa mtoto kuhusu mambo haya unaweza ukapotoshwa na hali hii.

Unapojishughulisha na watoto wakimbizi huna budi kujelimisha ipasavyo juu ya CRC. Mapatano hayo yanatamka kwa ufasaha haki za msingi za kila mtoto popote duniani pamoja na watoto wanaoishi maisha ya ukimbizi. Haki hizo hujumuisha haki ya kulindwa dhidi ya unyanyasaji na unyonyaji kingono. Kwa hakika CRC inatoa hifadhi kwa watoto wakimbizi wanaoishi katika nchi ambazo hazikuridhia Mapatano kuhusiana na wakimbizi. Itifaki ya Hiari ya CRC kuhusu Biashara ya Watoto, Ukahaba na Ponografia za Watoto (2000) na makubaliano yanayohusu masuala ya utoroshaji, uuzaji na utekaji nyara wa watoto.

Kanuni za Mwongozo

Zifuatazo ni kanuni za mwongozo zinazotambuliwa kiulimwengu kama zilivyoainishwa na CRC. Ni kanuni zinazopendekezwa kuzingatiwa kuongoza shughuli zote zinazohusu masuala ya watoto wakimbizi:

- **Haki ya kuishi, kulindwa na kukua:** Haki hii inapaswa kudhaminiwa kwa kuchukua hatua za kulinda maisha. Kanuni ya ‘kulindwa na kukua’ haihusu makuzi na maendeleo ya kimwili peke yake bali hujumuisha pia masuala ya utimamu wa akili na ubora wa maendeleo ya kihisia. Kwa mfano, ndoa za umri mdogo zinahatarisha, siyo tu haki ya maisha ya mama mwenye umri mdogo bali pia uhai wa mtoto wake – yaani usalama na ukuaji wa wahusika hao wawili huwa mashakani (Kifungu namba 6, CRC).
- **Kutobaguliwa:** Kila mtoto ndani ya nchi anamoishi, bila kujali hadhi yake ya kijinsia na kiuhamiaji, ana haki zote za CRC. Kanuni hii, hivyo basi, huwahuusu pia watoto wakimbizi [Ibara ya 2 CRC]
- **Maslahi bara zaidi ya mtoto:** Kanuni hii muhimu inapaswa kutumikakwa maamuzi yanayomhusu mtoto mmojammoja na kwa masuala mapana zaidi ya kisera na maamuzi yanayohusu makundi ya watoto. Katika kutafakari kila uamuzi unaomhusu mtoto, sharti wahusika wachunguze kwa makini aina mbadala za utatuzi wa suala husika na papo hapo wakielekeza uzito na nguvu zao zote kwenye maslahi bora zaidi ya watoto wakimbizi. (Ibara ya 3, CRC)
- Wakati wa kufanya maamuzi ya sera, kwa mfano, uelekezaji wa bajeti, kuna haja ya kufanya uchunguzi yakinifu kuhusu utekelezaji unaotakiwa utakavyowaathiri watoto. Siyo lazima kila sera itokane na mahitaji au maslahi ya watoto, lakini kama kuna migongano yoyote, viongoziwanaohusika na ufanyaji maamuzi wanapaswa kuongozwa na kanuni ya maslahi bora zaidi ya watoto na kulipa jambo hili uzito wa pekee
- Katika kuamua kuhusu maslahi bora zaidi ya mtoto mmoja, watendaji wanapaswa kuzingatia viwango halisi vinavyofikiriwa kukidhi maslahi bora ya watoto husika. Aidha wanapaswa pia kuzingatia ushauri mzuri unaojumuisha maoni ya mtoto. Uamuzi wa jinsi ya kuandaa maslahi bora zaidi ya mtoto mara nydingi huweza kuwa mgumu, na hakuna jibu moja huweza kuwa bayana na lisilo na migongano. Kwa maana kuna mambo mengi yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya zoezi hili, mathalani, umri, jinsia, masuala ya utamaduni na mazingira kwa jumla pamoja na viwango vya uzoefu wa mtoto. Kwa hiyo tafsili ya kanuni hii inapaswa kufanywa kwa kuzingatia kusudio la CRC na sharti ujumuushe ushauri wa kitaalamu ambao umejikita katika masuala ya kisheria na makuzi ya mtoto.

- Ushiriki: Umuhimu wa kifungu hiki ni kwamba watoto wana haki ya kutoa maoni yao juu ya maamuzi yanayogusa na kuathiri maisha yao na kwamba maoni yao hayo yanastahili kupewa "uzito unaostahili". Kanuni hii inapaswa kutumika katika masuala yote yanayohusu hifadhi ya kisiasa, mipango kwa ajili ya mtoto mmoja mmoja, pamoja na maandalizi ya programu pana zaidi (Ibara ya 12, CRC). Kadri mtoto anavyokuwa na umri mkubwa ndivyo anavyostahili kusikilizwa na kushirikishwa katika kufanya maamuzi yanayomhusu.

Kanuni zote hizi za mwongozo zina mchango muhimu katika zoezi zima la kuamua maslahi bora zaidi ya mtoto katika mazingira mahususi. Lakini kuna wakati ambao matakwa muhimu ya mtoto pamoja na maoni yanaweza kupishana na yale yaliyotaja yeye mwenyewe. Katika hali kama hiyo kunaweza kuwepo haja ya kuyapuuzia.

Tazama pia:

- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC): Viwango vya Kisheria vya Kimataifa (UNHCR, OHCHR, NICEF, Save the Children 2002)**
- **Kijitabu cha UNHCR kuhusu Kuwapatia Wakimbizi Makazi Mapya (UNHCR 2002)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC): Makuzi ya Mtoto na Kijana (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children 2001)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Masuala Muhimu: Unyanyasaji na Unyonyaji (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children Revised 2002)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC): Maandalizi ya Makazi Mapya (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children 1999)**
- **Watoto Wakimbizi: Miongozo kuhusu Ulinzi na Huduma (UNHCR 1994)**
- **Mapatano kuhusu Haki za Mtoto (1989)**

Makundi ya Watoto Wakimbizi walio katika hatari mahususi za unyanyasaji wa kingono na kijinsia

- Watoto wasio na wazazi/walezi au waliotenganishwa.
- Watoto waliowekwa kizuzini.
- Watoto askari.
- Vijana walio katika umri wa balehe.
- Watoto walemavu wa akili na wa viungo.
- Watoto wanaotumikishwa.
- Wasichana wanaozaa wakiwa na umri mdogo

- Watoto waliozaliwa kutohana na athari za vitendo vya ubakaji
- Wavulana waathiriwa/waathiriwa .
- Watoto wahalifu.

Watoto wasio na wazazi/walezi au waliotenganishwa

Dhana "watoto wasio na wazazi/walezi" au "watoto waliotenganiswa" zinapaswa zinapaswa kutumika badala ya dhana "watoto yatima". Kwa UNHCR, mtoto ni yatima pale tu wazazi wote wawili wanapothibitika kuwa wamekufa. Kuwaita watoto "yatima" kunahitaji uthibitisho wa uhakika na unahamasisha kuasili utoto badala ya kulenga hatua juu ya kutafuta familia na kuongeza msaada wa kijamii.

- Nijambo rahisi zaidi kwa watoto wakimbizi wasio na wazazi/walezi au ambao wametenganishwa kukabiliwa na hatari kubwa kama vile: kunyonywa kingono, kudhalilishwa, kulazimishwa kujunga na majeshi, kutekwa nyara, kuuzwa kwa njia za magendo na hata kuwekwa kizuizini. Hali hii inatokana na ukosefu wa mtu wa kuwalinda na kuwasaidia. Katika mazingira ya dharura watoto wakimbizi wanaweza kuishi na jamaa zao kutohana na mfumo wa familia pana za Kiafrika, na kwa maana hiyo wakaonekana kana kwamba hawaishi peke yao, lakini bado wanaweza wakawa wanakabiliwa na hatari zile zile kama zinazowakabili watoto wakimbizi waishio peke yao.
- Kumbuka pia kwamba makundi ya watoto wasio na wazazi /walezi na au ambao wametengwa yanaweza kujumuisha kaya zinazoongozwa na watoto ambapo wale wenye umri mkubwa kidogo ndio wenye wajibu wa kuwalea wadogo zao.
- Kumbuka vile vile kwamba yatima ambao vifo vya wazazi wao vimesababishwa na UKIMWI wanajumuishwa katika makundi ya watoto wasio na wazazi/walezi au waliotenganishwa. Inawezekana kwamba kabla ya kuwa yatima watoto hao ambao ni waathiriwa wa UKIMWI wanaweza kulazimika kuwatanza wazazi wao kabla ya kufa. Kwa kawaida hali hii huwfanya watoto hao kuanza kubebmajukumuyautuuzima, kuachashulenakuwatanza wadogo zao. Watoto ambao uyatima wao husababishwa na UKIMWI, hususani wasichana, aghalabu hufanyiwa vitendo vya ubaguzi na unyanyapaa vikiambatana na kunyimwa huduma muhimu ambazo ni haki na stahili ya kila mkimbizi. Kwa sababu hizi wako katika hatari kubwa zaidi ya kunyanyaswa na kunyonywa kijinsi. Kadri idadi ya yatima wanaosababishwa na UKIMWI inavyoongezeka ndivyo idadi ya watoto wanaolazimika kufanya vitendo

vya ukahaba, wanaolazimika kufanya kazi za "mitaani" au zile za majumbani kwa watu itakavyozidi kuongezeka pia.

Watoto waliowekwa kizuzini

Watoto waliowekwa kizuzini au ambao wamenyang'anywa uhuru wao wanaweza kabiliva na hatari kubwa mno ya kudhalilishwa na kunyanyaswa kijinsia hivyo wanastahili kuhudumiwa kwa kuzingatia mahitaji yanayoendana na umri wao halisi.

Vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia hutokea mara kwa mara katika vituo vya kuzuilia watu na ndani ya magereza, hususani kama wafungwa wanakaa pamoja. Katika mazingira kama haya watoto huwa walengwa wakuu wa vitendo viovu kwa sababu maalumu. Hali hii hutokana na sababu kadhaa, kwa mfano, imani kwamba watoto hawana VVU/UKIMWI au kwa sababu ya thamani kubwa ambayo tamaduni nyingi zinaipa hali ya ubikira. Kwa hiyo ni muhimu sana kuwatenganisha watoto na watu wazima katika vituo vya kuzuilia watu isipokuwa kama inadhaniwa kwamba kuwachanganya pamoja ni kwa maslahi bora zaidi kwa mtoto anayezuiliwa.

Askari watoto

Askari Mtoto ni mtu yelete mwenye umri chini ya miaka 18 ambaye ni sehemu ya jeshi, kwa kazi yoyote ya kijeshi na wale wote wanaoambatana na na kundi hilo ambao si wanafamilia hali kadhalika wasichana walioandikishwa kwa ajili ya ngono na ndoa za lazima.

*Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa
Ripoti ya Baraza la Usalama, 2000*

Watoto wakimbizi huwa askari watoto kuitia njia kadhaa: baadhi yao huandikishwa jeshini kwa mujibu wa sheria, wengine hukamatwa kwa nguvu, wengine hujunga kwa hiari yao ili kujinusuru au kulinda familia zao. Aidha wengine hutekwa nyara ikijumuisha wasichana waliochukuliwa kwa madhumuni ya kutumiwa kwa vitendo vya ngono.

Kwa kawaida wavulana na wasichana huandikishwa jeshini kwa madhumuni tofauti: wavulana wanatumika kama wapiganaji na hufanya kazi za kivita ambapo wasichana zaidi hutumika kama watumwa wa vitendo vya ngono na kazi nyingine za lazima.

Watoto waliomo au walio karibu na kanda za migogoro/ mapigano na wale wasio na wazazi/walezi na walio tenganishwa,

wako katika hatari kubwa ya kuandikishwa jeshini kunakofanywa na serikali nchi au vikundi visivyo vya kiserikali. UNHCR inakataza uandikishaji wa watoto katika jeshi. Vitendo vya unyanyasaji wa kingono kwa wavulana, na hususani kwa wasichana, wanavyotendewa wakati wanapokuwa jeshini vina athari mbaya sana za kijamii na kiutamaduni. Wanapokuwa huru bada ya kuvunjwa kwa majeshi, madhara hayo huweza kuwa kipingamizi kikubwa dhidi ya juhud za kuunganisha familia au uwezo wa vijana husika kujunga tena na jamii kwa jumla. Aidha kuna tabia ya kuwapuuzia watoto, hususani wasichana, wakati wa kuachiwa huru baada ya vita. Ni jambo muhimu sana kuhimiza ushirikishwaji wa wasichana katika hatua za uvunjaji majeshi baada ya mapigano.

Vijana walio katika umri wa balehe

Tafsili ya dhana ya "vijana walio katika umri wa balehe" huweza kutofautiana kutoka tamaduni moja hadi nyingine hivyo inapaswa kutafsiliwa kulingana na mazingira mahususi ya ukimbizi. Iwapo kijana aliye katika umri wa balehe ameshaanza kufanya majukumu ya watu wazima pia hutegemea na na tofauti za kiutamaduni na hali ya ukimbizi

Mahitaji ya kijana aliye katika umri wa balehe katika masuala ya ulinzi na misaada hayako wazi kama ilivyo kwa yale ya watoto, lakini nayo pia ni muhimu kwa sababu wao nao hukabiliwa na unyanyasaji mahususi kuhusiana na vitendo vya ngono na jinsia. Na kwa kawaida mahitaji yao huwa hayapewi uzito unaotakikana.

Vijana walio katika umri wa balehe, hususani wasichana, hukabiliwa na hatari kubwa zaidi ya kudhalilishwa na kunyonywa kingono kwa sababu wahalifu wao huwafikirii kwamba hawana magonjwa ya zinaa. Kwa hiyo vijana wa kike na wa kiume wanakabiliwa na hatari ya kuambukizwa VVU/UKIMWI na maradhi mengine ya zinaa. Aidha wasichana wanaweza pia kupata mimba wasizozitaka na zenye hatari kutokana na vitendo vya kubakwa. Tofauti na watu wazima, aghalabu vijana huwa na taarifa na uelewa finyu kuhusu afya ya uzazi kwa sababu mara nyingi wao sio walengwa wa mipango ya mafunzo kuhusu masuala haya.

Watoto walemvu wa akili na wa viungo

Kwa kawaida familia nyingi zina tabia ya kuwaficha watoto walemvu wa akili na wa viungo. Tabia hii ya kuwafanya wasionekane hadharani huwanyima fursa za kufikiwa na huduma zinazopatikana. Kutengwa na mara nyingi kushindwa kuwakwepa wahalifu hawa, hukabiliwa na hatari kubwa ya

kudhalilishwa kijinsi. Watoto hawa wanahitaji uzingatizi maalum wakati wa kuandaa mipango ya ulinzi na ukabilianaji dhidi ya unyanyasaji na unyonyaji wa kingono .

Makundi mengine ya watoto wanaoweza kukabiliwa na hatari ya kudhaliliswa na kunyanyaswa kingono ni wale walioajiriwa kufanya kazi za nyumbani, hususani wasichana, na/au watoto wa mitaani. Watoto wasio na wazazi/walezi au waotenganishwa hali kadhalika wale ambao ni viongozi wa kaya zinazoundwa na watoto peke yao wanalamikia kutafuta kazi za kulipwa. Waajiri wanaotumikiwa na watoto wa kununuliwa (watumwa) mara nyingi huwakandamiza na kuwaweka katika mazingira ambayo ni rahisi kuwadhalilisha na kuwanyanya.

Wasichana waliozaa wakiwa na umri mdogo

Wakati wa kuwashughulikia wasichana waliozaa wakiwa na umri mdogo, ni muhimu kudumisha mtazamo usio wa hukumu wakati wote.

Mara nyingi, wasichana wanaozaa wakiwa na umri mdogo na papo hapo hawana uwezo wa kukidhi mahitaji yao wala yale ya watoto wao wanakuwa katika hatari ya kunyanyaswa kingono ili waweze kukidhi mahitaji yao ya lazima pamoja na kujipunguzia hali yao ya umaskini. Wasichana wadogo wenye watoto na wajawazito kutokana na vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono hukabiliwa na hatari ya kutengwa, kubaguliwa na hata kunyanyapaliwa—hali ambazo zinaweza kuwasababishia kushindwa kupatiwa huduma za lazima. Mambo yote haya yanaweza kuwasababishia hatari zaidi za kudhalilishwa na kunyanyaswa kingono

Ni jambo muhimu sana kuhakikisha kwamba mara tu baada ya kujifungua wasichana wadogo wanaendelea na masomo shuleni au wanashirikishwa katika shughuli za kijamii na kiuchumi ili kuzuia uwezekano wa kuendelea kukabiliwa na hatari zaidi za kudhalilishwa na kunyonywa kingono na kijinsia.

Watoto wanaotokana na athari za vitendo vya ubakaji

Kuna uwezekano mkubwa wa watoto wanaotokana na athari za vitendo vya ubakaji kuonewa au hata hutekelezwa na mama au familia zao. Watoto wa aina hii wanakabiliwa na hatari kubwa mno ya kufanyiwa vitendo vya kudhalilishwa na kunyanyaswa, na hivyo wanahitaji sana ulinzi na ufuatiliaji. Aida kuna haja ya kuhakikisha kwamba familia na hata jamii haziwafanyii watoto au mama zao hawa vitendo vya kuwanyanyapaa. Juhudi zifanyike ili mtoto aliyekataliwa, au aliyetelekezwa au anayedhalilishwa kwa aina yoyote ile atafutiwe mahali bora

pa kuishi na hata ikiwezekana kufanyiwa mipango ya kupatiwa wazazi wa walezi.

Wavulana walioathiriwa

Tabia ya kulawiti watoto wa kiume ni vitendo visivyotambulika, kuripotiwa wala haishughulikiwi ipasavyo. Kutokana na sababu fulani zinazohusiana na masuala ya utamaduni, imani za kisasili, na miiko kuhusu vitendo vya kujamiana kwa jinsia moja, ni vigumu na/au aibu kubwa kwa wavulana, kuliko ilivyo kwa wasichana, kutoa taarifa ya kudhalilishwa kingono . Jamii zinaweza kukataa au kukubali shingo upande kwamba wavulana wanaweza kuathiriwa na vitendo kama hivi na wavulana wenyewe wanaweza kuamini kwamba wanapaswa ‘kukabiliana na aibu hii’ kimya kimya.

Watoto wahalifu

Watoto, kama walivyo watu wazima, wanaweza pia kufanya vitendo vya udhalilishaji wa kingono na kijinsia kwa kujinufaisha kutokana na tofauti za kimamlaka.zilizopo kati yao Kumlazimisha msichana au mvulana kufanya naye vitendo vya kujamiihana bila idhini yake ni aina mojawapo ya udhalilishaji wa kingono. Bila kujali ridhaa yake, mtoto mdogo anaweza asifahamu kitu kinachoendelea na kuridhia kwa usahihi. Jambo hili pia ni udhalilishaji wa kingono .

Kihoro cha mwathiriwa na haja ya mharifu kurekeblishwa, mambo yote kwa pamoja, yanapaswa kushughulikiwa. Mtoto mhalifu anaweza pia akawa mwathiriwa wa vitendo vya kingono na kijinsia na hivyo kuhitaji msaada na ulinzi. Wakati ambapo ni kweli kuwa idadi kubwa ya wahalifu wana historia ya udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono, si kweli kwamba idadi kubwa ya waathiriwa wa vitendo hivyo nao huwadhalilisha watoto. Vijana wengi wanaofanya vitendo hivyo wakati wa umri wa balehe, kwa kawaida huachana na tabia hiyo wakati wa utu uzima wao hasa baada ya kupata msaada na ushauri nasaha wakiwa bado wadogo.

Watoto wahalifu wanastahili kulindwa dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wanapokuwa gerezani. Jambo hili linaweza kufanikishwa kwa njia mbili: kuunda mfumo wa kutatua kesi haraka iwezekanavyo na kujenga tabia ya ufuatiliaji wa matukio kama hayo. Aidha watoto kama hao wanahitaji marekebisho ya kisaikolojia na kijamii. Mahali ambako hakuna sheria na michakato inayoshughulikia usalama wa watoto wahalifu kuna haja ya kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo au kuhimiza uzingatiaji wa sheria na michakato hiyo kama tayari ipo.

Rejea pia:

- **Mwongozo wa Kanuni zitumikazo miongoni mwa Mashirika kuhusu Watoto wasio na wazazi/walezi au waliotenganishwa (Inter-Agency 2003)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Masuala Muhimu: Watoto Walioengwa UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children Revised 2002)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Masuala Muhimu: Ulemavu (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children 2001)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Masuala Muhimu: Askari Watoto, (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children 2000)**
- **Itifaki ya Hiari kwa CRC kuhusu Ushirikishaji Watoto katika Migogoro inayohusisha Mapigano (2000)**
- **Marekebisho ya Miongozo kuhusu vigezo na viwango vinavyotumika juu ya Kuzuiliwa kwa Waombaji wa Hifadhi ya Kisiasa (UNHCR 1999)**
- **Kiongozi kitumikacho baina ya Mashirika kuhusu Afya ya Uzazi kwa hali za Wakimbizi (Inter-Agency 1999)**
- **Sheria ya Roma kuhusu Mahakama ya Kimataifa ya Kusikiliza Kesi za Jinai (1998)**
- **Watoto wakimbizi : Miongozo kwa ajili ya Ulinzi na Utunzaji wao (UNHCR 1994)**
- **Itifaki ya Ziada kwa Makubaliano ya Jiniva ya mwaka 1949 kuhusu Ulinzi wa Mateka/waathiriwa wa Migogoro inayojumuisha vita baina ya mataifa (1977)**

Aina mahususi za vitendo vyatya unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya watoto

Kwa mujibu wa majadiliano katika Sura 1, watoto wanaweza kuwa waathiriwa wa aina nyingi za unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Hata hivyo, mara nyingi watoto hukabiliwa zaidi na aina zifuatazo za vitendo unyanyasaji:

- Vitendo hatari vyatya kimila na kitamaduni.
- Biashara ya magendo ya watoto.
- Ukahaba wa watoto.
- Unyanyasaji wa kingono ndani ya familia.
- Unyonyaji, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono, unaofanywa na wazazi au walezi au watu karibu na watoto .

Vitendo hatari vya kimila na kitamaduni

Jamii za wakimbizi zinapaswa kuhimizwa kuheshimu na kuzingatia mila na desturi nzuri za kijadi kama njia mojawapo ya kudumisha utambulisho na utamaduni wao. Lakini baadhi ya mila na desturi zina madhara kwa afya, ustawi na makuzi ya watoto. Mila na desturi za aina hiyo zinalaaniwa na kukataliwa duniani kote kwa sababu ya madhara yake kwa afya pamoja na uvunjaji wa hakiza binadamu. Mila na desturi dhalimu mara nyingi hufanywa wakati wa utoto ambapo mtoto hana uwezo wowote wa kuzipingga. Mila na desturi dhalimu zinazowadhuru na kuwaathiri watoto, hususani wasichana ni pamoja na: ukeketaji, ndoa katika umri mdogo, upendeleo wa watoto wa kiume, ugomvi utokanao na malipo ya mahari, ndoa za kulazimisha, (k.m. baada ya kosa la ubakaji), pamoja na imani za uchawi (k.m. imani kwamba tendo la kujamiiana na mtoto lina manufaa kwa familia).

Utoroshaji wa watoto

Watoto wakimbizi, hususani wale wasio na wazazi/walezi au waliotenganishwa, hukabiliwa na hatari ya kurubuniwa au hata kulazimishwa kutoroshwa kwa njia za magendo ili wakafanyishwe biashara za ukahaba. Maana halisi ya utoroshaji wa watoto inajumuisha mambo yafuatayo: kumrubuni, kumsafirisha, kumhamisha, kumhifadhi na kumpokea mtoto kwa lengo moja tu la kumnyonya. Hapana haja ya kudhihirisha matumizi ya nguvu, udanganyifu au vitisho ili kuthibitisha madai ya kufanyika kwa magendo ya aina hii.

Itifaki ya Kuzuia, Kuzima na Kuadhibu Biashara ya Kuwauza Watu, hususani Wanawake na Watoto ambayo ni Kijalizo cha Mapatano ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Makosa ya Jinai Yanayovuka Mipaka ya Mataifa, 2000 haijumuishi kuwepo kwa "Ridhaa" kutoka kwa mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. Mara nyingi biashara hii ya kuuza watu hufanyika kwa kutanguliza malipo au mafao mengine kwa ajili ya kupata ridhaa ya mtu/watu wenyewe mamlaka na udhibiti juu ya mtoto. Watoto waliouzwa wanapofanikiwa kutoroka utumwani au anaporudi aghalabu hukabiliwa na hatari za aina nyingi. Waliohusika na biashara hiyo wanaweza kuwafanya watoto hao waliofanikiwa kutoroka utumwani mambo yafuatayo: kulipiza kisasi, kuwakamata na kutoroshwa tena, kuwadhuru kimwili au kuwanyang'anya tena uhuru wao, kuwatenga katika jamii na familia au hata kuwabagua kabisa.

Ukahaba wa watoto

Ukahaba wa watoto humaanisha kumshirikisha mtoto katika vitendo vya kujamiiana kwa ajili ya malipo. Sheria zote za

nchimakosa ya jinai na utoaji adhabu kuhusiana na vitendo vya ukahaba unaowahuisha watoto zinapaswa kujumuisha mambo yafuatayo: kutafuta, kusaka, ukuwadi, au kumtoa mtoto kwa ajili ya ukahaba. Kimsingi, ukahaba wa mtoto ni unyonyaji wa kingono . Pindi watoto wakimbizi wanaposhiriki katika vitendo vya ukahaba papo hapo wanajiweka katika hatari zaidi ya kufanyiwa vitendo vingine vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Ufukara pamoja na tofauti za kijamii huwasababishia watoto wakimbizi hatari kubwa zaidi za kunyonywa kingono , hususani kuptitia ukahaba. Watoto, hususani wasichana, ndio wanaokabiliwa na hatari kubwa zaidi kwa sababu wahalifu wao wanawathamini zaidi kutokana na imani kwamba bado ni mabikira, watakatifu, na wachanga kimwili.

Unyanyasaji wa kingono unaotokea ndani ya familia

Vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji wa mtoto vinavyotokea ndani ya familia vinatoa changamoto kubwa kuhusiana na suala la ulinzi wa watoto kwa sababu mtu anayetegemewa kumlinda na kumlea mtoto, mara nyingi akiwa ni jamaa yake wa kiume, huwa hatekelezi wajibu wake. Mara nyingi unyanyasaji wa kingono unaotokea ndani ya familia huchukuliwa kama masuala binafsi ambayo hayahitaji kuingiliwa au kuwahuisha watu wa nje. Kwa hiyo mtoto husika anaweza hata akalaumiwa kwa tukio la uovu aliofanyiwa na akaendelea kunyanyasika. Kwa hakika si jambo rahisi kutoa mwongozo wa jumla unaoweza kutumika katika kukabiliana na matukio ya aina zote. Hata hivyo, maandalizi ya utaratibu wa kumlinda mtoto yanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo: uainishaji wa kitendo, uadilifu na usiri wakati wa kutoa taarifa kuhusu madai ya matukio, ushirikishaji wa wahudumu wa afya, walimu, viongozi wa jamii pamoja na uchunguzi yakinifu wa matukio husika. Wakati mwingine inaweza ikasaidia au hata ikawa lazima kumshirikisha mzazi ambaye hamfanyii vitendo vibaya mtoto wake, na papo hapo kumwondoa mhalifu/mhalifu katika familia wakati wote wa uchunguzi wa tukio.

Katika familia ambamo mmoja wao au zaidi amenusurika au anakabiliwa na udhalilishwaji wa kingono na kijinsia, watoto wote wa familia hiyo hata kama wao siyo walengwa wa moja kwa moja bado wanakabiliwa na matatizo ya aina nyingine. Inawezekana kabisa kwamba kwa kushuhudia vitendo hivyo viovu watoto hao waliathiriwa kisaikolojia na kifikra. Kwa sababu hiyo wanahitaji sana huduma za ushauri na maoni kutoka kwa wataalam husika. Zaidi ya hapo, matukio ya kuumiza yanaweza kumpunguzia mtu mzima uwezo wa kuwatunza watoto wake; katika hali kama hiyo wazazi na watoto wa familia husika wanapaswa kufuutiliwa kwa makini sana.

Unyonyaji, Udhalilishaji na Unyanyasaji wa kingono Unaofanywa na Watu wenyewe Uhushiano wa Karibu dhidi ya Watoto

Unyonyaji, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono unaweza kufanyika pale watu wasio wanafamilia wanapokuwa na fursa zisizo na vikwazo vyovyote za kuwfikia watoto katika mazingira yaliyojtenga. Watu hao wanaweza kuwa walimu, wakufunzi wa kidini, wasimamizi, watoa huduma za kibinaadamu na wengine wanaoweza kuwfikia watoto wawapo shulen, wakati wa baada ya shule na shughuli za kidini, michezoni, vituo vya kulelea watoto n.k. Ikiwa ni hatua ya kwanza ni muhimu kubainisha vyanzo hivi muhimu vya hatari. Mikakati ya kukabiliana na hatari za aina hii inaweza kujumuisha uchujaji makini wa waajiriwa na watu wa kujitolea, kupunguza fursa za muda ambaو watu hao wanaweza kuka na watoto bila kuwepo watu wazima wengine, ufuatiliaji na usimamizi wa karibu, matumizi ya majengo yasiyo na sehemu za maficho na ushiriki mkubwa wa wazazi katika shughuli za watoto wao.

Rejea pia:

- **Utekelezaji Haki za Watoto (ARC) Masuala Muhimu: Udhalilishaji na Unyonyaji (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children Revised 2002)**
- **Chagua kwa Uangalifu (ECPAT Australia 2001)**
- **Itifaki ya Hiari kwa CRC kuhusu Uuzaji wa Watoto, Ukahaba na Ponografia ya Mtoto (2000)**
- **Mapatano kuhusu Uzuiaji na Hatua ya Haraka kwa ajili ya Ukomeshaji aina mbaya za kazi za lazima kwa watoto, C 182 (1999)**
- **Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Ukomeshaji wa Vitendo vya Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake (1994)**

Mazingatio muhimu katika Uzuiaji wa Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia dhidi ya Watoto

Pamoja na mikakati ya kuzuia unyanyasaji wa kingono na kijinsia kujadiliwa katika Sura ya 3, uchambuzi wa hali ya uzingatiaji mtoto utasaidia kubainisha maeneo mahususi ya hatari, nyenzo zinazohitajika pamoja na mkabala ambaو unashirikisha sekta anuwai kwa wakati mmoja. Aidha pana haja ya kuchambua kwa makini na kuunga mkono wajibu wa jamii ya wakimbizi katika kulinda watoto wao.

Kubadili desturi za kijamii-kitamaduni

MKAKATI:

Imarisha Taarifa, Elimu, Mawasiliano (IEC)

- Kampeni za kukuza uelewa wa suala la unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya watoto sharti zikitwe kwenye CRC na Itifaki zake mbili za Hiari. Aidha kampeni hizo ziwalenge wabia wote, pakiwemo jamii ya wakimbizi, majeshi na vikosi vya kulinda amani.
- Utetezi sharti ukitwe kwenye desturi na maadili ya kijadi kwa ajili ya ulinzi wa watoto pale ambapo mambo haya yapo na wakati huohuo yatoe changamoto dhidi ya fikra zitokanazo na mazoea ya udhalilishaji wa kijinsia (k.m. kushughulikia ukweli kuwa wavulana wanaweza kuwa waathiriwa). Juhudi zozote za ukabilianaji zinapaswa kukitwa kwenye uelewa kamili wa desturi za kijadi, mila na miiko kuhusu tabia za kijinsi.
- Kampeni za afya ya jamii kuhusu "ngono salama" pamoja na uenezaji wa VVU/UKIMWI zinaweza kusaidia kufuta visasili vinavyozunguka miongoni mwa wakimbizi, kwa mfano, imani kwamba kufanya mapenzi na msichana bikira hutibu VVU/UKIMWI. Kampeni hizi ziwalenge wanaume na wavulana.
- Mikakati ya kuzuia vitendo hatari vya kitamaduni mara nyingi hupingana na desturi madhubuti za kitamaduni hivyo ni muhimu sana kuzingatia mambo hayo. Kunahitajika uelewa kamili wa asili na uzito wa mila mahususi, chimbuko lake pamoja na athari zake. Elimu na taarifa zinazosisitiza matokeo yenye madhara kwa afya na ukuaji wa watoto, badala ya ile inayohusu sheria au haki za binadamu, yanaweza kufanikiwa zaidi. Elimu juu ya mambo hayo inapaswa kuelekezwa kwa viongozi wa kidini wa kike na kiume, viongozi wa kijadi, viongozi wa kikabila, viongozi wa kisiasa, wakunga wa jadi, watoaji wengine wa huduma za afya, na watoto wakimbizi, wanawake na wanaume. Makundi ya kijadi yanayopinga desturi hatari za kijadi yanastahili kuungwa mkono kwa sababu yanaweza kubuni na kuongoza hatua za kufutilia mbali mila hizo potofu za kitamaduni. Shughuli mbadala za upatikanaji kipato kwa ajili ya watu wanaoendeleza mila na desturi hizo potofu zinaweza kubainishwa na heshima ya watu hawa katika jamii idumishwe. Umuhimu wa kuwaelimisha wasichana na wanawake usipuuuzwe kwakuwa vitendo vya kimila na tamaduni potofu vinahusiana sana na ukosefu wa elimu.

MKAKATI:**Shirikisha watoto na vijana**

Ni jambo muhimu kuwahimiza watoto wakimbizi kushiriki katika kubuni na kutekeleza programu zinazohusu masuala ya unyonyaji na udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Kila inapoonekana inafaa, na baada ya uzingatiaji makini wa maslahi bora kwa watoto, watoto waathiriwa wanaweza kuombwa ushauri au kualikwa kuja kushiriki.

MKAKATI:**Fanya kazi na wavulana**

Kufanya kazi na wavulana ni muhimu ili kuhakikisha kuwa wanafahamu na wanaelewa kuwa wana haki sawa na wasichana. Kuelewa huko kutawawezesha kwa mfano, kuwasaidia dada zao katika kupata elimu na kukuza mtazamo chanya pamoja na heshima dhidi ya wasichana wawapo darasani au katika viwanja vya michezo

Kujenga upya mifumo ya kusaidia familia na jamii**MKAKATI:****Hakikisha upatikanaji wa elimu**

Kiwango cha hatari za vitendo vya unyonyaji kinaweza kupunguzwa kwa kuhakikisha kwamba watoto wakimbizi wote wanapatiwa elimu ya msingi na kila inapowezekana, elimu ya sekondari na mafunzo ya ufundi. Aidha programu zilizoandaliwa mahususi kwa ajili ya mahitaji ya wasichana walioacha shule zinaweza kusaidia pia kupunguza tatizo hili. Watoto wakiel mishwa kuhusu haki zao kuitia mifumo anuai ya mafunzo ya stadi maisha na kijamii kutawasaidia pia vijana kufanya maamuzi bora ya kimaisha na kuwasaidia kujikinga dhidi ya unyanyaswaji. Ushirikishwaji sawa wa wasichana shulenii unapaswa kuendelezwa.

Jamii ishirikishwe kikamilifu katika kuajiri na kusimamia walimu na waelimishaji wanaodhani wanaweza kuwaamini, kwakuwa walimu wanaweza kuwa wadhalilishaji wa kingono wa watoto. Aidha inapendekezwa kwamba zichukuliwe hatua mahususi na za makusudi kuwaajiri walimu wa kike. Wataalamu wa masuala ya elimu waliochaguliwa kwa makini washirikishwe katika kufuatilia watoto kwa ajili ya ishara za unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Wasichana wapewe nguo zinazofaa pamoja na vifaa

muhimu kwa ajili ya usafi wao. Kadhalika uanzishaji wa klabu za wasichana baada ya wakati wa shule kunaweza kutoa fursa ya ushauri wa kirika na usaidizi.

Kuweka Mazingira ya Kuboresha Mifumo ya Uwajibikaji

MKAKATI:

Tathmini na chunguza watu walio na uhusiano wa karibu na watoto wakimbizi

Kutathmini maarifa, fikra na tabia za watu wote walio karibu na watoto wakimbizi kunaweza kufichua unyonyaji katika mazingira yasiyotarajiwa, mathalani, shulenii na katika vituo vya kulelea watoto. Mafunzo kwa wafanyakazi kama hao na ufuatiliaji wa kazi zao ni mambo muhimu katika mkakati wowote wa kuzuia unyonyaji na unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa watoto.

Kubuni Huduma na Nyenzo Madhubuti

MKAKATI:

Msajili Kila Mtoto

Usajili na uwekaji kumbukumbu, ikijumuisha usajili wa uzazi, ni muhimu kwa kila mkipimo, hususani kwa watoto wasio na wazazi/walezi na waliotenganishwa, kwakuwa usajili wao ni sharti la msingi katika kupata haki na huduma. Usajili husaidia pia katika kubainisha na kufuatilia makundi ya watoto wanaokabiliwa na hatari maalum, kusaidia upatikanaji wa haki kwa mujibu wa sheria zinazotawala haki za watoto, kuzuia kuandikisha watoto jeshini pamoja na kuzuia biashara ya watoto.

MKAKATI:

Hakikisha Upatikanaji wa Huduma

Hakikisha kuwa watoto wanapata mgao wa chakula na huduma zingine unaolingana na wanaopewa watu wengine na fikiria kuwapa misaada ya ziada kama inahitajika, kwa mfano, kwa kujenga makazi maalumu kwa ajili ya kaya zinazoongozwa na watoto.

MKAKATI:**Tafuta Familia**

Mahitaji ya watoto wasio na wazazi/walezi na waliotenganishwa yashughulikiwe haraka kwa njia ya kutafuta familia zao; kuwapatia makazi ya muda yanayofaa na aina zinazofuatiliwa za matunzo ya muda na uunganishaji wa familia, iwapo ni maslahi bora ya mtoto mwenyewe.

MKAKATI:**Wahusishe Watoto katika Kubuni, Kupanga, Kutekeleza Shughuli**

Watoto wakimbizi, hususani walio katika umri wa balehe, wanapaswa kushirikishwa katika kupanga kambi/makazi, ikiwa ni pamoja na maeneo ya shule na sehemu za burudani/michezo na katika ugawaji wa nyumba za kuishi na shughuli na mipango mingine inayohusika.

Rejea pia:

- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Masuala Muhimu: Udhalilishaji na Unyonyaji (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children Revised 2002)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Asasi: Uhamashajii wa Jamii (UNHCR, OHCHR UNICEF, Save the Children 2001)**
- **Utekelezaji wa Haki za watoto (ARC) masuala muhimu watoto Waliotenganishwa (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children Revised 2002)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Asasi : Uchambuzi wa Hali (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children 1999)**
- **Hiiimisho la Kamati Tendaji ya UNHCR kuhusu Usajili wa Wakimbizi na Waombaji wa Hifadhi ya Kisiasa, Na. 91 (LII) (2001)**

Mazingatio Muhimu katika Kukabiliana na Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia dhidi ya Watoto

Kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia kunapaswa kujumuisha vitendo na huduma zilizoelezwa katika Sura ya 4. Masuala ya ziada yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa

kuwashudumia watoto yamejadiliwa pia katika utekelezaji wa Haki za Watoto, Mambo Muhimu: Udhaililishaji na Unyonyaji (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children, 2001).

Zingatia maslahi bora ya mtoto.

Watoto waliotendewa au wamenusurika na udhalilishaji wa kingono wanahitaji kupeta huduma za matibabu ya haraka na msaada wa kisaikolojia. Aidha wanaweza kuhitaji huduma za kisheria.

Vitendo vyote lazima vikubaliane na maslahi bora ya mtoto Maelezo ya mtoto mwenyewe kuhusu matakwa na hisia zake yatumike kubaini maslahi yake bora.

Anzisha taratibu za kurufaa, kuripoti, kufuatilia na kutathmini zinazoenda na watoto.

Nimuhimu kuwa na mbinu za kuripoti zinaendana na watoto, zilizo bayana na zinazofahamika vyema zikisimamiwa na wafanyakazi na au wakimbizi wenyewe uzoefu na ujuzi. Toa kwa pamoja taarifa za vitendo vya unyanyasaji wa Kingono na kijinsia ndani ya mchakato wa utoaji taarifa unaoshughulikia uvunjaji mwingine wa haki za watoto, badala ya kuanzisha mchakato tofauti wa kushughulikia taarifa za unyanyasaji wa Kingono na kijinsia dhidi ya watoto.

Ufuatiliaji wa watoto walio hatarini, kama wale wasio na wazazi/walezi na waliotenganishwa katika makazi ya muda, watoto wanaoishi katika familia zinazojitolea kulea watoto, watoto wa mitaani, watoto waliowekwa kizuizini, wasichana waliozaa wakiwa na umri mdogo, pamoja na watoto walemavu ni muhimu kwa utoaji ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa Kingono na kijinsia.

Kusaili Mtoto

Msaili wa mtoto anapaswa kuwa na maarifa ya hali ya juu na aliyefundishwa vema na anayeweza kudhibiti mhemko mkubwa wa mtoto na anayeweza kumfanya mtoto kuelezea kwa ufasaha masuala magumu sana. Aidha kuelewa utamaduni wa mtoto ni muhimu sana: kwa sababu hiyo inafaa zaidi kama watu wanaoshughulikia watoto wakimbizi wangekuwa wanaongea lugha moja na wanatokana na utamaduni mmoja.

Kwa ujumla, inapendekezwa pia msaili awe wa jinsi moja na mtoto anayesailiwa. Hata hivyo masuala ya kitamaduni na kijamii ni muhimu kuzingatiwa wakati wa kuamua jinsi ya msaili. Kwa mfano, katika jamii nyingi, wavulana huona aibu kuwaelezea waziwazi wanaume wenzao kuhusu kitendo cha kulawitiwa, badala yake huweza kujisikia huru zaidi kumwelezea mwanamke.

Kuandaa Mazingira Salama

Kuandaa mazingira salama huhusu uamuzi wa watu gani wanapaswa kuwepo wakati wa usaili na uchunguzi. Inawezekana mwanafamilia akawa ndiye mtenda uovu hata kama mtoto anakana ukweli huo. Inaweza ikawa bora zaidi iwapo mzazi au mlezi akatoka nje wakati wa usaili na uchunguzi na badala yake awepo mtu huru lakini ambaye ni mwadilifu na mwaminifu. Inashauriwa kumuuliza mtoto faraghani kama angependelea mzazi au mlezi wake awepo au la wakati wa usaili na majibu yake yaheshimiwe. Kwa mwongozo zaidi tazama sehemu kuhusu Stadi za Uhojaji na Maandalizi na Uendeshaji wa Usaili katika Jinsi ya Kuwashudumia Watoto Wasio na Wazazi/Walezi: Mkabala wa Kijamii.

Kumbuka kwamba kuna njia nyingine za kukusanya taarifa, mathalani, kupitia kwenye michezo, utambaji hadithi, drama, pamoja na kuwaomba watoto kuchora picha. Mbinu hizi zinahitaji ujuzi wa hali ya juu wa uchunguzi na uchambuzi wa wataalamu au wafanyakazi walifundishwa vema.

Mbinu za Usaili

- **Kama mila na desturi zinaruhusu mkae kwa jinsi ambayo mtawezza kuangaliana machoni.**
- **Mhakikishie mtoto kwamba hayuko katika hatari yoyote na jitahidi kumtunzia heshima yake ya kimwili/kiutu.**
- **Jitambulishie wewe mwenyewe (na mkalimani) na ueleze kwa ufasaha madhumuni ya usaili, aina ya maswali yatayouлизwa na sababu zake. Hatua hizi zinachukuliwa ili kumwondolea mtoto hofu na mashaka—mambo ambayo kama hayatawekwa sawa yanaweza kumfanya mtoto kutoa majibu potofu.**
- **Mhakikishie mtoto kwamba anaweza kujibu swali lolote kwa kusema “Sijui” na anaweza kuuliza maswali.**
- **Muulize mtoto maswali machache ya kawaida ambayo si sehemu ya malengo halisi ya usaili, kwa mfano, kuhusu shule yake, marafiki zake, watu anaoishi nao, mambo anayoyapendelea kuyafanya, na mruhusu mtoto aongee kwa dakika chache. Hatua hii itamfanya mtoto kujenga hali ya kujiamini zaidi na kukuwezesha wewe kumsikiliza na kujifunza jinsi mtoto anavyowasiliana.**
- **Kama mtoto anaona shida kuzungumzia tukio fulani, lakini anaweza kujibu maswali mengine, basi ahirisha kumuuliza maswali juu ya tukio hilo walau kwa kipindi fulani.**
- **Kuwa mstahimilivu, endesha usaili kulingana na kasi wa mtoto mwenyewe uliza maswali wazi yanayohitaji majibu huru ili mtoto aweze kukupatia maelezo kamili kuhusu tukio kwa maneno yake mwenyewe. tumia maswali ambayo majibu yake ni ‘ndiyo’ au ‘hapana’ kwa lengo moja tu la kupata ufanuzi wa suala husika.**
- **Jiandae kutambua wakati ambao mtoto amefikia kikomo cha uwezo wake.**
- **Usaili uhitimishwe kwa kujadili matukio ya kawaida ya siku hiyo ili kumrejeshea mtoto hisia za usalama.**

Kuandaa Namna ya Kukabiliana na Mahitaji ya Kiafya/Kitiba ya Waathiriwa/ Wanusurika.

Usimshurutishe, usimshinikize wala usimlazimishe mtoto mwoga au mkaidi kukamilisha usaili au uchunguzi. Njia zinazojumuisha kumzuilia mtu, kumlazimisha kumshurutisha au kumrubuni, mara nyingi hutafsiriwa kama sehemu ya udhalilishaji wa kingono na kama mbinu hizo zikitumiwa na watu wanaajaribu kumsaidia, badala ya kufanikisha lengo lao, zitaongeza tu hofu na wasiwasi wa mtoto, na hivyo kuzidisha madhara ya kisaikolojia yatokanayo na maovu aliyotendewa.

Mbali na kuandaa mazingira mazuri na yanayoimarisha uaminifu, mwandae mtoto kwa ajili ya uchunguzi na kumhimiza kuuliza maswali wakati wowote wa usaili juu ya kitu chochote kinachomhusu au jambo lolote asilolifahamu.

Maandalizi mazuri huwawezesha watoto wengi kushiriki vyema usaili na kwa kujiamini pia.

Inawezekana mtoto akawa ana maumivu na kwa sababu hiyo akashindwa kukaa kwa utulivu na kushiriki vizuri usaili. Ni vizuri kutumia lugha nyepesi na anayoelewa mtoto kumwelezea mambo yatakayotakea wakati wa usaili na uchunguzi.

Mara nyingine inafaa kuwa na doli au mwanasesere kwa ajili ya kuelezea mienendo na misimamo. Mwonyeshe mtoto vifaa, kwa mfano, glovu, sifongo, n.k. na umpatie ruhusa ya kutumia vifaa hivi kwenye doli.

Kuna uwezekano wa wasichana waliofanyiwa waliodhalilishwa kukabiliwa na matatizo ya kiafya yatokanayo na kuharibu mimba wao wenyewe, kwa mfano, yale yanayohusiana na utoaji mimba, mimba zisizohitajika na kuharibika kwa mimba. Baadhi yao wanaweza kuwa na watoto wao wenyewe na hivyo kuhitaji utunzaji maalumu. Aidha kuna uwezekano pia watoto walioathiriwa wakatelekezwa wakawa wameambukizwa magonjwa ya zinaa ukiwemo VVU/UKIMWI.

Wasichana waliookeketwa wanahitaji utunzaji maalumu, hususani wakati wa ubebaji mimba, wakati wa kujifungua na kwa kipindi fulani baada ya kujifungua.

Wasichana wanaozaa wakiwa na umri mdogo wanastahili kupatiwa misaada inayofaa kimatibabu na kisaikolojia kabla na baada ya kujifungua ikiwa ni pamoja na maelekezo kuhusu utunzaji na malezi ya mtoto.

Kupanga namna ya kukidhi mahitaji ya kisaikolojia na kijamii ya waathiriwa / wanusurika

Mtaalamu aliyefundishwa vema kushughulikia watoto anahitajika wakati wa kukabiliana na mahitaji ya kisaikolojia na kijamii ya mtoto. Ni bora zaidi kama mtaalamu huyo atakuwa anachangia kabilia na mtoto au angalau awe mwenye ujuzi wa tamaduni mchanganyiko. Jukumu la mtaalamu huyo linaweza kuwa ni kumhudumia na kumtibu mtoto moja kwa moja au kuwashauri na kuwasaidia wanafamilia au wanajamii watakaota huduma hizo.

Kazi ya kuwarekebisha waathiriwa, ikijumuisha watoto waliowahi kuandikishwa jeshini, huhitaji uangalifu maalumu. Mafunzo endelevu na programu za elimu ya harakaharaka ni muhimu kwa waathiriwa ili kushinda udhalilishaji waliotendewa na kuweza kujijengea maisha mapya ya baadaye.

Inaweza kukawa na umuhimu wa kuwapa wasichana waliozaa wakiwa na umri mdogo uangalizi wa ziada na msaada wa kisaikolojia. Hatua hii inaweza kujumuisha kumsaidia msichana kama huyo kuendelea na masomo yake na kumtafutia shughuli itakayompatia kipato kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake ya lazima na yale ya mtoto wake hata kama bado anaishi na au karibu na familia yake. Wanafamilia wengine watahitaji pia ushauri kuhusu njia bora za kumsaidia msichana huyo na mtoto wake.

Kuwa na Usalama Pamoja na Ukabilianaji Salama

Mtoto asitenganishwe na familia au jamii yake kwa sababu ya matibabu isipokuwa kama hatua hiyo inabidi ichukuliwe ili kumwepushia vitendo vya udhalilishaji au kupuuzwa.

Ni muhimu kuchukua hatua za haraka pale vitendo hatari vya kimila na desturi vinaporipotiwa. Katika vitendo hivi, kunaweza kukawa na uvunjaji wa haki za msingi za mtoto ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi, haki ya kuwa huru, na haki ya kuheshimiwa utu wake. Iwapo usalama wa kimwili wa mtoto unahatarishwa, ufumbuzi wa ndani utafutwe, ikiwa ni pamoja na kumtafutia makazi na malezi nje ya jamii yake. Kama haiwezekani kutumia njia hizo, inashauriwa mtoto huyo ahamishiwe katika nchi nydingine ambako atahakikishiwa usalama wake.

Kuanzisha Ukabilianaji wa Kisheria/Haki

Taarifa zote kuhusu vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya watoto zinapaswa kuchunguzwa kikamilifu. Wafanyakazi wanapaswa wawe wavumilivu na waangalifu

sana dhidi ya taarifa hizi. Mtoto anaweza kukana kudhalilishwa kwa sababu nyingi, ikiwa ni pamoja na hofu dhidi ya mhalifu wake. Matumizi ya mbinu zisizofaa huweza kusababisha fadhaa zaidi mtoto na huweza kuwakatisha tamaa wengine kutafuta misaada. Inapowezekana, wafanyakazi wapewe mafunzo ya jinsi ya kushughulikia masuala ya watoto. Aidha inaweza ikasaidia kuomba msaada kutoka kwa wataalamu wenyewe uzoefu wa kufanya kazi na watoto wakimbizi. Kadhalika wafasiri au wakalimani wanaweza wakahitajika. Hakikisha kuwa jeshi la polisi lina askari walipatiwa mafunzo ya mbinu za kushughulikia masuala ya waathiriwa wa vitendo vya unyanyasaji wa Kingono na kijinsia hali kadhalika wanyanyasaji. Kuhakikishwe kuwa kuna taratibu za kisheria zinazoendana na watoto panapokuwa na kesi zinazohusisha watoto.

Kushirikisha Familia na Jamii

Huduma zinazoilenga familia: Mtoto anapodhalilishwa Kingono, kunaweza kuwepo haja ya kuishauri familia pia ili kuhakikisha inachangia katika jitihada za kumrejesha mtoto katika maisha yake ya kawaida kwa kumwamini, kuungwa mkono na kumpatia misaada anayoihitaji. Wakati mwingine wanafamilia wenyewe wanaweza kuhitaji msaada: mathalani, wazazi wanaweza wakajilaumu kwamba walishindwa kumlinda mtoto wao ipasavyo. Kuna haja ya kuchukua tahadhari kubwa mno hususani kama hisia ya upotevu wa thamani ya mtoto hupelekea familia yake imkatae. Kuna tamaduni kadhaa na mifumo ya kisheria ya kijadi ambapo familia ambayo binti yao amedhalilishwa Kingono, humlazimisha msichana huyo kuolewa na mtu aliyemfanya uonevu kama huo. Katika hali kama hizi kuna haja ya kuchukua hatua za haraka kwa ajili ya kumwepushia mwathiriwa madhara zaidi ya kisaikolojia na kijamii. Kama ni muhimu, hatua zichukuliwe za kumhamisha mwathiriwa.

Huduma zinazolenga jamii: Tahadhari kubwa ichukuliwe ili kuzuia uwezekano wa kumnyanyapaa mwathiriwa. Mifumo iliyopo kwa ajili ya kusaidia jamii pamoja na ile ya kusimamia ustawi wa mtoto, sharti itumike kuimarisha misaada na ulinzi.

Baadhi ya vitendo viovu vya kijadi hufanyika wakati msichana anapokuwa bado na umri mdogo sana, kwa mfano, ndoa za mapema na za kulazimishwa na mila ya ukeketaji. Kuna umuhimu wa kuhimiza uelewa kuhusu matokeo na madhara ya vitendo kama hivi, ndani ya familia na jamii husika. Jukumu hili lifanyike kwa manufaa ya mtoto mwenyewe na jamii nzima kwa jumla.

Rejea pia:

- **Usimamizi wa Matibabu ya Waathiriwa wa Vitendo vyatubakaji (WHO/UNHCR 2002)**
- **Kiongozi cha Maandalizi ya Makazi Mapya (UNHCR 2002)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Masuala Muhimu : Udhaliilishaji na Unyonyaji (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children Revised 2002)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Masuala Muhimu: Askari Watoto (UNHCR, OHCHR, UNICEF, Save the Children 2000)**
- **Utekelezaji wa Haki za Watoto (ARC) Asasi :Makazi Mapya (UNHCR, OHCHR, UNICEF Save the Children 1999)**
- **Kiongozi Kitumikacho Kati ya Mashirika kuhusu Afya ya Uzazi katika Kambi za Wakimbizi (Inter-Agency 1999)**
- **Jinsi ya Kuwashudumia Watoto Wasio na Wazazi/Walezi: Mfumo wa Kijamii (UNHCR 1996)**

Masuala Muhimu ya Kukumbuka

Hatua zote zaukabilianaji kwa lengo kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya watoto zinapaswa kuongozwa na kanuni nne zifuatazo:

- ◎ Haki ya Maisha, kuishi na kukua.
- ◎ Kutokubaguliwa.
- ◎ Maslahi bora ya mtoto.
- ◎ Ushirikishwaji.

Fahamu kwamba makundi yafuatayo ya watoto yanakabiliwa na hatari mahususi za kunyanyaswa kingono na kijinsia:

- ◎ Watoto wasio na wazazi/walezi au waliotenganishwa.
- ◎ Watoto wanaoishi kizuizini.
- ◎ Watoto-wanajeshi (wanaofanyishwa kazi za kijeshi).
- ◎ Vijana walio katika umri wa balehe.
- ◎ Watoto walemavu wa akili na wa viungo.
- ◎ Watoto wanaofanya kazi.
- ◎ Wasichana waliozaa wakiwa na umri mdogo.
- ◎ Watoto watokanao na athari za vitendo vyatubakaji.
- ◎ Wavulana waathiriwa
- ◎ Watoto wahalifu.

Mifano maalumu ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya watoto hujumuisha mambo yafuatayo:

- ◎ Mila na desturi potofu
- ◎ Utoroshaji wa watoto

- ◎ Ukahaba wa watoto
- ◎ Unyanyasaji wa kingono ndani ya familia
- ◎ Vitendo vya unyonyaji, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono vinavyofanywa na watu wanaowafikia kiraishi watoto

Mambo ya kuzingatia wakati wa kubuni na kuandaa hatua za kuzuia vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya watoto:

- ◎ Andaa na kukuza kampeni kwa ajili ya utoaji taarifa na elimu, na kufanikisha mawasiliano.
- ◎ Washirikishe watoto na vijana.
- ◎ Hakikisha upatikanaji wa elimu.
- ◎ Tathmini na uwachunguze watu wanaoshughulika na masuala ya watoto.
- ◎ Buni mifumo ya ufuatiliaji.
- ◎ Hakikisha kuwa kila mtoto anasajiliwa.
- ◎ Hakikisha kuwa walengwa wanafikiwa na huduma husika.
- ◎ Tafuta familia kwa madhumuni ya kuwaunganisha wahusika.
- ◎ Washirikishe watoto katika shughuli zote za kuandaa, kuratibu na kutekeleza mipango.

Mambo ya kuzingatia wakati wa kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya watoto:

- ◎ Anzisha mifumo-rafiki kwa watoto kuhusu masuala ya ukataji rufaa, utoaji wa taarifa, ufuatiliaji na tathmini.
- ◎ Andaa mazingira mwafaka kwa ajili ya kuendeshea usaili na uchunguzi wa mtoto.
- ◎ Mtayariske vizuri mtoto kwa ajili ya kuchunguza afya yake.
- ◎ Hakikisha kwamba watu wanaoshiriki katika kumsaili, kumchunguza na kumshauri mtoto ni wataalamu waliopatiwa mafunzo katika masuala ya kuwashudumia watoto.
- ◎ Shirikisha familia na jamii pia.
- ◎ Andaa huduma zinazohitajika kwa ajili ya familia.
- ◎ Saidia mifumo na miundombinu ya kijamii iliyopo tayari kwa ajili ya kumlinda mtoto.

SURA YA 6

MUUNDO WA UTEKELEZAJI

Programu za kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia ambazo zimepata ufanisi wa hali ya juu ni zile ambazo maandalizi yake yameshirikisha jamii ya wakimbizi kwa upande mmoja, na sekta na mashirika mbalimbali kwa upande mwingine. Timu ya waandaaji inahitaji kubuni mpango wa pamoja wa utekelezaji ili iweze kuandaa programu zinazofaa. Sehemu mpango kama huo wa utendaji zimefafanuliwa hapa chini.

Uandaaji wa Mpango wa utekelezaji

Programu zenye mafanikio ni zile ambazo uandaaji wake umeshirikisha na kujumuisha maoni ya jamii ya wakimbizi, hasa wanawake na vijana. Aidha programu za aina hiyo sharti zijkite kwenye ushirikiano baina ya sekta na mashirika mbalimbali katika mazingira husika. Baadhi ya hatua zinazohitajika katika uandaaji wa mpango wa utekelezaji inabidi zichukuliwe kwa wakati mmoja; lakini hatua nyingine zinaweza kuchukuliwa baada ya kufanya ufuatiliaji na kutathmini mikakati iliyopo kwa ajili ya kuzia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Andaa Mpango wa utekelezaji

- Bainisha na husisha watendaji.
- Jenga uelewa mmoja kuhusu maana ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, na kubalianeni juu ya wigo wa utekelezaji.
- Chambua hali halisi: kwa kukusanya taarifa kwa ajili ya kupata uelewa sahihi wa mahitaji, matatizo, huduma zinazopatikana, pamoja na uwezo na upungufu wa jamii ya wakimbizi.
- Fikia makubaliano kuhusu kanuni za mwongozo.
- Fafanua dhima na majukumu ya watendaji wote.
- Panga malengo na madhumuni; fafanua mambo yanayohitaji kufanyika, shabaha, matokeo na viashiria; bainisha rasilimali zinazohitajika.
- Kubaliana kuhusu mifumo ya ufuatiliaji na tathmini, zikiwemo njia za utoaji taarifa, ukataji rufaa pamoja na mwenendo wa uratibu.
- Jenga mpango wa kudumisha ustawi na ubora wa mazingira ya watumishi na watu wa kujitolea.

Bainisha na Husisha Watendaji

Anza mchakato huu kwa kubainisha washiriki wanaofaa halafu waalike katika mkutano au mikutano kadhaa kwa ajili ya majadiliano. Zoezi la mikutano na majadiliano huamuliwa kulingana na mambo kadhaa, mathalani, idadi ya watendaji, lugha zitumikazo, pamoja na tamaduni zinazohusika. Aidha inawezekana ikaamuliwa kuendesha majadiliano kwa kuzingatia vigezo vingine, kwa mfano, kujadili katika makundi ya jinsia, rika au kabila moja badala ya kujumuisha makundi yote hayo katika mkutano mmoja tu. Inashauriwa kwamba idadi inayofaa ya watendaji wa kuhudhuria majadiliano ya aina hii iwe kati ya watu 15 na 20 badala ya makundi makubwa zaidi. Kadhalika inasisitizwa kwamba majadiliano yanayokuwa na matokeo mazuri zaidi ni yale ambayo watendaji wake wanajumuisha wanawake, wanaume, vijana, viongozi na wawakilishi wa vikundi vyta wanaharakati katika jamii.

Inatarajiwa kuwa watendaji muhimu watatoka walau kwenye:

- ◎ Viongozi wa wakimbizi—wanaume kwa wanawake.
- ◎ Makundi ya wanawake na vijana wakimbizi
- ◎ Makundi ya wakimbizi na watu wenye ushawishi katika jamii (k.m. waumini wa madhehebu ya kidini na wanachama wa asasi za kitamaduni, wataalamu wa masuala ya elimu na wanataluma wengine).
- ◎ Wawakilishi wa jamii za wenyeji
- ◎ Wawakilishi wa serikali ya nchi mwenyeji kutoka: ofisi ya kusimamia wakimbizi, majeshi ya polisi na usalama, idara ya mahakama na vyombo vingine vinavyosimamia utoaji wa haki, wizara ya afya, vitengo vinavyohusika na masuala ya maendeleo, ustawi wa wanawake, familia, na watoto.
- ◎ Watoa huduma za afya
- ◎ Mashirika ya huduma za kijamii
- ◎ Makundi ya wataalamu wa utoaji ushauri, pamoja na watumishi wa vituo vya kudhibiti vurugu
- ◎ AZISE za kitaifa na za kimataifa zinazojishughulisha na masuala haya, wakiwemo wataalamu wa kusimamia na kuendesha kambi za wakimbizi
- ◎ Wanasheria wazalendo ambao wanafahamu sheria za nchi zinazohusu unyanyasaji wa kijinsii na kijinsia
- ◎ Wakuu wa ofisi za UNHCR na watumishi wa ugani, maofisa na wasaidizi wa vitengo vya hifadhi, huduma za jamii, ulinzi na programu
- ◎ Mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN)

Inafaa washiriki katika mikutano ya majadiliano wapatiwe nakala za Mwongozo wa Kanuni hizi ili wausome na kuuchambua kabla ya mikutano. Kama jambo hili haliwezekani inapendekezwa kwamba iandaliwe semina kuhusu Mwongozo wa Kanuni, mapema kabla ya mkutano, kwa ajili ya kuwaelimisha watendaji ambao hawakuweza kusoma kabla ya mkutano. Kwa kufanya hivi watendaji wote watafika mkutanoni wakiwa na maandalizi yanayolingana.

Unaweza kujumuisha mambo yafuatayo katika mkutano wa kwanza na washiriki:

- ◎ Warsha ya nusu siku kwa ajili ya kuwapatia watendaji mafunzo na uelewa wa maeneo haya: haki za binadamu, unyanyasaji wa kingono na kijinsia, pamoja na masuala ya ulinzi.
- ◎ Kuwatumia watu wazoefu kuelezea vipengere mahususi kuhusiana na matukio halisi ya vitendo vya udhalilishajji wa kingono na kijinsia. Maelezo kama hayo yatasaidia kupanua taarifa za watendaji na kuimarisha mshikamano na ushirikiano. Mifano:

 - kiongozi katika jeshi la polisi anaweza akafafanua taratibu na mbinu za kukabiliana na matukio ya ubakaji, magomvi ya majumbani, na aina nyingine za unyanyasaji wa kingono na kijinsia;
 - mwakilishi kutoka kituo cha afya anaweza akaelezea huduma za afya zinazopatikana kwa ajili ya kukabiliana na dharura za vitendo viovu, taratibu za kupata huduma hizo, na/au mahitaji ya kituo chake kwa ajili ya kuboresha huduma na mafunzo ya watumishi;
 - afisa hifadhi anaweza akawaelezea watendaji kuhusu viwangoyahakizabinadamuzakimataifavinavyokubalika na akatumia takwimu/data kutokana na ripoti za matukio zilizopokelewa karibuni—mwaka, robo mwaka au hata mwezi uliopita;
 - mwanausheria wa nchini anaweza akawaelimisha watendaji kuhusu sheria za taifa na taratibu zake;
 - mwakilishi wa wakimbizi anaweza akaelezea mtazamo wa jamii kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia na jinsi ambavyo matukio kama hayo yangeshughulikiwa katika nchi walikotoka.

- ◎ Mjadala kuhusu Kanuni zenyewe katika mwongozo, hususani sehemu ya Uchambuzi wa Hali Halisi (angalia hapo chini) na jinsi ya matumizi yake.
- ◎ Kufanya uamuzi kuhusu ‘shirika kiongozi’ katika masuala ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia (maana ya shirika

kiongoziimeelezwapiakatikasehemuinayoelezeaUratibu). Shirika hilo litawajibika pia na kazi za kuitisha mikutano, kusambaza ripoti, na kufuatilia hali ya ushirikiano baina ya sekta na mashirika mbalimbali kuhusiana na mipango wa utekelezaji.

- ◎ Mjadala na makubaliano kuhusu mpango-shirikishi kwa ajili ya kukusanya taarifa, kuchambua hali na kukutana tena ili kujadili matokeo na kuanza kuandaa mikakati ya kuzuia na kukabiliana na matukio ya vitendo viovu vilivyodhahirishwa.

Jenga Uelewa Mmoja wa Maana ya Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia, na Kubalianeni kuhusu Wigo wa Utekelezaji

Ni jambo muhimu kwa watendaji wote wakaewa sawa kuhusu maana dhahiri ya istilahi za unyanyasaji wa Kingono na kijinsia na kubaliana kuhusu utaratibu mmoja wa kuripoti matukio. Jambo hili litasaidia kujenga na kuimarisha mkabala mmoja mionganoni mwa watendaji katika kupeana taarifa, kufanya kazi za ufuatiliaji na tathmini kwa pamoja.

Matumizi ya istilahi sahihi na zisizotatanisha yataboresha shughuli zifuatazo: ukusanyaji data sahihi; uchambuzi makini wa hali; ufuatiliaji wa mielekeo; ulinganishaji wa data za vipindi maalumu pamoja na kuhakikisha ufuatiliaji mzuri. Matumizi ya istilahi zinazofanana duniani kote yanasakiya kufanyika kwa mazoezi ya kulinganisha hali za kambi mbalimbali za wakimbizi na yanaweza pia kufanikisha upatikanaji wa data muhimu kwa ajili ya maandalizi ya kuandaa programu na mipango ya maendeleo kwa kifupi mambo ambayo hayakuwepo huko nyuma.

Fanya Uchambuzi wa Hali Halisi

Uchambuzi wa hali halisi ndio msingi wa kukuwezesha kuainisha matatizo, kuelewa mahitaji, na kugundua rasilimali zilizopo. Aidha zoezi hili lincasakiya kujengesha uwezo wa kubainisha malengo, madhumuni, matendo yanayotakikana pamoja na matokeo yanayotarajiwa. Kwa kuwa hakuna shirika moja pekee ambalo ndilo linalowajibika na programu zinazohusiana na masuala ya unyanyasaji wa Kingono na kijinsia, mashirika mbalimbali pamoja na watu binafsi wanapaswa kushiriki katika uandaaji wa uchambuzi wa hali halisi. Aidha hatua ya kuwashirikisha watendaji/wadau wote itasakiya kujenga msukumo uliojikita katika jamii na hivyo kusababisha mapenzi ya programu husika kuanzia hatua za awali kabisa.

Rejea pia:

- **Uzuiaji na Ukabilianaji wa Unyanyasaji wa kingono na Kijinsia: Warsha kuhusu Kupanga Hali pamoja na Kadi za Maelezo (UNHCR 2000)**
- **Tathmini ya Haraka ya Maeneo ya Vijijini na Tathmini ya Ushiriki wa Maeneo ya Vijijini: Kiongozi cha Watumishi wa Uwandani wa CRS na Wabia wao (Catholic Relief Services 1999)**
- **Upangaji Unaotokana na Watu Unavyotumika Kuboresha Kazi za Uandaaji wa Mipango katika UNHCR (UNHCR 1994)**
- **Upangaji Unaotokana na Watu: Mfumo wa Upangaji Unaotokana na Watu Katika Kambi za Wakimbizi kwa Kuzingatia Wanawake, Wanaume na Watoto (UNHCR 1992)**

Kazi ya kukusanya taarifa inajumuisha mapitio ya rekodi zilizopo, kuzungumza na watu, masailiano na kusikiliza. Ni jambo muhimu kuelewa matatizo na mahitaji ambayo hayakutekelezwa pamoja na uwezo wa jamii. Aidha inakubidi uzielewe pia tabia maalumu za jamii pamoja na masuala mengine, mathalani, mila na desturi zao, miiko ya kijadi na binafsi - yaani mambo ambayo yanaweza kuwa vikwazo katika mazingira yako ya kazi. Uelewa wako wa tabia na mienendo ya jamii utaboresha mipango yako.

Programu zenyе ufanisi mkubwa katika vita vya kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni zile ambazo zimetokana na uchambuzi makini wa hali halisi kuhusu mahusiano ya kimamlaka kati ya wanaume na wanawake, wanawake na wanawake, wanaume na wanaume na kati ya watu wazima na watoto. Hii inatokana na ukweli kwamba programuzaainahiyohuhakikishakwambahatuzaukabilianaji zitazaa matokeo yanayotakiwa kwa upande mmoja na kwa upande mwingine hazichochei wala haziendelezi misigano ya usawa.

Kulingana na rasilimali zinazopatikana pamoja na viwango vya utaalamu, njia za kukusanya taarifa zinaweza kujumuisha mambo yafuatayo:

- Masailiano na watu binafsi.
- Utembaleaji na Ugaguzi wa Maeneo.
- Mikutano ya majadiliano.
- Makundi ya walengwa maalumu.
- Uendeshaji wa tafiti..
- Mapitio na ukusanyaji wa kumbukumbu na data zilizopo.

Ni jambo la lazima kwamba taarifa zikusanywe kutoka kwenye orodha ya vyanzo vinavyoaminika vikiwemo vifuatavyo:

Jamii ya Wakimbizi	Wanawake, wanaume na vijana mmojammoja Makundi na jumuiya za wanawake, wanaume, vijana wa kiume na wa kike Viongozi na makundi ya kidini Wazee na viongozi wa jamii Kamati za uongozi katika kambi, viongozi wa vitengo na kamati nyinginezo Shule Makundi ya wafanyabiashara wa kiume na kike, wafanyabiashara wadogowadogo Walinda usalama Waganga wa kijadi
Mashirika misaada kibinadamu	ya ya Watumishi wa afya, wakiwemo watoa huduma za afya katika vituo vyta afya na wahudumu wa vituo vyta afya ya jamii kwa jumla Watoa huduma za maji na usafi Wajenzi na watunzaji wa majengo Wasambazaji wa vyakula na bidhaa nyinginezo Watoa huduma za jamii Watumishi wa sekta ya elimu Wasimamizi wa kambi Wakufunzi na washauri katika miradi na masuala ya uzalishaji mali
UNHCR na Mashirika mengine wa Umoja wa Mataifa (UN)	Wakuu wa ofisi Maafisa wa programu na wasaidizi wao Maafisa wa hifadhi na wasaidizi wao Maafisa wa jamii na wasaidizi wao Maafisa wa uwandani na wasaidizi wao Maafisawa masuala yajinsia, wanawake, watoto na wasaidizi wao Maafisa wa usalama na wasaidizi wao Maafisa wa kitaifa katika sekta zote
Asasi za Serikali mwenyeji wa wakimbizi	Maafisa wa Jeshi la Polisi Watumishi wa Idara ya Sheria na Mahakama Watumishi wa wizara zinazohusika na: afya; ustawi wa jamii, wanawake, familia na watoto
Asasiza Kitifa Zisizo za Serikali (AZISE) na Wataalamu binafsi	Vikundi vyta harakati na vyta huduma katika masuala ya ubakajina unyanyasaji wa kingono na kijinsia Makundi ya wanaharakati wa haki za binadamu Makundi ya wanasheria wanawake Wanasheria

Kubalianeni kuhusu Seti ya Kanuni Elekezi

Rejea Sura 2 kwa maelezo ya kina kuhusu kanuni elekezi. Ni jambo muhimu kwa timu ya watendaji kijadili waziwazi kanuni ambazo zitaongoza kazi zao. Watendaji wote wanapaswa kukubaliana juu ya kanuni hizi na kuelewa jinsi zinavyogusa na kuathiri kazi zao pia.

Kanuni Elekezi kwa Watendaji Wote

Programu

- Shirikisha kikamilifu jamii ya wakimbizi
- Hakikisha fursa sawa katika ushiriki wa wanaume na wanawake, wavulana na wasichana katika upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya programu
- Hakikisha utendaji ulioratibiwa wa watendaji wote na unaoshirikisha sekta mbalimbali
- Jitahidi kuoanisha na kubainisha majukumu makuu katika programu za UNHCR za ngazi zote.
- Hakikisha uwepo wa uwajibikaji katika ngazi zote

Mtu mmojammoja

- Hakikisha usalama wa kimwili wa waathiriwa/ wanusurika
- Tunza usiri
- Heshimu matakwa, haki na hadhi za waathiriwa/ wanusurika, na zingatia maslahi bora ya mtoto wakati wa kutoa maamuzi wowote kuhusu hatua bora zaidi ya kuchukuliwa kuzuia au kukabiliana na tukio la unyanyasaji wa kingono na kijinsia
- Hakikisha kutokuwepo na aina yoyote ya ubaguzi

Fafanua dhima na majukumu kwa watendaji wote

Kwa sababu ya kuwepo kwa watendaji tofautitofauti kutoka katika sekta na mashirika mbalimbali, nijambo muhimu kufafanua dhima na majukumu ya kila mmoja wao. Kuna baadhi ya kazi ambazo zinahitaji kushughulikiwa na zaidi ya mtendaji mmoja. Lakini hatimaye lazima pawepo na mtu mmoja tu ambaye ndiye mtendaji na mwajibikaji mkuu kwa kila kazi. Huyo ndiye anayetarajiwa kutoa taarifa za kazi husika na kuwajibishwa endapo kazi haikukamilika.

Katika mazingira ya wakimbizi shirika la UNHCR libebe jukumu la kuratibu mkabala wa sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na watendaji wote muhimu.

Kubalianenikuhusu mifumo ya ufuatiliajina tathmini, pamoja na utaratibu wa kuripoti na kurufaa

Kuna umuhimu wa kuandaa utaratibu wa kufuatilia na kutathmini hatua za uzuiaji na ukabilianaji. Watendaji wote wanapaswa kushiriki katika kuratibu mambo haya wakiishirikisha hasa jamii husika ya wakimbizi, husani wanawake, wanaume na vijana. Ufuatiliaji endelevu hutuhakikishia kuwa hatua za uzuiaji na ukabilianaji zinaendelea kama ilivyopangwa. Kwa upande mwingine tathmini husaidia kubaini ufanisi wa mikakati ya uzuiaji na ukabilianaji dhidi ya manyanyaso yanayowasibu wakimbizi wa kike, kiume, wavulana na wasichana. Rejea Sura ya 7 kwa ajili ya maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuandaa mbinu za ufuatiliaji na uendeshaji wa tathmini. Ni jambo muhimu kwa watendaji wote kukubaliana juu ya : madhumuni ya mbinu za ufuatiliaji na tathmini, ubainishaji wa malengo, matokeo pamoja na viashirio vya kila aina ya ukabilianaji. Aidha mpango wa utekelezaji sharti uonyeshe rasilimali za kifedha na za watu zinazohitajika kwa ajili kufuatilia na kutathmini hatua za ukabilianaji.

Andaa Utaratibu wa Kuripoti, Kurufaa na Kuratibu

Ni jambo muhimu sana kwa watendaji kuratibu mifumo ya kutoa ripoti na kurufaa. Mifumo ya pamoja ya rufaa iandaliwe kwa ajili ya matumizi katika maeneo yafuatayo: huduma za afya, unasihi, usalama na mahitaji ya kisheria. Mfumo thabiti wa kuripoti uandaliwe kama sehemu ya mchakato wa ufuatiliaji. Zoezi hili linajumuisha uandaaji wa fomu ya kwa ajili ya kuripoti matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia pamoja na utaratibu wa kubadilishana taarifa kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Mkakati wa aina hii wa kubalishana habari uweke pia bayana jinsi watendaji watakavyoweza kujadili na kutua matatizo ya uzuiaji na ukabilianaji.

Matumiziyamfumowa aina mmojakatika utoaji taarifayatajenga na kuimarisha rekodi za kitakwimu ambazo zinawawezesha watendaji, yakiwemo mamlaka mbalimbali ya nchi mwenyeji, kupima kiwango cha tatizo, mabadiliko yoyote katika mazingira ambayo yanaweza kuathiri unyanyasaji wa kingono na kijinsia pamoja na matokeo ya hatua za uzuiaji wake. Fomu ya ripoti ya aina moja itarahisisha utaratibu wa ukataji rufaa na shughuli wa uratibu, na faida kubwa zaidi ni kwamba itaondoa adha na kero za kurudiarudia masailiano na waathiriwa/wanusurika wanaohusika. Rejea Sura 4 kwa ajili ya mfano wa mfumo wa utoaji taarifa/ukataji rufaa, na Sura 7 kwa ajili ya maelekezo kuhusu jinsi ya kutayarisha mfumo wa aina moja wa kutolea ripoti.

Zingatia usiri katika ngazi zote za kubadilishana na kuchambua taarifa.

Miongoni mwa shughuli nyingine kazi za uratibu zinajumuisha mambo yafuatayo:

Uanzishaji na upitiaji wa mara kwa mara wa njia za kuripoti na kurufaa miongoni na kati ya watendaji mbalimbali. Mitando ya kurufaa sharti ilenge kwenye utoaji haraka wa huduma bora kwa waathiriwa/wanusurika.

Kubadilishana taarifa za maandishi miongoni mwa watendaji bila kusahau uzingatiaji wa kanuni ya usiri.

Uitishaji wa mikutano ya mara kwa mara kwa ajili ya watendaji wakuu:

- ◎ Mikutano ya kila mwezi kwa ngazi ya kambi kwa ajili ya kujadili taarifa , data na shughuli mahususi za kambi husika
- ◎ Mikutano ya kila mwezi kwa ngazi ya mkoa (k.m. kituo cha ugani, kituo kidogo, ngazi ya wilaya) kwa ajili ya kujadili na kupitia taarifa, data, na shughuli zinazoendelea katika mkoa husika
- ◎ Mikutano ya robo mwaka kwa ngazi ya taifa kwa ajili ya kujadili na kupitia taarifa, data, na shughuli zinazoendelea kitaifa

Washiriki wa mikutano ya uratibu sharti wafanye mambo yafuatayo:

- ◎ Wabadilishane na kupeana taarifa miongoni na baina ya sekta, mashirika na jamii ya wakimbizi.
- ◎ Wabaini mapungufu katika huduma na mikakati kwa ajili ya kuboresha na kuimarisha shughuli zinazoendelea kwa wakati huo; na wasimamie utekelezaji wa mikakati iliyoamuliwa kutumika.
- ◎ Waombe maelekezo na msaada kutoka kwa watendaji wenzao; watoe taarifa murua za matukio; maoni ya kutatua matatizo; wafanye usaili kuhusu matukio yenye utata au ugumu mkubwa
- ◎ Wakubaliane kuhusu dhima na majukumu ya kila mtu anayehusika katika shughuli za uandaaji, utekelezaji na ufuatiaji wa hatua za uzuiaji na ukabilianaji na vitendo viovu.
- ◎ Waandae mipango ya mafunzo kwa ajili ya watumishi, elimu ya jamii na shughuli za kukuza na kuhamasisha viwango vya uelewa.

- ◎ Wajengeumilikajiwapamojawaprogramuzinazoshughulikia unyanyasaji wa kingono na kijinsia na waimarishe ubia na ushirikiano mionganoni mwa watendaji wote.

- ◎ Waandae mipango ya pamoja kwa ajili ya mafunzo

Shirika ambalo limeteuliwa kama ‘shirika kiongozi’ ndilo lenye wajibu wa kushughulikia maandalizi ya kuitisha mikutano ikiwemo kazi za kuhimiza mahudhurio na uratibu wa watendaji.

Dumisha Ustawi wa Watumishi na Watu Wanaojitolea

Watumishi na watu wanaojitolea kufanya kazi katika programu zinazohusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia, hususani wale wanaofanya kazi kama washauri au mawakili wa waathiriwa/wanusurika, wanapaswa kuelewa kwamba wanakabiliwa na hatari za aina mbili: ukosefu wa usalama na uwezekano wa madhara yatokanayo na kihoro pamoja na fadhaa.

Usalama na Ulinzi

Mtu ye yote ambaye amepokea ripoti kuhusu unyanyasaji wa kingono na kijinsia na kujaribu kutoa msaada kwa mwathiriwa/mnusurika, anakabiliwa na hatari ya kulipiziwa kisasi na mhalifu na wakati mwingine hata jamii yenye. Kimsingi maovu yanayohusiana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia ni makosa mazito sana dhidi ya waathiriwa na wanusurikaji, na kwa mantiki hiyo mtu ye yote ambaye anajaribu kumsaidia mlalamikaji naye pia hukabiliwa na hatari za kushambuliwa.

Uzoefu kutoka duniani kote unaonyesha kwamba wahalifu wana tabia ya kuwashambulia na kuwadhuru watu ambao hutoa misaada kwa waathiriwa/wanusurika. Hali hii hujitokeza kwa wingi zaidi katika kesi zinazohusu magomvi ya majumbani, hususani dhidi ya washauri au watu wanaojitolea kuwasaidia walalamikaji katika vituo vya polisi. Katika kesi nyngi za aina hii mhalifu huwa ni mume au rafiki wa karibu sana wa mlalamikaji. Polisi wenye silaha wameuwawa au kujeruhija katika nchi nyngi wakati wa wakishughulikia ripoti kuhusu kesi za magomvi ya nyumbani.

Mameneja na wasimamizi wanapaswa kufuatalia na kuimarisha usalama wa watumishi na kuchukua hatua za haraka kwa ajili ya kuwalinda pindi wanapokabiliwa na vitisho au mashambulizi. Na tukio lolote la kuwatishia watumishi wanaofanya kazi katika kambi za wakimbizi linapaswa kuripotiwa haraka kwa afisa hifadhi wa UNHCR ili hatua mwafaka zichukuliwe mara moja kwa ajili ya ulinzi wao. Asasi zinapaswa kuwa na sera pamoja na kuandaa hatua madhubuti kwa ajili ya kupunguza hali za hatari dhidi ya watumishi/wafanyakazi wa kujitolea kwa upande mmoja, na kuongeza viwango vya usalama na ulinzi wao kwa upande mwingine.

- ◎ Andaa sera ya kuwatumia wafanyakazi wazalendo au wa kimataifa (ambao hawaishi kambini), na ambao wao siyo wakimbizi, kushughulikia kesi za walalamikaji ambazo ziko mikononi mwa polisi au vyombo vya usalama. Lakini pana tatizo la kutumia mbinu hii katika kesi za dharura.
- ◎ Viongozi wa wakimbizi na watu maarufu katika jamii watumike nawashirikishwe katikashughulizote. Kwamaana kama jamii imeshirikishwa kikamilifu katika programu, watu watakuwa na uelewa mzuri zaidi wa huduma, matatizo na hatari zilizopo na hivyo kuweza kuchangia vizuri zaidi jitihada za uandaaji wa mikakati ya uzuaji wa mashambulizi na uimarishaji wa usalama.
- ◎ Zoezi la kubuni na kutekeleza mpango wa usalama na ulinzi lishirikishe vyombo vya ulinzi wa amani, usalama na usimamizi wa sheria na haki.

Kihoro kitokanacho na Kusimuliwa na Fadhaa

Kihoro kwa kusimuliwa ni mfadhaiko wa kihisia unaowasonga watu ambao wamekuwa wakisikiliza maeleo ya mara kwa mara kuhusu vitendo dhalimu vya kisaikolojia na kimwili ambavyo vimewasibu watu wengine. Maana halisi ya fadhaa ni uchovu-kihisia Hali hizi mbili za kihoro kwa kusimuliwa na uchovu-kihisia mara nyingi huwakumba wafanyakazi wanaoshughulika na programu za unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Dalili za Kihoro kitokanacho na kusimuliwa na fadhaa ni pamoja na:

- ◎ Matatizo ya kukosa usingizi na hamu ya kula.
- ◎ Maumivu ya mwili au matatizo ya kiafya ambayo sababu zake hazieleweki
- ◎ Majibu yenye hisia kali mno dhidi ya matukio maovu au mifadhaiko; au kinyume chake, yaani ukosefu wa mifadhaiko au hisia yoyote katika majibu dhidi ya matukio ya kidhalimu.
- ◎ Matatizo yanayohusiana na utendaji wa kazi.
- ◎ Hali ambapo mtu hujitenga na kuacha kushiriki katika shughuli za watumishi wenzake, familia, marafiki pamoja na zile za jamii kwa jumla.
- ◎ Maoni na tabia inayoonyesha kwamba mhusika anajiona ni mtu muhimu ambaye mchango na kazi yake kwa waathiriwa/wanusurika haviwezi kutekelezwa na mtu mwingine. Kwa maneno mengine hali ambapo mtu anajikweza na kujipendezesha mno kwa wakimbizi, maarufu kwa jina la 'hisia ya ushujaa-nafsi'.
- ◎ Kujiweka katika hali ya hatari kimwili kwa ajili ya kuwasaidia wakimbizi badala ya kuomba msaada kutoka kwa watu wengine

Kinga ndiyo njia bora zaidi ya kukabiliana na hali ya fadhaa. Mikakati inayostahili kutumika katika programu inajumuisha mambo yafuatayo:

- ◎ Majadiliano na masailiano baada ya matukio makubwa na ya hatari sana.
- ◎ Fursa za kupunguza mifadhaiko, mathalani, mazoezi ya mwili, ushiriki katika shughuli za kimakundi, ubadilishanaji wa taarifa kiutani kuhusu furaha na matatizo ya kazi.
- ◎ Mahudhurio ya warsha kwa ajili ya kuboresha stadi, kujenga hali ya kujiamini pamoja na kuhimiza upanuzi wa mipaka ya utaalamu.
- ◎ Ratiba ya ukaguzi wa mara kwa mara kwa ajili ya kufuatilia utendaji wa mtumishi, kumpatia misaada inayohitajika pamoja na kutathmini utimamu wake wa kiakili.
- ◎ Kwenda likizo/kujipumzisha na kazi.
- ◎ Unasihi kuhusu mifadhaiko wa kirika

Masuala muhimu ya kukumbuka

Katika kuandaa mpango wa utekelezaji:

- ◎ Bainisha na uwashirikishe watendaji wanaofaa.
- ◎ Jenga uelewa wa pamoja kuhusu maana unyanyasaji wa kingono na kijinsia, na kisha kubalianeni kuhusu wigo wa utendaji.
- ◎ Chambua hali halisi: kwa kukusanya taarifa kwa ajili ya kupata uelewa sahihi wa mahitaji, matatizo, huduma zinazopatikana, pamoja na uwezo na upungufu wa jamii ya wakimbizi.
- ◎ Kubalianeni kuhusu seti ya kanuni za mwongozo.
- ◎ Fafanua dhima na majukumu ya watendaji wote.
- ◎ Panga malengo na madhumuni; fafanua mambo yanayohitaji kufanyika, viashiria vyake na bainisha rasilimali zinazohitajika.
- ◎ Kubalianeni kuhusu mifumo ya ufuatilaji na tathmini inayohusisha jamii.
- ◎ Andaa taratibu za kuripoti, kurufaa na kuratibu.
- ◎ Jengampangowakudumishaustawinauborawamazingira mazuri kwa ajili ya watumishi na watu wanaofanya kwa kujitolea.

SURA YA 7

UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ufuatiliaji na tathmini ni utaratibu muhimu katika kuendeleza mipango madhubuti ya kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Utaratibu huu unaimarisha uwajibikaji ambao ni moja ya Kanuni Elekezi zilizofafanuliwa katika sura ya 2, na pia ni sehemu ya Muundo wa Utekelezaji ulioelezwa katika sura ya 6. Taratibu hizi zinakuwa na ufanisi zaidi zinapoandaliwa kwa pamoja na sekta zote, ikiwemo pia jumuiya ya wakimbizi.

Timu ya wajumbe wa sekta mbalimbali haina budi kuchukua hatua sita zifuatazo wakati wa kuandaa mfumo wa ufuatiliaji au wa tathmini; kuamua madhumuni ya taratibu za ufuatiliaji na tathmini na kisha kutoa tathmini ya mahitaji ya taarifa; kuhakikisha kuwa malengo, matokeo na viashiria vimewekwa bayana kwa ajili ya uingiliaji kati wa uzuiaji na ukabilianaji, kuanzisha vyombo vya kutolea habari vya aina moja kwa watendaji wote na vinavyoratibiwa; kufanya uamuzi kuhusu mbinu za kupata taarifa za viashiria; kugawa majukumu ya ukusanyaji wa taarifa; kufanya uamuzi kuhusu muda na viwango vya ukusanyaji wa data na pia kugawa rasilimali, kuanzisha utaratibu wa kubadilishana taarifa na kujumuisha matokeo kwenye mipango ya uzuiaji na ukabilianaji.

KUBAINISHA UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ufuatiliaji na Tathmini ni shughuli mbili tofauti, lakini zenyé kuhusiana.

Ufuatiliaji ni uhakiki unaoendelea kila wakati ambao hufanywa na timu ya sekta mbalimbali kuhusu uingiliaji kati katika kuzuia na kukabiliana na jambo kwa lengo la kuamua kama shughuli zinazofanyika zinakwenda kama zilivyopangwa na kwa kadri ya mahitaji ya bajeti na kama marekebisho yeyote yatahitajika, ili kufanikisha malengo yaliyotarajija. Ufuatiliaji unaofaa hujumuisha mfumo ulioratibiwa wa utoaji taarifa

Tathmini ni usaili wa ubora, umadhubuti na ufanisi wa mbinu za uzuiaji na ukabilianaji wa timu ya sekta mbalimbali. Tathmini huchanganua hatua kwa hatua matokeo ya uzuiaji ya sera, programu, matendo, ushirikiano na hata taratibu zitumiwazo na wakimbizi wanawake, wanaume, wavulana na wasichana. Vigezo vya tathmini vinaweza kujumuisha uendelevu wa vitendo vya uzuiaji na vya ukabilianaji, uratibu na uthabiti, na ubora wa mifumo ya ufuatiliaji na utoaji taarifa.

Shabaha za Taratibu za Ufutiliaji na Tathmini

Taratibu bayana za ufutiliaji na tathmini

- ◎ Huwasaidia watendaji kubaini athari za shughuli za uzuiaji na ukabilianaji.
- ◎ Hupima ubora wa uingiliaji kati kwa kuzuia au kukabiliana na kama unakidhi malengo yaliyokusudiwa.
- ◎ Huweza kudokeza mabadiliko katika mazingira husika ambayo yanaweza kuathiri kiwango cha unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- ◎ Hubainisha matendo mzuri, na kutoa mafunzo kutokana na ujuzi wa kiutendaji na huweza kuboresha utendaji.
- ◎ Huweza kuhamasisha ujenzi wa timu, kuendeleza uwazi na kuimarisha uwajibikaji kwa wakimbizi wanawake, wanaume na vijana na kwa wahisani.

Ufutiliaji makini hujibu maswali haya :

- ◎ Je! Tunafikia malengo tuliojiwekea? Kwa vipi? Kwa nini au kwa nini hatufikii?
- ◎ Kuna vikwazo gani katika utekelezaji?
- ◎ Je! Tunaratibu ipasavyo?
- ◎ Ni yapi mapengo ya kiutekelezaji?, Na vipi tutayazibe mapengo hayo?

Tathmini makini hujibu maswali yafuatayo:

- ◎ Tulifanya nini?
- ◎ Je tulifanikiwa kupata nini?
- ◎ Je tulipata tuliyotarajia?
- ◎ Je tumejifunza nini?
- ◎ Je tunashughulikia kikamilifu vyanzo vyaa unyanyasaji wa kingono na kijinsia? Kama sio mianya iko wapi?

- ◎ Je tunashughulikia kikamilifu madhara yatokanayo na vitendo vya unyanyasaji wa kingono na kijinsia ? Kama sio mianya iko wapi?
- ◎ Nini kingine kihitajikacho?

Aina za Taratibu za Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini vinaweza kutofautiana kwa upeo, kina na shabaha. Lengo la ufuatiliaji na tathmini linaweza kuelekezwa katika sera, aina ya kazi, aina ya programu, utendaji (kuripoti, kurufaa, kupanga mikakati au shughuli za bajeti) au uingiliaji kati mahsus.

Taratibu za Ufuatiliaji na Tathmini zinahusika katika ngazi zote za uingiliaji kati kwa uzuijji na ukabilianaji, zikiwemo ngazi zinazomlenga mtu mmoja, au miundo ya kijamii / kisheria / kisiasa. Ufuatiliaji na Tathmini vinaweza pia kutumika katika sekta, yani, katika ujumla wa shughuli na taratibu za uingiliaji kati kwa uzuijji au ukabilianaji, kwenye nyanja za afya, saikolojia-jamii usalama/ulinzi na sheria/haki.

Ufuatiliaji na Tathmini unaweza kufanyika katika awamu ye yeyote ya operesheni. Ufuatiliaji una maana zaidi unapofanywa kwa mtindo wa kuendelea. Tathmini nzuri ya programu hufanyika kwa mtindo wa kila mwaka. Tathmini inayofanyika mwanzoni mwa awamu ya utekelezaji inaweza kutoa taarifa zitakazosaidia katika uchambuzi wa hali halisi. Ufuatiliaji unaofanyika katika kipindi chote cha operesheni huwasaidia mameneja katika kuhakikisha kuwa shughuli zilizokubaliwa zinaendeshwa kama ilivyopangwa. Tathmini zinazofanyika mwishoni mwa operesheni husaidia katika kupima kiasi cha kazi kilichotendeka pamoja na kubainisha utendaji uliokuwa mzuri.

Rejea pia:

Tathmini za Kiutu kwa Nyakati halisi ; Baadhi ya FAQ (UNHCR 2002)

Kubuni Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya Programu Zinazolenga unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia.

Kama ambavyo Kanuni Elekezi zilivyoelezwa katika sura ya 2, ni muhimu kuhamasisha ushiriki mkubwa katika uandaaji wa mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini. Mkabala wa kutumia sekta mbali mbali, ikwa ni pamoja na ushirikishaji wa jamii ya wakimbizi huimarisha ujifunzaji, hujenga umiliki na kuongeza uwazi mionganoni mwa watendaji. Hii inachukua umuhimu zaidi wakati

wa kujadili madhumuni ya Ufuatiliaji na Tathmini na jinsi taarifa zitakavyotumika, changanuliwa na jinsi zitakavyochangia katika mipango inayoendelea.

Ni lazima watendaji watambue kuwa baadhi ya vikundi vinakabiliwa na vikwazo kwenye ushiriki katika mchakato huu. Kwa mfano, wakimbizi wa kike na watoto mara nyingi hukosa mamlaka ya kushirikisha mawazo yao katika mazingira ya aina hii. Mipango mahsusini inaweza ikahitajika kuhakikisha kuwa wakimbizi vijana na hasa walio katika makundi yaliyo hatarini (angalia Sura ya 5) wanashirikisha katika kuunda mifumo hii. Uchambuzi wa hali halisi uliopendekezwa katika Sura ya 2 umeelezea baadhi ya mambo haya. Watendaji wote watakapokuwa wametahadharishwa kuhusu vikwazo hivi, wataweza kutafuta mbinu za kuvikwepa.

Uandaaji wa mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini lazima uzingatie hatua sita zifutazo:

1. Amua madhumuni ya utaratibu huo wa ufuatiliaji na tathmini na kukadiria mahitaji ya taarifa.
2. Hakikisha kuwa uingiliaji kati kwa njia ya uzuiaji na ukabilianaji umewekewa malengo, matokeo na viashiria bayana.
3. Anzisha zana za kuripotia zilizoratibiwa na za aina moja kwa watendaji wote.
4. Amua taratibu za kupata taarifa na viashiria.
5. Gawa majukumu ya ukusanyaji wa taarifa, amua muda wa zoezi na vipindi vya ukusanyaji data na gawa rasilimali.
6. Anzisha utaratibu wa kubadilishana taarifa, na kujumuisha matokeo kwenye mipango ya uzuiaji na ukabilianaji.

Rejea pia:

Kupanga na kuandaa Tathmini bora (UNHCR 1998)

HATUA 1:

Amua madhumuni ya utaratibu huo wa ufuatiliaji na tathmini na kukadiria mahitaji ya taarifa

Timu ya wajumbe toka sekta mbalimbali ijadili na kukubaliana kuhusu madhumuni ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Majadiliano hayo yataamua aina ya mifumo ya utoaji taarifa inayohitajika, kiwango cha matumizi ya taratibu hizo, na jinsi

zitakavyochangia katika mipango inayoendelea ya uzuiaji na ukabilianaji.

Kusaidia katika kujenga makubaliano kuhusu madhumuni ya mifumo ya ufuatiliaji na tathmini, pia yaweza kuwa muhimu kuamua kuhusu mahitaji ya taarifa ya kila mtendaji/sektä. Ukadiriaji huu wa mahitaji ya taarifa unaweza kuandaliwa kama kifano na kupangiliwa kisekta au kwa mujibu wa mahitaji ya kila mtendaji anayehusika.

Mfano

Timu ya watendaji wa sekta mbalimbali	<ul style="list-style-type: none"> Mahitaji ya Taarifa 	Sura ya 1
Kundi/ watu waliokusudiwa kunufaika	<ul style="list-style-type: none"> Athari katika ubora wa maisha Matatizo ya kupata huduma Uwezo wa kushiriki na kuathiri utoaji wa maamuzi 	Sura ya 2
Watumishi wa ugani	<ul style="list-style-type: none"> Matokeo ya shughuli Matatizo yanayoathiri shughuli/ utendaji wa kikundi Maendeleo kwa mujibu wa mpango wa kazi Mambo yaliyotathminiwa ambayo ni ya hatari kwa unyanyasaji wa kingono na kijinsia 	Sura ya 3
Waratibu/ Wasimamizi	<ul style="list-style-type: none"> Matokeo ni nini? Watumishi wa ugani wamekumbana na matatizo gani? Ni maendeleo gani yamepatikana kwa mujibu wa mpango wa kazi? Utendaji wa watumishi wa ugani 	Sura ya 4
Menejimenti ya mradi	<ul style="list-style-type: none"> Ubora na ufanisi wa mikakati Je, matokeo yaliyotarajiwा yamepatikana? Madhara chanya na hasi kwa wanawake na wanaume Maendeleo ya utekelezaji Sababu za nje zinazoathiri utendaji Udhaifu wa ndani unaoathiri matokeo Ufanisi na ubora wa matumizi ya rasilimali 	Sura ya 5
Mashirika/ asasi wabia wa ugharamiaji	<ul style="list-style-type: none"> Kiwango cha ufikiwaji wa madhumuni/malengo Mikakati ya mradi Sababu za nje zinazoathiri utendaji wa mradi Udumishikaji wa matokeo ya mradi kwa kundi lengwa na katika ngazi ya asasi 	Sura ya 6
		Sura ya 7
		Sura ya 8
		Sura ya 9
		Sura ya 10

HATUA YA 2:

Hakikisha kuwa Uingiliaji kati kwa njia ya Uzuiaji na Ukabilianaji Umewekewa Malengo, Matokeo na Viashiria bayana

Kila uingiliaji kati sharti uwe na malengo bayana ambayo yataakisiwakatika viashiria matokeo, athari na utendaji. Malengo, matokeo na viashiria hivyo hutoa njia sahihi ya kubainishia athari za uingiliaji kati wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa njia ya uzuiaji na ukabilianaji. Aidha viashiria hupendelekeza aina ya data itakayokusanywa pamoja na aina ya utaratibu wa kuripoti unaohitajika.

Kuandaa malengo

Malengo ni lazima yaonyeshe matokeo yanayokusudiwa pamoja na athari za uzuiaji kwa kila programu ya uingiliaji kati ambazo zinachangia katika ufanikishaji wa malengo ya programu.

Kwa mfano: Uchambuzi wa hali halisi unabainisha kwamba bidhaa za chakula hazigawanywi kwa kuzingatia fursa sawa kwa makundi yote. Baadhi ya makundi hayapati rasilimali za kutosha na hali hii imeongeza hatari ya kuwepo kwa unyanyasaji wa kingono na kijinsia na unyonyaji wa kijinsi.

Lengo hapa lingekuwa kupitia upya michakato iliyopo ya ugawaji chakula kwa shabaha ya kupunguza hatari za kuzuka kwa unyanyasaji wa kingono na kijinsia na kuhakikisha ongezeko kubwa la usawa wa kijinsia.

Zingatia: Malengo ni lazima yaelezwe kwa kuzingatia mabadiliko chanya ambayo yataokea katika hali za wakimbizi. Malengo haya yanaweza kuwa ni kujenga uratibu bora zaidi, taratibu bora zaidi za kukabiliana na matatizo, uelewa bora zaidi wa jamii au ushiriki bora zaidi wa wanaume katika masuala ya usawa wa kijinsia.

Kuamua matokeo: Matokeo ni mafanikio mahususi na halisi. Ili kusaidia kutambua matokeo yanayotarajiwa, fafanua kile kinachohitajika kufanya ili kufikia malengo.

Mfano: Kama lengo ni kuongeza idadi ya uwakilishi wa wanawake katika kamati za usambazaji wa chakula, moja ya matokeo inaweza ikawa ni kuhakiki na kubadili makubaliano ya kamati za usambazaji ili kuhakikisha uwakilishi wa wanawake unakuwepo.

Kuamua aina ya utendaji na viashiria matokeo
Viashiria ni zana za upimaji zinazosaidia katika kueleza vitu

vitakavyo tathminiwa au kufuatiliwa na kurekodi mafanikio yaliyotarajiwa. Viashiria vya ubora na vya uwingi vyote vinahitajika katika tathmini ya matokeo ya uingiliaji kati wa njia ya uzuiaji na ukabilianaji. Viashiria vya uwingi ni vile ambavyo vinaweza kufuatiliwa kila wakati kwa urahisi na kwa njia ya fomu za ripoti. Viashiria ubora husaidia kuonyesha vitendo vizuri, kudokezea matatizo yaliyojitokeza na kubainisha mapengo katika hatua za uzuiaji na ukabilianaji.

UNHCR hutumia viashiria vya aina mbili: Viashiria matokeo na vya utendaji.

Viashiria matokeo husaidia katika kupima mabadiliko katika huduma za jamii na tabia pamoja na mabadiliko katika mifumo na asasi. Viashiria matokeo kwa kawaida huwa ni vya ubora, ambapo hupima mabadiliko yanayotarajiwa katika maamuzi na mitazamo ya watu kuhusu mada husika. Viashiria matokeo huhusiana kwa karibu na malengo.

Kwa Mfano: kama lengo ni kuongeza ushiriki wa wanawake katika kamati za usambazaji wa chakula, kiashiria matokeo kinaweza kuwa kwamba wanawake waliopo katika kamati hizo za ugavi wajione kuwa wanatoa mchango wa maana kwenye mchakato wa utoaji maamuzi.

Viashiria utendaji mara nyingi huwa vya uwingi. Viashiria utendaji vinahusiana na uzalishaji.

Kwa Mfano: Kama matokeo ni kupitia na kubadili makubaliano ya kamati za usambazaji wa chakula ili kuongeza ushiriki wa wanawake, viashiria utendaji vinaweza vikawa ni ongezeko la ushiriki wa wanawake kwenye kamati za ugavi kutoka asilimia 30 hadi 50.

Viashiria vyote lazima vivuke mipaka ya jinsia na umri. Kila inapowezekana viashiria ni lazima vieleze vipengele vingine vinavyohusu walengwa, ikiwa ni pamoja na kabila, makazi (kambi za mijini au vijijini) au kwa makundi yaliyo hatarini.

Rejea pia:

Kupanga Miradi katika UNHCR: Kiongozi halisi kuhusu matumizi ya malengo, matokeo na viashiria (UNHCR 2002)

HATUA YA 3:

Anzisha zana za kuripotia zilizoratibiwa na za aina moja kwa watendaji wote

Vifaa vya kutolea ripoti husaidia katika kuwa na utaratibu na njia thabiti za ukusanyaji wa taarifa kuhusu viashiria viliviyotajwa hapo juu. Ni muhimu kuwa na vifaa vya kutolea ripoti vya aina moja

kwa asasi zote ndani ya sekta mbalimbali (k.m. watoa huduma za afya wote wakusanye seti za taarifa zinazo fanana).

Timu ya watendaji toka sekta mbalimbali ianze kwa kutambua mifumo yote iliyopo ya kutolea ripoti na utunzaji wa kumbukumbu, kadi za muhtasari wa data, pamoja na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini inayotumiwa na watendaji mbalimbali katika kila sekta.

Kwa kuzingatia vifaa vilivyoko vya kutolea ripoti kama vile ripoti ya kila mwezi ya afya, huduma za kijamii za AZISE,/ ripoti za uzuiaji za UNHCR, ripoti za hali , ripoti za mwaka za ulinzi, na plani za uendeshaji za nchi, timu ya watendaji toka sekta mbalimbali ianze kutathmini hali ya kutolea ripoti ilivyokuwa mwanzoni, na aina ya mabadiliko yanayohitajika ili kuingiza taarifa za shughuli za uzuiaji na ukabilianaji na unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Ni muhimu kwamba ripoti hizi mbalimbali zifafanue mafanikio yaliyopatikana, changamoto na matatizo yaliyosalia pamoja na taratibu za ufuatiliaji na tathmini zilizopo.

Zana zote za kutolea ripoti kuhusu matokeo ya kiulinzi ya taratibu za uzuiaji na ukabilianaji ni lazima zizingatie masuala ya jinsia na umri. Yani zibainishe matokeo mbalimbali ya uingiliaji kati kwa wakimbizi wanawake, wasichana, wanaume na wavulana.

Mfano wa zana za kutolea ripoti.

Fomu ya ripoti ya matukio na fomu ya ripoti ya mwezi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

Fomu ya ripoti ya matukio ni zana muhimu ya kutolea ripoti kwa matumizi ya watendaji wote. Wakati tukio lolote la unyanyasaji wa kingono na kijinsia linaporipotiwa kwa mtendaji yeyote ni lazima uwepo mtindo mmoja kwa ajili ya kurekodi tukio kama hilo. Zana nyingine ya kutolea ripoti ni Fomu ya Ripoti ya Mwezi ya Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia. Utaratibu huu wa kutoa ripoti ni muhimu katika kufuatilia mabadiliko katika mazingira yanayo sababisha matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Ripoti hii pia hutoa mwanga kuhusu mambo yanayoweza kuwa chanzo cha magomvi katika ngazi ya jumuiya. Kwa upande wa fomu ya ripoti ya mwezi kumbuka kwamba data zikusanywe kwa kila mtu/kambi/tukio; jumuisho zinazotolewa kwa ajili ya ofisi za ugani, kanda au nchi nzima ni za muhimu pia. Kwa fomu za mfano, tazama viambatisho 2 na 3.

Data za Ripoti za Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia

Ni muhimu kuwa taarifa za aina fulani ziwemo katika ripoti. Ili kuwa na ufanisi, watendaji wote wakubaliane kuhusu istilahi zinazotumika ili kuwa na ripoti zenye maana zinazolingana. Taratibu zote za kutoa ripoti lazima zizingatie usiri mkubwa kwa mwathiriwa/mnusurika au mhalifu.

Aina ya Data kwa ajili ya Fomu za Ripoti ya Mwezi

- Idadi ya ripoti zote za matukio.
- Aina za unyanyasaji wa kingono na kijinsia yaliyoriipotiwa.
- Idadi, umri na jinsia ya mwathiriwa/mnusurika.
- Idadi, umri na jinsia ya mhalifu.
- Idadi ya matukio kwa maeneo (k.m. nyumba, soko, nje ya kambii) (ikionyesha mahali nje ya kambii).
- Idadi ya waathiriwa/wanusurika wa ubakaji wanapatiwa huduma afya ndani ya siku mbili baada ya tukio.

Aina ya Data kwa ajili ya Fomu ya Kisheria

- Idadi ya matukio yaliyo ripotiwa kwa afisa hifadhi.
- Idadi ya kesi zilizoripotiwa polisi.
- Idadi ya kesi zilizopelekwa mahakamani.
- Idadi ya kesi zilizofutwa.
- Idadi ya walioachiliwa/walioadhibiwa.
- Aina ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia yaliyotokea.
- Idadi ya kesi za ubakaji zilizofikishwa vituo vyta afya ndani ya siku mbili.
- Idadi ya kesi ambazo ushahidi wa kitabibu ulitayarishwa na kupelekwa mahakamani.
- Asilimia ya ongezeko/punguo la idadi ya kesi za ubakaji katika mwezi.
- Asilimia ya ongezeko / punguo la unyanyasaji wa kingono na kijinsia katika mwezi.
- Maoni ya ziada.

Aina ya Data kwa ajili ya Ripoti ya Hali:

- Wasiwasi, masuala na matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- Hali ya uratibu na upangaji.
- Uingiliaji kwa uzuiaji kisekta.
- Uingiliaji kwa ukabilianaji kisekta.
- Mafunzo ya uwezeshaji watumishi / wanufaika.
- Matokeo ya Ulinzi; shughuli za ufuatiliaji na tathmini.

Angalia kiambatisho 4 kuhusu mfano wa fomu ya Kumbukumbu na Uchunguzi wa Kitabibu.

Kiwango cha Ripoti za Kingono na Kijinsia

Kiwango cha ripoti za kingono na kijinsia nijumla ya ripoti zote za matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia zilizopokelewa katika kipindi fulani ikilinganishwa na idadi ya watu katika eneo husika. Ili kukokotoa kiwango ripoti kwa kila watu 10,000 kwa mwezi, mwaka au vipindi maalumu vilivyo teuliwa:

Idadi ya matukio yaliyoripotiwa katika vipindi vilivyoteuliwa

Jumla ya watu kwa wakati ulioteuliwa

X 10,000 = Ripoti za matukio kwa kila watu 10,000 kwa wakati.

Kulinganisha kiwango cha ripoti katika kipindi fulani, huisaidia timu kubaini mielekeo. Mara nyingi inategemewa kuwa kiwango cha ripoti kitaongezeka kadri muda unavyopita. Ongezeko la kiwango cha ripoti laweza kuwa ishara kuwa waathiriwa/wanusurika wana uelewa kuhusu usaidizi uliopo na kwamba wana imani na huduma zinazotolewa na hivyo wako tayari kutoa ripoti. Ni muhimu kukumbuka kwamba matukio ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa kiwango kikubwa huwa hayatolewi taarifa. Kwa sababu hii, ongezeko la namba/viwango vya ripoti linaweza kuwa ishara tosha ya kufanikiwa kwa programu.

HATUA YA 4:

Amua taratibu za kupata taarifa na viashiria.

Baada ya kuandaa utaratibu wa kutolea ripoti, unaweza kuanza kuchagua mbinu utakazotumia kupata taarifa za viashiria ambavyo havimo ndani ya fomu za taarifa. Unapofanya uamuzi kuhusu mbinu hizo ni muhimu kutanabahi kama viashiria ni vya ubora au wingi.

Data za uwingi zinaweza kupatikana kwa njia ya uchunguzi wa kumbukumbu za serikali/wabia wa utekelezaji. Taarifa zinaweza pia kupatikana kuitia takwimu za idadi ya walengwa. Ni muhimu kutathmini vyanzo vya taarifa vilivyopo kwa watendaji mbalimbali wa timu ya sekta mbalimbali.

Data za ubora zinaweza kupatikana kwa njia ya masailiano, makundi lengwa na kwa kutumia mbinu shirkishi wakati wa tathmini za ugani.

Maoni ya wakimbizi wanawake, wavulana, na wasichana lazima yachunguzwe kwa taratibu za ufuutiliaji na tathmini. Taarifa hii ya ubora ni muhimu katika kutambua mapengo ya uzuiaji na kuimarisha taratibu za uzuiaji na ukabilianaji.

HATUA YA 5:

Gawa majukumu ya ukusanyaji wa taarifa, amua muda wa zoezi na vipindi vyta ukusanyaji data na gawa rasilimali.

Gawa majukumu:

Ni muhimu kugawa majukumu kwa sehemu mbalimbali za mifumo ya ufuatiliaji na tathmini.

Muda wa utekelezaji

Ni muhimu kutenga muda wa utekelezaji kwa ajili ya zana zote za kutolea ripoti. Muda wa utekelezaji pia ubainishwe kwa ajili ya taratibu nyingine zote za ufuatiliaji na tathmini. Timu ikubaliane muda wa utekelezaji unaofaa kwa uingiliaji kati au kwa programu. Ufuatiliaji unaweza ukafanyika kila mwezi, kwa kutumia Fomu ya Ripoti ya Mwezi ya unyanyasaji wa kingono na Kijinsia. Taarifa za kina zaidi zinaweza kuandaliwa kila baada ya mwaka mmoja

Amua kuhusu rasilimali na bajeti:

Mipango ya utekelezaji na bajeti inaweza zisitoe rasilimali za kutosha kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza taratibu za ufuatiliaji na tathmini. Hivyo ni muhimu kubainisha mahitaji halisi ya muda wa utumishi yanayohitajika. Aidha tafakari uwezo wa wafanyakazi katika maeneo hayo na kuona kama mafunzo zaidi yanahitajika kwa ajili ya kukuza stadi za ufuatiliaji na tathmini (k.m. stadi za ukusanyaji na uchambuzi wa data, utekelezaji wa ugani wa hatua za ufuatiliaji na tathmini na za mchakato wa tathmini pamoja na utekelezaji wa tathmini shirikishi)

Kwa ajili ya utekelezaji wa tathmini shirikishi ya kijamii inawezekana ikalazimu kuajiri wafanyakazi zaidi wenye ujuzi unaostahili na kufikiria mahitaji kwa ajili ya kugharamia ushirikishaji wa jamii katika vikao vyta tathmini. Mahitaji hayo yanaweza kuwa ni pamoja na wakalimani, ufasiri, na uangalizi wa watoto. Mwongozo wa tathmini shirikishi ya kijamii unaweza ukapatikana katika kitengo cha tathmini na sera cha Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR).

HATUA YA 6:

Anzisha Utaratibu wa Kubadilishana Taarifa, na Kujumuisha Matokeo kwenye Mipango ya Uzuiaji na Ukabilianaji

Mojawapo ya madhumuni ya taratibu za ufuatiliaji na tathmini ni kuboresha utendaji. Ili kufanikisha lengo hili uamuzi hauna budi kufikiwa kuhusu namna ya kubadilishana taarifa baina na mionganini mwa watendaji. Aidha ni muhimu kuamua kuhusu

watendaji watakaohusika moja kwa moja na ufuatiliaji na jinsi ambavyo matokeo ya utaratibu wowote wa ufuatiliaji au wa tathmini yatakavyoweza kuathiri upangaji wa programu.

Mbinu za kubadilishana taarifa hujumuisha:

- ◎ Mikutano ya kambi/jamii ya mara kwa mara (kila mwezi au mara mbili kwa mwezi) kuzungumzia matokeo ya ripoti za ufuatiliaji/tathmini/, kutathmini matokeo ya ulinzi, kupitia data za matukio, kuchambua matokeo ya ukusanyaji wa data na kupitia matokeo kutoka kwa jamii, kuratibu shughuli, kupanga mukutano mwingine wa ufuatiliaji, kubainisha vikwazo na masuluhisho yake.
- ◎ Mikutano ya kila mwezi ya ngazi za ugani, ofisi ndogo/wilaya, kujadili ripoti ya mwezi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia, matokeo ya uingiliaji kati kwa njia ya uzuijiji, data zilizokusanywa wakati wa uingiliaji kati, kupitia mafanikio yaliyopatikana kwa mujibu wa viashiria kama yaliyyotolewa na wafuatiliaji wa ngazi za kambi./jamii, na kiwango cha mafanikio katika kufikia malengo.
- ◎ Mikutano ya mara kwa mara, (pengine kila baada ya miezi mitatu) ya ngazi ya kitaifa kupitia ripoti zitokazo na mikutano ya ngazi ya kambi/ jumuiya, mikutano ya ngazi za ofisi za ugani, data zilizokusanywa wakati wa uingiliaji kati, ripoti za tathmini mbalimbali na kujadili masuala ya kifedha yanayoathiri utekelezaji.

Kila mukutano utatolewa ripoti fupi ya maandishi yenye kuonyesha mambo makuu yaliyobainishwa, hatua zilizochukuliwa na majukumu yaliyopangiwa utekelezaji.

Mambo Muhimu ya Kukumbuka

Taratibu bayana za ufuatiliaji na tathmini

- Huboresha uwajibikaji, ambao ni moja ya kanuni elekezi za uingiliaji kati kwa lengo la kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia.
- Ni sehemu ya Muundo wa Utekelezaji.
- Huwa na ufanisi zaidi endapo zitaandalialiwa na sekta zote, ikiwa ni pamoja na jumuiya za wakimbizi, kwa kufanya kazi pamoja.

Wajumbewatimu ya sekta mbalimbali hawana budi kuongozwa na hatua sita wakati wanapoandaa mifumo ya ufuatiliaji na tathmini:

- ◎ Amua madhumuni ya utaratibu huo wa ufuatiliaji na tathmini na kukadiria mahitaji ya taarifa.
- ◎ Hakikisha kuwa uingiliaji kati kwa njia ya uzuijiji na ukabilianaji umewekewa malengo, matokeo na viashiria bayana.
- ◎ Anzisha zana za kuripotia zilizoratibiwa na za aina moja kwa watendaji wote.
- ◎ Amua taratibu za kupata taarifa na viashiria.
- ◎ Gawa majukumu ya ukusanyaji wa taarifa, amua muda wa zoezi na vipindi vyta ukusanyaji data na gawa rasilimali.
- ◎ Anzisha utaratibu wa kubadilishana taarifa, na kujumuisha matokeo kwenye mipango ya uzuijiji na ukabilianaji.

Sura ya 1

Sura ya 2

Sura ya 3

Sura ya 4

Sura ya 5

Sura ya 6

Sura ya 7

Sura ya 8

SURA YA 8

UTESAJI KIJINSIA

Kushughulikia Unyanyasaji wa Kingono na Kijinsia Katika Kuamua Hadhi ya Ukimbizi

Sura hii inatoa mwongozo wa jinsi ya kushughulikia madai ya wakimbizi yanayohusu masuala ya kijinsia wakati wa kufanya maamuzi kuhusu hadhi ya ukimbizi. Sura inanukuu miongozo ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) iliyotolewa mwaka 2002 kuhusu Utesaji wa Kijinsia. Miongozo hiyo inatoa ushauri halisi kuhusu jinsi Makubaliano ya Wakimbizi ya mwaka 1951 yanavyowahusu watu wote wanaokimbia utesaji, bila kujali hadhi na majukumu yao ya kijinsia katika kijamii.

UNHCR na dola wanapaswa kuhakikisha kuwa mamlaka za Serikali, mawakili wa kisheria na maafisa wa hifadhi ambao wanahuksika katika kutoa uamuzi kuhusu hadhi ya ukimbizi chini ya Makubaliano ya mwaka 1951 kuhusu Hadhi ya Ukimbizi au chini ya Sheria ya mwaka 1950 ilioanzisha Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), wanaelewa vizuri Miongozo kuhusu Utesaji wa Kijinsia iliyofafanuliwa vizuri katika sura hii.

Inalaani vikali utesaji kutokana na unyanyasaji wa kingono na kijinsia, ambao sio tu kwamba unakiuka vibaya haki za binadamu pamoja na uvunjaji wa sheria ya kibinadamu pale unapofanywa katika mazingira ya migogoro ya silaha, bali pia ni kosa kubwa kwa heshima ya binadamu.

Inaunga mkono kutolewa kwa hadhi ya ukimbizi kwa watu ambao maombi yao ya ukimbizi yanatokana na sababu za woga dhahiri dhidi ya uteswaji kwa njia ya unyanyasaji wa kingono, kwa sababu za kimbari, dini, utaifa, uanachama kwenye kundi fulani la kijamii au msimamo wa kisiasa

Inapendekeza kuwa katika utaratibu kuamua kuhusu hadhi ya ukimbizi waomba hifadhi ya kisiasa, ambao pia wanaweza kuwa wameathiriwa na vitendo vyta unyanyasaji wa kingono na kijinsia wapewe umaalumu wa pekee katika kuhudumiwa.

Imenukuliwa kutoka ExCom conclusion Namba 73(xliv) (1993)

Unyanyasaji wa kingono na kijinsia unaweza kuwa na uzito katika mchakato wa kuamua hadhi ya ukimbizi kwa waombaji

walioathiriwa/wanusurika na unyanyasaji huo au hata kwa wahalifu wanaoomba au wenyе hadhi ya ukimbizi.

Miongozo hii inajikita katika kufafanua maana ya mkimbizi kwa kutumia mkabala wa kijinsia, ikitoa mapendekezo ya kiutaratibu yenye lengo la kuhakikisha kuwa taratibu za kutoa uamuzi wa hadhi ya ukimbizi zinaweka uzito wa kutosha katika wanawake wanaoomba hadhi ya ukimbizi. Aidha miongozo inatoa taarifa muhimu zenye lengo la kuhakikisha kwamba wasaili au watoa uamuzi wanao ujuzi wa kuelewa na kutambua madai ya kijinsia ya waomba hifadhi.

Pale ambapo ubakaji au ugomvi mwagine wowote wa kijinsia vimefanywa kutokana na sababu za kimbari, kidini, kiutaifa, msimamo wa kisiasa au uanachama wa kundi fulani kwenye jamii, hali hiyo yaweza kuchukuliwa kama utesaji kwa mujibu wa fasili ya neno mkimbizi kwenye Makubaliano ya mwaka 1950 yanayohusu Hadhi ya Wakimbizi na Sheria ya Ofisi ya UNHCR. Umakini wa pekee unahitajika katika maombi ambapo mwomba hifadhi atakuwa ameathiriwa na unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Maafisa hifadhi, wasaili au watoa uamuzi, hawana budi kutambua kuwa mwombaji hapaswi kutoa udhibitisho wa kimaandishi kuonyesha kuwa aliteswa kwa misingi ya jinsia yake. Watu hawa wazingatie kwamba kwa jumla matukio mengi ya utesaji wa kijinsia hayariptiwi katika jamii nydingi.

Watu walio na sifa tu ndio watatakiwa kutoa huduma za kisheria. Watu hawa ndio watakaotoa taarifa, ushauri na hata uwakilishi. Ili kuwa na mwendelezo na uwakilishi wa kufaa, suala husika lishughulikiwe na mtu mmoja hadi lifikie mwisho. Hata hivyo, wafanyakazi wote wa UNHCR na hasa wale wanaowasaili wanusurika/ waathiriwa ni lazima waifahamu vyema miongozo ya UNHCR, waweze kuhusisha sheria za kimataifa na zile za nchi husika. Mashirika ya shughuli za kibinadamu yanayofanya kazi na watu walioharibiwa makazi yao na wale waliokimbia makwao pia yanapaswa kuifahamu miongozo yote inayohusu sheria ya ukimbizi pamoja na matumizi yake, ili kuhakikisha kwamba wanawake na wanaume wana haki sawa ya kufurahia ulinzi wa kimataifa.

Utesaji wa Kijinsia; Miongozo ya Mwaka 2000 Inayotumika pamoja kwa ajili ya Taratibu na Vigezo vya Kuamua Hadhi ya Ukimbizi.

UNHCR inatoa Miongozo hii kwa mamlaka iliyo nayo, kama yalivyofafanuliwa kwenye Sheria ya Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, pamoja na Kifungu cha 35 cha Makubaliano ya mwaka 1951 kuhusu Hadhi ya Ukimbizi na Kifungu II cha Nyongeza ya 1967 katika Makubaliano hayo. Miongozo hii inakamilisha Kiongozi cha UNHCR kuhusu Taratibu na Vigezo vya Kuamua Hadhi ya Ukimbizi chini ya Makubaliano ya mwaka 1951 na Nyongeza yake ya mwaka 1967 kuhusiana na Hadhi ya Ukimbizi (Kilichohaririwa upya, Geneva, Januari

1992). Adha miongozo hiyo inafuta Andiko la Msimamo wa UNHCR kuhusu Utesaji wa Kijinsia (Geneva, Januari 2000) pamoja na Fuatilio la Pili la Mashauriano ya Dunia kuhusu mchakato wahifadhi ya kimataifa ambapo wataalamu walipitia mada huko San Remo mwezi Septemba 2001.

Miongozo hii inakusudiwa kutoa kiongozi cha tafsiri ya kisheria kwa ajili ya serikali, wanasheria, watoa maamuzi na mahakama, na pia wafanyakazi wa UNHCR wanaoshiriki ugani katika kutoa uamuzi kuhusu hadhi za ukimbizi.

Utesaji wa Kijinsia kwa Mujibu wa Kifungu 1A(2) cha Makubaliano ya 1951 na /au Nyongeza yake ya mwaka 1967 kuhusu Hadhi za Wakimbizi.

1. UTANGULIZI

1. "Utesaji wa Kijinsia" ni neno ambalo maana yake sio ya moja kwa moja. Neno hili hutumika kusemea madai mbalimbali yanayotumia jinsia kama kigezo cha msingi katika kuamua hadhi ya ukimbizi. Miongozo hii inalenga katika kufasiri maana ya mkimbizi, kwa kutumia mkabala wa kijinsia, kama ilivyo kwenye Kifungu 1A (2) cha Makubaliano ya mwaka 1951 kuhusu Hadhi ya Wakimbizi (yatakayotajwa kama "Makubaliano ya 1951"). Aidha miongozo inapendekeza taratibu za kiutendaji kwa lengo la kuhakikisha kwamba umakini wa kutosha unawekwa katika mchakato wa kutoa uamuzi kuhusu maombi ya wanawake ya hadhi ya ukimbizi, na kwamba madai mbalimbali ya kijinsia yanatambulika kama inavyotakikana.
2. Ni kanuni iliyozoeleka kwamba fasili ya mkimbizi kwa jumla itolewe kwa kuzingatia masuala ya kijinsia ili iakisi sawasawa madai yanayotolewa katika uombaji wa hadhi ya ukimbizi. Utaratibu huu umeidhinishwa na Kamati Kuu ya Programu ya UNHCR¹.
3. Ili kujua undani wa utesaji wa kijinsia ni muhimu kutambua

1. Katika Mahitimisho yake ya Oktoba 1999, Na. 87 (n) Kamati Kuu "ilizitambua kwa furaha juhudu maalum za Serikali za kuingiza mtazamo wa kijinsia katika sera za kutoa hifadhi, kanuni na utekelezaji; ilihimiza Serikali mbalimbali, UNHCR pamoja na watendaji wengine wanaohusika, kuhamasisha mwiflikio mpana zaidi, na kuingiza katika vigezo vyao vya ulinzi wa wakimbizi hoja kwamba utesaji unaweza kuwa wa kijinsia au kufanywa kwa kupitia unyanyasaji wa kijinsia; zaidi ilihimiza UNHCR pamoja na watendaji wengine wanaohusika, kuandaa, kuhimiza na kutekeleza miongozo, kanuni za maadili ya kazi, na programu za mafunzo kuhusu masuala ya Wakimbizi ya kijinsia, ili kuunga mkono urasimishwaji wa mtazamo wa kijinsia na kuimarisha uwajibikaji kwa ajili ya utekelezaji wa sera za kijinsia" Rejea pia Mahitimisho ya Kamati Kuu: Na. 39, Wanawake Wakimbizi na Ulinzi wa Kimataifa, 1885; Na. 73, Ulinzi wa Wakimbizi na Unyanyasaji wa Kijinsia, 1993; Na. 77 (g). Hitimisho la Jumla kuhusuhifadhi ya kimataifa wa

na kutofautisha kati ya maneno "jinsia" na "jinsi". Jinsia ni neno linalotumika kuelezea uhusiano kati ya mwanamke na mwanaume kwa misingi ya mitazamo iliyojengeka kijamii au kiutamaduni katika kuhusisha utambulisho, hadhi, nafasi na majukumu na jinsi moja au nyingine. Jinsi ni sifa ya kibiojolia. Jinsia sio kitu kisichobadilika au cha kuzaliwa nacho bali maana yake kijamii na kitamaduni hubadilika kulingana na wakati. Malalamiko ya kijinsia yanaweza kutolewa na mwanamke au mwanaume, japokuwa yako malalamiko ambayo kwa mujibu wa asili yake hutolewa zaidi na wanawake. Wakati mwingine malalamiko yanaweza yakahusiana kwa kiasi kikubwa na jinsi ya mlalamikaji. Watoa uamuvi wanaoshughulikia malalamiko ya aina hii inabidi wawe makini zaidi. Kwa upande mwingine hata hivyo maombi ya mwomba hifadhi mwanamke yanaweza yasihuishwe na chochote kuhusu jinsi yake. Kimsingi malalamiko ya kijinsia, japo sio wakati wote, yamehusishwa zaidi na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia, magomvi ya kifamilia/kinyumbani, uzaziwa mpango wa kulazimisha, ukeketaji wa wanawake, adhabu kwa uvunjaji wa miiko ya kijamii, na unyanyaapaaji wa wasenge na wasagaji.

4. Kuridhia tafsiri yenye mrengo wa kijinsia ya Makubaliano ya mwaka 1951, hakumaanishi kuwa mwanamke wote wanaumba hadhi ya ukimbizi wanastahili kupewa hadhi hiyo. Mwomba hadhi ya ukimbizi ni lazima adhibitishé kwanza kwamba anazo hoja za msingi kuhusu hofu yake ya kuteswa kwa sababu za kimbari, kidini, kiutaifa, uanachama katika kundi fulani au msimamo wake wa kisia.

11. UPAMBANUZI HALISI

A. USULI.

5. Kihistoria, fasiri ya mkimbizi imekuwa ikitolewa kwa misingi ya mitazamo ya kiume. Hii ikimaanisha kuwa maombi mengi ya hadhi ya ukimbizi toka kwa wanawake na wasenge na mashoga hayakutiliwa maanani. Hata hivyo katika muongo uliopita, uchambuzi na uelewa wa jinsi na jinsia katika masuala ya wakimbizi umeongezeka kwa kiasi kikubwa katika sheria maalum, katika utendaji wa jumla wa Serikali na katika maandiko ya kitaaluma. Mabadiliko hayo yametokea sambamba, na yamechochewa na, maendeleo katika sheria na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu² pamoja na maeneo yanayohusu sheria

za kimataifa kupitia Sheria ya Mahakama za Kimataifa kwa iliyokuwa Yugoslavia na kwa Rwanda, na sheria ya kimataifa ya makosa ya jinai iliyopitishwa Rome. Kwa hali hii, kwa mfano, ieleweke kuwa madhara yatokanayo na ukiukwaji wa sheria na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, hayawezi kuhalalishwa kwa misingi ya kihistoria, kimila, kidini au kiutamaduni

6. Japokuwa jinsia haikurejelewa katika fasiri ya mkimbizi, inakubalika sana kwamba jinsia inaweza kushawishi au kuamrisha aina ya utesaji au aina ya mteswaji pamoja na sababu za utesaji huo. Hivyo fasiri ya mkimbizi, ikitazamwa kwa undani, inajumuisha malalamiko ya kijinsia. Kwa hiyo hakuna haja ya kuongeza lolote kwa ile tafsiri ya Makubaliano ya mwaka 1951³.
7. Katika kujaribu kutumia kigezo cha tafsiri ya mkimbizi kwenye taratibu za kuamua hadhi ya ukimbizi, ni muhimu kufanya hivyo kwa misingi ya kihistoria na kuangalia mazingira yote muhimu yanayo husiana na suala husika. Ni muhimu kuwa na taarifa kamili kuhusu tabia yake, maisha yake pamoja na jinsi anavyofahamika, pamoja na uchambuzi wa taarifa za wakati uliopo za kihistoria, kijiografia na za kitamaduni za nchi alikotoka mwombaji ukimbizi. Kufanya maamuzi ya jumla tu kwa misingi ya eti ni wanaume au wanawake haisaidii maana kwa kufanya hivyo, tofauti za misingi ambazo ni muhimu kwa masuala fulanifulani zinaweza zisitiliwe maanani au zikasahaulika.
8. Vipengele vya tafsiri vilivyojadiliwa hapa chini ni vile vinavyohitaji mtizamo yakinifu wa kijinsia. Vigezo vingine (mfano, kuwa nje ya nchi ulikozaliwa) vinabakia kama vigezo muhimu katika kutoa uamuzi kuhusu lalamiko lolote. Mahali popote katika andiko hili matumizi ya neno “wanawake” yanajumuisha pia mtoto wa kike.

B. SABABU HALISI YA HOFU YA UTESWAJI.

9. Sababu halisi ya hofu ya uteswaji itategemea mazingira halisi ya kila shauri. Wakati ambapo wanaume na wanawake waomba ukimbizi wanaweza kukabiliwa na tishio la aina moja, wanaweza pia kukabiliwa na aina
2. Maandiko muhimu ikiwa ni pamoja na Tamko la Dunia kuhusu Haki za Binadamu 1948, Mapatano ya Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa 1966, Mapatano ya Kimataifa kuhusu Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni 1966, Makubaliano kuhusu Haki za Kisiasa za Wanawake 1953, Makubaliano dhidi ya Utesaji pamoja na Ukatili mwagine, Matendo ya Kinyama au ya Udhaliilishaji au Adhabu 1984, Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto 1988, na hasahasa, Makubaliano kuhusu Utokomezaji wa Aina zote za Ubaguzi wa Wanawake 1979 pamoja na Azimio kuhusu Utokomezaji wa Unyanyasajji Dhidi ya Wanawake 1993. Maandiko muhimu ya kikanda ni pamoja na Makubaliano ya Uropa kuhusu Haki za Binadamu na Uhuru wa Misingi 1950, Makubaliano ya Amerika kuhusu Haki za Binadamu 1969, pamoja na Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu 1981.
3. Tazama Mahitimisho ya Muhtasari – Utesaji wa Kijinsia, Ushauri wa Kidunia kuhusu Ulinzi wa Kimataifa, Meza ya Majadiliano ya Watalamu, San Remo, Septemba 6-8 2001. Na. 1 na 3 (Mahitimisho ya Muhtasari – Utesaji wa Kijinsia)

za utesaji kwa msingi wa jinsi zao. Sheria ya kimataifa ya haki za binadamu na sheria ya kimataifa ya makosa ya jinai zinabainisha matendo fulani, kwa mfano unyanyasaji wa kingono, kama ukiukwaji sheria hizo. Aidha Sheria hizo zinaunga mkono kutambuliwa kwa matendo hayo kama ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu unaostahili kuchukuliwa kama utesaji⁴. Kwa hali hii, sheria ya kimataifa inaweza kusaidia watoa maamuzi katika kutambua kama aina fulani ya tendo ni la kiutesaji. Ni dhahiri kuwa ubakaji na aina nyingine za unyanyasaji kijinsia, kama vile magomvi yatokanayo na masuala ya mahari, ukeketaji na magomvi ya nyumbani na utoroshaji⁵ ni vitendo vinavyosababisha maumivu na mateso makali - kiakili na kimwili - na ambayo yamekuwa yaktumika kama aina ya utesaji, kwa kustawishwa ama na nchi au watu binafsi.

10. Kutathmini sheria ya utesaji au inayochangia katika utesaji kumedhibitika kusaidia katika kuamua malalamiko ya kijinsia. Hii inatokana na ukweli kwamba sheria halalizaweza kutokana na mila au desturi na matendo ya kitamaduni, vitu ambavyo si lazima viendane na viwango vya sheria za kimataifa za haki za binadamu. Hata hivyo, kama ilivyo kwa mashauri mengine yote, bado mlalamikaji ni lazima aonyeshe kuwa anao woga halali wa kuteswa kutokana na sheria hizo. Hii haitakuwa hivyo pale ambapo sheria kandamizi bado zipo lakini hazitumiki
11. Hata pale ambapo serikali fulani imepiga marufuku vitendo vya utesaji (kama ukeketaji) bado serikali husika inaweza kuendelea kuvumilia vitendo hivyo au kushindwa kuvikomesha kabisa. Katika hali ya namna hii, matendo hayo bado yatachukuliwa kama ni utesaji. Kwa hiyo, ukweli tu kwamba sheria imepitishwa kuzuia au kupinga vitendo fulani vya utesaji hautatosha kutumika katika kuamua kuwa maombi fulani ya hadhi ya ukimbizi hayana uhalali.
12. Pale ambapo adhabu iliyotolewa kwa kutozingatia sera, au kuvunja sheria imekuwa kali sana na inagusa masuala ya kijinsia, adhabu hiyo itakuwa sawa na utesaji⁶. Hata kama sheria husika ni moja ya sheria halali, mazingira ya adhabu au ushughulikiaji wa mhalifu hayapaswi kuwa ya kinyama sana kiasi cha kuwa kinyume cha lengo la sheria yenyewe. Hivyo adhabu kali sana kwa wanawake ambao, kwa kuvunja sheria, huwa wameenda kinyume na miiko ya kijamii, inaweza kuchukuliwa kama utesaji.
13. Hata pale ambapo sheria au sera zina malengo halali, taratibu za kutekeleza wake zinazosababisha matokeo

4. Tazama Kiongozi cha UNHCR, aya ya 51

5. Tazama aya ya 18 hapo chini

6. Watu wanaokimbia utesaji au adhabu kwa kuvunja sheria ya nchi kwa kawaida sio wakimbizi, hata hivyo mkanganyiko unaweza kuwepo katika utofautishaji, hasa katika mazingira ya kutolewa kwa adhabu kali sana kwa kuvunja sheria halali. Tazama Kiongozi cha UNHCR aya ya 56 na 57

yenye madhara kwa anaye husika zitachukuliwa kama kitendo cha utesaji. Kwa mfano, kwa jumla inakubalika kuwa uzazi wa mpango ni jambo zuri katika kudhibiti ongezeko holela la watu. Hata hivyo kutekeleza sera za namna hii, kwa njia ya utoaji mimba na ufungaji kizazi usio wa hiari kutakiuka haki za msingi za binadamu. Utekelezaji wa namna hiyo, licha ya kuwa unaweza ukawa unafanyika chini ya sheria halali, unatambulika kama ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na hivyo kuchukuliwa kama utesaji.

Ubaguzi Unaolingana na Utesaji

14. Wakati ambapo inakubalika kwa jumla kuwa ‘ubaguzi’ tu kama ubaguzi hauwezi, katika mazingira ya kawaida, kuwa au kusababisha utesaji, aina fulani ya ubaguzi au uonevu vinaweza kuchukuliwa kama utesaji unaostahili ulinzi wa kimataifa. Kwa mfano ubaguzi utachukuliwa kama utesaji ikiwa vitendo vyake vinasababisha kutotambuliwa kwa mhusika, kwa mfano, katika haki ya kujipatia kipato, haki ya kuamini dini anayotaka au kupata elimu⁷.
15. Aidha uchambuzi wa aina za ubaguzi wa Kiserikali kama vile kushindwa kutoa ulinzi kwa mtu binafsi dhidi ya hatari fulanifulani ni muhimu sana katika masuala ya malalamiko ya kijinsia. Endapo serikali, ama kwa misingi ya kisera au kiutendaji haitoi haki fulanifulani au ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa hali ya juu, yani ubaguzi katika kutoa ulinzi, kisha hali hiyo ikasababisha mhusika kutendewa madhara makubwa bila ya woga wa kisheria, hali hiyo itachukuliwa kama utesaji. Matukio mahususi ya magomvi ya nyumbani au unyanyasaji unaotokana na tofauti za malezi kijinsia, yanaweza, kwa mfano, kuchambuliwa katika mazingira ya namna hii.

Utesaji kwa Misingi ya Malezi ya Mtu Kingono

16. Malalamiko ya wakimbizi yanayotokana na tofauti za malezi kijinsia ni kipengele cha kijinsia. Jinsi au vitendo vya kingono vya mlalamikaji vinaweza kuwa muhimu katika ombi la ukimbizi pale ambapo muhusika amekuwa akifanyiwa vitendo vya utesaji (pamoja na ubaguzi) kwa sababu tu ya jinsi yake au vitendo vyake vya kijinsi. Katika matukio mengi ya aina hiyo mlalamikaji huwa amekataa kukubaliana na desturi na mila zilizowekwa zifuatwe na jinsi yake. Malalamiko ambayo ni ya mara kwa mara ni yale yanayohusiana na usenge au ushoga, ubadilishaji wa jinsi, au uvaaji wa mavazi ya jinsi nyingine. Wahusika wa malalamiko haya wamekuwa wakikabiliwa na hali ngumu sana kijamii ikiwa ni pamoja na ukatili, unyanyasaji na ubaguzi wa hali ya juu.

7. Tazama Kiongozi cha UNHCR aya ya 54

17. Mahali ambapo tabia ya usenge na ushoga haikubaliki kisheria, utoaji wa adhabu kali sana dhidi ya matendo ya usenge na ushoga unaweza kuwa sawa na utesaji, sawa na ambavyo ingefanyika kwa mwanamke aliyekataa kucaa baibui katika baadhi ya jamii. Hata pale ambapo usenge na ushoga haukatazwi kisheria, bado mlalamikaji anaweza kutoa malalamiko halali ikiwa Serikali haimlindi dhidi ya kubaguliwa au kufanyiwa madhara au imeshindwa kumlinda kikamilifu dhidi ya hali kama hiyo.

Kutorosha ili Kutumikisha katika Ukahaba au Unyonyaji Kingono kama Aina ya Utesaji⁸

18. Baadhi ya wanawake na watoto walitoroshwa wana maombi halali ya hadhi ya ukimbizi chini ya Makubaliano ya mwaka 1951. Utoroshaji wa wanawake na watoto kwa nguvu au kwa udanganyifu kwa lengo lwa kuwatumia katika ukahaba wa kulazimishwa na unyonyaji wa kingono ni aina ya unyanyasaji wa kijinsia ambao wakati mwingine huweza kusababisha kifo. Ukatili huu unaweza kuchukuliwa kama aina ya mateso na ukatili, unyama au uonevu. Aidha ukatili huu unaoweza kumnyima mwanamke uhuru wa kutembea, kwa kuhofia kukamatwa na kutoroshwa, kufungiwa na/au kunyang'anywa hati za kusafiria au aina nyingine za vitambulisho. Pia wanawake na watoto walitoroshwa, hukabiliwa na utesaji makali pale wanapotoroka au kurejea kwao. Utesaji huo ni pamoja na ulipizaji kisasi unaofanywa na makundi ya watoroshaji au watu binafsi, uwezekano wa kukamatwa na kutoroshwa tena, kutengwa na familia au jamii au kubaguliwa kwa hali ya juu. Hivyo, utoroshwaji wa mtu kwa ajili ya kutumiwa katika ukahaba wa kulazimishwa au katika unyonyaji wa kingono unaweza kuwa sababu ya msingi ya kuomba ukimbizi pale ambapo Serikali imeshindwa au haitilii maanani kumlinda mtu anayekabiliwa na tishio hilo⁹.

Mawakala wa Utesaji

19. Upo upenyo katika fasiri ya mkimbizi wa kuweza kuwatambua mawakala wa utesaji wa Serikali na wasio wa Serikali. Wakati ambapo mara nyingi utesaji hufanywa na mamlaka za nchi, ubaguzi wa hali ya juu au matendo
-
8. Kwa minajili ya Miongozo hii, 'utoroshaji' umefasiriwa kama ilivyo katika kifungu cha 3 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia, Kutokomeza na Kuadhibu Watoroshaji wa Binadamu, hususan Wanawake na watoto, nyongeza katika Makubaliano ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Makosa ya Kimataifa, 2000. Kifungu cha 3 (1) kinaneleza kuwa utoroshaji wa watu maana yake ni 'ukusanyaji, usafirishaji, ubadilishanaji, ufichajji au upokeajji wa watu kwa kutumia vitisho au nguvu au aina nyingine za shurutisho, utekaji nyara, hila au udanganyifu, madaraka, matatizo ya mtu au kwa kutoa au kupokea malipo au faida ili kumfanya mtu mmoja akubali kumilikiwa na mtu mwingine, kwa lengo la unyonyaji. Unyonyaji utajumuisha, kwa chini kabisa, utumiaji wa ukahaba wa watu wengine au aina nyingine za unyonyaji wa kingono, kazi ya kulazimishwa, utumwa au matendo ya kitumwa, au kutolewa kiungo.
9. Utoroshaji wa binadamu kwa sababu nyingine yoyote ile utachukuliwa pia kama utesaji, kutegemea mazingira husika

mengine mabaya yanayofanywa na watu au mtu, yanaweza pia kuchukuliwa kama utesaji ikiwa matendo hayo yanajulikana kuwa yanashabikiwa na mamlaka za nchi au kama mamlaka hizo zinakataa, au hazina uwezo wa kutoa ulinzi wa kutosha¹⁰.

C. CHANZO CHA SABABU (kwa sababu ya)

20. Woga halisi wa kuteswa ni lazima uhusishwe na msingi mmoja au zaidi ya Makubaliano ya mwaka 1951. Yani ni lazima hofu hiyo itokane na "sababu za" mbari, dini, utaifa, uanachama wa kundi fulani la kijamii au msimamo wa kisiasa. Msingi wa Makubaliano ni lazima uwe mojawapo ya sababu ya hofu hiyo, pamoja na kuwa haupaswi kuonyeshwa kama sababu pekee, au sababu ya msingi. Katika mamlaka nyingi za kisheria chanzo cha sababu ("kwa sababu ya") lazima kiwekwe bayana (mfano, katika baadhi ya Sheria za Kawaida za Nchi) wakati ambapo katika nchininyingine sababu haipewi uzito wa kuchunguzwa kipekee; bali hujumuishwa katika uchunguzi wa pamoja wa fasiri ya mkimbizi. Katika madai mengi ya kijinsia suala gumu kwa mtoa uamuza linaweza lisiwe ni kufanya uamuza kwa msingi unaokubalika bali kwa chanzo cha sababu: kwamba hofu halisi ya woga wa kuteswa ndio sababu ya msingi. Mtesaji wa Serikali au asiye wa Serikali anapotumia msingi wa Makubaliano kwa mlalamikaji inatosha kupata chanzo cha tatizo kinachohitajika.
21. Pale ambapo kuna hatari ya kuteswa na mtu binafsi asiyehusika na serikali, kama (mume, au rafiki au mtu mwingine) kwa sababu zinazohusiana na moja ya misingi ya Makubaliano, chanzo cha sababu hubainika, yani kama kukosekana kwa ulinzi wa Serikali kunahusiana kukumbatia Makubaliano au la. Vinginevyo, pale ambapo hatari ya kuteswa mikononi mwa mtu asiye wa Serikali haiusiani na msingi wa Makubaliano, lakini kutokuwa na uwezo au kutokuwa tayari kwa Serikali kutoa ulinzi kunatokana na sababu za msingi wa Makubaliano, chanzo cha sababu huwa pia kimebainika¹¹.

D. Misingi ya Makubaliano ya mwaka 1951.

22. Kuhakikisha kwamba tafsiri ya kijinsia inahusishwa na kila msingi wa Makubaliano ni muhimu katika kuamua kama kila muombaji wa hadhi ya ukimbizi amekidhi vigezo vya fasiri ya mkimbizi. Mara nyingi walalamikaji huweza kukumbana na mateso kwa sababu ya msingi wa Makubaliano wanaohusishwa nao. Katika jamii nyingi maoni ya mwanamke ya kisiasa, mbari yake, utaifa wake, dini yake au kundi lake la kijamii, kwa mfano, mara nyingi

10. Tazama Kiongozi cha UNHCR, aya ya 65

11. Tazama Mahitimisho ya Muhutasari – Utesaji wa Kujinsia, no. 6

huchukuliwa kuwa yanafungamana na ya ndugu, marafiki, au hao walioko katika jumuia hiyo.

23. Ni muhimu pia kutambua kuwa katika madai mengi ya kijinsia, mateso yanayohofiya yanaweza kuhusishwa na moja au zaidi ya misingi ya Makubaliano. Kwa mfano, ombi la hadhi ya ukimbizi lenye misingi ya ukiukaji wa desturi za kijamii au za kidini linawenza kuchunguzwa kwa misingi ya kidini, ya msimamo wa kisiasa au ya uanachama katika kundi fulani la kijamii. Mlalamikaji hapaswi kuweka bayana sababu za kuwa na woga wa kuteswa.

Mbari

24. Kwa ajili ya fasiri ya mkimbizi, mbari imefasiriwa kujumuisha aina zote za makabila yanayotajwa kama "mbari" katika matumizi ya kawaida¹². Utesaji wa wanaume na wanawake kwa sababu za kimbari unaweza kuelezeza kwa njia tofauti. Kwa mfano, mtesaji anaweza kuamua kuharibu utambulisho wa kikabila na/au mafanikio ya kundi la mbari kwa kuua, kuchopoa viungo au kuhasi wanaume, wakati ambapo wanawake wanaoonekana kama wadumishaji wa utambulisho wa kabilo au mbari wanawea kuteswa kwa njia tofauti kama vile kwa kunyanyaswa kijinsia au kwa kudhibiti uzazi.

Dini

25. Katika baadhi ya nchi/serikali, dini huelekeza majukumu fulanifulani au kanuni za tabia fulani kwa wanawake na wanaume pia. Ikiwa mwanamke anashindwa kutimiza jukumu au kukataa kutii kanuni husika ya kidini, hapa mwanamke anayehusika anaweza kuwa na sababu za misingi za kuhofia kuteswa kwa sababu za kidini. Kushindwa kutii kanuni hizi kunaweza kuchukuliwa kama uthibitisho kuwa mwanamke huyu anashikilia mambo yasiyokubalika katika dini hiyo bila kujali imani yake halisi. Mwanamke anaweza kunyanyaswa kwa sababu ya imani au matendo ya imani yake ya kidini, au kwa imani na matendo anayohusishwa nayo ikiwa ni pamoja na kukataa kuzingatia imani fulanifulani, pamoja na kukataa kushikamana na maagizo na mafundisho fulanifulani ya kidini
26. Kuna mwingiliano baina ya imani ya dini na msimamo wa kisiasa katika madai ya kijinsia hasa katika ulingo wa upinzani wa kisiasa. Wakati ambapo imani za kidini huhusisha mwanamke na tabia fulanifulani za kidini, kwa mwanamke kwenda kinyume na tabia hizo kunaweza kuchukuliwa kama uthibitisho wa mwanamke huyo kuwa

12. Tazama Kiongozi cha UNHCR, aya ya 68

na msimamo tofauti wa kisiasa. Kwa mfano, katika baadhi ya jamii, majukumu aliyopewa mwanamke yanaweza kuwa yametokana na msimamo wa Serikali au wa dini ya nchi husika. Mamlaka au wahusika wengine wa utesaji wanaweza kuchukulia kitendo cha mwanamke cha kushindwa kuzingatia majukumu hayo kama uthibitisho wa kushindwa kuzingatia maadili ya imani ya kidini. Wakati huohuo, kushindwa huko kutii majukumu kukatafsiriwa kama kushikilia msimamo tofauti wa kisiasa ambaao ni tishio kwa mfumo uliko madarakani. Hili ni dhahiri kabisa hasa katika jamii ambazo hazitofautishi sana kati ya dini na asasi za serikali, sheria na imani.

Utaifa

27. Utaifa usichukuliwe tu kama "uraia". Una maana pia ya kuwa mwanachama wa kikundi fulani cha kabilia au lugha na wakati mwingi huweza kuchanganywa na neno "mbari".¹³ Japokuwa utesaji kwa misingi ya kiutaifa (kama mbari) sio tu kwa wanawake au wanaume, mara nydingi mazingira ya utesaji huchukua mkondo wa kijinsia, hasa ule wa unyanyasaji kingono ambaao huelekezwa kwa wanawake na wasichana.

Uanachama wa Kundu fulani katika Jamii¹⁴

28. Madai ya kijinsia yamekuwa yakichunguzwa kwa kutumia kigezo cha msingi huu na hivyo kuleta umuhimu wa kuielewa vyema dhana hii. Hata hivyo kwa upande mwingine, msisitizo unaowekwa katika msingi wa kundi la kijamii umeonekana kama wa kutojali makundi mengine husika kama ya kidini au kisiasa. Hivyo fasiri inayotolewa kwa msingi huu haiwezi kuiondolea umuhimu misingi mingine minne ya Makubaliano.
29. Kwa hiyo kikundi fulani cha kijamii ni mkusanyiko wa watu wenye mawazo na tabia zinazofanana achilia mbali woga wao wa kuteswa, au watu ambaao wanatambuliwa na jamii kama kikundi. Mfanano wao mara nydingi utakuwa unatokana na kuzaliwa, kutokebadilika, au ambaao ni msingi wao wa utambulisho, dhamira au uzingatiaji wa haki za binadamu.
30. Kwa msingi wa fasiri ya kikundi fulani cha kijamii, ni dhahiri kwamba jinsi inaweza kuwa sifa ya ukundi, ambapo wanawake ni kundi mojawapo la kijamii linalojibainisha kwa sifa za kuzaliwa na zisizobadilika. Kundi ambalo mara nydingi huchukuliwa tofauti na lile la wanaume¹⁵. Sifa za wanawake pia zinawabainisha kama kikundi ndani ya

13. Rejea Kiongozi cha UNHCR, aya ya 74

14. Kwa taarifa za kina zaidi, rejea Miongozo ya UNHCR kuhusuhifadhi ya kimataifa " Uanachama wa kikundi fulani cha kijamii" katika mazingira ya Kifungu 1A(2) cha Makubaliano ya mwaka 1951 na /au Nyongeza yake ya 1967 kuhusu Hadhi ya Wakimbizi (UCR/GIP/02/02, Mei 7, 2002)

jamii, kinachopewa hadhi na huduma tofauti katika baadhi ya nchi.¹⁶ Vivyo hivyo kwa fasiri hiyo ya kikundi fulani cha kijamii, yamo makundi ya wasenge na mashoga, waliobadili jinsi zao au wenyewe tabia ya jinsi nyiningine.

31. Mara nyingi ukubwa wa kikundi umetumika katika kipinga dhana ya kuwachukulia wanawake kama kikundi cha kijamii. Upinzani wa namna hii hauna msingi wowote kwani kigezo cha ukubwa hakitumiki popote katika misingi mingine ya kuflikia maamuzi. Pia hakuna sababu ya kushikilia kuwa kikundi fulani cha kijamii kiwe na mshikamano fulani au kwamba wanachama wake washirikiane kihiar¹⁷ au kwamba kila mwanachama yuko katika hatari ya kuteswa¹⁸. Inakubalika kabisa kuwa ni lazima uwepo uwezekano wa kufanya utambuzi wa kikundi bila kigezo muhimu katika kuamua utambulisho wa kundi kwenye mazingira maalumu.¹⁹

Msimamo wa Kisiasa

32. Kwa msingi huu, mwomba hadhi ya ukimbizi lazima aonyeshe dhahiri kuwa ana woga au hofu ya kuteswa kwa sababu ya msimamo wake fulani wa kisiasa (kwa kawaida unaotofautiana na ule wa serikali inayotawala au sehemu ya jamii), au kwa sababu anahuishwa na kuwepo kwa msimamo huo wa kisiasa. Msimamo wa kisiasa lazima utizamwe kwa mapana ili kujumlisha mtazamo wowote kuhusu jambo lolote ambalo linaloweza kuhuishwa na vyombo vya Dola, Serikali au jamii au sera. Hii inaweza pia kujumuisha msimamo kuhusu majukumu ya kijinsia. Itahus pia tabia ya kutokukubaliana ambayo humfanya mtesaji kumlazimishia kufuata msimamo fulani wa kisiasa. Kwa sababu hii basi, kunakuwa hakuna shughuli za kisiasa au zisizo za kisiasa ambazo mtu analazimishwa kuzifuata kwa msingi wa kurithishwa bali mazingira ya tukio yataamua undani wake ulivyo. Hata hivyo, uombaji wa hadhi ya ukimbizi kwa msingi wa msimamo wa kisiasa unachukuliwa kwamba mwombajji ana au anachukuliwa kuwa na msimamo wa kisiasa usiokubaliwa na mamlaka husika au jamii, ambao unakosoa sera, mila au mbinu za mamlaka au jamii hiyo. Aidha inachukuliwa kuwa msimamo wa aina hiyo umefahamika au utafahamika kwa mamlaka kwa jamii inayohusika, au unahuishwa na mwombajji wa hadhi ya ukimbizi. Sio lazima kila mara muhusika awe

-
15. Rejea Mahitimisho ya Muhtasari – Utesaji wa Kijinsia, no. 5.
 16. Rejea pia Hitimisho la Kamati Kuu Na. 39, Wanawake Wakimbizi na Ulinzi wa Kimataifa, 1985: "Dola ... zina uhuru wa kuridhia tafsiri kwamba waomba hifadhi wanawake wanaokabiliwa na matendo ya kinyama kwa sababu ya kutokubaliana na kaida za kijamii katika jamii wanamoishi wanaweza kuchukuliwa kama "kundi fulani la kijamii" kwa mujibu wa maana katika Kifungu cha 1A(2) cha Makubaliano ya Umoja wa Mataifa Kuhusu Wakimbizi ya mwaka 1951"
 17. Rejea Mahitimisho ya Muhtasari – Wanachama wa Kundi Fulani la Kijamii, Mashauriano ya Kidunia kuhusu Ulinzi wa Kimataifa, Majadiliano ya Wataalamu, San Romeo Septemba 6-8 2001, na.4 ("Mahitimisho ya Muhtasari – Uanachama wa Kundi Fulani la Kijamii")
 18. Rejea Mahitimisho ya Muhtasari – Uanachama wa Kundi Fulani la Kijamii, ibid., na.7
 19. Rejea Mahitimisho ya Muhtasari – Uanachama wa Kundi Fulani la Kijamii, ibid., na 6

ameshaeleza msimamo wake huo au awe amenyanyaswa kwa kubaguliwa au kwa kuteswa. Kwa matukio ya aina hii, uamuzi kuhusu uhalali wa woga wake ufanywe kwa msingi wa kutafakari mambo ambayo yangemfika mwombajji endapo angerejea kwenye nchi yake.

33. Dhana ya kumchukulia mkimbizi wa kisiasa kama mtu anayekimbia utesaji kwa kuhusika kwake moja kwa moja kwenye masuala ya kisiasa haioani siku zote na ukweli wa uzoefu wa wanawake kwenye baadhi ya jamii. Sio kawaida kwa wanawake kujihusisha katika siasa za ngazi ya juu sana kama ilivyo kwa wanaume. Mara nyingi wao huendesha siasa zao katika ngazi za chini, hali ambayo inaakisi majukumu makuu yalivyo kijinsia. Kwa mfano, mwanamke anaweza kufanya kazi za kuwahudumia kimatibabu askari wagonjwa, kutafuta wasamaria wa kujitolea, au katika kuandaa na kusambaza vipeperushi. Aidha wanawake huhushwa na misimamo ya kisiasa ya familia au ya ndugu zoa wa kiume. Wakati ambapo hali hii inaweza kuchunguzwa chini ya upinzani wa mawazo ya kisiasa, inaweza pia kutazamwa kama utesaji kwa misingi ya uanachama wake katika kundi mahususi la kijamii, kuwa ‘familia yake’. Sababu hizi hazina budi kuzingatiwa katika maombi ya hadhi ya ukimbizi kijinsia.
34. Muhimu pia kwa maombi ya hadhi ya ukimbizi kijinsia ni kutambua kuwa mwanamke anaweza asipende kuhusika katika shughuli fulani, kama vile kugawia wanajeshi wa serikali chakula, uamuzi ambaa unaweza kuchukuliwa na watesaji kama kushikilia msimamo tofauti wa kisiasa.

III MASUALA YA KIUTARATIBU

35. Watu wanaoomba hadhi ya ukimbizi kutokana na madai ya kijinsia, pamoja na wanurusika wa utesaji au hasahaha waliokumbwa na kihoro, wanapaswa kuhudumiwa katika hali ambayo itawahakikishia kuwa maombi yao yatatunzwa kama siri. Baadhi ya waombaji, kwa sababu ya kuona aibu kutokana na yaliyowafika, au kutokana na kihoro, wanaweza kukataa kutoa maelezo ya kina kuhusu mateso waliyoyapata au woga unaowakabilii. Wanaweza kuendelea kuwaogopa watu wenye mamlaka au, kuwa na hofu ya kukataliwa na/ama kulipizwa kisasi na watu wa familia na/au jamii zao.
36. Kwa hali hiyo, ili kuhakikisha kwamba maombi ya hadhi ya ukimbizi yanayotokana na madai ya kijinsia, hasa kwa wanawake, yanafanyiwa uamuzi ufaao wakati wa mchakato wa kutoa uamuzi kuhusu hadhi ya ukimbizi, ni lazima mambo yafuatayo yazingatiwe:

- (i) Wanawake wanaoomba hifadhi wanapaswa kusailiwa peke yao bila kuwepo kwa ndugu wa familia wa kiume. Hii ni ili kuhakikisha kuwa wanapata nafasi ya kutosha ya kuelezea matatizo yao. Ni lazima wafahamishwe kwamba kukubaliwa kwa maombi yao kunawategemea wao wenyewe.
- (ii) Ni muhimu wanawake wapewe taarifa kuhusu mchakato wa kuamua hadhi ya ukimbizi, namna ya kupata hadhi hiyo pamoja na ushauri wa kisheria. Wapewe taarifa hizo kwa lugha na mazingira yatakayowawezesha kuzielewa.
- (iii) Waombaji wa hadhi ya ukimbizi wafahamishwe kuwa wana uhuru wa kuwa na wakalimani pamoja na wasaili wa jinsi kama yao na waombaji wote wa kike wapatiwe watu wasaidizi hawa. Wasaili na wakalimani, kwa upande wao, wanapaswa kuzingatia na kuheshimu mambo nyeti ya kitamaduni au kidini au sababu binafsi kama vile umri na kiwango cha elimu.
- (iv) Kwa kawaida, mazingira ya uwazi na ya kutotiliana mashaka husaidia sana kujenga uaminifu kati ya masaili na msailiwa (mwomba hadhi ya ukimbizi). Aidha mazingira hayo yatasaidia katika kutoa dukuduku pamoja na taarifa nyeti za kibinafsi. Mpangilio wa chumba cha usaili uwe katika hali ya kuruhusu majadiliano, kulinda usirina kuondoa uwezekano wowote wa kuwa na hisia za upande mmoja kuhofia mwengine.
- (v) Msaili achukue nafasi ya kujitambulisha yeye mwenyewe na kumtambulisha mkalimani kwa mwomba hadhi ya ukimbizi. Katika kufanya hivyo afafanue bayana jukumu lake na la mkalimani pamoja na lengo hasa la usaili. Mwombaji ahakikishiwe kwamba maombi yake yatashughulikiwa kwa siri kabisa, na taarifa atakazotoa hazitawafikia watu wa familia yake. Aidha msaili amfahamishe mwombaji kwamba yeye sio mnasihi wa waliofikwa na kihoro cha hofu au mateso.
- (vi) Msaili asionyeshe kuegemea upande wowote, awe mwenye huruma na mkweli wakati wa usaili. Aidha, msaili aepuke kutumia lugha au uchezeshaji wa viungo vyake katika njia itakayoweza kuchukuliwa kama ni utishaji, au ukiukaji wa maadili ya kitamaduni au utovu wa nidhamu. Msaili amruhusu muombaji atoe hoja zake bila kuingiliwa kati mara kwa mara.
- (vii) Maswali yote ya jumla na yale maalumu ambayo yataweza kusaidia katika kuibua masuala ya kijinsia yaliyo muhimu kwa muombaji wa hadhi ya ukimbizi yaingizwe katika saili zote za waomba hifadhi. Mathalani, mara nyingi wanawake ambao wamekuwa wakijihuisha na masuala

- ya kisiasa kwa njia isiyo ya moja kwa moja au ambao wamekuwa wakihuushwa na msimamo fulani wa kisiasa, huwa hawatoi taarifa muhimu wakati wa usaili kutokana na uulizaji wa maswali kwa njia ambayo huwalenga zaidi wanaume. Waombaji wanawake pia wanaweza kushindwa kuhusisha maswali yanayohusu 'ukatili' na aina ya matendo maovu wanayohofia (kama vile ubakaji, udhalilishaji wa kingono, ukeketaji, 'mauaji ya heshima' ndoa za kulazimishwa)
- (viii) Ni muhimu kuwa na usaili wa pili hasa kwa walioathiriwa wa unyanyasaji wa kingono au waliokumbwa na aina nyingine za kihoro cha hofu, ili kujenga mazingira ya kuaminiana yatakayowezesha kupatikana kwa taarifa zote muhimu. Kuhusu usaili wa pili, wasaili waonyeshe huruma kwa hali ya kihoro na hisia za msailiwa na wasimamishe usaili pale msailiwa anapoonekana kusongwa sana na hisia za kukata tamaa.
 - (ix) Pale inapohisiwa kuwa shauri fulani litaibua madai ya kijinsia, utahitajika muda wa kutosha wa maandalizi kwa ajili ya kumjengea msailiwa mazingira ya kujiamini na kumuamini msaili. Vilevile muda huo wa maandalizi utampa nafasi msaili kuandaa maswali sahihi pamoja na kushughulikia tatizo lolote litakalojitokeza wakati wa usaili
 - (x) Taarifa ambazo zitasaidia katika upitiasi wa maombi ya wanawake zikusanywe kutoka katika nchi walikotoka. Taarifa hizo ni kama vile: nafasi ya wanawake mbele ya sheria, haki za kisiasa za wanawake, haki za kijamii na kiuchumi za wanawake, miiko ya kitamaduni na kijamii katika nchi hiyo pamoja na matokeo ya kutoizingatia, kiwango cha ukumbatiaji wa mila zenyne madhara, matokeo na aina ya matukio ya unyanyasaji wa kijinsia yaliyopotiwa, ulinzi walio nao wanawake, adhabu zozote ambazo zimetolewa kwa wale wanaoendezea unyanyasaji wa kijinsia, na hatari zinazomkabili mwanamke endapo atarejea nchini kwake baada ya kuomba hadhi ya ukimbizi.
 - (xi) Aina na kiwango cha hisia zitakazojitokeza wakati wa kuelezea mambo yaliyomfika visitumiwe kama sababu za kumwondoleauaminifu. Wasailipamojanawatoamaamuzi hawana budi kuzingatia kwamba tofauti za kiutamaduni pamoja na hali ya kuwa na kihoro vina umuhimu mkubwa na usio wazi katika kuamua tabia ya mtu. Kwa baadhi ya matukio, itabidi kutafuta ushahidi dhahiri wa kitiba na kisaikolojia. Sio lazima kutafuta undani wa tendo la kubaka au wa shambulio la kingono. Cha muhimu ni kutafuta matukio yaliyopelekea na yaliyofuatia tendo lenyewe, mazingira yaliyohusika pamoja na taarifa nyingine (kama vile matumizi ya bunduki, maneno au kauli fupi zilizotolewa na mnyanyasaji, aina ya shambulio liliofanyika, mahali

lilikotokea na kwa vipi lilitokea, taarifa kuhusu waliotenda kosa (mfano, ni askari au raia) n.k. Vilevile zitahitajika taarifa kuhusu sababu iliyomsukuma mhalifu akatenda hilo kosa. Ni vyema kuzingatia kuwa katika baadhi ya mazingira mwanamke anaweza asifahamu sababu za kudhalilishwa kwake.

- (xii) Kila inapowezekana pawepo na taratibu za kurufaa mwathiriwa au mnusurika kwenda kupatiwa unasihi wa kisaikolojia na kijamii pamoja na huduma nyingine za kumsaidia. Kutokana na uzoefu, ni vizuri wataalamu wa unasihi wa kisaikolojia na kijamii wawepo kuwasaidia wasailiwa kabla na baada ya usaili.

Masuala ya Ushahidi

37. Hakuhitajiki ushahidi wo wote wa maandishi ili mamlaka husika itambue maombi ya hadhi ya ukimbizi. Hata hivyo, taarifa kuhusu mila na desturi katika nchi alikotoka zitaweza kusaidia katika masuala mahususi. Ni muhimu kutambua kuwa, kuhusiana na madai ya kijinsia, ushahidi ambao kwa kawaida hupatikana katika maombi ya aina nyingine ya hadhi ya ukimbizi unaweza usipatikane kirahisi. Data za kitakwimu au ripoti kuhusu matukio ya unyanyasaji wa kingono vinaweza visipatikane. Hii inaweza kutokana na ama kutoripotiwa kwa matukio mengi ya aina hiyo au kukosekana kwa mashtaka. Aina mbadala ya taarifa inaweza kusaidia, kwa mfano taarifa za ushuhuda uliotolewa na wanawake wenziwe kwa maandishi au kwa mdomo, au ushuhuda uliotolewa na asasi zisizo za serikali au za kimataifa au uliotolewa na mchunguzi mwingine huru.

IV MBINU ZA UTEKELEZAJI

38. Kutegemeana na sheria zinavyotumika katika mazingira husika, pamekuwa na mikabala miwili ya kijinsia inayotumiwa na Serikali katika kuhakikisha matumizi ya sheria ya wakimbizi katika masuala nyeti ya kijinsia na hasa katika tafsiri ya mkimbizi. Baadhi ya Serikali zimeingiza mwongozo wa ufanuzi wa kisheria na/au kinga katika utaratibu wa sheria yenye. Aidha Serikali nyingine zimebuni sera pamoja na miongozo ya kisheria kwa ajili ya watoa maamuzi wa masuala nyeti ya kijinsia. Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, huzishawishi Serikali ambazo bado hazijachukua hatua za namna hiyo zihakikishe kuwa kunakuwa na matumizi ya sheria ya wakimbizi, taratibu na amri ambazo zitazisaidia Serikali hizo katika masuala hayo.

KIAMBATISHO 1

KANUNI ZA MAADILI YA UNHCR

Utangulizi

Ufanisi wa UNHCR katika kuwahakikisha wakimbizi na wahusika wengine ulinzi na msaada sahihi unategemea uwezo wa wafanyakazi wake katika kuzingatia na kudumisha viwango vya juu kabisa vya maadili na uanataaluma. Sisi, watumishi wa UNHCR, tunawajibika kudumisha viwango hivi - kila mmoja wetu pake yake na kwa ushirikiano pia. Mameneja wana jukumu mahususi la kuwa mfano mzuri wa uzingatiaji wa viwango hivi na kuwajengea wafanyakazi mazingira yanayowasaidia na kuwawezesha kutekeleza vizuri kazi zao.

Ni dhahiri kwamba kazi za UNHCR aghalabu huwapa watumishi wake madaraka makubwa juu ya watu wanaowahudumia. Watumishi hao wana wajibu mkubwa wa kujiza kutumia vibaya madaraka hayo.

Madhumuni ya Kanuni hizi za Maadili ni kuwaongoza wafanyakazi ili waweze kufanya maamuzi adilifu katika maisha ya taaluma zao na wakati mwagine katika maisha yao binafsi pia. Ni mwongozo wa kimaadili amba hauna nguvu ya kisheria. Lengo lake ni kuwasaidia watumishia kuelewa vizuri zaidi majukumu waliyobebeshwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa pamoja na Masharti na Kanuni za Utumishi, mambo ambayo kisheria ndiyo vigezo vinavyoelekeza na kuhalalisha mwenendo wa UNHCR. Tendo la kusaini kanuni hizi za maadili haliwanyang'anyi watumishi wa UNHCR haki zao nyingine.

Kwa kutambua kwamba sheria na desturi mahalia zinaweza kutofautiana kati ya nchi moja na nyingine, Kanuni za Maadili zimejitegemeza kwenye vigezo vya kisheria vya kimataifa. Kwa mfano, watoto wanafafanuliwa kuwa ni vijana amba umri wao uko chini ya miaka 18. Maelekezo kuhusu ufanuzi sahihi yanapatikana katika Maelezo juu ya Kanuni za Maadili.

Kanuni hizi zinawahu watumishi wote wa UNHCR, amba wataombwa kuzisaini. Watu amba wana mikataba ya kuishauri UNHCR pamoja na wakufunzi watapatiwa Kanuni hizi pia na kuombwa kuthibitisha uzingatiaji wake pale ambapo zinagusana na hadhi au majukumu yao. Asasi za serikali na zisizokuwa za kiserikali pamoja na makampuni ambayo yanashughulika na UNHCR kupitia watumishi wake yataombwa kutumia njia mwafaka kuwafahamisha waajiriwa wao hao kuhusu Kanuni hizi za Maadili.

Watumishi wote wa UNHCR wanawajibika kuhimiza, kulinda na kudumisha usambazaji wa Kanuni hizi za Maadili. Aidha wana wajibu pia wa kutekeleza, kufuatilia na kuhimiza uzingatiaji wa viwango vya kanuni hizi. Kadhalika watumishi wa UNHCR wanapaswa kuwahimiza wabia wa shirika hili kukumbatia viwango hivyo na kushirikiana nao katika uzingatiaji wake.

MAADILI YA MSINGI NA KANUNI ELEKEZI

Watumishi wa UNHCR wanapaswa kuzingatia maadili na kanuni za msingi zifuatazo:

- Kutokana na wadhifa wetu wa kuwa watumishi katika mfumo wa Umoja wa Mataifa, tutahakikisha kwamba tabia zetu zinaendana na zinaakisi maadili ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa: kwa kuheshimu haki za msingi za binadamu, haki ya kijamii na hadhi ya utu, na kwa kutambua na kuzingatia haki sawa kati ya wanaume na wanawake. Tuta saidia UNHCR kuhimiza uzingatiaji wa misingi ya sheria ya kimataifa kuhusu wakimbizi, sheria ya kimataifa kuhusu hakiza binadamu pamoja na sheria ya kimataifa kuhusu ubinadamu. Tutaongozwa na maadili ya msingi ya mfumo wa Umoja wa Mataifa, pakiwemo uanataaluma, hadhi na kuheshimu kutofautiana. Aidha tutazingatia daima mtizamo wa kimataifa.
- Tukiwa watumishi wa UNHCR, wajibu wetu mkuu utakuwa ni kuwahakikishia wakimbizi wa wahusika wengine ulinzi na misaada kulingana na mamlaka ya Ofisi. Tunaahidi kuunga mkono kikamilifu ushirikishwaji wa wakimbizi na wahusika wengine, kwa ngazi ya mtu mmoja mmoja, familia na jamii, katika maamuzi ya masuala yanayohusu maisha yao.
- Tutaenzi hadhi na heshima ya kila mtu; tutadumisha na kuzingatia uelewa, taadhima, huruma na uvumilivu; na tutakuwa waadilifu na kutunza siri kama inavyotakiwa. Tutajitahidi kujenga mahusiano na ushirikiano mzuri wa kikazi kati yetu na wabia wetu; daima tutajitahidi kuboresha utendaji wetu. Aidha tutakazana kujenga mazingira ambayo yanahamasisha kujifunza na kuijendeze, mabadiliko chanya na tutatumia vizuri mafunzo yatokanayo na uzoefu wetu.
- Tutawaheshimu watu wote kwa usawa pasipokujali kabilia, jinsia, dini, rangi, utaifa, lugha, hali ya ndoa ya mhusika, mionjo yake ya kimapenzi, umri, hadhi yake ya kijamii na kiuchumi, ulemavu, itikadi ya kisiasa, au jambo lingine lolote linalomtofautisha na wengine. Tutajitahidi kung'oa vikwazo vyote vinavyokinzana na usawa.
- Tutaheshimu tamaduni, mila, na desturi za watu wote, na tutajitahidi kuepukana na vitendo ambavyo havikubaliki katika muktadha wa utamaduni mahususi. Lakini tukikumbana na desturi au vitendo ambavyo vinahisiwa kunkinzana na haki za binadamu au viwango vinavyokubalika kimataifa, hapo itatulazimu kufuata na kuongozwa na haki za binadamu au viwango vya kimataifa.

Kujitolea kwa Kanuni za Maadili ya UNHCR

Nikiwa mtumishi wa UNHCR, najitolea kama ifuatavyo:

- 1. Nitawahudumia wakimbizi na waathiriwa wengine kwa kuzingatia haki, heshima na staha zao.**

Nitajitahidi daima kuelewa matatizo ambayo wakimbizi na watu wengine wanaohudumiwa na UNHCR walikumbana na kunusurika nayo. Aidha nitajitahidi pia kuelewa hali ya hatari ambayo waathiriwa hao wanaweza kujikuta wakikabiliwa nayo, hususani kwa sababu za unyanyasaji wa kingono na kijinsia, umri au ulemavu, kutokana na watu ambaao wana madaraka na mamlaka juu ya maisha yao.

Daima nitalinda na kudumisha haki za watoto, na nitahakikisha kuwa jambo pekee la kuongoza utekelezaji wa majukumu yangu kwao ni ubora wa mahitaji na maslahi yao.

Kama kazi zangu zinawahusu wakimbizi au waathiriwa wengine moja kwa moja, nitahakikisha kuwa nakutana nao mara kwa mara kwa ajili ya kuongeza uelewa wangu wa uzoefu wao na mahitaji yao. Aidha nitatumia fursa hizo kuelezea majukumu ya UNHCR pamoja na upeo wa kazi zake.

Daima nitajielimisha kuhusu sera za UNHCR, malengo na shughuli zake, na sambamba na hiyo nitajielimisha kuhusu masuala ya wakimbizi huku nikijitahidi kadiri ya uwezo wangu kutekeleza majukumu ya Ofisi kuhusiana na kazi za ulinzi na utoaji wa misaada.

- 2. Nitalinda hadhi ya UNHCR, kwa kuhakikisha kuwa tabia yangu binafsi na ya kitaaluma inaonekana dhahiri kuwa ya kiwango cha juu kabisa.**

Kupitia vitendo vyangu nitadhihirisha uadilifu, ukweli, uaminifu na moyo wa kujitolea. Nitatumia ustahimili, heshima, adabu kwa watu wote ambaao nitakuwa na mahusiano nao rasmi ya kikazi, pakiwemo wakimbizi pamoja na wahusika wengine, wawakilishi wa washiriki wetu wengine, mathalani, serikali na wafadhili.

Nitatii sheria zote za nchi na mahali pangu pa kazi; nitatekeleza majukumu yangu binafsi, ya kisheria na yale ya kifedha, na sitotumia njia haramu kujinufaisha kupitia fursa zangu zitokananzo

na utumishi wangu kwa Umoja wa Mataifa. Nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kuhakikisha kuwa tabia na matendo ya wanafamilia wangu haviharibu jina na hadhi ya UNHCR.

3. *Ili kulinda na kudumisha imani ya umma katika UNHCR, nitatekeleza majukumu rasmi na mambo yangu binafsi kwa jinsi ambayo haitaleta mgongano wa maslahi.*

Matendo yangu hayatotawaliwa wala kuongozwa na tamaa ya kujinufaisha, na nitajizuia kufanya maamuzi yatokanayo na mashinikizo ya kisasa. Katika utekelezaji wa majukumu yangu, sitoomba wala kukubali maelekezo ya serikali yoyote, pakiwemo mamlaka za taifa langu, au mamlaka yoyote isiyohusika na Umoja wa Mataifa.

Kwa mujibu wa Masharti na Kanuni za Utumishi, sitokubali tuze yoyote, nishani, fadhila, zawadi, au malipo kutoka kwa serikali yoyote wala kutoka kwa chanzo chochote ambacho hakihuiani na Umoja wa Mataifa bila na kabla ya kupata kibali cha kufanya hivyo. Sitofanya kazi yoyote iliyo nje ya ajira yangu bila na kabla ya kupata kibali cha kufanya hivyo. Sitokubali malipo yoyote ya ziada au ruzuku kutoka kwa serikali yoyote au chanzo kingine chochote; kadhalika sitoshiriki katika shughuli za kisasa kwa mfano kufanya kazi katika ofisi ya umma.

Nitajizuia kumsaidia mtu binafsi au kampuni kuingia mahusiano ya kikazi na UNHCR iwapo hatua kama hiyo inaweza kutafsiriwa kama kitendo cha upendeleo. Sitojihuisha na shughuli zinazohusu ununuvi wa vifaa au huduma, michakato ya uandikishaji kazi, hususani pale ambapo kuhusika kwangu kunaweza kuleta mgongano wa maslahi.

4. *Nitachangia kujenga mazingira mazuri ya kufanya kazi yaliyojikita katika ushirikiano, heshima na uelewa kati ya wahusika.*

Nitawaheshimu wafanyakazi wenzangu pasipokujali hali wala nyadhifa zao, na nitawapatia fursa za kutoa maoni yao na kuchangia juhudzi za kazi zetu kutohuna na maarifa na uzoefu wao. Nitakuwa muwazi katika mawasiliano yangu na nitatoa taarifa kwa wenzangu (pasipokuvunja masharti halali ya usiri). Aidha nitajitahidi kuyatolea majibu haraka iwezekanavyo masuala yote yatakayohitaji maoni yangu.

Nitaheshimu faragha ya wenzangu, na nitajizuia kutoa taarifa zisizokuwa za kweli. Nitajitahidi kusuluuhisha mifarakano na kututua matatizo yatakayojitokeza. Nitachangia kujenga utamaduni wa majadiliano yenye manufaa, yanayoongozwa na tabia za

kuheshimiana, uwazi, pamoja na ukweli kati ya menejimenti na wawakilishi wa wafanyakazi.

Nikiwa meneja/msimamizi nitakuwa muwazi kwa kupokea maoni na mawazo ya kila mjumbe wa timu. Nitakuwa ninatumia mbinu ya uelekezi kutoa maoni yangu ya mara kwa mara kuhusu utendaji wa kila mjumbe wa timu, motisha na hata kutambua na kusifia vipaji vyao.

5. *Nitaboresha usalama, afya na ustawi wa matumishi wa UNHCR kama sharti muhimu la kudumisha utendaji bora na endelevu.*

Daima nitakumbuka na kuzingatia maelekezo yaliyowekwa kwa ajili ya afya, ustawi na usalama wangu. Maamuzi yangu kuhusu masuala ya utendaji daima yataongozwa na usalama wa wafanyakazi. Nikiwa na mashaka yoyote kuhusu jambo ambalo ninahisi linahatarisha usalama wangu au usalama wa watu wengine, nitaomba ushauri mara moja kutoka kwa msimamizi wangu.

Nikiwa meneja/msimamizi nitajitahidi kuhakikisha kuwa hakuna jambo lolote linalohatarisha usalama na ustawi wa wafanyakazi na familia zao. Nitapigania uwiano mzuri kati ya kazi na maisha ya wafanyakazi na nitaheshimu maslahi yao pia.

6. *Nitahifadhi na kutumia kwa uadilifu taarifa na rasilimali zitakazonifikia kutokana na wadhifa wangu katika utumishi wangu kwa UNHCR.*

Nitatumia uadilifu mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu yote na sitofichua taarifa zozote za siri kuhusu wakimbizi, wafanyakazi wenzangu, na masuala mengine kulingana na masharti na kanuni za utumishi pamoja na kanuni zozote elekezi zinazotumika sasa hivi.

Nitalinda, nitasimamia na nitatumia rasilimali zote za hali na mali za UNHCR, pakiwemo wafanyakazi, kwa uangalifu na ufanisi, huku nikizingatia kuwa rasilimali hizi zimetolewa kwa UNHCR kwa manufaa ya wakimbizi na watu wengine wanaohudumiwa na shirika hili.

7. *Nitazuia, nitapinga na nitapambana dhidi ya unyonyaji na udhalilishaji wa wakimbizi na waathiriwa wengine.*

Naapa kwamba kutokana na wadhifa wangu sitotumia vibaya madaraka na uwezo nilio nao dhidi ya maisha na ustawi wa wakimbizi na waathiriwa wengine.

Kamwe sitomwomba mkimbizi au mwathiriwa mwingine huduma au fadhila ili nimpatie ulinzi au msaada. Sitoruhusu ujenzi wa mahusiano kati yangu na wakimbizi au waathiriwa wengine kwa lengo la kujinufaisha kingono , kihisia, kifedha au kikazi.

Lakini mahusiano kama hayo yakijitokeza kati yangu na mnufaika ambapo siyafikirii kama yanatokana na azma ya kujinufaisha, nitatoa taarifa kwa msimamizi wangu ili kuomba ushauri nasaha na maelekezo kwa imani kwamba jambo hili litashughulikiwa kwa uadilifu. Ninaelewa kuwa kuna taratibu na miongozo mwafaka ambayo inaweza kutusaidia mimi na msimamizi wangu katika masuala kama haya.

Nitazingatia sifa za uadilifu na uwajibikaji katika kuwaajiri wakimbizi au waathiriwa wengine kunifanyia kazi zangu binafsi. Aidha nitamwarifu msimamizi wangu kwa maandishi kuhusu aina na masharti ya ajira yenyewe.

8. *Sitojihuisha na uhalifu wowote, wala vitendo vinavyovunja maadili, hakiza binadamu au vile ambavyo vinaharibu jina la UNHCR au kukinzana na ragba zake.*

Sitouna mkono wala kushiriki katika kitendo chochote cha uhalifu, unyonyaji au udhalilishaji, pakiwemo utumikishaji wa watoto, biashara ya uuzaji wa binadamu au bidhaa nyiningine haramu.

Kwa kuwa UNHCR inasisitizia sana viwango vya juu kabisa kuhusu masuala ya ulinzi na malezi ya watoto, ninaelewa fika kwamba ninakatazwa kuwa na mahusiano ya kimpenzi na mtu ambaye umri wake uko chini ya miaka 18. (Ufafanuzi zaidi kuhusu jambo hili unapatikana katika Maeleo kuhusu Kanuni za Maadili).

9. *Nitajizuia kutenda aina yoyote ya unyanyasaji, ubaguzi, udhalilishaji wa kimwili au matusi, kutoa vitisho au upendeleo katika mahali pa kazi.*

Sitotenda wala sitovumilia aina yoyote ya unyanyasaji, pakiwemo mashambulizi ya kimpenzi au matumizi mabaya ya madaraka, katika mahali pa kazi.

Nikiwa meneja/msimamizi, sitoomba fadhila, mikopo au zawadi kutoka kwa wafanyakazi. Aidha sitokubali kupokea vitu vya

aina hiyo hususani kama gharama yake ni kubwa hata kama vimetolewa bure.

Ninatambua kwamba hali hii aghalabu huficha mgongano wa maslahi na uwezekano mkubwa wa kuibuka kwa mapenzi haramu kati yangu na mfanyakazi aliye chini ya usimamizi wangu. Nikijikuta katika mahusiano ya aina hii nitakomesha mara moja mgongano huu wa maslahi.

Kiambatisho 1

Kiambatisho 1.1

Kiambatisho 2

Kiambatisho 3

Kiambatisho 4

KIAMBATISHO 1.1

Misingi Muhimu ya Kanuni za Maadili

Unyonyaji wa Kimapenzi na Uonevu katika Magomvi ya Kibinadamu

Dondoo kutoka katika Mpango wa Utendaji wa Ripoti ya Kikosi Maalumu cha IASC kuhusu Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kimapenzi na Uonevu katika Magomvi ya Kibinadamu.

A. Misingi Muhimu ya Kanuni za Maadili

Jumuiya za kibinadamu zina jukumu la kuwatanza wanufaika na wajibu wa kuhakikisha kuwa wanufaika hao wanapewa hadhi na heshima walau kwa kuzingatia viwango fulani vya adabu. Ili kuzuia unyanyasaji na uonevu wa kimapenzi, misingi muhimu ifuatayo lazima iingizwe katika Kanuni za Maadili²⁰

- ◎ Unyonyaji na uonevu wa kimapenzi ni vitendo viovu na kwa ajili hiyo vinatosha kumfanya mtu afukuzwe kazi.
- ◎ Ushirikishaji wa watoto (watu ambao hawajatimiza umri wa miaka 18) katika vitendo vya ngono unakatazwa pasipokujali sheria za nchi kuhusu umri wa watu walio wengi au umri ambao mtu anaruhusiwa kutoa ridhaa yake. Mhalifu hawezi kujitetea kwa kudai kwamba alikosea umri wa mtoto.
- ◎ Ununuzi wa ngono kwa kutumia fedha, ajira, bidhaa au huduma, pakiwemo aina nyingine za fadhila za kimapenzi au udhalilishaji ni mambo ambayo yanakatazwa kisheria. Aidha ni makosa kumrubuni mtu kwa kutumia misaada ambayo kimsingi ni haki yake kupewa.
- ◎ Mahusiano ya kimapenzi kati ya watoaji huduma za kibinadamu na wanufaika wa huduma hizo yanakatazwa kwa sababu aghalabu yanajitegemeza kwenye misingi haramu. Mahusiano ya aina hii yanaharibu na kushusha heshima ya kazi za utoaji wa misaada ya kibinadamu.
- ◎ Mtumishi ye yeyote anayemhisi mwenzake kuwa na mahusiano haramu ya kimapenzi anapaswa kutoa taarifa kuhusu jambo hilo kupitia utaratibu iliokekwa hata kama mhalifu yuko katika shirika tofauti na la kwake.
- ◎ Watumishi wa jumuiya zinazotoa huduma za kibinadamu wanapaswa kujenga na kudumisha mazingira ambayo yanazuia unyonyaji na uonevu wa kimapenzi na badala yake kuhimiza uzingatiaji wa kanuni za maadili. Mameneja wa ngazi tofauti wana wajibu mahususi wa kujenga na kukuza mifumo ya kudumisha mazingira haya.

KIAMBATISHO 2

Fomu ya Kutolea Taarifa ya Tukio.

Ukurasa wa 1 wa kurasa 4

Maelekezo	Fomu ijazwe na mfanyakazi mtaalamu na mwenye kibali cha kufanya hivyo. Nakala halisi ihifadhiwe na asasi husika (iliyo nje ya kambi). Nakala moja itumwe kwa Afisa Hifadhi wa UNHCR, na ikiwezekana iwekwe mara moja ndani ya bahasha na kufungwa kwa lakiri. (Kama mnusurika anapenda kutoa taarifa ya tukio kwa kituo cha polisi, Afisa hifadhi lazima apatiwe nakala ndani ya muda wa saa 24.)
Tanbihi:	<i>Fomu hii siyo kielelezo cha usaili. Watumishi wanapaswa kupewa mafunzo sahihi Kwa ajili ya kuwasaili wanusurika/waathiriwa. Fomu tofauti zinapatikana kwa ajili ya ushauri na tathmini/matibabu</i>

AINA YA TUKIO		Aina ya tukio la pili
Idadi ya kesi	Kambi/Anuani (kwa ajili ya kesi za Wakimbizi walio mijini na waliorudio makwao)	Tarehe na wakati wa usaili
Idadi ya matukio ya zamani ya mteja huyu (kama zipo)		

TAARIFA ZA MWATHIRIWA/MNUSURIKA			
Jina	Umri	Mwaka wa kuzaliwa	Jinsi :
Anuani:	Usuli wa kabilalake:	Hali yake ya ndoa:	Kazi:
Idadi ya watoto:	Umri wao:	Mkuu wa familia (mwenyewe au jina, uhusiano wake na mnusurika)	
Tathmini ya UNHCR kuhusu hali ya hatari (kama ipo)		Namba ya kadi ya mgawo au ya kitambulisho	
Kama mwathiriwa/ mnusurika ni mtoto Jina la Mlezi:			Uhusiano:

TUKIO		
Mahali pa tukio:	Tarehe ya tukio:	Saa ya tukio
Maelezo ya tukio (toa muhtasari sahihi kuhusu kilichotokea, na kilichofuatia baadaye):		

Ukurasa wa 2 wa kurasa 4

TAARIFA KUHUSU MHALIFU			
Jina:	Idadi ya wahalifu:		Jinsia:
Anuani:	Utaifa:	Umri:	Usuli wa kabilä lake
Uhusiano wake na mwathiriwa/ Mnusurika	Hali ya ndoa:	Kazi:	
Kama mhalifu hajulikani, toa maelezo juu yake, yakijumuisha alama zozote za kuweza kumtambulisha:			
Mahali aliko mhalifu kama panajulikana. Je, mhalifu bado ni mtu wa hatari?			
Kama mhalifu ni mtoto: Jina la mlezi wake:	Uhusiano:		

MASHAHIDI	
Toa maelezo kuhusu mashahidi walioshuhudia tukio (pakiwemo na watoto):	
Majina na anuani:	

HATUA ZILIZOCHUKULIWA - hatua yoyote ambayo itakuwa tayari imeisha chukuliwa tarehe ya kujaza fomu hii		
Aliyepokea ripoti:	Tarehe ya kutoa ripoti	Hatua iliyochukuliwa
POLISI Jina		
AFISA USALAMA Jina		
UNHCR Jina		
KIONGOZI WA JAMII Jina		
AFISA WA AFYA Angalia ukurasa kuhusu Fomu ya Ripoti ya Afya		
WENGINEO Jina		

HATUA ZAIDI ZINAZOHITAJIKA NA KUPANGWA KUCHUKULIWA kuanzia tarehe ambayo fomu hii ili jazwa			
Kunahitajika tathmini ya usalama wa kimwili na mpango wa uimarishwaji wake haraka			
Je, mwathiriwa/mnusurika amepatiwa ushauri nasaha wowote - kama jibu ni ndiyo, je ni ushauri wa aina gani?			
Je, mwathiriwa/mnusurika anatarajia kuripoti tukio kwenye kituo cha polisi?		Ndiyo	Hapana
Je, mhusika anataka kusuluhishwa na wazee/mahakama za kijadi?		Ndiyo	Hapana
Je, ni hatua gani za ufuatiliaji zitakazotekelezwa na idara ya ustawi wa jamii/watumishi wa SGBV?			
Je, ni hatua gani zaidi zinazofaa kuchukuliwa na UNHCR/au watu wengine?			
Aliyejaza fomu (Andika jina kwa herufi kubwa):		Sahihi:	

Ukurasa wa 3 wa kurasa 4

FOMU YA RIPOTI YA AFYA

Baada ya kujaza kurasa za 1 na 2, na mistari miwili ya ukurasa wa 3 mtumishi anapaswa kuwasilisha fomu kwenye kituo cha afya akiwa ameambatana na mwathiriwa/mnusurika. Ukurasa wa 3 unapaswa kujazwa na mtumishi wa kituo cha afya. AU kamc mwathiriwa/mnusurika hakufanyiwa uchunguzi wa kiafya wakati wa kutoa ripoti, toc sababu za kutofanya hivyo hapa chini.

MUHTASARI WA UCHUNGUZI WA KIAFYA

Jina la mnusurika:	Mwaka wa kuzaliwa :	Jinsi:
--------------------	---------------------	--------

(Kama inahitajika) Toa sababu kwa nini mwathiriwa/mnusurika hakufanyiwa uchunguzi wa kiafya wakati ule:

IJAZWE NA MTUMISHI WA KITUO CHA AFYA

Tarehe ya uchunguzi:	Wakati :	Jina la IPD/OPD
----------------------	----------	-----------------

Kabla ya kumsaili/kumchunguza mwathiriwa/mnusurika, soma ukurasa wa 1 na wa 2 wa fomu hii

Jizue kumuuliza mwathiriwa/mnusurika maswali ambayo ameishayatolea majibu Matokeo ya uchunguzi wa kiafya yajazwe kwenye fomu sahihi za kituo cha afya, kwa kuzingatia utaratibu na maelekezo husika. Kumbukumbu za afya, makabrasha, fomu na mambo mengine ni vitu vya siri na vinapaswa kuhifadhiwa mahali ambapo ni salama katika kituo cha afya. Taarifa za kiafya zinapaswa kutolewa kwa idhini ya mwathiriwa/mnusurika anayehusika

UKURASA HUU HAUCHUKUI NAFASI YA FOMU YA UCHUNGUZI WA KIAFYA YA KITUO CHA AFYA. (NI UKURASA WA ZIADA KWA FOMU HIYO)

MUHTASARI WA MATIBABU YALIYOTOLEWA

Tanbihi: Taarifa hizi zinaweza kumsaidia mshauri wakati wa kutoa msaada wa ufuatiliaji. Lakini inakubidi uombe idhini ya mwathiriwa/mnusurika ili kupatiwa taarifa hizi

Mapendekezo ya matibabu ya ufuatiliaji

Rejea kwenye kituo cha afya baada ya wiki mbili
Rejea kwenye kituo cha afya baada ya miezi sita
Hatua nyinginezo, eleza:

Maeleo ya ziada:

Uchunguzi umefanywa na:

Andika jina lake kwa herufi kubwa:	Cheo:
------------------------------------	-------

Sahihi:

Jina la asasi na mhuri:

Ukurasa wa 4 wa kurasa 4

KIBALI CHA KUTOA TAARIFA

Kwa mtumishi au mtu wa kujitolea anayejaza fomu hii:

Msomee mteja fomu nzima, mweleze kwamba ana uhuru wa kuchagua taarifa za kutoa au kukataa kutoa idhini yake. Baadaye mwombe aweke sahihi yake au alama ya kidole mbele ya mashahidi.

Mimi.....(andika jina la mwathiriwa/mnusurika kwa herufi kubwa) natoa idhini yangu kwa asasi zifuatazo kupatiwa taarifa za tukio ambalo nimeliripoti kwenye fomu hii, pamoja na habari kuhusu mahitaji yangu ya sasa hivi. Ninalewa kuwa idhini hii inahitajika ili niweze kupatiwa huduma na msaada bora. Aidha ninaamini pia kuwa taarifa hizi zitatunzwa kwa siri na heshima na kutumika kwa ajili ya kunipatia msaada ninaouhitaji na ninaouomba.

(Weka alama ya X mahali panapohusika)

- Shirika linalohudumia jamii (jina).....
- Kituo cha Afya
(jina la asasi).....
- UNHCR
(Afisa Hifadhi, wengine).....
- Polisi
- Kiongozi wa kambi/mtaa.
Taja majina :.....
- Wengine, eleza:.....

Sahihi au alama ya kidole

Shahidi (sahihi au alama ya kidole).....

Tarehe

Maelekezo kuhusu jinsi ya kujaza kurasa za 1 na 2 za Fomu ya Kutolea Ripoti ya Tukio

Lengo na Madhumuni ya Matumizi

Wafanyakazi wanaobeba majukumu ya uzuiaji na ukabilianaji dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia katika kambi za wakimbizi wanashauriwa kutumia Fomu ya Ripoti ya Tukio la unyanyasaji wa kingono na kijinsia. Jumuiya zote husika zinachangia katika matumizi ya Fomu hii ya Kutolea Taarifa za Tukio ambayo imebuniwa kwa ajili ya kukidhi haja zifuatazo:

- Kutoa kwa uwazi kadiri iwezekanavyo muhtasari wa taarifa muhimu za tukio (katika kurasa nne zilizonakiliwa mbele na nyuma)
- Kama mwathiriwa/mnusurika atakubali: fomu hii itumike kama nyenzo ya kupeana taarifa. Aidha zitolewe nakala za fomu hii ili asasi na watoaji huduma waweze kuitumia katika kumsaidia mwathiriwa/mnusurika au katika shughuli zao za ufuatiliaji
- Iwapo kumefanyika masailiano tofauti mwepushe mwathiriwa/mnusurika na usumbufu wa kurudiarudia maelezo yale yale au kujibu maswali ambayo tayari ameishayatolea majibu.
- Kusanya data husika na za msingi kwa ajili ya matumizi katika shughuli za kufuatilia na kutathmini matukio na programu za SGBV.
- Kusanya data ambazo zina ulinganifu katika mazingira yoyote ya wakimbizi ili kurahisisha matumizi ya data zinazotumiwa na SGBV duniani kote katika kuandaa programu zinazofaa katika mazingira, nchi na kanda tofauti.

FOMU ILIYOJAZWA

Fomu ya Kutolea Taarifa za Tukio siyo mwongozo wa masailiano. Watumishi ambao huendesha masailiano wanapaswa kuwa wamepatiwa mafunzo katika stadi za kufanya hivyo pakiwemo uwezo wa kusikiliza kwa makini na kuonyesha uelewa wa kihisia unaotakikana katika kazi za kuwasaidia wanusurika. Pengine kutahitajika aina nydingine za fomu kwa ajili ya kuelekeza jinsi ya kuendesha masailiano na kurekodi maelezo kwa maandishi. Ni jambo muhimu kukumbuka kuwa mwathiriwa/mnusurika anaweza akadhusrika kihisia. Kwa hiyo masailiano yanapaswa kuendeshwa kwa uangalifu, huruma na heshima kubwa. Wakati mwingine ni vizuri kujaza fomu baada ya msailiwa kuondoka.

